# KISWAHILI

## Shule za Sekondari

### Kitabu cha Mwanafunzi

**Kidato cha 5**




Taasisi ya Elimu Tanzania

# Kiswahili

## Shule za Sekondari

## Kitabu cha Mwanafunzi

## Kidato cha Tano



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI
NA TEKNOLOJIA

*Cheti cha Ithibati*

Na. 1523

Jina la Chapisho: Kiswahili Shule za Sekondari Kitabu cha Mwanafunzi Kidato cha Tano

Mchapishaji: Taasisi ya Elimu Tanzania

Mwandishi: Taasisi ya Elimu Tanzania

ISBN: 978-9912-753-94-5

Kitabu hiki kimeidhinishwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia tarehe 27 Mei 2024 kuwa Kitabu cha Kiada kwa ajili ya Mwanafunzi wa Kidato cha Tano katika Ngazi ya Elimu ya Sekondari nchini Tanzania kulingana na Muhtasari wa mwaka 2023.

Dkt. Lyabwene M. Mtahabwa
Kamishna wa Elimu

FOR ONLINE READING ONLY

Taasisi ya Elimu Tanzania

© Taasisi ya Elimu Tanzania 2024

ISBN: 978-9912-753-94-5

Taasisi ya Elimu Tanzania

Eneo la Mikocheni

132 Barabara ya Ali Hassan Mwinyi

S.L.P. 35094

14112 Dar es Salaam

Simu: +255 735 041 168/ +255 735 041 170

Baruapepe: director.general@tie.go.tz Tovuti: www.tie.go.tz

FOR ONLINE READING ONLY

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kunakili, kurudufu, kuchapisha, kutafsiri wala kukitoa kitabu hiki au sehemu yake kwa namna yoyote ile bila idhini ya maandishi kutoka Taasisi ya Elimu Tanzania.

## Yaliyomo

**Orodha ya vielelezo** ........ vi
**Orodha ya majedwali** ........ vii
**Orodha ya alama na vifupisho** ........ viii
**Shukurani** ........ ix
**Dibaji** ........ x
**Sura ya Kwanza: Sarufi ya Kiswahili** ........ 1
Dhana za fonimu na alofoni za lugha ya Kiswahili ........ 1
Dhana na miundo ya silabi za Kiswahili ........ 4
Sifa na dhima za viarudhi vya lugha ya Kiswahili katika utamkaji ........ 6
Dhana za vipashio vinavyojenga neno ........ 8
Vipashio vinavyojenga neno na dhima zake ........ 12
Kuchanganua sentensi ........ 16
Tamrini ya 1 ........ 45
**Sura ya Pili: Kuwasiliana kwa njia ya mazungumzo na maandishi** ........ 47
Kutumia msamiati mpya katika mazungumzo ya kawaida ........ 47
Kutumia msamiati mpya katika mazungumzo changamani ........ 49
Kutumia msamiati mpya katika matini andishi za kawaida ........ 50
Kutumia msamiati mpya katika matini andishi changamani ........ 51
Kanuni za kipragmatiki katika lugha ........ 53
Dhana ya utata ........ 59
Sababu za utata katika lugha ........ 61
Kuondoa utata katika lugha ........ 62
Tamrini ya 2 ........ 64
**Sura ya Tatu: Asili na chimbuko la Kiswahili** ........ 65
Nadharia za asili na chimbuko la lugha ya Kiswahili ........ 65
Ubantu wa lugha ya Kiswahili kihistoria ........ 70
Ubantu wa lugha ya Kiswahili kiisimu ........ 73
Tamrini ya 3 ........ 84
**Sura ya Nne: Kukua na kuenea kwa Kiswahili** ........ 85
Kukua na kuenea kwa Kiswahili katika nchi za Afrika Mashariki kabla ya uhuru ........ 85
Kukua na kuenea kwa Kiswahili katika nchi za Afrika Mashariki baada ya uhuru ........ 97

FOR ONLINE READING ONLY

Kukua na kuenea kwa Kiswahili kutokana na maendeleo ya sayansi na teknolojia..125
Tamrini ya 4 ........ 128
**Sura ya Tano: Matumizi ya lugha ........ 129**
Hadhi ya Kiswahili kimatumizi ........ 129
Kiswahili kama lugha ya kwanza na ya pili ........ 131
Kiswahili kama lugha rasmi na ya taifa ........ 135
Dhana na sifa za lugha ya kimataifa ........ 136
Sifa za lugha ya Kiswahili kama lugha ya kimataifa ........ 137
Umahiri wa lugha ........ 140
Tamrini ya 5 ........ 143
**Sura ya Sita: Uhariri ........ 144**
Kanuni za uhariri ........ 144
Vipengele vya lugha na maudhui vinavyozingatiwa katika uhariri ........ 146
Alama za uhariri ........ 151
Kuhariri na kutathmini matini za kawaida ........ 153
Tamrini ya 6 ........ 155
**Sura ya Saba: Tafsiri ........ 156**
Mbinu za tafsiri na jinsi ya kuzitumia katika kutafsiri matini za kawaida ........ 156
Tamrini ya 7 ........ 164
**Sura ya 8: Ukalimani ........ 166**
Stadi ya kusikiliza na kunukuu kumbukumbu muhimu wakati wa ukalimani ........ 166
Kukalimani mazungumzo ya kawaida ........ 172
Tamrini ya 8 ........ 177
**Sura ya Tisa: Kuthamini kazi za fasihi ........ 178**
Mitazamo kuhusu dhana ya fasihi ........ 178
Nadharia za chimbuko la fasihi ........ 181
Maendeleo ya fasihi kabla ya ujio wa wageni ........ 183
Maendeleo ya fasihi baada ya ujio wa wageni ........ 184
Maendeleo ya fasihi baada ya uhuru ........ 190
Tamrini ya 9 ........ 197
**Sura ya Kumi: Uhakiki wa kazi za fasihi ........ 198**
Kuhakiki fani na maudhui katika riwaya ........ 198

FOR ONLINE READING ONLY

Kuhusianisha ujumbe unaopatikana katika riwaya na maisha ya kila siku ............205
Kuhakiki fani na maudhui katika tamthiliya ..............................................................207
Kuhusianisha ujumbe unaopatikana katika tamthiliya na maisha ya kila siku ........210
Tamrini ya 10 ...............................................................................................................212
**Sura ya Kumi na Moja: Utungaji wa kazi za fasihi ............................................ 213**
Mbinu za utungaji wa riwaya.......................................................................................213
Mbinu za utungaji wa tamthiliya ...............................................................................217
Kutunga riwaya ...........................................................................................................223
Kutunga tamthiliya .....................................................................................................223
Tamrini ya 11 ..............................................................................................................223
Faharasa .....................................................................................................................224
Bibliografia .................................................................................................................226

FOR ONLINE READING ONLY

# Orodha ya vielelezo

Kielelezo Na. 1.1: Alasauti ....................................................................................2

Kielelezo Na. 1.2: Aina za tungo .......................................................................... 17

Kielelezo Na. 1.3: Aina za sentensi kimuundo ...................................................27

Kielelezo Na. 1.4: Aina za sentensi kidhima .......................................................31

Kielelezo Na. 3.1: Ramani kuonesha maeneo ya Pwani ya Afrika Mashariki .......... 81

Kielelezo Na. 4.1: Ramani ya Afrika Mashariki ikionesha misafara ya biashara ....... 95

Kielelezo Na. 6.1: Alama za uhariri ....................................................................153

Kielelezo Na. 10.1: Vipengele vya uhakiki wa kazi za fasihi ................................204

FOR ONLINE READING ONLY

# Orodha ya majedwali

**Jedwali Na. 3.1 (a):** Muundo wa mzizi wa Kiswahili na lugha zingine za Kibantu...75

**Jedwali Na. 3.1 (b):** Muundo wa mashina ya Kiswahili na lugha zingine za Kibantu...75

**Jedwali Na. 3.2:** Kufanana kwa baadhi ya maneno ya lugha ya Kiswahili na lugha zingine za Kibantu ....................................................................75

**Jedwali Na. 3.3:** Mwanzo wa vitenzi vya Kiswahili na lugha zingine za Kibantu .76

**Jedwali Na. 3.4:** Miisho ya vitenzi vya Kiswahili na lugha zingine za Kibantu .......76

**Jedwali Na. 3.5:** Mnyambuliko wa vitenzi vya Kiswahili na lugha zingine za Kibantu ........................................................................................................77

**Jedwali Na. 3.6:** Uambishaji wa vitenzi vya Kibantu ............................................ 77

**Jedwali Na. 3.7 (a):** Ngeli za nomino za Kiswahili na lugha zingine za Kibantu kwa kigezo cha upatanisho wa kisarufi ..............................................79

**Jedwali Na. 3.7** (b): Ngeli za nomino za Kiswahili na lugha zingine za Kibantu kwa kigezo cha maumbo ya majina ...................................................79

**Jedwali Na. 3.8:** Muundo wa tungo za Kiswahili na lugha zingine za Kibantu ....... 80

**Jedwali Na. 3.9:** Upatanisho wa kisarufi wa tungo za Kiswahili na lugha zingine za Kibantu ..........................................................................................80

FOR ONLINE READING ONLY

## Orodha ya alama na vifupisho

| | |
|---|---|
| A | kiarifu |
| CH | chagizo |
| E | kielezi |
| H | kihusishi |
| I | irabu |
| K | kiima/konsonanti |
| k | kiyeyusho |
| KAR | King's African Rifles (KAR) |
| KE | kirai kielezi |
| KH | kirai kihusishi |
| KHr | kishazi huru |
| KN | kirai nomino |
| $KR^1$ | kishazi kirejeshi |
| KT | kirai kitenzi |
| KTg | kishazi tegemezi |
| KV | kirai kivumishi |
| N | nomino/nazali |
| S | sentensi |
| $S_1$ | sentensi ya kwanza |
| $S_2$ | sentensi ya pili |
| SH | shamirisho |
| T | kitenzi |
| TEHAMA | Teknolojia ya Habari na Mawasiliano |
| TET | Taasisi ya Elimu Tanzania |
| Ts | kitenzi kisaidizi |
| U | kiunganishi |
| UMCA | Universities Mission to Central Africa |
| STZ | Shilingi za Kitanzania |
| W | kiwakilishi |
| BK | Baada ya Kristo |
| Ø | kapa |
| ß | kishazi tegemezi |
| α | kishazi huru |

FOR ONLINE READING ONLY

# Shukurani

Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) inatambua na kuthamini mchango muhimu wa washiriki kutoka taasisi mbalimbali za umma na binafsi zilizoshiriki katika kufanikisha uandishi wa kitabu hiki cha mwanafunzi. Kipekee, TET inatoa shukurani kwa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Chuo Kikuu cha Dodoma, Chuo Kishiriki cha Elimu cha Dar es Salaam (DUCE), Idara ya Uthibiti Ubora wa Shule, vyuo vya ualimu na shule za sekondari.

Pia, TET inatoa shukurani za dhati kwa mchango uliotolewa na wataalamu wafuatao:

**Waandishi**: Bi. Aurelia F. Mutajunwa, Bw. Tumaini M. Mahendeka, Bi. Sarah O. Msafiri (TET), Dkt. Michael A. Mashauri, Dkt. Adventina Y. Buberwa (UDSM), na Dkt. Getruda E. Shima (UDOM)

**Wahariri**: Dkt. Titus M. Ngeme (UDSM), Dkt. Saul S. Bichwa (DUCE) na Dkt. Angelus J. Mnenuka (UDSM)

**Msanifu**: Bw. Maulid M. Ramadhani

**Wachoraji**: Bw. Fikiri A. Msimbe na Bw. Hance E. Wawar

**Mratibu**: Bi. Aurelia F. Mutajunwa

Vilevile, TET inatoa shukurani kwa walimu na wanafunzi wote wa shule za sekondari walioshiriki katika ujaribishaji wa kitabu hiki. Mwisho, TET inaishukuru Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutoa fedha zilizofanikisha kazi ya uandishi na uchapaji wa kitabu hiki.

Dkt. Aneth A. Komba
Mkurugenzi Mkuu
**Taasisi ya Elimu Tanzania**

FOR ONLINE READING ONLY

# Dibaji

Kitabu hiki cha *Kiswahili Shule za Sekondari Kitabu cha Mwanafunzi Kidato cha Tano* kimeandikwa mahususi kwa mwanafunzi wa kidato cha tano wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kitabu hiki kimeandaliwa kulingana na Muhtasari wa Somo la Kiswahili wa mwaka 2023 uliotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Baadhi ya maudhui ya kitabu hiki yamechukuliwa kutoka katika kitabu cha Kiswahili Shule za Sekondari Kidato cha Tano na Sita cha mwaka 2019 kilichoandaliwa kulingana na Muhtasari wa Somo la Kiswahili wa mwaka 2009 uliokuwa umetolewa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

Kitabu hiki kimegawanywa katika sura kumi na moja: Sarufi ya Kiswahili, Kuwasiliana kwa njia ya mazungumzo na maandishi, Asili na chimbuko la Kiswahili, Kukua na kuenea kwa Kiswahili, Matumizi ya lugha, Uhariri, Tafsiri, Ukalimani, Kuthamini kazi za fasihi, Kuhakiki kazi za fasihi na Kutunga kazi za fasihi. Maudhui ya kitabu hiki yamewasilishwa kwa njia ya matini, shughuli za kufanya, vielelezo ambavyo vinachochea ujenzi wa umahiri unaokusudiwa kwa kila sura. Vilevile, katika kila sura, kuna mazoezi yanayolenga kupima na kujenga uelewa pamoja na ujuzi katika somo hili. Pia unapaswa kuandaa mkoba wa kazi kwa ajili ya kutunza kazi mbalimbali zinazotokana na ujifunzaji. Hivyo, unapaswa kufanya mazoezi na shughuli zote zilizomo kwenye kitabu hiki pamoja na shughuli zingine utakazopewa na mwalimu.

Jifunze zaidi kupitia maktaba mtandao

https://ol.tie.go.tz/videos

**Taasisi ya Elimu Tanzania**

FOR ONLINE READING ONLY

# Sura ya Kwanza

# Sarufi ya Kiswahili

## Utangulizi

***Matumizi ya lugha huongozwa na kanuni za lugha husika. Kanuni hizo, kwa ujumla wake, huitwa sarufi. Katika sura hii, utajifunza dhana za fonimu na alofoni za lugha ya Kiswahili na dhana na miundo ya silabi za Kiswahili. Pia, utajifunza sifa na dhima za viarudhi vya lugha ya Kiswahili katika utamkaji. Aidha, utajifunza vipashio vinavyojenga neno na dhima zake. Vilevile, utajifunza kuchanganua sentensi kwa kutumia mikabala ya kidhima na kimuundo. Umahiri utakaoujenga utakuwezesha kutumia Kiswahili katika miktadha mbalimbali kwa kuzingatia misingi na kanuni za lugha ya Kiswahili.***

**Fikiri**

Mawasiliano bila misingi na kanuni za lugha

## Dhana za fonimu na alofoni za lugha ya Kiswahili

**Shughuli ya 1.1**

Chunguza kielelezo Na.1.1, kisha tamka sauti zinazotamkiwa katika kila ala ya matamshi iliyooneshwa.

FOR ONLINE READING ONLY




**Kielelezo Na. 1.1:** *Alasauti*

FOR ONLINE READING ONLY

### Je, wajua ?

Dhana za fonimu na alofoni hujitokeza katika tawi la sarufi matamshi. Vilevile, tawi hilo huitwa fonolojia. Hili ni tawi la sarufi linalohusika na uchunguzi na uchanganuzi wa mfumo wa sauti za lugha mahususi. Mfumo huo hujengwa na vipashio mbalimbali. Kipashio cha msingi katika fonolojia hujulikana kama fonimu. Hizi ni sauti zote za lugha zenye uwezo wa kupambanua au kutofautisha maana katika maneno ya lugha fulani mahususi. Fonimu za lugha zimegawanyika katika makundi mbalimbali ambayo ni konsonanti, irabu na viyeyusho na hutofautiana kwa idadi kutoka lugha moja hadi nyingine. Mathalani, Kiswahili kina jumla ya fonimu thelathini zilizogawanyika katika makundi yaliyotajwa. Katika Kiswahili, kuna irabu tano ambazo ni: /i/, /ɛ/, /u/, /ɔ/, na /a/; konsonanti ishirini na tano ambazo ni /p/, /b/, /t/, /d/, /k/, /g/, /f/, /v/, /s/, /z/,/θ/, /ð/, /č/ (au /ʧ/), /š/ (au /ʃ/), /ɟ/, /ɤ/, /h/, /m/, /n/, /ɲ/, /ŋ/, /l/ na /r/; na viyeyusho viwili ambavyo ni /w/, na /j/. Hapa, fonimu hizo zimeandikwa kwa alfabeti ya kifonetiki.

Fonimu hizi hubainishwa katika makundi mbalimbali kwa kuzingatia sifa zake za utamkaji. Sifa hizi huitwa sifa bainifu. Sifa hizo hutokana na mahali sauti inapotamkiwa, namna inavyotamkwa na hali ya nyuzisauti wakati wa kuitamka. Kutokana na namna zinavyotamkwa, tunapata sauti za vipasuo /p, b, t, d, k, g/, sauti za vikwamizi /f, v, s, z, θ, ð, š, h, ɤ/, sauti za vipasuo-kwamizi /č, ɟ/, sauti za viyeyusho /j, w/, sauti za ving'ong'o au nazali /n, m, ɲ, ŋ/, sauti ya kimadende /r/ na sauti ya kitambaza /l/. Kutokana na mahali pa matamshi, tunapata sauti za midomo /p, b, m, w/, sauti za ufizi /t, d, s, z, r, l, n/, sauti za meno / θ, ð/, sauti za midomo-meno /f, v/, sauti za kaakaa gumu / č, š, ɟ, ɲ, j/, sauti za kaakaa laini /k, g, ŋ, ɤ/, na sauti ya glota /h/. Kutokana na hali ya nyuzisauti, tunapata sauti ghuna /b, d, ɡ, v, z, ð, ɟ, ɤ, m, n, ɲ, ŋ, l, r/ na sauti zisizo ghuna ambazo ni /p, t, k, f, s, θ, ʧ, š, h/. Irabu zote ni sauti ghuna. Kwa hiyo, sifa bainifu za sauti, mathalani /t/ ni *kipasuo, ufizi, si ghuna*.

Irabu zina sifa bainifu zinazotokana na mwinuko wa ulimi kutoka chini kuelekea juu, sehemu ya ulimi inayoinuka na mkao wa midomo wakati wa kuzitamka. Kutokana na mwinuko wa ulimi, kuna irabu ya chini /a/, irabu za juu /i, u/ na irabu za kati /ɔ, ɛ/. Kutokana na mahali pa kutamkiwa, kuna irabu za mbele /i, ɛ/, irabu ya kati /a/, na irabu za nyuma /u, ɔ/. Kwa kigezo cha mkao wa midomo, kuna irabu viringe /u, ɔ/ na irabu si viringe /i, ɛ, a/ ambazo hutamkwa midomo ikiwa imejiviringa au imesambaa, mtawalia.

Aidha, fonimu moja inaweza kujitokeza kwa namna mbalimbali katika maneno fulani kutokana na mazingira ya ujitokezaji wa fonimu hiyo. Fonimu mbili au zaidi zenye maana moja huitwa alofoni. Kwa mfano, matamshi ya maneno nguo, ndoo, na mboga ni /ŋguo/, /ndoo/ na /mbɔga/. Hivyo, sauti /ŋ/, /n/, na /m/ ni alofoni za fonimu moja ambayo ni /n/. Sababu ya tofauti za fonimu hizo ni mazingira ya utokeaji wake. Fonimu /n/ imejitokeza kama [ŋ] katika mazingira ambapo imefuatiwa na sauti /g/. Fonimu hiyo imebaki kuwa /n/ katika mazingira ambapo imefuatiwa na sauti /d/. Kadhalika, fonimu /n/ imejitokeza kama /m/ katika mazingira ambapo imefuatiwa na sauti /b/.

Fonimu na alofoni zina uhusiano wa karibu ingawa zina tofauti pia. Tofauti ni kwamba, fonimu inabadilisha maana ya neno ilhali alofoni haibadilishi maana ya neno. Aidha, alofoni hutokea katika mazingira maalumu, yaani mfuatano wa aina fulani wa sauti ilhali fonimu hutokea mahali pengine popote isipokuwa pale tu inapotokea alofoni. Hivyo, fonimu na alofoni hukamilishana. Hata hivyo, fonimu na alofoni zina mwingiliano mkubwa kwani zote ni sauti za kundi moja na huchangia sifa muhimu za kimatamshi.

FOR ONLINE READING ONLY

**Zoezi la 1.1**

1. Tamka sauti /b/, /f/, /ʧ/, /g/, /z/, na /h/, kisha andika sifa zake bainifu kulingana na sifa za kimatamshi unazozisikia.
2. Tumia mifano ya maneno ya Kiswahili kubainisha uhusiano wa fonimu na alofoni katika matumizi ya lugha.
3. Andika maneno yafuatayo kwa unukuzi wa kifonetiki.

| | |
|---|---|
| (a) ng'ombe | (e) ngoma |
| (b) benki | (f) shaghalabaghala |
| (c) shughuli | (g) mvi |
| (d) thelathini | (h) mvua |

## Dhana na miundo ya silabi za Kiswahili

**Shughuli 1.2**

Kwa kutumia vyanzo mbalimbali, vikiwamo vya ki-TEHAMA, chunguza miundo ya silabi za Kiswahili, kisha tumia maarifa uliyoyapata kubainisha miundo ya silabi za data (a) - (f) uliyopewa.

(a) alisimama

(b) labda

(c) kabobo

(d) watakapomshusha

(e) walinyang'anywa

(f) lambwa

### Dhana ya silabi

Silabi ni dhana inayorejelea sauti au fungu la sauti linalotamkwa mara moja na kwa pamoja kama fungu moja la matamshi. Lugha ya Kiswahili ina silabi huru au wazi na silabi funge. Silabi wazi au huru ni zile zinazoishia na irabu, kwa mfano, *ma-* katika neno *mama*. Silabi funge ni zile ambazo hutumia sauti za nazali zenye sifa ya kusimama kama silabi kama vile *m* katika neno *mtoto*. Irabu zina uwezo wa kusimama peke yake kama silabi lakini ni silabi huru.

FOR ONLINE READING ONLY

## *Miundo ya silabi*

Lugha ya Kiswahili ina silabi zenye miundo mbalimbali. Kuna silabi zenye muundo wa irabu pekee (I); muundo wa konsonanti pekee (K); muundo wa konsonanti na irabu (KI); muundo wa konsonanti, kiyeyusho na irabu (KkI); muundo wa konsonanti, konsonanti na Irabu (KKI); muundo wa konsonanti, konsonanti, kiyeyusho na irabu (KKkI); na muundo wa konsonanti, konsonanti, konsonanti, na irabu (KKKI). Mifano ya miundo ya silabi imeoneshwa katika Jedwali Na. 1.1.

*Jedwali Na. 1. 1:* Mifano ya miundo ya silabi

| *Muundo* | *Mfano wa silabi* |
|---|---|
| I | *a* na *u* katika neno *au* |
| K | *m* katika neno *mti* |
| KI | *mi* katika neno *miti* |
| KkI | *kwe* katika neno *kweli* |
| KKkI | *mbwe* katika neno *mbweu* |
| KKKI | *spri* katika neno *springi* |

### *Je, wajua* ?

Silabi zenye muundo wa K hujengwa na nazali pekee. Muundo wa KKKI hutokana na maneno ya mkopo.

### *Zoezi la 1.2*

1. Chunguza maneno yafuatayo, kisha jibu maswali yanayofuata:

    *chungwa*
    *skrubu*
    *mvi*
    *kindumbwendumbwe*
    *mkoloni*

    (a) Tenga silabi za maneno hayo.

    (b) Bainisha muundo wa kila silabi katika maneno hayo.

2. Kwa kutumia mifano kutoka lugha ya Kiswahili, eleza tofauti baina ya silabi funge na silabi huru.

FOR ONLINE READING ONLY

3. Fafanua jinsi miundo ya silabi za maneno ya Kiswahili yaliyokopwa kutoka lugha za kigeni inavyotofautiana na miundo mingine ya silabi za Kiswahili.

## *Sifa na dhima za viarudhi vya lugha ya Kiswahili katika utamkaji*

### *Shughuli ya 1.3*

Soma kwa sauti sentensi zifuatazo kwa kuzingatia ufasaha wa matamshi, kisha jibu maswali yanayofuata.

(a) Mtoto ame*meza* dawa.

(b) Mtoto amekaa juu ya *meza*.

(c) Hiki ni kitabu.

(d) Hiki ni kitabu?

1. Umebaini tofauti gani za matamshi ya neno "meza" katika sentensi (a) na (b)?
2. Tofauti hizo zimesababisha athari gani kwenye maana ya neno hilo?
3. Kuna tofauti gani ya kimatamshi kati ya sentensi (c) na (d)?
4. Athari gani imetokea kwenye maana ya sentensi hizo?

### *Dhana ya viarudhi*

Viarudhi ni vipengele vya utamkaji vinavyoambatana na vitamkwa wakati wa utamkaji wa tungo za lugha. Viarudhi vinavyopatikana katika Kiswahili pamoja na dhima zake vinafafanuliwa katika vipengele vinavyofuata.

(a) *Mkazo na dhima zake*

Mkazo ni nguvu inayotumika katika kutamka baadhi ya silabi katika neno. Kuna lugha zenye mkazo na zisizo na mkazo. Kiswahili ni lugha yenye mkazo. Katika lugha zenye mkazo, kuna silabi ambazo zina mkazo msingi (zenye kutumia nguvu kubwa zaidi) na ambazo hazina mkazo msingi. Mkazo msingi katika lugha ya Kiswahili unaangukia katika silabi ya pili kutoka mwishoni mwa neno (silabi ya mwisho kasoro moja). Mkazo huu huoneshwa katika kamusi zenye matamshi kwa alama ya ritifaa (') inayopachikwa nyuma au mbele ya silabi inayobeba mkazo huo katika neno. Katika maandishi ya kawaida, hatuweki mkazo ingawa wasomaji wanajua pa kuweka wanaposoma.

Dhima ya mkazo katika lugha ya Kiswahili ni kuufanya utamkaji wa maneno uwe sahihi. Upachikaji wa mkazo katika silabi nyingine yoyote ile huondoa ufasaha. Vilevile, katika baadhi ya maneno, hususani ya mkopo, mkazo huweza kutumika katika kutofautisha maana za maneno yenye maumbo sawa ambayo maana zake hutofautishwa na mkazo.

FOR ONLINE READING ONLY

Kwa mfano, *sa'limu* na *'Salimu,* na *bara'bara* na *ba'rabara.* Aidha, mkazo hutumika kuonesha msisitizo wa ujumbe ambao msemaji anataka kuufikisha kwa kulitamka neno lenye ujumbe huo kwa mkazo zaidi. Kwa mfano, katika sentensi *Nimesema* **ondoka** *hapa,* msisitizo uko katika neno *ondoka* na katika *Nimesema ondoka* **hapa,** msisitizo uko katika neno *hapa.* Ikumbukwe kwamba, ingawa tumeonesha jinsi mkazo unavyowekwa kwenye maandishi, mkazo aghalabu ni kipengele cha kimatamshi.

### (b) Kiimbo na dhima zake

Kiimbo ni mpandoshuko wa mawimbisauti wakati wa usemaji. Kiimbo hubadilikabadilika kulingana na dhamira ya msemaji. Ikiwa msemaji amekusudia kutoa taarifa au kujibu swali kiimbo kitashuka mwishoni mwa tungo. Ikiwa atakuwa anauliza swali, kiimbo kitapanda mwishoni mwa tungo. Aidha, ikiwa msemaji anatoa amri, kiimbo kitashuka au kubaki kati mwishoni mwa tungo. Kuhusiana na mshangao, kiimbo kitategemea namna mzungumzaji anavyoshangaa; huweza kushuka, kuwa kati, kupanda, kupanda na kushuka au kushuka na kupanda.

Sanjari na dhima hizo, kiimbo husaidia katika kuweka mipaka mikubwa na midogo ndani ya tungo wakati wa usemaji. Mipaka hiyo ni ushukaji na upandaji wa kiimbo katika mipaka ya neno, kirai, kishazi na mwisho wa tungo. Ushukaji na upandaji huu husaidia kuifanya sentensi, hasa ndefu, iweze kutamkika na wakati mwingine, husaidia kutofautisha maana zilizokusudiwa na msemaji. Tazama, kwa mfano, jinsi tungo zifuatazo zinavyoweza kutatiza maana katika usemaji:

(a) *Wanafunzi wenye ufahamu na malengo katika maisha, ambao wana nia ya kufikia malengo hayo, hujituma kusoma kwa bidii, hasa wanapokumbuka kuwa muda wa masomo si mrefu.*

(b) *A: Baba mdogo mdogo amekuja.*
*B. Baba mdogomdogo amekuja.*

(c) *A: Watakao wale ng'ombe wote*
*B: Watakao, wale ng'ombe wote*

Maana ya tungo hizi hutegemea namna mzungumzaji anavyoshusha na kupandisha kiimbo wakati anapozitamka. Hivyo, maana ya tungo huweza kutegemea kulingana na ushushaji au upandishaji wa kiimbo.

### (c) Wakaa na dhima zake

Wakaa ni muda unaotumika wakati wa kutamka sauti fulani. Aghalabu, hujitokeza zaidi katika irabu. Katika taaluma ya fonolojia, wakaa huoneshwa kwa alama maalumu ya

FOR ONLINE READING ONLY

nuktapacha (:) ambazo huwekwa mbele ya sauti yenye wakaa mrefu. Sauti yenye wakaa mfupi haiwekewi alama yoyote. Katika matamshi ya maneno ya lugha ya Kiswahili, wakaa hujitokeza katika namna tofautitofauti. Katika maneno mengi, wakaa mrefu hujitokeza katika irabu za silabi zenye mkazo msingi, kama vile katika neno *ana'pi:ma*. Hata hivyo, si kila silabi yenye mkazo ina wakaa mrefu; mathalani, neno **tobo** halina sauti yoyote yenye wakaa mrefu. Kwa hiyo, mzungumzaji anapaswa kuzingatia wakaa sahihi kwa kila neno. Vilevile, wakaa huweza kutumika kutofautisha maana kwa baadhi ya maneno yenye maumbo sawa na maana tofauti, mathalani, **majini** na **ma:jini** kama katika sentensi *Majini yameingia ma:jini*. Vilevile, wakaa huweza kutofautisha maana katika ngazi ya tungo, mathalani, *majibu ya: kitabuni* (majibu yamo kitabuni) na **majibu ya kitabuni** (majibu yanayopatikana katika kitabu).

### *Zoezi la 1.3*

1. Soma kwa sauti sentensi zifuatazo, kisha bainisha maana ya kila tungo ukizingatia jinsi zinavyopaswa kutamkwa, hasa katika maneno yaliyolazwa.
   (a) Anaona **bara`bara**.
   (b) Anaona **ba`rabara**.
3. "Mzungumzaji wa Kiswahili anapaswa kuzingatia kiimbo sahihi ili kurahisisha mawasiliano." Thibitisha kauli hii kwa mifano maridhawa.
3. Bainisha maneno matano ya Kiswahili ambayo maana zake zinatofautishwa kwa wakaa, kisha tunga sentensi mbili kwa kila neno.

## *Dhana za vipashio vinavyojengu neno*

### *Shughuli ya 1.4*

Kwa kutumia vyanzo mbalimbali vya maktabani na/au mtandaoni, kusanya matini zenye aina mbalimbali za maneno, kisha fanya yafuatayo:

(a) Orodhesha nomino tano, kisha andika umoja na wingi wa nomino hizo.

(b) Andika vitenzi vya kauli mbalimbali katika uyakinishi na ukanushi.

(c) Bainisha viambajengo vinavyounda nomino na vitenzi ulivyovibainisha katika vipengele (a) na (b).

### *Dhana ya mofu*

Mofu ni dhana ya kimofolojia inayorejelea umbo dhahiri linaloandikika na kutamkika au lisilodhahiri ambalo linabeba maana ya kileksika au kisarufi. Mathalani, mofu{m-}, katika neno **mtoto,** inabeba mofimu ya nafsi ya tatu umoja na mofimu ya ngeli ya

FOR ONLINE READING ONLY

kwanza. Mofu zinaweza kugawanywa katika makundi kwa kuzingatia vigezo viwili: kigezo cha maana na kigezo cha umbo.

Kwa kuzingatia kigezo cha maana, kuna mofu huru na mofu tegemezi. Mofu huru ni mofu zinazoweza kusimama peke yake na kutoa maana inayojitosheleza, mathalani *kaka, chupa, ndoo,* na *maji*. Mofu tegemezi ni mofu zisizoweza kusimama peke yake na kutoa maana inayojitosheleza, mpaka ziungane na mofu nyingine; mathalani, katika neno *anapika*, mofu *a-*, *-na-*, *-pik-*, *na -a* haziwezi kusimama kila moja peke yake na kutoa maana bila kutegemeana. Mofu tegemezi ni mzizi wa neno pamoja na viambishi. Mzizi ni mofu ambayo hubeba maana ya msingi ya neno. Mathalani, *-pik-* katika neno ana*pik*a ndio mzizi. Kuna aina tatu za mzizi, ambazo ni mzizi sahili, ambatani na huru. Mzizi sahili ni ule ambao husimama peke yake bila kuambatana na mwingine kama vile *-pik-* na mzizi ambatani ni mzizi ulioundwa na mizizi miwili, kama vile *-anamwali* katika neno *mwanamwali*. Mzizi huru ni mzizi unaoweza kusimama kama neno kamili na kutoa maana baada ya kuondolewa viambishi; mathalani, mzizi wa neno *anatabiri (a-na-tabiri)* ambao ni *-tabiri*. Kwa upande wa viambishi, hivi ni mofu tegemezi zenye uamilifu mbalimbali wa kisarufi ambazo huambikwa au hupachikwa kabla au baada ya mzizi. Kuna viambishi awali, viambishi kati na viambishi tamati. Hata hivyo, katika lugha ya kiswahili, kuna viambishi awali na viambishi tamati pekee.

Kwa kigezo cha umbo, kuna mofu dhahiri na mofu kapa. Mofu dhahiri ni mofu zinazodhihirika kiumbo na kimatamshi ilhali mofu kapa ni zile ambazo hazina umbo linalodhihirika kimaandishi wala kimatamshi. Alama inayotumika kuonesha mofu kapa ni Ø kama inavyooneshwa katika mfano wa namba (i) - (iv).

(i) øjiko - majiko

(ii) øgari - magari

(iii) ukuta - økuta

(iv) ukucha - økucha

Alama ø katika mifano (i)-(v) inaonesha kutokuwapo kwa umbo linalobeba mofimu husika katika neno (umoja au wingi), ambayo ndiyo hali ya ukapa.

## Dhana ya mofimu

Mofimu ni kipashio kidogo cha kimofolojia kilichomo akilini mwa msemaji wa lugha, ambacho ni cha kidhahania. Mofimu hubebwa ndani ya mofu. Mofu moja inaweza kuwa na mofimu zaidi ya moja; mathalani, mofu {a-} katika neno *anakula* inabeba mofimu ya idadi (umoja) na mofimu nafsi (nafsi ya tatu). Vilevile, kuna uwezekano wa kuwa na mofimu moja katika mofu mbalimbali, kama ilivyoelezwa katika dhana ya alomofu.

FOR ONLINE READING ONLY

## Dhima za mofimu

Mofimu zina dhima mbalimbali katika neno kama ifuatavyo:

(a) Kuonesha nafsi na mtenda wa jambo. Kwa mfano:

(i) *ni*nakula - mofu *ni*- huonesha mofimu ya nafsi ya kwanza umoja

(ii) *a*nakula - mofu *a*- huonesha mofimu ya nafsi ya tatu umoja

(iii) *wa*takula - mofu *wa*- huonesha mofimu ya nafsi ya tatu wingi

(b) Kuonesha idadi. Kwa mfano:

(i) *m*-ku-lima - mofu *m*- huonesha mofimu ya umoja

(ii) *wa-li-m-saidia* - mofu *wa*- huonesha mofimu ya wingi

(c) Kuonesha njeo (wakati). Inaweza kuwa wakati uliopo, uliopita au ujao. Kwa mfano:

(i) u-*li*-lima - mofu -*li*- huonesha mofimu ya wakati uliopita

(ii) u-*na*-lima - mofu -*na*- huonesha mofimu ya wakati uliopo

(iii) u-*ta*-lima - mofu -*ta*- huonesha mofimu ya wakati ujao

(d) Kuonesha hali mbalimbali za matendo kama vile hali timilifu, masharti, mazoea na mfuatano wa matukio. Kwa mfano:

(i) Amani a-*me*-kula.

Mofu -*me*- huonesha mofimu ya hali timilifu.

(ii) U-*ki*-ja nitakupa zawadi.

Mofu -*ki*- huonesha mofimu ya hali ya masharti.

(iii) Mimi *hu*-anza kazi saa mbili asubuhi.

Mofu *hu*- huonesha mofimu ya hali ya mazoea.

(iv) Mkurugenzi alikuja, *aka*toa maagizo kisha *aka*ondoka.

Mofu *ka*- huonesha mofimu ya hali ya mfuatano wa matukio kwa masimulizi.

(e) Kuonesha urejeshi. Mofu -o-, -ye-, -vyo-, na -zo- zinaonesha mofimu za urejeshi. Kwa mfano:

(i) Wanafunzi wali -*o*- faulu walipewa zawadi.

(ii) Ng'ombe ali -*ye*- vunjika mguu yumo zizini.

(iii) Vyombo vili -*vyo*- nunuliwa ni vizuri sana.

(iv) Nyumba zili -*zo*- jengwa vizuri zinavutia.

FOR ONLINE READING ONLY

(f) Kuonesha kauli mbalimbali za vitenzi kama vile utendeshi, utendea, utendeka, utendwa, utendani na utenda. Tazama mifano ifuatayo kwa kuzingatia mfuatano wa kauli kama zilivyoorodheshwa:

(i) Waziri Mkuu ameend-*esh*-a kampeni ya kuchangia damu.(utendeshi)

(ii) Kazimoto alimpik-*i*-a Subira chakula. (utendea)

(iii) Ardhi hii inalim-*ik*-a vizuri. (utendeka)

(iv) Mbuzi amechinj-*w*-a. (utendwa)

(v) Dingiswayo na Zwida wanashauri-*an*-a. (utendani)

(vi) Mama anapik-*a*. (utenda, kiambishi tamati - uyakinishi)

(vii) Mama hapik-*i*. (utenda, kiambishi tamati - ukanushi)

Katika mfano wa (i)-(vi) hapo juu, mofu *-a* inaonesha kauli ya utenda (uyakinishi) kwa upande wa vitenzi vyenye asili ya Kibantu. Kwa upande wa ukanushi, katika vitenzi vyenye asili ya lugha za Kibantu, mofu *-i* huonesha kauli ya utenda (ukanushi) kama inavyoonekana katika mfano wa (vii) hapo juu. Aidha, mofu hizo hufanya kazi kama viambishi tamati maana. Viambishi tamati maana ni mofu zinazotokea mwishoni mwa kitenzi ili kukamilisha maana ya kitenzi hicho. Katika vitenzi vyenye asili ya Kiarabu, kama vile *sahau, safari,* na *shukuru,* shina zima linaonesha kauli ya kutenda (uyakinishi). Ikiwa vitenzi hivyo vitaambikwa mofu za ukanushi, basi shina hilo litaonesha kauli ya utenda-ukanushi. Kwa mfano, *usisahau, hasafiri,* na *sikushukuru*.

## Dhana ya alomofu

Mofu moja inaweza kujidhihirisha kwa namna tofautitofauti kulingana na mazingira ya utokeaji wake katika umbo la neno. Maumbo tofautitofauti ya mofu moja hujulikana kama alomofu. Hii ina maana kwamba mofu kadhaa zinabeba mofimu moja. Alomofu moja inapotokea, nyingine haiwezi kutokea. Mathalani, katika maneno *mw-ili, m-ti, mu-wa*, ambazo ni nomino za ngeli ya 1, mofu ya umoja ni {mu-}. Hata hivyo, umbo hilo huweza kujitokeza kama {mu-}, {mw-} na {m-}. Hivyo, ni mofu tofautitofauti za mofimu moja, yaani alomofu.

### Zoezi la 1.4

1. Fafanua tofauti zilizopo baina ya mofu na mofimu huku ukitoa mifano kutoka lugha ya Kiswahili.
2. Tumia mifano ya Kiswahili kueleza dhana zifuatazo:
    (a) mzizi tegemezi
    (b) mzizi huru

FOR ONLINE READING ONLY

(c) mzizi ambatani

3. Chunguza data za maneno yafuatayo, kisha bainisha alomofu zinazojitokeza.
   (a) mwalimu
   (b) muumini
   (c) mtu

## *Vipashio vya neno na dhima zake*

### *Shughuli ya 1.5*

Kusanya nomino tano (5) na vitenzi vitano (5) vilivyo katika njeo na kauli tofauti tofauti kutoka katika vyanzo mbalimbali, vikiwamo TEHAMA, kisha bainisha mofu na mofimu zake.

### *Je, wajua* ?

Neno hujengwa na mzizi na viambishi, ambavyo huitwa viambajengo au vipashio vya neno. Baadhi ya mizizi katika lugha ya Kiswahili inaweza kusimama peke yake na kutoa maana, kwa mfano, maneno *safari, sahau*, na *baba* ni mizizi yenye sifa hiyo. Mizizi mingine inahitaji viambishi ili neno liweze kukamilika kimaana, kwa mfano, *-guu (m-guu/mi-guu),* na *chez- (chez-a)*. Dhima kuu ya mzizi ni kubeba maana ya msingi ya neno, ambayo huwa haibadiliki hata baada ya kuondoa au kubadilisha viambishi. Viambishi, huwa na uamilifu au dhima mbalimbali za kisarufi katika neno. Viambishi ni mofu tegemezi zinazoambikwa kwenye mzizi wa neno ili kudokeza dhana fulani ya kisarufi au kuunda neno jipya. Viambishi huainishwa kwa kigezo cha nafasi ambapo vinatokea katika neno. Katika muundo wa maneno ya Kiswahili, viambishi hupachikwa kabla na baada ya mzizi wa neno. Kwa hiyo, kuna viambishi vinavyotokea kabla ya mzizi wa neno ambavyo huitwa viambishi awali na vile vinavyotokea baada ya mzizi wa neno ambavyo huitwa viambishi tamati. Tazama mifano ifuatayo:

(a) (i) *a-na*-pik-a
    (ii) *wa-ta*-kimbi-a
    (iii) *u-me*-ruk-a
    (iv) *ha-tu-ku-m*-som-e-a

(b) (i) a-ta-ni-pig-*i-a*
    (ii) a-me-m-som-*esh-a*
    (iii) m-chez-*o*

FOR ONLINE READING ONLY

Viambishi vilivyoandikwa kwa hatimlalo katika (a) ni viambishi awali na katika (b) ni viambishi tamati. Viambishi vina dhima ya kuonesha *nafsi, njeo, urejeshi wa mtenda* au *mtendwa, urejeshi, idadi, wingi, hali, ukanushi, umoja* pamoja na *kauli* mbalimbali ambazo ni *kutenda, kutendwa, kutendana, kutendeka, kutendesha, kutendea na kutendua.* Viambishi hivi hupachikwa katika mizizi kwa njia ya uambishaji. Uambishaji ni upachikaji wa viambishi katika mzizi ili kuwasilisha uamilifu au dhima mbalimbali. Kuna uambishaji wa aina mbili, uambishaji ambatizi na uambishaji nyambulishi.

*(a) Uambishaji ambatizi*

Huu ni uambikaji wa viambishi vyenye kazi za kisarufi. Uambishaji huu haubadilishi kategoria za maneno kwa sababu unahusisha viambishi vyenye dhima za kisarufi katika neno. Hii ndiyo sababu inayofanya uambishaji wa aina hii uitwe uambishaji kisarufi. Viambishi vyenye dhima za kisarufi ni kama vile viambishi vya ngeli, nafsi, njeo, urejeshi, au yambwa. Viambishi vilivyoandikwa kwa hatimlalo katika data ifuatayo ni mifano ya viambishi vyenye dhima za kisarufi:

-pig-

*a-na*-pig-a

*a-na-ye*-pig-a

*a-na-ye-m*-pig-a

*(b) Uambishaji nyambulishi (unyambulishaji)*

Huu ni uambishaji wenye uamilifu wa kuunda maneno mapya. Matokeo ya uambishaji huu ni kubadili aina ya neno au kupanua maana ya neno. Tazama mifano ifuatayo:

piga (T) - pig*o*, *ki*pig*o*, *m*piga*ji*, *m*pig*anaji*, pig*ano* (N)

*Kauli za vitenzi vya Kiswahili*

Kauli za vitenzi vya Kiswahili hubebwa katika viambishi tamati vya vitenzi. Viambishi hivi huwekwa kabla ya irabu tamati. Miongoni mwa kauli za vitenzi vya Kiswahili ni *utenda, utendwa, utendeka, utendani, utendea,* na *utendeshi.*

(a) *Kauli ya utenda*

Katika kauli hii, kitenzi hubainisha mtendaji wa tendo. Kitenzi huwa na kiambishi tamati ambacho ni irabu tamati. Kwa mfano, tukisema, *Mwalimu anafundisha,* mtenda ni *mwalimu* na kauli ni ya utenda. Tazama mifano zaidi katika data ifuatayo:

(i) Amani *anacheza.*
(ii) Rehema *anaandika.*

FOR ONLINE READING ONLY

(iii) Ali *atalima* bustani.

(iv) Wanafunzi *walifanya* mtihani.

(b) *Kauli ya utendwa*

Hii ni kauli inayoonesha mwathiriwa wa tendo linalotajwa na kitenzi. Katika kauli hii, mtenda wa jambo si lazima atambulike. Ikiwa italazimika kutambuliwa, basi kitaongezeka kihusishi *na* kikiambatana na jina la mtenda au kiwakilishi chake. Mofu ya utendwa ni *-w-*. Mifano ifuatayo inaonesha kauli ya utendwa katika Kiswahili:

(i) Chakula kimepik*w*a.

(ii) Mwizi amekamat*w*a.

(iii) Nyumba imejeng*w*a na mwashi.

(iv) Uchafu umetup*w*a na mama.

(c) *Kauli ya utendeka*

Hii ni kauli inayoonesha uwezekano wa jambo kufanyika au kuwa na hali ya kufanyika. Katika kauli hii, tendo haliwekwi wazi kuwa linatendwa na nani bali huonesha uwezekano wa kutendeka kwa tendo hilo. Mofu za kauli ya utendeka ni *-ek-*, *-ik-*, *-lik-* na *-lek-*. Tazama mifano ifuatayo:

(i) Kitabu kinasom*ek*a.

(ii) Kuta zilijeng*ek*a.

(iii) Wavivu wanafaham*ik*a.

(iv) Pori linaingi*lik*a.

(v) Mazoezi yatafany*ik*a.

(vi) Udongo ulizo*lek*a.

Mofu za kauli ya utendeka hujitokeza kama *-ik-* ikiwa mzizi wa kitenzi una irabu *a*, *i* au *u* na huwa *-ek-* ikiwa mzizi una irabu *e* au *o*. Ikiwa kitenzi kina irabu *a*, *i* au *u* katika mzizi na kuishia na irabu mbili basi mofu ya utendeka itakuwa *-lik-* na ikiwa mzizi una irabu *e* au *o* na kuishia na irabu mbili, basi mofu ya utendeka itakuwa *-lek-*.

(d) *Kauli ya utendani*

Katika kauli hii, watendaji hufanyiana tendo hilohilo kwa wakati mmoja. Mofu ya kauli ya utendani ni *-an-*. Mofu zilizoandikwa kwa hatimlalo katika mifano ifuatayo zinaonesha kauli ya utendani.

(i) Juma na Paulo watatembele*an*a.

(ii) Watoto wanape*an*a zawadi.

(iii) Mabasi yamepish*an*a vizuri.

(iv) Walimu walisaidi*an*a kazi.

FOR ONLINE READING ONLY

(e) *Kauli ya utendea*

Katika kauli hii, mtendaji hufanya tendo fulani badala, kwa niaba, au kuelekea kwa mhusika mwenyewe. Mofu za kauli hii ni *-i-*, *-e-*, *-li-* na *-le-*. Tazama mifano ifuatayo:

(i) Mwanahamisi amempik*i*a mtoto chakula.
(ii) Zabibu atamsom*e*a mama yake kitabu.
(iii) Wanafunzi walimkimbi*li*a mwalimu wao.
(iv) Kalimanzila alimzo*le*a bibi yake takataka.

Mofu za kauli ya utendea hujitokeza kama *-i-* ikiwa mzizi wa kitenzi una irabu *a, i* au *u* na huwa *-e-* ikiwa mzizi una irabu *e* au *o*. Ikiwa kitenzi kina irabu *a, i* au *u* katika mzizi na kuishia na irabu mbili, basi mofu ya utendea itakuwa *-li-* na ikiwa mzizi una irabu *e* au *o* na kuishia na irabu mbili, basi mofu ya utendea itakuwa *-le-*.

(f) *Kauli ya utendeshi au usababishi*

Hii ni kauli ambayo inaonesha hali ya kusababisha kutokea kwa tendo fulani. Mofu za kauli hii ni *-esh-*, *-ish-*, *-z-*, *-lish-*, *-lesh-*, *-fy-*, na *-vy-*. Mifano ifuatayo inaonesha utokeaji wa kauli hii katika Kiswahili:

(i) Bibi alimbeb*esh*a mjukuu mzigo wake.
(ii) Pit*ish*a kamba hii kwenye miti.
(iii) Kombo alimwo*z*a bintiye mwezi uliopita.
(iv) Sisi tutamka*lish*a mtuhumiwa kikao.
(v) Mama amemzo*lesh*a Pili uchafu.
(vi) Matukio ya mauaji yanaogo*fy*a.
(vii) Sanga alimeza dawa za malaria zikamle*vy*a

Katika kauli hii, kuna maumbo mbalimbali yanayoonesha kauli ya utendeshi. Mofu ya kauli ya utendeshi huwa *-ish-* ikiwa mzizi wa kitenzi una irabu *a, i* au *u* na huwa *-esh-* ikiwa mzizi una irabu *e* au *o*. Ikiwa kitenzi kina irabu *a, i* au *u* katika mzizi na kuishia na irabu mbili, basi mofu ya utendeshi itakuwa *-lish-* na ikiwa mzizi una irabu *e* au *o* na kuishia na irabu mbili, basi mofu ya utendeshi itakuwa *-lesh-*. Vitenzi vingine vichache kama vile *lia, lala, jua, toa,* na *oa* hutumia mofu *-z-*. Vilevile, kuna vitenzi vichache ambavyo hutumia mofu *-vy-* na *-fy-*. Kwa mfano, *levya* katika neno *lewa* na *ogofya* katika neno *ogopa*. Hata hivyo, maneno haya huweza kutumia *-esh-* kama ilivyo katika maneno *lewesha* na *ogopesha*.

Kutokana na mifano hiyo, ni dhahiri kuwa viambishi vya kauli za vitenzi hutokea baada ya mzizi. Viambishi hivi ndivyo huwakilisha kauli mbalimbali za vitenzi katika lugha ya Kiswahili. Aidha, imebainika kuwa viambishi vya kauli moja vinaweza kuwa

FOR ONLINE READING ONLY

na maumbo tofautitofauti lakini yakibeba dhana ileile ya kisarufi. Dhana au maana hiyo ya kisarufi huitwa mofimu. Kwa hiyo, maumbo hayo ni mofu tofauti za mofimu moja, yaani, alomofu. Kwa mfano, *-esh-*, *-ish-*, *-z-*, *-lish-*, *-lesh-*, *-vy-*, na *-fy-* ni alomofu za mofimu ya usababishi.

### Zoezi la 1.5

(1) Tofautisha kwa mifano dhana za uambishaji nyambulishi na uambishaji ambatizi.

(2) Bainisha mofu zinazounda maneno yafuatayo:

(a) lililonikera

(b) tutafahamiana

(c) walikikimbilia

(d) sababu

(e) magazeti

(f) hawajajadiliana

(3) Kwa kutumia mifano ya vitenzi vya lugha ya Kiswahili, bainisha alomofu za kauli ya utendea, utendeshi na kauli ya utendeka.

## Kuchanganua sentensi

### Shughuli ya 1.6

Kusanya sentensi kumi zenye miundo tofautitofauti kutoka katika matini yoyote, kisha bainisha mafungu ya maneno zaidi ya moja yanayohusiana.

### Dhana ya tungo

Kabla ya kuanza kuchanganua sentensi, ni muhimu kuelewa dhana ya tungo na aina zake kwani uchanganuzi wa sentensi unazingatia mgawanyo na uhusiano wa tungo ndogo zilizomo ndani yake. Tungo ni kipashio cha kimuundo kinachotokana na uwekaji pamoja wa vipashio vidogovidogo ili kujenga kipashio kikubwa zaidi. Uwekaji pamoja wa vipashio huongozwa na kanuni za kisarufi za lugha inayohusika. Tungo huweza kuwa neno au kifungu cha maneno chenye kutoa taarifa fulani. Tazama mifano ifuatayo:

(i) Anayecheza

(ii) Wanafunzi waliosajiliwa

(iii) Kijana mzuri

(iv) Sara alisafiri jana

Mifano yote iliyotolewa katika (i) - (iv) ni tungo lakini viwango vya kukamilika kwa taarifa zake ni tofauti. Tofauti hiyo inajitokeza katika maana na mpangilio wa maneno uliojenga tungo hizo. Kwa mfano (i) - (ii) ni tungo ambazo zinatoa taarifa lakini taarifa

FOR ONLINE READING ONLY

zake hazijakamilika kimaana. Tungo ya (iii) - (iv) ndizo zinazotoa taarifa kamili. Tungo hizi zimegawanyika katika viwango vinne. Viwango hivyo ni tungo neno, tungo kirai, tungo kishazi na tungo sentensi. Kwa hiyo, kuna aina nne za tungo katika lugha ya Kiswahili. Kielelezo Na.1.2 kinaonesha mpangilio wa viwango hivyo vya tungo. Alama ya mshale inaonesha uhusiano wa kidarajia.




*Kielelezo Na. 1.2:* **Aina za tungo**

*(a) Tungo neno*

Neno katika lugha ya Kiswahili linaweza kusimama peke yake kama tungo na likatoa taarifa fulani. Neno hilo linaweza kuwa shina kama vile **cheza** na **soma** au muunganiko wa shina na viambishi kama inavyojitokeza kwenye nomino **mwanafunzi** au kitenzi **analima**. Neno ndilo kipashio cha msingi cha kisintaksia na ndilo pia huwa msingi wa uundaji wa tungo nyingine kubwa zaidi yake.

*(b) Tungo kirai*

Kirai ni aina ya tungo yenye neno moja au zaidi ambayo uhusiano wake umekitwa katika neno kuu. Neno kuu katika kirai hutokana na aina za maneno. Aina hizo za maneno zinaweza kusimama peke yake kama kirai au kuandamana na maneno mengine kwa kuzingatia uhusiano maalumu baina ya maneno hayo na neno kuu. Kwa hiyo, katika Kiswahili, jina la kirai hutokana na aina ya neno kuu lililopo katika kirai hicho, ambalo ni neno la kwanza katika kirai. Kwa mfano, kama neno kuu ni nomino, kirai kitaitwa kirai nomino na kama neno kuu ni kielezi, basi kirai kitaitwa kirai kielezi.

FOR ONLINE READING ONLY

*Aina za virai*

Virai vinaweza kugawanywa katika aina mbalimbali kwa kuzingatia neno kuu. Aina za maneno zinazotupatia aina za virai ni nomino, vivumishi, vitenzi, na vielezi. Viwakilishi huingia katika kundi la kirai nomino. Hivyo, viwakilishi na maneno mengine kama vile viunganishi na vihisishi hayaundi kirai. Viunganishi hutumika kuunganisha virai. Aidha, vihisishi havifungamani wala kushikana na maneno mengine katika tungo za Kiswahili. Hivyo, aina hizi za maneno haziwezi kuunda virai. Kwa hiyo, tuna aina tano za virai katika lugha ya Kiswahili. Virai hivyo ni **kirai nomino, kirai kivumishi, kirai kitenzi, kirai kihusishi** na **kirai kielezi**.

*Kirai nomino (KN)*

Hiki ni kirai ambacho neno lake kuu ni nomino au kiwakilishi. Hii ina maana kwamba nomino au kiwakilishi hutawala upatanisho wa kisarufi wa neno au maneno yanayoandamana nalo katika tungo inayohusika. Maneno yaliyoandikwa kwa hati mlalo katika data ifuatayo ni mifano ya virai nomino.

(i) **Gari kubwa** limerudishwa.
(ii) **Gari kubwa kuliko yote** limerudishwa.
(iii) **Gari kubwa lililokuwa juu ya mlima** limerudishwa.
(iv) **Gari lililogongwa** limerudishwa.

*Miundo ya kirai nomino*

Kirai nomino huwa na miundo mbalimbali kama inavyooneshwa katika sehemu zinazofuata. Kwa kila muundo, mfano umeoneshwa kwa hatimlalo.

(a) Nomino moja peke yake

(i) **Mwanamichezo** amependeza.
(ii) **Mtoto** anacheza vizuri.
(iii) **Shule** imefunguliwa leo.

(b) Nomino mbili au zaidi zilizounganishwa na kiunganishi

(i) **Baba, mama na kaka** wamesafiri leo.
(ii) **Juma na Roza** wanapendeza sana.
(iii) **Mjomba, shangazi na binamu** watawasili kesho.

(c) Kiwakilishi kimoja au zaidi

(i) **Wao** walifika mapema sana.
(ii) **Sisi** tunasisitiza kwamba tutakuja.
(iii) **Huyu na yule** wanalima vizuri.



FOR ONLINE READING ONLY

(iv) *Vyake na vyangu* mtavikuta nyumbani.

(d) Kiwakilishi na kivumishi

(i) *Sisi sote* ni ndugu.
(ii) *Yule mrembo* amefaulu mtihani.
(iii) *Wale warefu* watakuja kesho.
(iv) *Kile kizuri* kimevunjika.

(e) Nomino na kivumishi kimoja au zaidi

(i) *Mtoto mzuri* anacheza.
(ii) *Mbwa mnene mweupe* amepotea.
(iii) *Meza ndogo fupi* imefunikwa vizuri.
(iv) *Magari mawili makubwa* yanakuja.

(f) Nomino na kishazi rejeshi

(i) *Wanafunzi waliokuja jana* wameitwa.
(ii) *Kalamu inayovuja* ni yangu.
(iii) *Redio iliyonunuliwa* imeibwa.
(iv) *Karatasi zilizoletwa leo* ni nzuri sana.

(g) Kitenzi-jina na kivumishi au bila kivumishi

(i) *Kucheza kwao* kutaleta balaa.
(ii) *Kulima kule* kunapendeza.
(iii) *Kula kuzuri* kumeshamiri kijijini kwetu.
(iv) *Kusoma* kunaburudisha.

**Kirai kivumishi (KV)**
Hiki ni kirai ambacho neno lake kuu ni kivumishi. Kirai hiki kina miundo ifuatayo:

(a) Kivumishi peke yake. Kwa mfano:

(i) Wanafunzi *wazuri* wanahudhuria darasani.
(ii) Mtu *mnene* anakimbia taratibu.
(iii) Mwalimu *hodari* huwahimiza wanafunzi wasome.
(iv) Mbuzi *mweusi* amepelekwa mnadani.

(b) Kivumishi na kielezi

(i) Chakula ni *kitamu mno*.

FOR ONLINE READING ONLY

(ii) Mboga ni **nzuri sana**.
(iii) Mtoto **mweupe sana** amekuja.
(iv) Mvulana **mrefu zaidi** aanike nguo.

(c) Kivumishi na kivumishi. Kwa mfano:

(i) Mtoto **wetu mwerevu** atafaulu masomo.
(ii) Watoto **kumi warefu** walifika shuleni.
(iii) Mbuzi **mmoja mnene** atachinjwa kesho.
(iv) Mtoto **wangu mfupi** anapenda kucheza mpira.

(d) Kivumishi na kishazi rejeshi. Kwa mfano:

(i) Kijana shupavu **aliyeshinda** tuzo amefika.
(ii) Msichana msafi **ambaye** amedhamiri kuwa balozi ni Nyembezi.

(e) Kivumishi na kirai kihusishi. Kwa mfano:

(i) Mzee maarufu **kwa wizi** amekamatwa.
(ii) Simba dume **mwenye masharubu meusi** amepotea.

*Kirai kitenzi (KT)*

Hii ni aina ya kirai ambacho neno lake kuu ni kitenzi. Hii ina maana kwamba muundo wake umeegemea katika uhusiano wa kitenzi na neno au mafungu mengine ya maneno katika tungo. Kirai hiki hutawaliwa na kitenzi kwa sababu hilo ndilo neno lake kuu. Kirai kitenzi kina miundo ifuatayo:

(a) Kitenzi kimoja au zaidi.
(i) Watoto **wanasoma**.
(ii) Watalii **walikuwa wamepumzika.**
(iii) Mwenyekiti **atakuwa anakuja.**
(iv) Mwalimu **anafundisha**

(b) Kitenzi na nomino moja au zaidi (na kivumishi)
(i) Malima **anapenda maua.**
(ii) Dada **alimpa mgeni zawadi**.
(iii) Anna **alimnunulia mgonjwa matunda**.
(iv) Waziri Mkuu **alisoma hotuba**.
(v) Dada **anapika chakula kitamu.**

(c) Kitenzi na kielezi

FOR ONLINE READING ONLY

(i) Baba *anatembea polepole.*

(ii) Mbuzi *anakula harakaharaka.*

(iii) Mama *amekwenda sokoni.*

(d) Kitenzi na kivumishi

(i) Walimu *ni wabunifu.*

(ii) Jadia *ni mpole.*

(iii) Antonio *hapendi wazembe.*

(iv) Mti huu *si mrefu.*

**Kirai kihusishi (KH)**

Hiki ni kirai ambacho neno lake kuu ni kihusishi. Kihusishi hutokea katika sentensi kikiwa kimekamilishwa na nomino. Rejelea mifano ifuatayo:

(i) Mzee Honoye anakula *kwa kijiko.*

(ii) Mama amenunua gari *la watoto.*

(iii) Kijana ameleta majani *ya ng'ombe.*

(iv) Huu ni mwezi *wa mvua.*

(v) *Kitabu chenye* kurasa nyingi

**Kirai kielezi (KE)**

Hiki ni kirai ambacho neno lake kuu ni kielezi. Kielezi huweza kukaa peke yake au kuambatana na kielezi kingine. Aidha, kielezi katika tungo huweza kuelezea kitenzi, kivumishi au kielezi kingine. Tazama mifano ifuatayo:

(i) Ntekaniwa anatembea *polepole sana.*

(ii) Mwalimu atakuja *kesho asubuhi.*

(iii) Alijigonga *mbele ya gari.*

(iv) Dada amechoka *sana.*

(v) *Kesho asubuhi*, tukutane *katika ukumbi huu.*

**Zoezi la 1.6**

1. Fafanua dhima ya neno kuu la kirai katika mawasiliano.
2. Kirai nomino kina dhima mbalimbali katika sentensi. Thibitisha kauli hii kwa hoja zisizopungua tano na mifano maridhawa ya Kiswahili.
3. Fafanua miundo mbalimbali ya kirai kitenzi kwa kutumia mifano ya Kiswahili.
4. Neno linaweza kuwa tungo ila si kila tungo ni neno. Jadili kauli hii kwa mifano ya Kiswahili.

FOR ONLINE READING ONLY

## Shughuli ya 1.7

Tumia vyanzo mbalimbali, ikiwamo vya ki-TEHAMA, kutafuta maana ya kishazi, kisha kusanya sentensi kumi zenye miundo tofautitofauti kutoka katika matini yoyote na bainisha vishazi vilivyomo katika kila sentensi na miundo ya vishazi hivyo.

### (c) Tungo kishazi

Kishazi ni tungo ya ngazi ya juu kuliko kirai na ya chini kuliko sentensi. Kishazi kinaweza ama kuwa na maana kamili au maana isiyo kamili kutegemeana na kitenzi kilichomo katika kishazi hicho. Kitenzi ni kipashio cha msingi katika kishazi. Kitenzi kinaweza kujitosheleza, yaani, kuwa na maana kamili, au kutojitosheleza na kutegemea kitenzi cha kishazi kingine ili kukamilisha maana. Kwa msingi huo, tunaweza kupata aina mbili za vishazi. Aina hizo ni kishazi huru na kishazi tegemezi.

**Kishazi huru**

Hiki ni kishazi kinachoweza kujitosheleza kimaana na kusimama peke yake kama sentensi. Hutambulishwa kwa alama *KHr au* $\alpha$. Ifuatayo ni mifano ya vishazi huru:

(i) Tukila vizuri *tutakuwa na afya njema.*

(ii) Ukiona mto umejaa maji, *usivuke*.

(iii) Chakula kilichopikwa jana, *kilikuwa na ladha nzuri,*

(iv) *Dada anapika chakula* anapokuwa nyumbani.

**Miundo ya kishazi huru**

Kishazi huru kina miundo mbalimbali kama ifuatavyo:

(a) Kitenzi kikuu pekee yake. Kwa mfano:

(i) Alicheza.

(ii) Tunalima.

(iii) Wanakimbizana.

(iv) Wataondoka.

(b) Nomino, kitenzi kikuu na nomino. Kwa mfano:

(i) Mama anapika ugali.

(ii) Mtoto anacheza mpira.

(iii) Diririja anatengeneza kinyago.

(iv) Manase anapiga gitaa.

FOR ONLINE READING ONLY

(c) Nomino na kitenzi kikuu. Kwa mfano:
   (i) Redio imeharibika.
   (ii) Kiswahili kinakua.
   (iii) Ng'ombe amezaa.

(d) Nomino, kitenzi kisaidizi na kitenzi kikuu. Kwa mfano:
   (i) Mama alikuwa anapika.
   (ii) Mgonjwa atakuwa amelala.
   (iii) Mwalimu alikuwa anafundisha.

(e) Nomino/kiwakilishi, kitenzi kishirikishi na nomino na /au kivumishi/. Kwa mfano:
   (i) Joel ni mtoto mzuri.
   (ii) Hii ni nchi kubwa.
   (iii) Manka ni mama yangu.
   (iv) Twiga ndiye mnyama mrefu.

**Sifa za kishazi huru**

Kishazi huru, kama kipashio cha msingi katika tungo, kina sifa mbalimbali ambazo huweza kutumika kukibainisha. Sifa hizo ni kama zifuatazo:

   (a) Hujitosheleza kimuundo na kimaana.
   (b) Kina sifa ya kuwa sentensi sahili.
   (c) Hukamilisha taarifa ya kishazi tegemezi.

**Kishazi tegemezi**

Hiki ni kishazi ambacho hakiwezi kutoa maana kamili mpaka kikamilishwe na kishazi huru. Kwa hiyo, kishazi tegemezi huacha maswali kwa msomaji kutokana na kutokamilika kwake. Hivyo, huhitaji kukamilishwa ili kuondoa maswali hayo. Kishazi tegemezi hutambulishwa kwa alama *KTg* au *β*. Tazama mifano ifuatayo:

   (a) Maswali yaliyosahihishwa …
   (b) Samaki waliovuliwa …
   (c) Alivyoingia …
   (d) Kwa sababu alikuwa mchangamfu …

**Miundo ya vishazi tegemezi vya Kiswahili**

Lugha ya Kiswahili ina miundo minne ya vishazi tegemezi. Miundo hiyo ni vishazi tegemezi vyenye viunganishi tegemezi, vyenye mofu za masharti, mofu za utegemezi wa urejeshi, na vyenye maneno *kwamba* au *kuwa*.

(a) Vishazi tegemezi vyenye muundo wa viunganishi tegemezi
   Vishazi tegemezi hivi hutokana na kuwapo kwa viunganishi tegemezi kama vile

FOR ONLINE READING ONLY

**ingawa, ijapokuwa, isipokuwa, ikiwa, kwa kuwa,** na **kwa vile.** Ifuatayo ni mifano ya vishazi tegemezi vya aina hiyo (vimeandikwa kwa hati mlalo):

(i) **Kwa kuwa wanafunzi wanajisomea kwa bidii,** watafaulu mitihani yao.

(ii) Hakuruka juu sana, **ijapokuwa alikuwa mwepesi.**

(iii) **Ingawa alikuwa mrefu,** hakuweza kuudaka mpira.

(iv) **Ikiwa wananchi tutashirikiana kuwalinda tembo,** vizazi vyetu vitanufaika kwa utalii.

(v) Mlifaulu vizuri, **kwa vile mlikuwa mnasoma kwa bidii**.

(b) Vishazi tegemezi vyenye muundo wa mofu za masharti
Hizi ni mofu zinazodokeza hali ya masharti. Mfano wa mofu hizo ni **-ki-, -nge-,-ngeli-** na **-ngali-.** Chunguza mifano ifuatayo (mofu za masharti zimeandikwa kwa hati mlalo.):

(i) A**ki**nipa pesa zangu, nitanunua vitabu.

(ii) Utaadhibiwa na mwalimu, u**ki**shindwa kufuata taratibu za shule.

(iii) Wa**nge**ondoka mapema, wa**nge**wahi kufika ukumbini.

(iv) U**ngeli**kuwa na pesa u**ngeli**nunua gari.

(v) A**ngali**kuwa mwaminifu a**ngali**pewa mtaji mkubwa.

(c) Vishazi tegemezi vyenye **kwamba** na **kuwa**
Kwa mfano:

(i) **Kusema kwamba hatupendi wali** ni kusema uongo.

(ii) **Kudai kuwa chakula hakitoshi** kutasababisha matatizo.

(d) Vishazi tegemezi vyenye mofu za urejeshi
Aina hii ya muundo wa vishazi tegemezi hutokana na kupachika mofu za urejeshi katika vitenzi au baada ya neno **amba-**. Kwa mfano:

(i) **Walimu wanaofundisha kwa juhudi** watapewa zawadi.

(ii) **Daraja lililobomoka** limejengwa.

(iii) **Kitabu ambacho kimeletwa** ni kizuri.

(iv) **Mwanafunzi aliyefaulu mitihani** atajiunga na chuo kikuu.

(v) **Michezo ambayo itafanyika mwaka huu** itawavutia wengi.

FOR ONLINE READING ONLY

Kitenzi cha kishazi tegemezi kinachotokana na mofu za urejeshi hushushwa hadhi na kufanya kazi ya kivumishi au kielezi. Kwa hiyo, kutokana na mofu za urejeshi, tunapata aina anuwai za vishazi rejeshi.

(a) Vishazi virejeshi vinavyorejelea nomino/viwakilishi. Kwa mfano:

(i) Wao **walioumia** wamepona

(ii) Miti **ambayo imekatwa** ilikuwa barabarani.

(iii) Wanafunzi **waliosimama mstari wa mbele** wasogee mbele hatua moja.

(iv) Mkulima **alimaye kwa bidii** hupata mazao mengi.

(b) Vishazi rejeshi vinavyoonesha wakati. Kwa mfano:

(i) Mwanahawa alifurahi sana **alipofaulu mtihani wa kidato cha sita.**

(ii) Sisi tulimlimia sehemu yake **alipoumia**.

(iii) Baba **alipokuja** tulifurahi sana.

(iv) Wakati **alipokuwa kijana** nilimfahamu vyema.

(c) Vishazi rejeshi vinavyoonesha mahali. Kwa mfano:

(i) Mahali **panapopendeza** ni hapa.

(ii) Mahali **mlimoingia** ni salama.

(iii) Kule **kunakopendeza** hakuna wadudu.

(d) Vishazi rejeshi vinavyoonesha namna/jinsi. Kwa mfano:

(i) Watu walishangaa **alivyoingia**.

(ii) Kabula hakuelewa **alivyoachwa na basi**.

(iii) **Tulivyoondoka** tuliwashangaza.

*Sifa za vishazi tegemezi*

(i) Havijitoshelezi kimaana. Hivyo, huhitaji vishazi huru ili kukamilisha maana.

(ii) Huundwa na:

(a) viambishi rejeshi;

(b) mofu za masharti;

(c) viunganishi tegemezi; na

(d) maneno **kwamba** au **kuwa**.

FOR ONLINE READING ONLY

(iii) Huweza kuondolewa katika sentensi bila kupoteza maana ya msingi ya sentensi hiyo.

(iv) Huweza kutanguliwa au kufuatwa na kishazi huru.

(v) Kishazi tegemezi kinaweza kufanya kazi kama ifanywayo na kielezi au kivumishi.

**Zoezi la 1.7**

1. Fafanua aina za vishazi kwa kutumia mifano mbalimbali.
2. Kwa kutumia mifano, bainisha miundo ya vishazi tegemezi.
3. Onesha vishazi tegemezi na vishazi huru kwa kutumia alama $\alpha$ na $\beta$ katika sentensi zifuatazo:
   (a) Hakutaka kabisa kumsikiliza Madebe kwa sababu ni mwongo.
   (b) Nitamwelewesha vizuri akinifuata.
   (c) Kaka alichukia alipochekwa.
   (d) Miwani yangu ilipovunjika, nilishindwa kusoma.
   (e) Aombaye hupewa.

**Shughuli ya 1.8**

Kila sentensi huundwa na vipashio mbalimbali vyenye dhima anuwai. Kusanya sentensi kumi zenye miundo tofautitofauti kutoka matini yoyote, kisha chambua vipashio vyake na onesha dhima ya kila kipashio.

**(d) Tungo Sentensi**

Sentensi ni neno au kifungu cha maneno chenye kiima na kiarifu na hutoa taarifa iliyokamilika. Hiki ndicho kipashio kikubwa kabisa cha kimuundo katika tungo. Sentensi huwa na muundo uliokamilika ambao hutoa taarifa kamili. Aidha, sifa ya kidhima au kiuamilifu inayotofautisha sentensi na vipashio vingine vya lugha ni kuwa na kiima (K) na kiarifu (A). Sentensi huundwa na vipashio vingine vidogo ambavyo ni neno, virai na vishazi.

**Aina za sentensi**

Uainishaji wa sentensi hufanywa kwa kutumia vigezo viwili ambavyo ni kigezo cha kimuundo na kigezo cha kidhima. Kigezo cha kimuundo huzingatia mjengo au mpangilio wa vipashio katika sentensi, ilhali kigezo cha kidhima huzingatia uamilifu wa vipashio vya sentensi.

FOR ONLINE READING ONLY

### Uainishaji wa sentensi kimuundo

Katika kigezo hiki, sentensi huainishwa kwa kuangalia vipashio vilivyounda sentensi na uhusiano uliopo baina ya kipashio kimoja na kingine. Uhusiano wa vipashio katika sentensi hurejelea namna vipashio vya sentensi vinavyoshikana, vinavyotegemeana na kutawalana katika kuunda sentensi. Kuna aina tatu za sentensi kwa kuzingatia kigezo cha kimuundo ambazo ni sentensi sahili, sentensi ambatani na sentensi changamani. Kielelezo Na. 1.3 kinaonesha uainishaji wa kimuundo.




**Kielelezo Na. 1.3:** *Aina za sentensi kimuundo*

FOR ONLINE READING ONLY

**(1) Sentensi sahili**

Hizi ni sentensi ambazo huundwa na kishazi huru kimoja. Sentensi za aina hii huwa na wazo kuu moja. Kimsingi, usahili wa sentensi sahili hutokana na sentensi kuwa na taarifa moja, ambayo hubebwa na kitenzi kamili. Ikiwa sentensi ina vitenzi zaidi ya kimoja vyenye taarifa tofauti, basi sentensi hiyo haitakuwa sahili. Sentensi sahili ndiyo msingi wa uundaji wa sentensi nyingine. Ifuatayo ni mifano ya sentensi sahili:

(i) Doto ana watoto wawili.

(ii) Mwalimu anaandika ubaoni.

(iii) Baba yangu alikuwa mkali.

(iv) Kaka alikuwa anaimba.

(v) Rais anahutubia wananchi wake.

**Miundo ya sentensi sahili**

Tunapozungumzia miundo ya sentensi sahili, tunaangalia vipashio vinavyozijenga sentensi

hizo. Sentensi sahili huundwa na kitenzi kimoja au zaidi kinachodokeza wazo kuu moja. Kwa kuzingatia ujitokezaji wa kitenzi katika tungo, sentensi sahili zinaweza kugawanywa katika miundo ya aina tatu ambayo ni kitenzi kikuu peke yake, kitenzi kisaidizi na kitenzi kikuu, na kitenzi kishirikishi.

(a) Kitenzi kikuu peke yake

Katika lugha ya Kiswahili, kitenzi kikuu kinaweza kusimama peke yake na kuunda sentensi sahili. Aidha, kitenzi kikuu kinaweza kuambatana na aina nyingine za maneno. Tazama mifano ya sentensi zifuatazo:

(i) **Anaimba**.

(ii) **Anatembea** polepole.

(iii) **Tunasoma** kitabu.

(iv) **Anaogelea** kwenye bwawa.

(b) Kitenzi kisaidizi na kitenzi kikuu

Muundo huu unajengwa na kitenzi kisaidizi kimoja au zaidi na kitenzi kikuu. Vilevile, vitenzi hivyo vinaweza kuandamana na maneno mengine katika sentensi. Tazama mifano hapa chini:

(i) Dereva **atakuwa amegonga** mti.
Ts T

(ii) Dada **alikuwa anapenda** nyimbo.
Ts T

(iii) Baba **alikuwa analima**.
Ts T

(c) Kitenzi kishirikishi

Muundo huu huwa na kitenzi kishirikishi ambacho huandamana na maneno mengine kuunda sentensi. Alama inayotumika kurejelea kitenzi kishirikishi ni **t**. Tazama mifano ifuatayo kwa kuzingatia vitenzi vishirikishi vilivyoandikwa kwa hatimlalo:

(i) Mtoto **angali** mgonjwa.

(ii) Juma na Paulo **ni** watoto wetu.

(iii) Maua **yalikuwa** machanga.

(iv) Maji safi **yamo** mtungini.

(v) Wao **si** wanafunzi.

FOR ONLINE READING ONLY

**Sentensi changamani**

Hizi ni sentensi ambazo huundwa na kishazi tegemezi kimoja au zaidi na kishazi huru au vishazi tegemezi viwili vinavyokamilishana. Vishazi hivi viwili au zaidi haviunganishwi kwa kutumia viunganishi. Tazama mifano ifuatayo:

(i) Mchezaji aliyecheza vizuri amepata zawadi.

(ii) Mgeni rasmi alipofika, sherehe ilianza rasmi.

(iii) Akifika tu, nitaarifu.

(iv) Kwa sababu alikuwa na adabu, watu wengi walimpenda.

(v) Angekuwa mwaminifu, angekabidhiwa duka la baba yake.

**Miundo ya sentensi changamani**

Sentensi changamani zina miundo miwili kama ifuatavyo:

(a) Kishazi tegemezi kimoja au zaidi na kishazi huru. Kwa mfano:

(i) Kiti kilichoharibika, kimetengenezwa.

(ii) Kila nilipokuwa nikitaka kumpiga, roho ilikataa.

(iii) Msichana aliyekuja juzi, akiwa amesuka nywele, ameondoka na begi langu.

(iv) Babu aliyewasili leo, tulipokuwa tunakula ugali, anaitwa Mzee Kidimo.

(b) Vishazi tegemezi viwili vinavyokamilishana. Kwa mfano:

(i) Angesoma kwa bidii, angefaulu vizuri.

(ii) Angalianza matibabu mapema, angalipona.

(iii) Angelikuwa na sauti nzuri, angelijiunga na kwaya ya shule.

**Sentensi ambatani**

Hizi ni sentensi ambazo huundwa na sentensi mbili au zaidi ambazo huunganishwa kwa kutumia kiunganishi. Kwa hiyo, aina hii ya sentensi ina taarifa zaidi ya moja. Kwa mfano:

(i) Mwalimu anafundisha na mwanafunzi anasikiliza.

(ii) Mtoto analia, mama anambembeleza na baba anamsaidia.

(iii) Dada anakuja leo na kaka atakuja kesho, lakini mjomba hatafika kabisa.

(iv) Mwanafunzi aliyeumia amepelekwa hospitalini na kijana aliyempiga ameadhibiwa.

FOR ONLINE READING ONLY

(v) Kwa sababu hakuwa mwadilifu alifukuzwa shule mara moja, lakini wenzake waliendelea na masomo kama kawaida.

**Miundo ya sentensi ambatani**

Sentensi ambatani ina miundo mitatu kama inavyooneshwa hapa chini.

(a) Sentensi sahili mbili au zaidi. Kwa mfano:

(i) Mtoto anacheza na mama anafua nguo.

(ii) Dada ameenda kuchota maji na kaka ameenda mjini.

(iii) Mwalimu anafundisha lakini wanafunzi hawazingatii.

(iv) Gawile anafanya kazi ila Elimboto anategea.

(v) Tulicheza vizuri lakini hatukufunga magoli wala hatukufungwa.

(b) Sentensi changamani na sentensi sahili. Kwa mfano:

(i) Watoto waliosafiri wamerudi, ila wamesahau mizigo yao.

(ii) Mtoto aliyefanya vizuri amekuja, lakini hajafika na mitihani yake.

(iii) Ingawa leo ni siku ya mnada, hakuchinja ng'ombe, bali amechinja mbuzi.

(iv) Akifika nitampa chakula isipokuwa sitampa kinywaji.

(c) Sentensi changamani mbili au zaidi. Kwa mfano:

(i) Kijana aliyevaa shati jekundu ni mwanafunzi, lakini yule aliyevaa shati jeupe ni kaka yangu.

(ii) Akija kwangu nitamsikiliza, lakini asipokuja sitamtafuta.

(iii) Kwa sababu alikuwa anaimba harakaharaka, sikupenda uimbaji wake, ila kucheza kwake kulinivutia.

(iv) Iwapo atakuuliza maswali, mwelekeze kwangu, lakini asipokuuliza usimwelekeze.

## Uainishaji wa sentensi kidhima

Kigezo hiki cha uainishaji wa sentensi hujikita katika uamilifu ambao umebebwa na sentensi inayohusika. Katika uainishaji huu, tunaangalia kama sentensi inatoa taarifa, amri, inauliza swali, au inadokeza hali ya mshangao. Kwa hiyo, sentensi zinazoainishwa kwa kutumia kigezo hiki ni: sentensi amrishi/agizi, sentensi arifu, sentensi ombi, sentensi ulizi, na sentensi mshangao. Kielelezo Na. 1.4 kinaonesha aina hizo.

FOR ONLINE READING ONLY




**Kielelezo Na. 1.4:** *Aina za sentensi kidhima*

### 1. Sentensi amrishi/agizi

Hizi ni sentensi ambazo hutoa maelekezo ya kutendeka kwa jambo fulani. Katika aina hii ya sentensi, msemaji ndiye mwamuzi, na mtendaji hutarajiwa atekeleze agizo. Katika sentensi amrishi, kitenzi huwa na umbo la shina na katika wingi hubeba kiambishi tamati *-ni* katika uyakinishi. Katika ukanushi, hubeba kiambishi cha nafsi na kiambishi cha ukanushi na irabu tamati ya kitenzi hubadilika na kuwa *-e*. Tazama mifano ifuatayo:

(i) Nendeni!

(ii) Ondoka!

(iii) Nenda darasani!

### 2. Sentensi ombi

Hizi ni sentensi ambazo humsihi mtu mwingine akubali kutenda jambo fulani. Sentensi za ombi hutumia sauti ya upole. Katika sentensi za ombi, kitenzi huanza kwa nafsi ya pili umoja au wingi, na irabu tamati hubadilika na kuwa *-e* katika vitenzi vyenye asili ya Kibantu. Tazama mifano ifuatayo:

(i) Unisaidie chenji.

(ii) Tafadhali mniombee.

(iii) Unifikirie vizuri.

### 3. Sentensi arifu

Hizi ni sentensi ambazo hutoa taarifa kuhusu jambo fulani. Tazama mifano ifuatayo:

(i) Mheshimiwa Rais atawasili kesho asubuhi.

(ii) Baba yao ameteuliwa kuwa mkuu wa wilaya.

FOR ONLINE READING ONLY

4. **Sentensi ulizi**
   Hizi ni sentensi ambazo msingi au ujumbe wake huwa katika swali. Hivyo, ni sentensi ambazo huwa na pengo linalohitaji jibu la taarifa fulani. Sentensi hizi huishia kwa alama ya kuuliza. Kwa mfano:
   (i) Mama atarudi lini?
   (ii) Mmeelewa?

5. **Sentensi mshangao**
   Hizi ni sentensi ambazo huonesha kustaajabu, au kushikwa na butwaa. Sentensi hizi huishia kwa alama ya mshangao. Kwa mfano:
   (i) Hee! Hata yeye amechaguliwa!
   (ii) Kumbe! Halipi kodi!

**Zoezi la 1.8**

1. Andika mazungumzo ya watu wawili kuhusu mada yoyote na upigie mstari sentensi changamani kumi ulizotumia, katika habari hiyo.
2. Kwa kutumia mifano ya Kiswahili, fafanua namna sentensi ambatani zinavyoweza kujitokeza.
3. Tumia maneno **ingawa, ijapokuwa, hata hivyo,** na **isipokuwa** kutunga sentensi ambatani.

### Uchanganuzi wa sentensi

Uchanganuzi wa sentensi ni uchambuzi wa sentensi kwa kubainisha vipashio vyake vya kimuundo au kidhima. Katika kubainisha vipashio vya sentensi, tunaanza na kipashio kikubwa hadi kidogo. Uchanganuzi wa sentensi za Kiswahili huongozwa na mikabala miwili ambayo ni mkabala wa kidhima na mkabala wa kimuundo. Hatua za uchanganuzi wa sentensi zinafanana kwa mikabala yote miwili, isipokuwa istilahi za vipashio vinavyounda sentensi. Aidha, mikabala hii haipaswi kutumiwa kwa kuchanganywa. Mkabala wa kidhima hutumia vipashio vya kidhima pekee, ilhali mkabala wa kimuundo hutumia vipashio vya kimuundo pekee.

**Mkabala wa kidhima**

1. Mkabala huu huzingatia uamilifu wa vipashio vinavyounda sentensi. Kwa hiyo, unatumia istilahi za kidhima zifuatazo:

FOR ONLINE READING ONLY

**(a) Kiima**

Kiima ni kipashio cha kiuamilifu cha sentensi ambacho hufafanuliwa na kitenzi. Sehemu ya kiima huweza kukaliwa na nomino, kiwakilishi, au kifungu kingine cha maneno kinachofanya kazi kama nomino. Katika sentensi za kauli ya kutenda, kiima huwa mtenda wa jambo ilhali katika sentensi za kauli ya kutendwa kiima huwa mtendwa wa jambo. Kiima hutambulishwa kwa alama **K**. Chunguza mifano ya kiima iliyoandikwa kwa hatimlalo katika mifano ifuatayo:

(i) **Mtoto mdogo** analia.

(ii) **Mbwa** amecharazwa viboko.

(iii) **Nguo** zimefuliwa vizuri.

**Vipashio vya kiima**

Kiima huundwa na vipashio mbalimbali. Chunguza mifano iliyoandikwa kwa hatimlalo katika vipengele vifuatavyo:

(a) Nomino moja au zaidi au nomino na kivumishi. Kwa mfano:

(i) **Paka** amekamata panya.

(ii) **Mariamu na Hamida** walialikwa kwenye sherehe.

(iii) **Kaka mkubwa** anacheza mpira.

(iv) **Mtoto mzuri** amefaulu mtihani.

(v) **Mwalimu mweledi** anafundisha.

(b) Kiwakilishi peke yake au kiwakilishi na kivumishi. Kwa mfano:

(i) **Yule** analima sana.

(ii) **Wao** watakuja kesho.

(iii) **Yule mrefu** ni kaka yetu.

(iv) **Wale wanene** walikuja jana.

(c) Nomino na kishazi rejeshi. Kwa mfano:

(i) **Mtoto aliyekuja leo** amefaulu.

(ii) **Kiatu kilichopotea** kimeonekana.

(iii) **Msichana aliyevaa vizuri** ni rafiki yangu.

(iv) **Kicheko ambacho alicheka** kilinishtua.

(d) Kitenzi-jina na kivumishi. Kwa mfano:

(i) **Kucheka kwao** kuliwafurahisha wote.

FOR ONLINE READING ONLY

(ii) **Kupotea kwake** kuliwaumiza wengi.

(iii) **Kukimbia kule** hakukuwa kwa kawaida.

**(b) Kiarifu**

Hiki ni kipashio cha kiuamilifu katika sentensi ambacho kina kitenzi ndani yake na kinafafanua kiima. Kipashio kikuu cha kiarifu ni kitenzi. Kiarifu hutokea upande wa kulia mwa kiima cha sentensi za Kiswahili. Kiarifu hutambulishwa kwa alama ya herufi A. Chunguza maneno yaliyoandikwa kwa hatimlalo katika mifano ifuatayo:

(i) Mtoto **anacheza.**

(ii) Mwalimu **alikuwa anacheza vizuri.**

**Vipashio vya kiarifu**

Kiarifu huundwa na vipashio mbalimbali kama inavyoonekana katika mifano iliyoandikwa kwa hatimlalo kwenye vipengele vifuatavyo:

(a) Kitenzi (T)

Hii ni sehemu muhimu ambayo hutoa taarifa kuhusu tendo katika sentensi. Kwa mfano:

(i) Mtoto **anacheza** vizuri.

(ii) Juma **ni** mrefu.

(iii) **Anacheza.**

(iv) Yeye **hucheza** kila jioni.

(v) Mwanamwema **alikuwa anaumwa**.

(b) Shamirisho (SH) au kijalizo

Shamirisho ni sehemu ya kiarifu ambayo hukaliwa na mtendwa au mtendewa. Mtendwa hujulikana pia kama **yambwa** na mtendewa hujulikana pia kama **yambiwa**. Yambwa ni kipashio ambacho huathiriwa na tendo, ilhali yambiwa ni mnufaika wa tendo linaloelezwa na kitenzi. Dhima ya shamirisho ni kukamilisha taarifa inayoelezwa na kitenzi elekezi. Vitenzi elekezi ni vitenzi vinavyobeba yambwa au yambiwa. Kwa mfano:

(i) Jana tulichinja **mbuzi wawili**.

(ii) Kaka amemjengea **baba nyumba kubwa**.

(iii) Mwalimu amewaonesha **wanafunzi vitabu vipya.**

(iv) Raina amempa **Ndola ukwaju mtamu sana.**

(v) Baba amemnunulia **dada nguo nzuri**.

FOR ONLINE READING ONLY

Katika lugha ya Kiswahili, kitenzi kikiwa kinahitaji kukamilishwa kwa nomino mbili basi nomino ya kwanza ni yambiwa na nomino ya pili ndiyo yambwa.

(c) Chagizo (CH)

Chagizo ni sehemu ya kiarifu ambayo hukaliwa na kielezi. Kielezi kinaweza kuhamahama katika sentensi bila kuathiri maana. Kwa mfano:

(i) Mwalimu aliwaambia wanafunzi waondoke **upesi**.

(ii) Ngoswe alikimbia **mapema**.

(iii) Unapenda kula **polepole**.

(iv) Abel anachora **ubaoni**.

Aidha, vielezi vinaweza kuhamahama katika sentensi. Kwa mfano:

(i) **Leo** nitakula ugali.

(ii) Nitakula ugali **leo**.

Uchanganuzi wa sentensi kidhima hufuata hatua mbalimbali ambazo huanzia katika kipashio kikubwa kabisa kwenda kipashio kidogo. Hatua hizo ni hizi zifuatazo:

(i) Kubainisha aina ya sentensi ili kujua vipashio vinavyounda sentensi hiyo. Aina za sentensi katika mkabala wa kidhima ni sentensi arifu, amrishi, ulizi na mshangao

(ii) Kubainisha vipashio vinavyounda sehemu kuu mbili za sentensi. Katika mkabala wa kidhima, vipashio hivyo ni kiima (K) na kiarifu (A)

(iii) Kubainisha vipashio vinavyounda kiima na kiarifu ambavyo kwa upande wa mkabala wa kidhima, ni nomino (N) au kiwakilishi (W) na kivumishi (V) katika kiima, na kitenzi (T), shamirisho (SH) na chagizo (CH) katika kiarifu

(iv) Kuandika aina za maneno zilizomo katika sentensi inayohusika. Aina hizo huandikwa kwa kutumia vifupisho vya aina za maneno kama vile N, T, V, E, W, H, na U. Hii hutumika kwa namna sawa katika mikabala yote ya uchanganuzi.

Chunguza mifano ifuatayo:

FOR ONLINE READING ONLY

**Njia ya Jedwali**

(i) Sentensi ulizi

Maziwa ni lishe bora?

| S. Ulizi | | | |
|---|---|---|---|
| K | A | | |
| N | T | SH | |
| | t | N | V |
| Maziwa | ni | lishe | bora? |

(ii) Sentensi arifu

Wanafunzi wanafagia darasani na wengine wanapanga viti.

| S. Arifu | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| $S_1$ | | | | $S_2$ | | |
| K | A | | | K | A | |
| | | CH | | | | SH |
| N | T | E | U | W | T | N |
| Wanafunzi | wanafagia | darasani | na | wengine | wanapanga | viti |

(iii) Sentensi arifu

Mtoto aliyepotea amepatikana leo.

| S. Arifu | | | |
|---|---|---|---|
| K | | A | |
| | | | CH |
| N | $KR^1$ | T | E |
| Mtoto | aliyepotea | amepatikana | leo |

FOR ONLINE READING ONLY

**Njia ya maelezo**

(i) Sentensi ulizi

Maziwa ni lishe bora?

- Hii ni sentensi ulizi.
- Sentensi hii imeundwa na kiima na kiarifu.
- Kiima kimeundwa na nomino.
- Nomino ni *maziwa.*
- Kiarifu kimeundwa na kitenzi kishirikishi na shamirisho.
- Kitenzi kishirikishi ni *ni.*
- Shamirisho imeundwa na nomino na kivumishi.
- Nomino ni lishe.
- Kivumishi ni bora.

(ii) Sentensi arifu

Wanafunzi wanafagia darasani na wengine wanapanga viti.

- Hii ni sentensi arifu.
- Sentensi arifu imeundwa na sentensi mbili zilizounganishwa na kiunganishi 'na'.
- Sentensi ya kwanza imeundwa na kiima na kiarifu.
- Kiima kimeundwa na nomino.
- Nomino ni *wanafunzi.*
- Kiarifu kimeundwa na kitenzi na chagizo.
- Kitenzi ni *wanafagia.*
- Chagizo imeundwa na kielezi.
- Kielezi ni *darasani.*
- Kuna kiunganishi *na.*
- Sentensi ya pili imeundwa na kiima na kiarifu.
- Kiima kimeundwa na kiwakilishi.
- Kiwakilishi ni *wengine.*
- Kiarifu kimeundwa na kitenzi na shamirisho.
- Kitenzi ni *wanapanga.*
- Shamirisho imeundwa na yambwa.
- Yambwa ina nomino
- Nomino ni *viti.*

FOR ONLINE READING ONLY

**Njia ya matawi**

(i) Sentensi arifu

Dada yangu anasoma kitabu cheusi.




(ii) Sentensi arifu

Watoto wanacheza mpira uwanjani.




FOR ONLINE READING ONLY

**2. Mkabala wa kimuundo**

Mkabala huu hutumika kuchanganulia sentensi kwa kuzingatia muundo wa vipashio vya sentensi. Kwa hiyo, istilahi za kimuundo kama vile kirai nomino (KN), kirai kitenzi (KT), kirai kivumishi (KV), kirai kielezi (KE), na kirai kihusishi (KH) ndizo hutumika katika uchanganuzi wa sentensi.

## Uchanganuzi wa sentensi kimuundo

Uchanganuzi wa sentensi kimuundo hufuata hatua mbalimbali ambazo huanzia katika kipashio kikubwa kabisa kwenda kipashio kidogo. Hatua hizo ni hizi zifuatazo:

(i) Kubainisha aina ya sentensi ili kujua vipashio vinavyounda sentensi hiyo. Katika mkabala wa kimuundo, kuna sentensi sahili, ambatani na changamani.

(ii) Kubainisha vipashio vinavyounda sehemu kuu mbili za sentensi, ambavyo ni kirai nomino (KN) na kirai kitenzi (KT)

(iii) Kubainisha vipashio vinavyounda kirai nomino (KN) na kirai kitenzi (KT). Vipashio vinavyounda kirai nomino (KN) ni nomino (N) au kiwakilishi (W) vikifuatwa na kirai kivumishi (KV) au kishazi rejeshi (KR). Vipashio vinavyounda kirai kitenzi (KT) ni kitenzi (T) ambacho kinaweza kuambatana na kirai nomino (KN), kirai kivumishi (KV), kirai kielezi (KE), au vyote kwa pamoja.

(iv) Kubainisha vipashio vyote vinavyounda virai katika sentensi inayohusika ambavyo ni aina za maneno zinazowakilishwa kwa vifupisho N, T, V, E, W, H, U, na kadhalika.

Mkabala huu huzingatia njia zote za uchanganuzi wa sentensi kama ifuatavyo:

**Njia ya Jedwali**

(i) Sentensi sahili

Maziwa ni lishe bora

<table>
<tr><th colspan="4">S. S</th></tr>
<tr><td>KN</td><td colspan="3">KT</td></tr>
<tr><td rowspan="3">N</td><td>T</td><td colspan="2">KN</td></tr>
<tr><td rowspan="2">T</td><td rowspan="2">N</td><td>KV</td></tr>
<tr><td>V</td></tr>
<tr><td>Maziwa</td><td>ni</td><td>lishe</td><td>bora</td></tr>
</table>

FOR ONLINE READING ONLY

(ii) Sentensi ambatani

Wanafunzi wanafagia darasani na wengine wanapanga viti.

<table>
<tr><th colspan="7">S. A</th></tr>
<tr><td colspan="3">$S_1$</td><td rowspan="4">U</td><td colspan="3">$S_2$</td></tr>
<tr><td>KN</td><td colspan="2">KT</td><td>KN</td><td colspan="2">KT</td></tr>
<tr><td rowspan="2">N</td><td rowspan="2">T</td><td>KE</td><td rowspan="2">W</td><td rowspan="2">T</td><td>KN</td></tr>
<tr><td>E</td><td>N</td></tr>
<tr><td>Wanafunzi</td><td>wanafagia</td><td>darasani</td><td>na</td><td>wengine</td><td>wanapanga</td><td>viti</td></tr>
</table>

(iii) Sentensi changamani

Mtoto aliyepotea amepatikana leo.

<table>
<tr><th colspan="5">S. Ch</th></tr>
<tr><td colspan="3">KN</td><td colspan="2">KT</td></tr>
<tr><td rowspan="3">N</td><td colspan="2">$S_2$</td><td rowspan="3">T</td><td rowspan="2">KE</td></tr>
<tr><td>KN</td><td>KT</td></tr>
<tr><td>N</td><td>T</td><td>E</td></tr>
<tr><td>Mtoto</td><td>Ø</td><td>aliyepotea</td><td>amepatikana</td><td>leo</td></tr>
</table>

FOR ONLINE READING ONLY

**Njia ya kanuni**

(i)Sentensi sahili

Maziwa ni lishe bora.

**S. S**

**S→ KN + KT**
**KN→ N+ KT**
**N→ Maziwa**
**KT→ t + KN**
**t →ni**
**KN→ N +KV**
**N → Lishe**
**KV→ V**
**V→ bora**

(ii) Sentensi ambatani

Wanafunzi wanafagia darasani na wengine wanapanga viti.

**S. A**

**S→ $S_1$ + U + $S_2$**
**$S_1$→ KN+ KT**
**KN→ N**
**N→ Wanafunzi**
**KT→T + KE**
**T→ wanafagia**
**KE→E**
**E→ darasani**
**U→na**
**$S_2$→ KN +KT**
**KN→W**
**W→wengine**
**KT→T + KN**
**T→wanapanga**
**KN→N**
**N→viti**

FOR ONLINE READING ONLY

(iii)Sentensi changamani

Mtoto aliyepotea amepatikana leo.

*S. Ch*

**S→ KN1+ KT1**
**KN1→ N1+ S2**
**N1→ Mtoto**
**S2→ KN2 + KT2**
**KN2→N2**
**N2→ Ø**
**KT2→Ts**
**Ts→ aliyepotea**
**KT1→T + KE**
**T→ amepotea**
**KE→E**
**E→leo**

*Njia ya maelezo*

Njia hii hutumia maelezo katika kuchanganua sentensi.

(i) Maziwa ni lishe bora.

- Hii ni sentensi sahili.
- Sentensi hii imeundwa na kirai nomino na kirai kitenzi.
- Kirai nomino kimeundwa na nomino.
- Nomino ni ***maziwa***.
- Kirai kitenzi kimeundwa na kitenzi kishirikishi na kirai nomino.
- Kitenzi kishirikishi ni ***ni***.
- Kirai nomino kimeundwa na nomino na kirai kivumishi.
- Nomino ni ***lishe***.
- Kirai kivumishi kimeundwa na kivumishi.
- Kivumishi ni ***bora***.

(ii) Wanafunzi wanafagia darasani na wengine wanapanga viti.

- Hii ni sentensi ambatani.
- Sentensi hii imeundwa na sentensi mbili.
- Sentensi ya kwanza imeundwa na kirai nomino na kirai kitenzi.

FOR ONLINE READING ONLY

- Kirai nomino kimeundwa na nomino.
- Nomino ni *wanafunzi*.
- Kirai kitenzi kimeundwa na kitenzi na kirai kielezi.
- Kitenzi ni *wanafagia*.
- Kirai kielezi kimeundwa na kielezi.
- Kielezi ni *darasani*.
- Kuna kiunganishi *na*.
- Sentensi ya pili imeundwa na kirai nomino na kirai kitenzi.
- Kirai nomino kimeundwa na kiwakilishi.
- Kiwakilishi ni *wengine*.
- Kirai kitenzi kimeundwa na kitenzi na kirai nomino.
- Kitenzi ni *wanapanga*.
- Kirai nomino kimeundwa na nomino.
- Nomino ni *viti*.

(iii) Mtoto aliyepotea amepatikana leo.

- Hii ni sentensi changamani.
- Sentensi hii imeundwa na kirai nomino na kirai kitenzi.
- Kirai nomino kimeundwa na nomino na sentensi ya pili.
- Nomino ni *mtoto*.
- Sentensi ya pili imeundwa na kirai nomino na kirai kitenzi.
- Kirai nomino kimeundwa na nomino.
- Nomino ni *kapa*.
- Kirai kitenzi kimeundwa na kitenzi na kirai kielezi
- Kitenzi ni *amepatikana*.
- Kirai kielezi kimeundwa na kielezi.
- Kielezi ni *leo*.

FOR ONLINE READING ONLY

*Njia ya matawi*

(i) Sentensi sahili

Mtoto yule alikuwa anacheza uwanjani.




(ii) Sentensi ambatani

Wanafunzi hawa wanasoma vitabu lakini wale watatu wanaandika.




FOR ONLINE READING ONLY

(i) Sentensi changamani

Kiti kilichovunjika kimetengenezwa.




*Zoezi la 1.9*

1. Eleza changamoto unazokutana nazo wakati wa uchanganuzi wa sentensi kwa kila njia ya uchanganuzi uliyojifunza.
2. Fafanua kwa mifano hatua za uchanganuzi wa sentensi kimuundo.
3. Changanua sentensi zifuatazo kwa njia ya matawi na ya majedwali kwa kutumia mkabala wa kimuundo:
   (a) Kasabanganya amempa Ruboza karatasi.
   (b) Msichana aliyekuja jana ameondoka leo.
   (c) Mama anapika na baba anaosha vyombo.
   (d) Sisi tulikubali makosa ila wao walikataa.

*Tamrini ya 1*

1. Uchambuzi wa miundo ya sentensi una umuhimu gani kwa mtumiaji wa lugha?
2. Sentensi changamani zina miundo mbalimbali. Bainisha miundo hiyo kwa mifano ya Kiswahili.
3. Kitenzi cha Kiswahili kina ukwasi wa viambishi vya kisarufi. Fafanua ukweli huu kwa kutumia mifano maridhawa.

FOR ONLINE READING ONLY

4. Changanua sentensi ifuatayo kimuundo kwa njia ya maelezo.

*Wanafunzi waliofaulu mtihani wanasoma vyuo vikuu.*

5. Changanua kimuundo sentensi zifuatazo kwa njia ya matawi.

(a) Mbuzi aliyeuzwa jana amesafirishwa kwa basi.

(b) Mwaka jana, nilinunua mpira wa miguu.

(c) Soma maswali kisha andika majibu sahihi.

(d) Kiti kilichovunjika kimeondolewa sebuleni.

6. Changanua kidhima sentensi zifuatazo kwa njia ya mishale.

(a) Shangazi yangu ndiye mpole.

(b) Nini kimetupwa hapa?

(c) Ondoka hapa!

(d) Baba amempa mtoto zawadi.

FOR ONLINE READING ONLY

# Sura ya Pili

## *Kuwasiliana kwa njia ya mazungumzo na maandishi*

*Utangulizi*

**Mazungumzo na maandishi ni njia kuu za mawasiliano katika miktadha mbalimbali** *kama vile nyumbani, shuleni, kazini au ofisini. Katika sura hii, utajifunza kubaini na* **kutumia msamiati mpya katika mazungumzo na maandishi ya kawaida na changamani katika miktadha mbalimbali. Vilevile, utajifunza kutumia kanuni za kipragmatiki katika mawasiliano. Aidha, utajifunza dhana ya utata, sababu za utata na namna ya kuuondoa. Umahiri utakaoujenga utakusaidia kuwasiliana kwa ufasaha kwa njia ya mazungumzo na maandishi katika miktadha mbalimbali.**

*Fikiri*

Mawasiliano yatakavyoathirika kutokana na wazungumzaji kutumia maneno mapya

### *Kutumia msamiati mpya katika mazungumzo ya kawaida*

*Shughuli ya 2.1*

Soma mazungumzo kati ya Fute na Simbwi, kisha fanya yafuatayo:

(a) Bainisha msamiati mpya uliotumika katika mazungumzo uliyoyasoma.

(b) Tumia kamusi kufafanua msamiati mpya ulioubainisha katika mazungumzo uliyoyasoma.

(c) Tumia msamiati mpya ulioubaini katika mazungumzo uliyoyasoma kuandaa mazungumzo ya kawaida.

*Fute:* **Hodi! Hodi! Hodi, Simbwi!**

*Simbwi: Karibu, rafiki!*

FOR ONLINE READING ONLY

*Fute*: **Nabisha hodi kadha wa kadha lakini huitikii. Hutaki wageni leo au vipi?**

*Simbwi*: *Hapana, rafiki yangu! Siwezi kukataa wageni abadani. Wageni ni baraka, bwana. Karibu sana, rafiki yangu! Karibu uketi hapa karibu nami.*

*Fute*: **Asante sana! Unaendeleaje, ndugu yangu?**

*Simbwi*: **Niko salama kabisa. Karibu na karibu tena! Kuja kwako hapa kwangu ni adhama kwelikweli; kwangu na kwa familia yangu yote.**

***Fute***: **Asante! Asante! Ila acha utani bwana. Mimi kuja kwako ni jambo la kawaida kabisa.**

***Simbwi***: *Hapana, rafiki yangu! Usichukulie kawaida. Karibu! Karibu! Umekuja wakati* **mzuri sana maana muda huuhuu nimetoka kuvuna matunda. Nikuandalie karakara au boribo?**

***Fute***: *Mmh! Nipatie boribo, rafiki yangu. Si unajua ninapenda maboribo kuliko* **makarakara?**

***Simbwi***: **Sawasawa! Nimefurahi umetimiza ahadi yako ya kututembelea. Usingekuja kama ulivyofanya mwezi jana, ningekufanyia apizo.**

***Fute***: **Du! Ninaomba uniwie radhi sana. Mwezi uliopita, shughuli zilinibana sana kiasi cha kushindwa kutoka. Ila, kama nisingekuja awamu hii, ningekuwa fedhuli kabisa.**

***Simbwi***: **Hamna bwana! Wakati mwingine tunabanwa na shughuli. Hivi hukukutana na afwaji pale njiapanda? Nilikuwa na kimuyemuye cha kukupokea lakini** *nikahofia afwaji ile.*

***Fute***: **Njiapanda kulikuwa kweupe kabisa ila niliona baadhi ya watu wakichanyatia kuelekea bondeni.**

***Simbwi***: *Kumbe! Sawasawa. Karibu tunda! Karibu sana, rafiki yangu!*

***Fute***: **Asante sana! (Ananawa mikono na kula tunda alilopewa.) Asante sana, Simbwi! Tunda ni tamu sana. Sasa nimekuona. Ninaomba niondoke ili niwahi majukumu mengine kabla ya jua kuzama.**

***Simbwi***: **Sawa! Tunashukuru kwa kuja kutuona kwa kweli.**

***Fute***: **Asante sana! Wape salamu mama na watoto maana sijabahatika kuwakuta.**

***Simbwi***: *Sawa, rafiki yangu! Zimewafikia. Karibu tena!*

***Fute***: **Asante!**

FOR ONLINE READING ONLY

**Je, wajua**

Mazungumzo ya kawaida ni mazungumzo ya kila siku ambayo yanahusu mada za kawaida na yanatumia maneno yasiyo istilahi, yaani, yasiyo ya uwanja maalumu.

*Shughuli ya 2.2*

Tumia vyanzo mbalimbali, vikiwamo vya ki-TEHAMA kutafuta hotuba yoyote ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kisha sikiliza hotuba hiyo na ubainishe maneno yote ambayo ni msamiati mpya kwako. Tafuta maana zake kwenye kamusi, kisha yatumie kuandaa hotuba yenye maneno kati ya 250 na 300 na kuisoma kwa wenzako.

## *Kutumia msamiati mpya katika mazungumzo changamani*

*Shughuli ya 2.3*

*Chunguza mazungumzo uliyopewa hapa chini, kisha fanya yafuatayo:*

Bainisha msamiati mpya uliotumika katika mazungumzo changamani uliyopewa.

(a) Kwa kutumia vyanzo mbalimbali, ikiwamo kamusi, fafanua maana za msamiati mpya ulioubainisha kutokana na mazungumzo changamani uliyopewa.

(b) Kwa kuzingatia maana ulizozibainisha katika kipengele (b), msamiati mpya uliotumika katika mazungumzo changamani uliyopewa unahusu mchoro gani?

**Boti:** ***Shate, mtihani wa leo umeuonaje?***

**Shate:** ***Upi huo? Kiswahili au Baiolojia?***

**Boti:** ***Baiolojia.***

**Shate:** ***Ulikuwa mzuri ila mchoro ulinikamata kidogo.***

**Boti:** ***Mchoro upi?***

**Shate:** ***Mchoro wa swali la sita.***

**Boti:** ***Hata wewe, Shate! Mimi nimepambana na huo lakini nimeshindwa kuchora kongosho na uchengelele. Wewe je?***

**Shate:** ***Mimi hivyo nimeviweza ila nimepata changamoto kuchora tokoni, kibole na ujovu.***

FOR ONLINE READING ONLY

*Boti:* **Pole! Uliweza kuchora mtulinga?**

*Shate:* **Ndiyo!**

*Boti:* **Inabidi tusome vizuri mchoro ule ili kuepuka kujibu maswali kwa kubabaisha.**

*Shate:* **Ni kweli, Boti.**

*Boti:* **Jioni njema, Shate.**

*Shate:* **Nawe pia.**

**Je, wajua**

Mazungumzo changamani ni mazungumzo ambayo yanatumia msamiati wa kawaida na istilahi, yaani, msamiati wa uwanja maalumu. Mara nyingi, mazungumzo changamani huhitaji wazungumzaji wenye utaalamu au ufahamu wa kina juu ya mada inayozungumzwa.

## Kutumia msamiati mpya katika matini andishi za kawaida

### Shughuli ya 2.4

**Chunguza matini ifuatayo, kisha fanya yafuatayo:**

(a) Bainisha msamiati mpya uliotumika.

(b) Tumia msamiati mpya ulioubainisha katika kipengele (a) kutunga sentensi.

(c) Eleza tofauti baina ya matini andishi ya kawaida na mazungumzo ya kawaida.

*Kutoka kwa:* **kalikwendalimited@viwanda.com**

*Kwa:* **msambajzajikalikwendalimited @viwanda.com**

**Tarehe: 20 Machi 2024**

*Mada: TAARIFA KUHUSU MABADILIKO YA BEI ZA BIDHAA NA NJIA ZA MALIPO*

**Mpendwa msambazaji wa bidhaa zetu,**

**Ninatumaini kwamba u buheri wa afya na unaendelea na idili ya usambazaji wa bidhaa zetu. Ninapenda kukujulisha kuwa tumefanya mabadiliko ya bei za bidhaa na njia za malipo. Hivyo, ninaomba uwahabarishe wateja wetu kuhusu mabadiliko hayo.**

FOR ONLINE READING ONLY

*Kuanzia tarehe 1 Aprili 2024, bidhaa zetu zitaongezeka bei kwa kiasi cha STZ 20,000* **hadi 25,000. Aidha, tunatazamia kuboresha mfumo wetu wa malipo na kuanza kutumia lipa namba kwa ajili ya kufanya miamala ili kuwawezesha wateja wetu kufanya malipo kwa njia rahisi na ya haraka zaidi. Hii ni sehemu ya jitihada zetu za kuboresha na kuwezesha kupatikana kwa huduma mujarabu kwa wateja wetu.**

**Kupitia mfumo huu mpya, wateja wetu watachagua kufanya malipo zaidi kwa njia isiyo na adha kwao ikiwa ni pamoja na malipo kupitia simumaizi au miamala ya kibenki. Tunatarajia kwamba mabadiliko haya yataleta ahueni ya kuondoa afwaji inayongojea kufanya malipo ya fedha taslimu. Njia hii ina tija na itasaidia wateja wetu kuokoa muda na kujishughulisha na kazi zingine. Ninatumaini kuwa njia hizi mpya za malipo zitarahisisha malipo na kuondoa adha kwa wateja wetu.**

**Tafadhali, jisikie sabili kuwasiliana nasi kupitia anwani ya baruapepe yetu au simu ya kampuni ikiwa una maswali au unahitaji msaada wowote. Aidha, kumbuka kuhifadhi nywila vizuri ili kuhakikisha kwamba miamala inayofanyika iko salama. Tutakuwa tayari kukuhudumia. Tunawashukuru kwa ushirikiano wenu.**

**Tunakutakia mafanikio katika shughuli zako zote.**

**Wakatabahu,**

**Majani Marefu**
*Afisa Masoko*
**Kalikwenda Limited Tanzania**

### Je, wajua

Matini andishi za kawaida ni matini zilizoandikwa ambazo zinashughulikia mada zinazohusu maisha ya kawaida ya kila siku. Aghalabu, matini za aina hii hazitumii istilahi.

## *Kutumia msamiati mpya katika matini andishi changamani*

### Shughuli ya 2.5

*Chunguza matini andishi ya Hali za Mwili na Dalili Zake, kisha fanya yafuatayo:*

(a) Bainisha uwanja mahususi wa matini andishi uliyoichunguza.

(b) Fafanua maana za msamiati mpya uliotumika katika matini andishi uliyoichunguza.

FOR ONLINE READING ONLY

(c) Tumia msamiati mpya ulioubainisha kuandika kifungu cha habari chenye mada mojawapo kati ya hizi:

(i) Umuhimu wa afya

(ii) Umuhimu wa lishe katika kulinda afya

**Hali za Mwili na Dalili Zake**

*Kuna hali mbalimbali ambazo hutokea katika mwili ambazo huweza kuathiri afya ya mwili na kusababisha mwili kudhoofu. Katika somo hili, tutaeleza dalili za baadhi ya hali zinazotokea katika mwili ili kukuwezesha kutambua dalili anuwai za kila changamoto. Hali yoyote, isiposhughulikiwa mapema, inaweza kusababisha changamoto zaidi. Hali zinazofafanuliwa katika somo hili ni usonji, anemia, pumu, selimundu, kifafa, na bawasiri.*

*Kwa kuanza na usonji, hali hii haifahamiki kwa watu wengi. Wakati mwingine, wazazi au jamii huwalaumu watoto kwa kuwa na tabia ambazo hufikiri kwamba watoto huzionesha kwa kukusudia. Mtoto mwenye usonji huwa na dilili kadha wa kadha, zikiwamo kushindwa kutafsiri hisia za watu wengine, kupendelea kucheza peke yake na kupendelea kucheza michezo inayojirudiarudia. Dalili ya mtoto kucheza michezo ileile kila wakati huchukuliwa na baadhi ya wazazi au walezi kuwa ni uraibu wa michezo hiyo bila kutambua kwamba hali hiyo ni dalili ya hali fulani ya mwili.*

*Changamoto nyingine ambayo hutokea katika mwili ni pumu. Dalili za mtu mwenye pumu ni kupumua kwa shida, kukohoa sana, na kubanwa na kifua. Baadhi ya watu hupata shida hii kutokana na mzio wa vyakula fulani, vinywaji vya baridi au vumbi. Watu wanaopata shida hii kutokana na mzio wanatakiwa kuepuka vyakula au hali inayowasababishia kuwa hivyo.*

*Zaidi ya hayo, baadhi ya watu huweza kuwa na anemia. Dalili za anemia ni kuhisi uchovu wa viungo vya mwili na akili. Pia, mtu mwenye anemia hupata mabadiliko ya ngozi, usingizi huongezeka, hushindwa kupumua vizuri, na kichwa kuuma. Anemia inaweza kusababishwa na upungufu wa madini chuma na vitamini B12 mwilini. Watu wenye anemia inayotokana na upungufu wa madini chuma wanaweza kutumia virutubisho vyenye madini chuma ili kuongeza madini hayo mwilini.*

*Kwa upande wa kifafa, hali hii humfanya mtu kuanguaka na kupoteza fahamu kwa muda huku akifafaruka na kutoa povu kinywani. Dalili zake ni pamoja na mtu kuishiwa nguvu, kichwa kuuma, na kuwa na dilili za kuchanganyikiwa. Dalili nyingine ni kupoteza fahamu. Kifafa hutokea utotoni na wakati mwingine hutoweka.*

FOR ONLINE READING ONLY

*Hali nyingine inayodhoofisha mwili ni selimundu. Dalili za selimundu ni mtu* **kushindwa kupumua vizuri, kuhisi baridi kwenye viganja na nyayo, maumivu ya vipindi, kizunguzungu na changamoto katika uoni.**

**Mwisho, hali nyingine inayoweza kuathiri mwili ni bawasiri. Dalili za hali hii ni pamoja na kuhisi maumivu na kutokwa na damu wakati wa kujisaidia haja kubwa. Kwa ujumla, ni vyema kuwa makini na mabadiliko yanayotokea katika mwili ili kuweza kuchukua hatua stahiki.**

*Je, wajua* ?

Matini andishi changamani ni matini zilizoandikwa ambazo hutumia istilahi au msamiati maalumu wa kiufundi kwa kiwango kikubwa.

*Zoezi la 2.1*

1. "Kutumia maneno ambayo hayajulikani kwa wasikilizaji hukwamisha mawasiliano". Jadili kauli hii kwa mifano maridhawa.
2. Fafanua mbinu unazoweza kutumia ili kutambua maana za maneno mapya yaliyotumika kwenye matini.
3. Eleza tofauti iliyopo baina ya matini andishi ya kawaida na matini andishi changamani.

## *Kanuni za kipragmatiki katika lugha*

*Shughuli ya 2.6*

Tembelea maeneo mawili kati ya sokoni, shuleni, mtaani, nyumbani na hospitalini. Chunguza namna mawasiliano yanavyofanyika katika mazingira hayo. Eleza kwa nini mawasiliano yanafanyika kwa namna hiyo uliyoibaini. Kisha, eleza tofauti ulizozibaini za kimawasiliano katika maeneo uliyoyatembelea.

*Je, wajua* ?

Pragmatiki ni taaluma inayohusu maana katika matumizi, yaani maana ya tamko inayopatikana pale lugha inapotumika katika muktadha mahususi. Hutazama jinsi lugha inavyofungamana na muktadha wa matumizi yake. Hivyo, kanuni za kipragmatiki ni kaida za kimawasiliano ambazo huwaongoza wazungumzaji wa lugha kuelewa na kutafsiri mazungumzo yao kulingana na muktadha husika wa kimawasiliano. Kanuni hizi huchangia katika kuelewa maana au ujumbe unaowasilishwa na huongoza namna

FOR ONLINE READING ONLY

ya kutumia lugha. Hii ni kwa sababu kujua lugha peke yake hakutoshi bali hukamilishwa na ujuzi wa namna ya kuitumia katika mawasiliano katika muktadha husika. Kwa hiyo, muktadha ni jambo muhimu linalopaswa kuzingatiwa katika matumizi ya lugha.

Muktadha unajumuisha eneo au mazingira ambamo mawasiliano hufanyikia, uhusiano wa wahusika, utamaduni wa jumla wa wahusika au wa eneo husika (taratibu za eneo husika), mada, tukio, lengo, na mambo mengine ya nje ya lugha. Mambo haya husaidia katika matumizi yenye ufanisi wa kanuni za kipragmatiki. Katika sehemu hii, utajifunza mambo hayo kabla ya kuangazia kanuni za kipragmatiki.

**1. Uhusiano wa wahusika**

Uhusiano wa wazungumzaji huamua aina ya lugha ya kutumia, uteuzi wa maneno, na utamkaji. Kwa mfano, mtu mwenye cheo cha chini ataonesha tofauti ya jinsi atakavyotumia lugha anapoongea na mkuu wake wa kazi, tofauti na anapoongea na mtu mwenye cheo kama chake. Uhusiano wa wahusika unaweza kuwa wa rika, madaraka, familia, umri, shughuli au kazi, na kadhalika. Chunguza mazungumzo yafuatayo ya marafiki wawili:

**Mazungumzo 1**

**Kibude:** Oya! Mtu wangu, vipi mambo?

**Kwezu:** Poa mwanangu. Inakuwaje?

**Kibude:** Baridi mshikaji. Mambo leo siyo shwari wangu!

**Kwezu:** Vipi, maji shingoni siyo! Usikonde. Kuna mchongo nausikilizia; ukienda poa basi …

**Kibude:** Basi taim, taim … nistue. Nipo maskani.

**Kwezu:** Poa!

**Mazungumzo 2**

**Nduke:** Hujambo, Ndosi?

**Ndosi:** Sijambo mama, shikamoo!

**Nduke:** Marahaba! Umeshindaje?

**Ndosi:** Nimeshinda salama mama; wewe je?

**Nduke:** Mimi pia nimeshinda salama. Unaelekea wapi?

FOR ONLINE READING ONLY

**Ndosi:** Ninaelekea sokoni, mama.

**Nduke:** Sawa mwanangu, kila la kheri!

**Ndosi:** Asante, mama!

Mazungumzo ya kwanza yanaonesha jinsi vijana wa rika moja walivyo na uhuru wa kutumia maneno kulingana na rika lao. Unaposoma mazungumzo haya, unaona jinsi vijana hawa wa rika moja wanavyozungumza lugha ya Kiswahili ambapo mzungumzaji wa Kiswahili wa rika jingine si rahisi kuelewa kile kinachozungumzwa. Maana za maneno wanayoyatumia zinategemea mtazamo na uzoefu wao wa pamoja. Mazungumzo ya pili yanaonesha kuwa yamejaa heshima na staha. Tena, yamejaa matumizi ya Kiswahili sanifu. Hivyo, ni dhahiri kuwa uhusiano wa wahusika hutawala matumizi ya lugha na maana za maneno wanayotumia.

**2. Mada inayozungumziwa**

Mada huwafanya wanaozungumza wachague maneno yanayohusiana na jambo linalozungumziwa na kuhakikisha kuwa maneno hayo yanawasilisha dhana na ujumbe uliokusudiwa. Kwa mfano, wazungumzaji wanaozungumzia mambo ya ufundi wa magari watatumia maneno kama vile *injini, giaboksi, breki padi, rejeta,* na *klachi*. Wazungumzaji wanaozungumzia mambo ya utabibu wa hospitalini watatumia maneno kama vile *vipimo vya malaria, vidonge* na *sindano*. Iwapo tiba hiyo inahusiana na uganga wa kijadi, wazungumzaji watatumia maneno kama vile *tunguli, ramli, mavumba, ubani, kifungua mkoba,* na kadhalika.

**3. Mazingira au eneo**

Hapa ni mahali ambapo tukio au jambo hutendeka. Mazingira au eneo ni suala la kuzingatia katika matumizi ya lugha kwa sababu humsaidia mtumiaji wa lugha kutumia lugha inayotakiwa katika mazingira ya tukio linalohusika. Lugha inayotumika katika maeneo mbalimbali hujibainisha kwa shughuli za mazingira ambamo lugha hiyo inatumika. Mazingira yanaweza kuwa ya mgodini, mahakamani, taasisi za kisiasa, sokoni, bandarini, hotelini, ofisini, na kadhalika. Katika matumizi ya lugha, mazingira kama hayo ndiyo yanayowafanya wazungumzaji waibue maneno maalumu yanayotumika katika mazungumzo yao. Hivyo, maana ya lugha inayotumika itategemea eneo walilopo wazungumzaji. Chunguza mazungumzo yafuatayo kama mfano mmojawapo:

**Hakimu:** Ninakuuliza, jaribio la kuvunja nyumba kwa kutumia silaha na kukusudia kuiba lilitendeka?

FOR ONLINE READING ONLY

**Mbiche:** Hapana, mheshimiwa! Mimi sikuwa na kusudio hilo mheshimiwa kwani nilipopita na kuusogelea mlango sikuwa ninajitambua mheshimiwa kwa sababu nilikuwa nimelewa.

**Hakimu:** Ulikuwa na silaha gani ulipousogelea mlango?

**Mbiche:** Sikuwa na silaha yoyote, bali kulikuwa na shoka nje ya nyumba ambalo lilisahaulika wakati wenye nyumba walipokwenda kulala.

**Hakimu:** Umewezaje kukumbuka shoka ulililoliona usiku ilhali wewe ulikuwa umelewa kiasi cha kutojitambua?

**Mbiche:** Kwa neema tu, mheshimiwa.

**Hakimu:** Shauri lako linaahirishwa hadi tarehe 03.04.2016 litakaposikilizwa tena. Dhamana yako imekataliwa na utarudi tena rumande.

Haya ni mazungumzo ya mahakamani kwa sababu kuna msamiati wa kisheria kama vile *hakimu, shauri, dhamana,* na *rumande,* pamoja na matumizi ya lugha rasmi. Mara nyingi, mahojiano katika mahakama hayaendi harakaharaka. Kwa mfano, kila mtu anayehusika, hususani hakimu, mwendesha mashtaka, wakili, mshtakiwa, na mashahidi hujieleza kwa uwazi bila kujali urefu wa maelezo yake. Hivyo, maana za maneno yanayotumika hutegemea mazingira hayo ya mahakamani.

Kwa upande mwingine, lugha ya mahakamani ni tofauti na lugha ya hotelini, mahali ambapo watu hupata huduma ya chakula. Lugha ya hotelini ina mtindo wake ambao, katika hali ya kawaida, huenda isieleweke kwa mtu asiyehusika katika mazungumzo hayo. Chunguza mazungumzo yafuatayo:

**Mhudumu:** Nani mbuzi?

**Mteja:** Mimi!

**Mhudumu:** Kuku?

**Mteja:** Hapa!

**Mhudumu:** Biriani?

**Mteja:** Mimi!

FOR ONLINE READING ONLY

Mzungumzaji anapouliza, "**Nani mbuzi?**", haimaanishi kuwa anamuulizia mtu anayeitwa **Mbuzi,** bali anaulizia mteja aliyeagiza nyama ya mbuzi. Pia, anaposema **kuku,** anamaanisha mteja aliyeagiza nyama ya kuku. Aidha, anaposema **biriani,** hakuna mteja anayeitwa **biriani,** bali mteja aliitikia akiwa na maana angehitaji kula **biriani**.

**4. Lengo la mazungumzo**

Lengo la mazungumzo humwezesha mtumiaji wa lugha kuteua mtindo wa lugha ya kutumia. Mtu mwenye lengo la kuomba fedha atatumia lugha ya unyenyekevu na upole. Mtu huyohuyo, akiwa na lengo la kuelimisha kuhusu athari za matumizi ya simu, atatumia lugha ya kuonya, kusisitiza, na kushauri. Aidha, maana za tungo zilizoteuliwa zitategemea lengo la wazungumzaji hao.

**5. Utamaduni**

Utamaduni hurejelea jumla ya utaratibu wa mwenendo wa maisha uliokubaliwa na jamii husika. Huhusisha mila, asili, desturi, na jadi ya jamii husika. Utamaduni hutawala jinsi lugha inavyotumika. Kwa hiyo, maana za maneno na dhana pamoja na uteuzi wake hutawaliwa na utamaduni wa jamii husika. Mathalani, katika utamaduni wa jamii nyingi za Kiafrika, mtu mdogo huanza kumsalimia mkubwa.

Mambo yaliyoelezwa hapo juu yanasaidia kuzitumia kwa ufanisi kanuni za kipragmatiki. Kuna kanuni kuu mbili za kipragmatiki ambazo zina vikanuni vidogo ndani yake. Kanuni hizo ni kanuni ya ushirikiano na kanuni ya staha.

(a) Kanuni ya ushirikiano

Kanuni hii inamweleza msemaji kusema yale tu yanayohitajika. Si zaidi wala pungufu ya yale yanayohitajika. Kanuni hii huzingatia vikanuni vinne ambavyo ni kiasi, ukweli, uhusiano na njia.

Kiasi: (i) Toa taarifa inayohitajika kwa kuzingatia lengo la mawasiliano.

(ii) Usitoe taarifa zaidi ya ile inayohitajika.

Ukweli: (i) Usiseme lolote unaloamini kuwa si kweli.

(ii) Usiseme lolote usiloweza kulithibitisha.

Uhusiano: Sema yanayohusiana na mada.

Njia: (i) Epuka tungo zisizoeleweka.

(ii) Epuka utata.

(iii) Sema kwa ufupi.

(iv) Sema kwa mpangilio na mtiririko mzuri.

FOR ONLINE READING ONLY

(b) Kanuni ya staha

Kanuni hii inamwelekeza msemaji kupunguza kusema mawazo yasiyo na staha ili kudumisha amani na utulivu. Hili linafanikishwa kwa kupunguza kabisa matumizi ya lugha ya kutweza. Matumizi ya lugha ya kutweza yanaweza kuepukwa kwa kufanya yafuatayo:

(i) Kutowachukulia wasikilizaji wetu kama watu wa kututumikia

(ii) Kutotweza wala kudharau mawazo ya wasikilizaji wetu

(iii) Kutosema mambo mabaya kwa wasikilizaji wetu au watu wanaowahusu

(iv) Kutojikweza

Kanuni ya staha ina vikanuni saba, ambayo ni busara, ukarimu, kusifu, masikilizano, unyenyekevu, huruma, na kuchukuliana.

(a) Busara:

(i) Punguza kabisa uwezekano wa kumuumiza msikilizaji.

(ii) Ongeza manufaa kwa wasikilizaji kadiri inavyowezekana.

(b) Ukarimu:

(i) Punguza kabisa kujinufaisha kwa ubinafsi.

(ii) Ongeza uwezekano wa kujiumiza wewe mwenyewe badala ya msikilizaji.

(c) Kusifu:

(i) Punguza kabisa kutomsifu msikilizaji.

(ii) Ongeza kumsifu msikilizaji kadiri inavyowezekana

(d) Masikilizano:

(i) Punguza kabisa sintofahamu kati yako na msikilizaji

(ii) Ongeza masikilizano na msikilizaji kadiri inavyowezekana

(e) Unyenyekevu:

(i) Punguza kabisa kujisifu.

(f) Huruma:

(i) Ongeza huruma kwa msikilizaji kadiri inavyowezekana.

(ii) Punguza kabisa uhasama kwa msikilizaji.

FOR ONLINE READING ONLY

(g) Kuchukuliana:

(i) Punguza kabisa kero au maudhui kwa msikilizaji.

(ii) Ongeza faraja kwa msikilizaji kadiri inavyowezekana.

### Zoezi la 2.2

1. Muktadha ni nyenzo muhimu sana katika matumizi ya lugha. Thibitisha hoja hii kwa mifano maridhawa.
2. Bainisha masuala mengine yaliyo nje ya lugha ambayo yanasaidia kupata maana ya matamko katika mawasiliano tofauti na yaliyojadiliwa darasani.
3. Fafanua jinsi ukiukwaji wa kanuni za kipragmatiki unavyoweza kuathiri mawasiliano.

## Dhana ya utata

### Shughuli ya 2.7

**Soma mazungumzo kati ya Chaasu na Chausiku, kisha jibu maswali yanayofuata.**

**Chaasu**: Rafiki yangu, habari za leo?

**Chausiku**: Ni nzuri tu rafiki yangu.

**Chaasu:** Rafiki, leo nina furaha sana. Nimefanikiwa kununua mbuzi na kanga. Nimebakiza kima tu ili nikamilishe mahitaji yangu yote.

**Chausiku**: Mbona sikuelewi, rafiki yangu?

**Chaasu**: Huelewi nini? Hujui kanga? Au mbuzi? Au kima?

**Chausiku:** Yaani, bado unazidi kunichanganya, rafiki yangu. Unaibua utata katika mazungumzo yako mpaka ninashindwa kukuelewa.

**Chaasu**: Sawa! Ngoja basi niachane na hayo usiyoyaelewa; nilete habari za Baba Jimbi kumpigia Jimbi mpira ukamtegua mguu.

**Chausiku**: Kwa hakika, nimetambua kuwa hujui matumizi ya lugha yasiyo na utata. Hapo sasa una maana gani tena? Unamaanisha nini unaposema kumpigia mpira? Tena ni nani ambaye mpira umemtegua mguu?

**Chaasu:** Tatizo lako, huniachi niendelee kutoa ufafanuzi wa mazungumzo yangu. Basi, kama huelewi tena habari hii, ngoja nilete nyingine; au unasemaje?

**Chausiku:** Ah! Habari zako zinachosha kusikiliza kwa sababu hazieleweki. Tumia

FOR ONLINE READING ONLY

maneno kwa namna inayoondoa utata. Pia, sentensi zako ziwe zimenyooka na kueleza waziwazi unachokusudia ili mawasiliano yetu yafanikiwe.

**Chaasu:** Samahani rafiki yangu kwa kupata utata kuelewa mazungumzo yangu! Nitajitahidi kueleweka siku nyingine.

**Chausiku:** Nimekusamehe, ingawa bado sijaelewa mpaka sasa ulimaanisha nini.

**Chaasu:** Mh! Hata mimi sijui sasa nikusaidiaje. Ngoja tutafute namna ya kuondoa huo utata.

**Chausiku:** Usijali, mimi ninajua cha kufanya. Kwa kutumia kamusi na vyanzo vingine, tutaeleza maana mbalimbali za tungo ulizotumia halafu wewe utasema ulikuwa na maana ipi kati ya hizo.

**Maswali:**

1. Unafikiri kwa nini Chausiku alipata utata kutokana na maneno mbuzi, kanga na kima?
2. Elezea utata unaojitokeza katika tungo ya Chaasu "… Baba Jimbi kampigia Jimbi mpira ukamtegua mguu".
3. Utata unaojitokeza katika mazungumzo hayo ni wa aina gani? Toa sababu za majibu yako.

**Je, wajua ?**

Utata ni hali ya tungo kuwa na maana zaidi ya moja. Kiswahili, kama zilivyo lugha zingine, kina sentensi na maneno yenye maana zaidi ya moja. Kuna aina kuu mbili za utata unaojitokeza katika matumizi ya lugha ambazo ni utata wa kileksika na utata wa kimuundo.

(a) *Utata wa kileksika*

Huu ni utata unaojitokeza katika tungo wakati neno linapokuwa na maana zaidi ya moja. Aghalabu, maana hizi hujitokeza katika maneno yenye maumbo sawa lakini maana zake ni tofauti. Maneno haya, katika kamusi, yamendikwa kwa kuwekewa namba kipeo. Tazama mfano wa maneno hayo.

(i) Anapaa

**Maana ya kwanza:** Anaruka kuelekea angani.

**Maana ya pili:** Anatoa magamba katika samaki.

FOR ONLINE READING ONLY

(ii) Ua

**Maana ya kwanza:** Sehemu ya mmea iliyochanua

**Maana ya pili:** Mzunguko au boma lililofanywa kwa miti, mabati, na kadhalika

**Maana ya tatu:** Toa uhai wa kiumbe.

(b) *Utata wa kimuundo*

Huu ni utata unaojitokeza kutokana na muundo wa tungo. Unaweza kusababishwa na mpangilio wa maneno katika tungo au matumizi ya viambishi fulani katika neno. Utata wa aina hii unaweza pia kusababishwa na namna ya utamkaji. Aina hizi zote zinajumuishwa katika aina ya utata wa kimuundo. Mifano inaweza kudhihirika katika tungo zifuatazo:

(i) Ameshauriwa na baba yake.

**Maana ya kwanza:** *Baba amemshauri mtoto wake.*

**Maana ya pili:** *Baba na mtoto wake wameshauriwa na mtu fulani.*

(ii) Nitambebea kitenge.

**Maana ya kwanza**: *Nitambeba kwa kutumia kitenge.*

**Maana ya pili:** *Nitabeba kitenge kwa ajili yake.*

(iii) Baba Farida amekuja.

**Maana ya kwanza:** Baba Farida amekuja (Baba wa Farida amekuja)

**Maana ya pili:** Baba, Farida amekuja (Mtu anamtaarifu baba kuwa Farida amekuja)

Utata katika tungo ya kwanza unasababishwa na mpangilio wa maneno *na baba yake* ambapo yanaweza kumaanisha 'pamoja na baba yake' au 'aliyetenda ni baba yake'. Katika tungo ya pili, utata unasababishwa na kiambishi cha utendea -e- ambacho kinaweza kufanya kazi ya kueleza kutendea au matumizi ya kitu. Tungo ya tatu inapata utata kutokana na namna ya utamkaji, ambapo msemaji akiweka mkato (akishusha kiimbo) mara tu baada ya kutamka neno *baba*, maana itakuwa tofauti na ile atakayotamka bila kuweka mkato.

## Sababu za utata

Utata katika lugha husababishwa na mambo anuwai. Miongoni mwa mambo hayo yanafafanuliwa kama ifuatavyo:

FOR ONLINE READING ONLY

(a) *Neno kuwa na maana zaidi ya moja*

Katika lugha, kuna maneno yenye maana moja na yenye maana nyingi lakini zenye uhusiano mkubwa. Hali hiyo haisababishi utata. Utata wa neno moja kuwa na maana nyingi unaletwa na neno kuwa na maana mbili au zaidi zilizo tofauti kabisa, yaani zisizo na uhusiano kabisa.

(b) *Kutozingatia alama za uakifishaji katika uandishi*

Alama za uakifishaji zinatumika katika maandishi ili kumwezesha mwandishi kufikisha ujumbe uliokusudiwa. Hivyo, wakati wa kuandika, mwandishi akiweka alama ya uakifishaji pasipotakiwa au asipoweka ilhali inahitajika, anaweza kusababisha utata katika ujumbe uliotolewa.

(c) *Matumizi ya viambishi vya utendea katika tungo*

Viambishi vya utendea vina dhima mbalimbali katika matumizi ya lugha. Vinaweza kuonesha kutenda kwa niaba, kuonesha matumizi ya kitu, sababu za kutenda jambo fulani, au uelekeo. Hivyo, vinapotumika katika neno, huweza kusababisha utata

## Kuondoa utata katika lugha

Kufanikisha mawasiliano ndilo lengo kuu la matumizi ya lugha. Ili mawasiliano yaweze kufanikiwa, ni lazima lugha inayotumika ieleweke kwa urahisi miongoni mwa wazungumzaji husika. Hivyo, lugha inayotumika inapaswa isiwe na utata. Kuna njia mbalimbali za kuondoa au kuzongoa utata katika matumizi ya lugha. Njia hizo zinafafanuliwa katika vipengele vinavyofuata.

(a) *Kufafanua maneno au tungo zenye maana zaidi ya moja*

Hii ni njia ambayo hutumika zaidi katika mazungumzo kwani mzungumzaji huwa anaonana ana kwa ana na msikilizaji wake. Hivyo, msikilizaji ana nafasi ya kuomba ufafanuzi na mzungumzaji ana nafasi ya kufafanua. Katika maandishi, pia mwandishi anaweza kufafanua maana yake wakati anaandika pale anapohisi kuwa utungo aliotumia hautaeleweka kirahisi.

(b) *Kutumia alama za uakifishaji au kiimbo kwa usahihi*

Hii ni mbinu inayomsaidia mwandishi kuwa makini katika utumiaji wa alama za uakifishaji na kuziweka mahali panapotakiwa kulingana na ujumbe uliokusudiwa. Ikiwa ni katika matamshi, basi msemaji ahakikishe anatumia kiimbo sahihi, aweke mkazo mahali panapotakiwa kuzingatia na maana aliyoikusudia na azingatie wakaa.

(c) *Kutumia maneno kwa kuzingatia muktadha na hadhira*

Muktadha ni muhimu sana katika kupata maana ya utungo. Hii inaweza kuwa aina ya mada, uga au eneo la kijamii. Matahalani, wazungumzaji wanapoongea kuhusu vyombo

FOR ONLINE READING ONLY

na vifaa vya jikoni, halafu wakatamka 'mbuzi', basi lazima neno mbuzi litakuwa na maana ya kifaa cha kukunia nazi. Ikiwa wanazungumzia masuala ya wanyama na ufugaji, basi neno *mbuzi* litakuwa na maana ya mnyama. Hivyo, kuzingatia muktadha wa matumizi ya lugha ni muhimu sana katika kupata maana ya tungo.

(d) *Kuzingatia upatanisho wa kisarufi*

Uzingatiaji wa viambishi vya upatanisho husaidia katika kuondoa utata wa kileksika, hasa ikiwa maana zinarejelea ngeli tofauti. Kwa mfano, msemaji akisema, "*Nimenunua mbuzi mmoja,*" itaeleweka kuwa amenunua mbuzi mnyama na akisema, "*Nimenunua mbuzi moja,*" itabainika kabisa kuwa amenunua kifaa. Hivyo, matumizi sahihi ya upatanisho wa kisarufi huondoa utata katika matumizi ya lugha.

## Zoezi la 2.3

1. Ondoa utata katika tungo zifuatazo:
   (ii) Baba babu amekuja kutoka kazini.
   (iii) Anakula wali na kijiko
   (iv) Kitumbua kimeingia mchanga.
   (v) Chai imeingia nzi.
   (vi) Dada anamchezea mama.

2. Bainisha sababu za utata. Kwa kila sababu, toa mifano ya utata na uuondoe huku ukitaja njia uliyoitumia kuundoa.
3. Soma matini ifuatayo, kisha bainisha kwa mifano aina za utata zinazojitokeza katika matini hiyo, kisha uuondoe.

Siku moja, nilisoma sehemu ya makala gazetini. Makala hiyo ilikuwa imeandikwa sentensi iliyosomeka, "Mimi nina paka na taa". Sikuelewa hata kidogo alichomaanisha mwandishi. Nilipoendelea kusoma matini hiyo, nikakutana na tungo nyingine ambayo ilisema, "Mwanafunzi amwandikia mwalimu wake barua ya kuomba ruhusa". Nilishindwa kuelewa maana ya tungo hiyo pia. Basi, niliendelea kusoma kwa makini angalau niweze kuambulia chochote. Hata hivyo, mambo yalikuwa tofauti kwani nilikutana na tungo nyingine iliyosomeka, "Wanafunzi wanashindwa kwenda shule kwa kuwa walilalia uji". Niliamua kuacha kuendelea kusoma gazeti hilo kwani sikuelewa alichomaanisha mwandishi.

FOR ONLINE READING ONLY

*Tamrini ya 2*

1. Mzungumzaji asiye makini katika uteuzi wa maneno na miundo huibua utata. Eleza athari zinazoweza kuibuka kutokana na mzungumzaji asiyekuwa makini katika uteuzi wa maneno na miundo sahihi.
2. "Utata katika lugha unaweza kukwamisha mawasiliano." Pendekeza njia unazoweza kutumia kuepuka utata.
3. Eleza jinsi unavyoweza kuzingatia vikanuni saba (7) vya kanuni ya staha katika mazungumzo.
4. Onesha namna utata wa kimuundo unavyojitokeza katika lugha ya Kiswahili.

FOR ONLINE READING ONLY

# Sura ya Tatu

# Asili na chimbuko la Kiswahili

**Utangulizi**

*Lugha yoyote ina asili na chimbuko. Katika sura hii, utajifunza nadharia za asili na chimbuko la lugha ya Kiswahili. Aidha, utajifunza hoja za kiisimu na kihistoria zinazothibitisha kuwa Kiswahili kina sifa ya Ubantu. Umahiri utakaoujenga utakusaidia kutambua asili na chimbuko la Kiswahili. Vilevile, utakusaidia kuthamini na kujivunia lugha ya Kiswahili.*

**Fikiri**

Watu walivyoanza kuwasiliana

## Nadharia za asili na chimbuko la lugha ya Kiswahili

**Shughuli ya 3.1**

Tumia vyanzo mbalimbali, vikiwamo vya ki-TEHAMA, kufafanua nadharia mbalimbali za asili ya Kiswahili, kisha toa msimamo wako kuhusu asili ya Kiswahili.

### Asili ya Kiswahili

Neno *asili* lina maana ya mwanzo wa kitu. Kwa hiyo, tunaposema asili ya Kiswahili, tunamaanisha namna lugha hii ilivyoanza. Kuna nadharia kuu nne za asili ya Kiswahili ambazo ni: Kiswahili ni Kiarabu, Kiswahili ni lugha chotara, Kiswahili ni pijini au krioli, na Kiswahili ni Kibantu. Nadharia hizo zinafafanuliwa kwa kina katika vipengele vinavyofuata.

(a) *Kiswahili ni Kiarabu*

Nadharia hii inaeleza kuwa asili ya lugha ya Kiswahili ni Kiarabu. Wafuasi wa nadharia

FOR ONLINE READING ONLY

hii wanadai kuwa Kiswahili kilianza kuwapo mara baada ya Waarabu kufika Pwani ya Afrika Mashariki. Hoja zao ni mbili: kuwapo kwa maneno mengi yenye asili ya Kiarabu katika Kiswahili na Kiswahili kuhusishwa na dini ya Kiislamu.

Kwanza, inadaiwa kuwa lugha ya Kiswahili ina maneno mengi yenye asili ya Kiarabu, hususani yale yanayotumika katika biashara na uchumi. Baadhi ya maneno hayo ni *fedha, biashara, ushuru* na *bei*. Aidha, inadaiwa kuwa msamiati unaohusu sehemu kama vile *theluthi, thumni* na *sudusi* unatokana na lugha ya Kiarabu. Vilevile, inadaiwa kuwa, kwa kiasi kikubwa, maneno yanayorejelea namba kama vile *ishirini, thelathini, arobaini* na *hamsini* yana asili ya lugha ya Kiarabu.

Wafuasi wa nadharia hii wanaendelea kudai kuwa neno lenyewe "Kiswahili" linatokana na neno la Kiarabu *sahil,* likiwa katika umoja na *sawahil* likiwa katika wingi. Maneno haya yana maana ya *upwa* au *nyupwa* mtawalia, huku neno *Waswahili* likiwa na maana ya *Wanaupwa* au *Wapwani*. Kwa hiyo, wanaona kuwa huo ni uthibitisho kwamba asili ya Kiswahili ni Kiarabu.

Hata hivyo, hoja hii imekosolewa na wanaisimu wanaodai kuwa hoja ya wingi wa maneno ya Kiarabu katika Kiswahili haina mashiko kwa sababu kila lugha ina maneno ya mkopo. Mathalani, Massamba (2017) anadai kuwa, hata baadhi ya maneno hayo yanayoelezwa kuwa ni ya Kiarabu, kiasili, si ya Kiarabu bali yanatokea katika lugha zingine. Hii inaonesha kuwa lugha ya Kiswahili imekopa maneno kutoka lugha zingine mbalimbali. Kuna idadi kubwa ya maneno yenye asili ya lugha zingine kama vile Kiingereza, Kijerumani, Kihindi, Kireno, Kiajemi, Kifaransa, na nyinginezo. Kwa kawaida, lugha yoyote ina tabia ya kuathiriana na lugha zingine. Lugha ya Kiswahili imeathiriana na lugha zingine kwa sababu ya mwingiliano wa watumiaji wa lugha hizo katika shughuli za kiuchumi, kiutamaduni, na kisiasa.

Sambamba na hayo, inadaiwa kuwa lugha hukopa maneno ambayo hayahusu msamiati wa msingi wa lugha hiyo. Msamiati wa msingi ni ule unaohusu mambo ambayo hayabadilikibadiliki kutokana na mabadiliko ya kiutamaduni. Mfano wa maneno yanayohusu msamiati wa msingi ni pamoja na msamiati unaohusu maumbo ya kijiografia, viungo vya mwili, na kadhalika. Kwa mfano, ni vigumu kukuta msamiati unaohusu viungo vya mwili wa binadamu kama vile *jicho, mkono, mguu, pua, mdomo, sikio, kidole, paja,* na kadhalika ukiwa umekopwa kutoka lugha zingine. Hali kadhalika, ni vyema ikaeleweka kuwa lugha haiwezi kufafanuliwa kwa kipengele kimoja tu cha msamiati. Lugha inapaswa kufafanuliwa kwa kutumia pia vigezo vya matamshi, maumbo, na miundo ya tungo. Vipengele vyote hivi vinaonesha kuwa Kiswahili kina mnasaba wa wazi kabisa na lugha zingine za Kibantu.

FOR ONLINE READING ONLY

Aidha, madai kwamba maneno mengi ya Kiswahili yametoka katika lugha ya Kiarabu yanapingwa kwa hoja kwamba hayana ushahidi yakinifu wa kitakwimu. Kuna baadhi ya watafiti waliojaribu kutoa takwimu ambazo bado zina dosari za wazi. Mathalani, Krumm (1940) anakadiria kuwa kuna asilimia 20 ya maneno ya mkopo katika Kiswahili cha mazungumzo, asilimia 30 katika Kiswahili cha maandishi na takribani asilimia 50 ya Kiswahili cha ushairi wa kale. Katika takwimu hizo, Massamba (2017) anaibua dosari mbili. Kwanza, Krumm haoneshi kama maneno yote ya mkopo yaliyomo katika Kiswahili yametoka katika lugha ya Kiarabu. Kwa hiyo, kuna uwezekano mkubwa kuwa baadhi ya maneno yalitoka katika lugha zingine tofauti na Kiarabu. Pili, makadirio ya asilimia hizo hayakutolewa kwa kutafiti lahaja zote za Kiswahili. Krumm alitafiti kupitia usomaji wa vitabu vya sarufi, kamusi na magazeti ya *Mambo Leo* yaliyochapishwa mwaka 1931 tu. Kwa hiyo, kisayansi, sampuli hii haitoshi kujumuisha lugha ya Kiswahili kwa upana wake na lahaja zake zote.

Mfano mwingine unaotolewa na Massamba, unaohusu takwimu za msamiati wa Kiswahili, ni ule uliotolewa na Sassoon, (1980). Yeye anadai kuwa asilimia 80 ya msamiati wa Kiswahili unashabihiana na msamiati wa lugha za Kibantu na asilimia 20 ni msamiati wa Kiarabu. Takwimu za Sassoon zinaonesha kwamba msamiati wa Kiarabu katika Kiswahili si mwingi kama inavyodhaniwa. Hata hizo asilimia 20 zinazotajwa si za msamiati wa Kiarabu pekee bali kuna maneno yenye asili ya Kijerumani kama vile *shule* na *hela*, lugha ya Kiingereza kama vile *shati, sketi* na *soksi,* na lugha ya Kireno kama vile *meza, gereza, kanisa,* na kadhalika. Kwa hiyo, tunaweza kusema kuwa takwimu zilizotolewa na Sassoon pia zinatia wasiwasi.

Hoja nyingine inayotumiwa na wafuasi wa nadharia ya Kiswahili ni Kiarabu ni ile inayoegemea katika dini ya Kiislamu. Inadaiwa kuwa Kiswahili kililetwa na Waarabu sambamba na dini ya Kiislamu. Ndiyo maana wakazi wengi wa Pwani ya Afrika Mashariki ni Waislamu. Wafuasi wa nadharia hii wanasisitiza kuwa hata dini ya Kiislamu ilisambazwa na kuenezwa kwa kutumia lugha ya Kiswahili. Hivyo, Kiswahili kinatokana na Kiarabu.

Hoja hii inakosolewa na wanazuoni mbalimbali kwa hoja kwamba dhana za 'lugha' na 'dini' hazipaswi kuchanganywa kwa sababu Kiswahili ni tofauti na Uislamu. Wanaeleza kuwa Uislamu ni utamaduni unaofuatwa na waumini wake ambao haufungamani na lugha yoyote. Kuna Waislamu wengi duniani ambao hawawezi kuzungumza Kiswahili na baadhi ya Waswahili si Waislamu. Lugha si dini, na utamaduni wa Kiswahili unatofautiana na wa Kiarabu.

FOR ONLINE READING ONLY

(b) *Kiswahili ni lugha chotara*

Nadharia hii inadai kuwa lugha ya Kiswahili imetokana na mwingiliano kati ya lugha ya Kiarabu na lugha za Kiafrika. Madai haya yaliibuka na kupata umaarufu mkubwa kwa wanaakiolojia wa miaka ya 1950 hadi 1960. Mtazamo huo unadai kuwa Waarabu walipofika katika Upwa wa Afrika Mashariki, waliwaoa wanawake wa Kiafrika na kuzaa nao watoto. Watoto hao walikuwa chotara wa Kiarabu na Kiafrika. Lugha ya Kiarabu (upande wa baba) iliingiliana na lugha za Kiafrika (upande wa mama), na mwingiliano huo ndio ulizaa lugha ya Kiswahili. Watoto waliozaliwa hawakuzungumza lugha ya Kiarabu wala lugha ya Kiafrika, bali waliongea mchanganyiko wa lugha hizo ambao ndio lugha chotara. Lugha hiyo ikawa ni lugha yao ya kwanza. Kwa hiyo, lugha ya Kiswahili ni chotara ya lugha ya Kiarabu na lugha za Kiafrika.

Nadharia hii imekosolewa kwa kukosa ushahidi thabiti. Kwanza, madai kuwa Kiswahili ni mchanganyiko wa Kiarabu na lugha zingine za Kiafrika yana kasoro kubwa. Kwa mfano, haikuelezwa wazi ni lugha zipi za Kiafrika zilichanganyika na Kiarabu na kuzaa Kiswahili. Pia, haikuelezwa kuhusu wenyeji walioolewa na Waarabu kuwa walikuwa ni Wabantu, Wanailoti, Wakushiti, na kadhalika. Aidha, kuwapo kwa lahaja mbalimbali za Kiswahili katika Upwa wa Afrika ya Mashariki kunatoa nafasi ya kupinga madai haya. Haiwezekani kila mahali Waarabu wanapochanganyikana na Waafrika ipatikane lahaja ya Kiswahili. Ingelikuwa hivyo, kungelikuwa na lahaja nyingi za Kiswahili katika sehemu mbalimbali za Afrika Magharibi ambapo kulikuwa na mwingiliano mkubwa kati ya Waarabu na Waafrika katika himaya za Ghana, Mali, Taghaza, Songhai, na kadhalika. Kwa hiyo, Chiraghdin, Mnyampala (1977), na Massamba (2017) wanadai kuwa nadharia hii ina kasoro kubwa katika kueleza asili ya Kiswahili.

(c) *Kiswahili ni pijini au krioli*

Nadharia hii inadai kuwa lugha ya Kiswahili ilianza kama pijini ambayo baadaye ilikuwa krioli. Inaelezwa kuwa Kiswahili ni lugha iliyopatikana baada ya Waarabu kutagusana na Waafrika. Kwa kuwa walikuwa hawaelewani, basi kila mtu alizungumza lugha yake. Hali hii ilisababisha kuzaliwa kwa lugha ya mseto wa lugha hizi mbili ambayo si lugha ya Kiafrika wala Kiarabu. Lugha hii iliitwa pijini.

Mazrui na Shariff (1994) wanadai kuwa Kiswahili kilianza kama pijini ambayo ilikuwa mchanganyiko wa lugha ya Kiarabu kwa kiasi kikubwa na lugha zingine za Kiafrika. Baadaye, pijini hiyo ilikomaa na kuwa krioli. Kwa hiyo, lugha ya Kiswahili ikaonekana kuwa krioli ya Waarabu waliokuwa Afrika. Wanaendelea kudai kuwa, baadaye, krioli hiyo ilianza kubadilika na kufanana na lugha zilizokuwa jirani yake ambazo zimetajwa kuwa ni Kipokomo na Kimijikenda.

FOR ONLINE READING ONLY

Madai haya, yakichunguzwa kitunduizi, hayaelekei kuwa na uthibitisho wowote kwani wataalamu hawa hawakuonesha muundo wa pijini hiyo ulivyokuwa kabla ya kubadilika na kuwa krioli. Aidha, hawakuonesha mfumo wa krioli hiyo kifonolojia, kimofolojia wala kisintaksia. Sambamba na hayo, wafuasi wa mtazamo huo hawaoneshi huo msamiati mwingi wanaodai kuwa wa Kiarabu. Vilevile, hawaelezi msamiati huo umechukua asilimia ngapi ya msamiati wote wala hawafafanui hiyo sehemu ndogo ya msamiati ambao ulikuwa wa lugha ya Kiafrika ulichukua asilimia ngapi.

Upungufu mwingine unajitokeza wanapodai kuwa krioli ilibadilika na kufanana na lugha za Kibantu zilizokuwa jirani yake. Kwa hali ya kawaida, lugha huweza kubadilika na kuchukua sifa za lugha zingine pale inapotokea lugha hiyo nyingine inazungumzwa na watu wa tabaka tawala, tabaka la juu kiuchumi (matajiri), watu mashuhuri, wasomi, au watu wenye maendeleo makubwa. Katika kipindi hicho, Waarabu ndio waliokuwa watu wenye sifa hizo za tabaka la juu. Kwa minajili hiyo, ingetarajiwa kuwa krioli hiyo ingebadilika na kufanana na Kiarabu kabisa kuliko kufanana na lugha za wenyeji. Hivyo, nadharia hii pia haina ushahidi wenye mashiko wa kufanikisha kuweka bayana asili ya lugha ya Kiswahili.

## Zoezi la 3.1

1. Maneno hukopwa kutoka lugha moja kwenda lugha nyingine. Eleza kwa nini msamiati wa msingi huweza kuhimili mabadiliko.
2. Chukulia kuwa wewe ni Ofisa Utamaduni katika Wizara ya Utamaduni na Michezo. Umepewa jukumu la kuishauri serikali kutoa msimamo juu ya madai kwamba Kiswahili ni Kiarabu. Fafanua hoja utakazoishauri serikali izitoe katika msimamo wake.
3. Kwa kutumia mifano kutoka vyanzo mbalimbali vya maktabani na/au mtandaoni, bainisha maneno ya Kiswahili yanayodhaniwa kuwa ni ya Kiarabu ilhali kietimolojia ni ya lugha zingine.

(d) *Kiswahili ni Kibantu*

Nadharia hii inadai kuwa Kiswahili ni lugha mojawapo ya Kibantu. Tofauti na nadharia zingine, nadharia hii inaonekana kuwa na mashiko kwa wanaisimu wengi na wachambuzi mbalimbali wa lugha. Nadharia hii inasisitiza kuwa Kiswahili ni lugha yenye asili ya Kibantu, na inaweza kuthibitishwa kwa ushahidi wa kihistoria na kiisimu.

FOR ONLINE READING ONLY

### *Shughuli ya 3.2*

Tumia vyanzo mbalimbali vya maktabani na vya ki-TEHAMA kutafuta hoja za kihistoria zinazothibitisha Ubantu wa lugha ya Kiswahili. Fafanua ushahidi huo kwa kutumia maneno yako.

### *Je, wajua* ?

Ushahidi wa kihistoria unatokana na matokeo ya uchunguzi wa mfumo mzima wa maisha katika maeneo ya Pwani ya Afrika Mashariki kabla na baada ya ujio wa wageni. Ushahidi huu unadhihirisha kuwa, kabla ya kuja kwa wageni, eneo la Pwani ya Afrika Mashariki lilikuwa likikaliwa na wenyeji. Bila shaka, wenyeji hao walikuwa na lugha yao. Kuna ushahidi unaodhihirisha kwamba wenyeji wa Pwani ya Afrika Mashariki walikuwa na lugha zao ambazo baadaye ndizo zilikuja kujulikana kama lahaja za Kiswahili. Kwa maneno mengine, ushahidi huu unathibitisha kuwa Kiswahili kilikuwapo hata kabla ya ujio wa wageni. Hoja zinazotolewa katika vipengele vinavyofuata zinathibitisha madai hayo.

(a) **Kitabu cha Periplus of the Erythrean Sea (Mwongozo wa Safari kupitia Bahari ya Shamu)**

Inaelezwa kwamba kitabu cha **Periplus of the Erythrean Sea** kiliandikwa na nahodha wa meli ya Alexandria ambaye hakutajwa kwa jina. Kitabu hiki kinatoa maelezo ambayo ni mwongozo kuhusu Bahari ya Hindi. Katika kitabu hicho, kuna majadiliano na maelezo mengi yanayohusu historia ya eneo la Pwani ya Afrika Mashariki. Massamba (2002) anaeleza kuwa maneno **periplus** na **erythrean** ni ya Kiyunani ambayo tunaelezwa kuwa asili yake hasa ni Kilatini. Neno **periplus** humaanisha **safari ya kuzunguka** na neno **erythrean** linamaanisha **ekundu**. Hivyo, **Erythrean Sea** maana yake **bahari nyekundu** (**Bahari ya Shamu**). Haijulikani hasa kitabu hicho kiliandikwa mwaka gani ila inadhaniwa kuwa kiliandikwa huko Alexandria karne ya kwanza ya Majilio ya Masihi. Kitabu hicho kinataja na kusimulia habari za bandari mbalimbali za **Azania** (Afrika Mashariki) na habari za vyombo kama vile **ngalawa**, **madema,** na **mitepe**. Kuwapo kwa maneno kama hayo, ambayo yamo katika Kiswahili cha leo, kunadhihirisha kuwa lugha hii ilikuwapo kabla ya ujio wa wageni.

(b) **Ushahidi wa Al-Masudi (karne ya 10)**

Al-Masudi alifika Pwani ya Afrika Mashariki kati ya mwaka 915 na 945 B.K. Yeye alisema kuwa wenyeji wa Pwani ya Afrika Mashariki waliitwa **Wazanji** na watawala wao

FOR ONLINE READING ONLY

waliitwa *Wakilimi*. Watawala hao waliaminika kuwa walitawala kwa nguvu za Mungu, na kwamba *Kiazania* ndiyo lugha yao iliyotumika katika mawasiliano. Al-Masudi anadai kuwa neno *Zanzibar* linatokana na *Zenjibar*, yaani Pwani ya Zanji. Ushahidi huu unaonesha kuwa wenyeji wa Pwani ya Afrika Mashariki walikuwa na lugha yao hata kabla ya wageni.

(c) *Ushahidi wa Al-Idrisi (karne ya 12)*

Huyu alikuwa mfanyakazi katika mahakama ya Mfalme Rogers II kutoka kisiwa cha Sicily. Ugunduzi wake ulijikita katika jina la Zanzibar. Yeye anasema kuwa jina la zamani la Zanzibar ni Unguja. Vilevile, aliandika kitabu ambacho kilikuwa na majina ya ndizi kama vile *mkono wa tembo*, *muriani*, na *sukari*, ambayo ni maneno ya Kiswahili. Kwa kuwa maneno haya ni ya Kiswahili cha leo, basi hatuna shaka kusema kuwa lugha hii ilikuwapo kabla ya ujio wa wageni.

(d) *Ushahidi wa Marco Polo*

Marco Polo alikuwa mgeni aliyeandika kitabu kilichoeleza kuwa Zanguabar (Zanzibar) iliitwa *Ungudya* kutokana na lugha ya wakazi hao. Vilevile, anadai kuwa chakula cha wenyeji wa Zanzibar kilikuwa ndizi aina ya *muriyani*, *mkono wa tembo* na vyakula vingine kama *kundi* (*kunde*) na *fili* (aina ya maharage). Maneno haya yanadhihirisha kuwa lugha ya Kiswahili ilikuwapo hata kabla ya wageni kufika katika upwa wa Afrika Mashariki.

(e) *Historia ya Kilwa*

Hii ni historia ya Kilwa Kisiwani na Kilwa Kivinje kunako karne ya 10-16 B.K. Historia hii inahusisha majina ya utani ya masultani wa kwanza, Ali Ibn Husein, ambaye aliitwa *Nguo nyingi*, na mwanawe, Mohamed Ibn Ali, aliyeitwa *Mkoma watu*. Kutokana na habari hizi, inasemekana kuwa Kiswahili kiliwahi kusemwa kunako karne ya 10 au ya 11 B.K. Pia, kuna maelezo ya Talt Ibn al- Husein ambaye aliitwa *Hasha Hazifiki* kama jina la utani. Majina haya ya utani, ambayo ni ya Kiswahili, yanathibitisha kuwepo kwa lugha ya Kiswahili hata kabla ya ujio wa wageni.

(f) *Ushahidi wa Ibn Batuta (karne ya 14)*

Ibn Batuta alifika Pwani ya Afrika Mashariki mwaka 1331 B.K. Alisafiri kutoka Mogadishu kwenda Kilwa kupitia Mombasa. Batuta anaelezea maisha ya watu wa nchi ya Afrika Mashariki ingawa aliita nchi ya *Sahel*. Katika maelezo yake, anadai kuwa alianza safari baharini kutoka Mogadishu kwenda nchi ya Sahel na mji wa Kilwa ambao umo katika nchi za Zanj. Pia, anaeleza kuwa safari ya kutoka Mombasa katika nchi ya Sahel ilichukua siku mbili. Vilevile, alieleza kuwa watu wa Mombasa huagiza nafaka kutoka Uswahilini.

FOR ONLINE READING ONLY

Inasemekana kuwa, Ibn Batuta alipofika Kilwa, alikutana na washairi wenyeji walioandika mashairi na tenzi kwa lugha ya Kiswahili. Hivyo, ushairi ni ushahidi mwingine unaoonesha kuwa Kiswahili kilikuwapo hata kabla ya ujio wa Waarabu.

(g) *Ushairi wa Kiswahili*

Ushahidi wa ushairi wa Kiswahili umejitokeza katika tendi na tenzi ambazo zilitungwa kwa vipindi tofauti. Utendi wa *Fumo Liyongo,* ambao ulitungwa na Mohamed bin Abubakar kunako miaka ya 1160 - 1204, ni mfano wa ushahidi wa ushairi wa Kiswahili. Utendi huu, wenye beti 234, ulitungwa kwa lahaja za Kiswahili za Kiamu na Kimvita. Ufuatao ni mfano wa beti za Utendi wa Fumo Liyongo kama ulivyonukuliwa kutoka kwa Mulokozi (1999):

1. Hadithi niwandikiye,
   Ya ajabu musikiye,
   Yalojiri amriye,
   Mupate kufahamiya.

2. Niweleze kwa utungo,
   Hadithi yake Liyongo,
   Niweleze na mazingo,
   Mambo yalomzingiya.

**Chanzo:** *Tenzi Tatu za Kale* (Mulokozi,1999)

Vilevile, kuna utenzi wa Tambuka uliotungwa kunako miaka ya 1700. Utenzi huu uligunduliwa na E.A. Alpers wa Goa ambaye pia aligundua barua 14. Ushahidi huu unaonesha kuwa barua hizo ziliandikwa kwa lahaja ya Kimvita ambayo ni lahaja mojawapo ya Kiswahili. Mfano wa ubeti wa utenzi wa Tambuka ni huu ufuatao:

450. Kwa mau mema mekundu,
   Yali mivazi ya ngandu,
   Na ukundufu ya tundu,
   Haiba yakwe ya pua.

Utenzi mwingine unaothibitisha Ubantu wa Kiswahili ni utenzi wa Mwanakupona. Utenzi huu ulitungwa na Mwanakupona (Nana) kwa lahaja ya Kipate kunako miaka ya 1850 akimuusia bintiye aliyejulikana kwa jina la Hashima binti Sheikh Mataka. Zifuatazo ni baadhi ya beti za utenzi huo:

FOR ONLINE READING ONLY

28. Keti naye kwa adabu,
Simtie ghadhabu,
Akinena simjibu,
Jitahidi kunyamaa.

31. Kilala siikukuse,
Mwegeme umpapase,
Na upepo asikose,
Mtu wa kumpepea.

34. Mnyoe mpalilize,
Sharafu umtengeneze,
Na udi umfukize,
Bukurata wa ashia.

*Chanzo:* **Utenzi wa Mwanakupona** (Mwanakupona,1858)

Tenzi hizi za kale, zilizotungwa kwa Kiswahili, ni uthibitisho kuwa Kiswahili ni lugha ya Kibantu kwa kuwa kilitumika hata kabla ya ujio wa wageni.

## *Ubantu wa lugha ya Kiswahili kiisimu*

### *Shughuli ya 3.3*

Kwa kutumia vyanzo mbalimbali vya maktabani au vya ki-TEHAMA, tafuta mifano 20 ya maneno ya Kiswahili ambayo yanashabihiana na maneno mengine kutoka lugha tano za Kibantu, kisha bainisha vipengele vinavyoshabihiana.

### *Je, wajua* ?

Ushahidi wa kiisimu ni matokeo ya uchunguzi wa lugha kwa kuzingatia misingi ya kisayansi ya lugha inayohusu msamiati, vipengele vya kifonolojia, vipengele vya kimofolojia, pamoja na vipengele vya kisintaksia. Ushahidi wa kiisimu unaothibitisha Ubantu wa Kiswahili unafafanuliwa katika vipengele vinavyofuata.

(a) **Ushahidi wa msamiati**

Tafiti mbalimbali zimefanywa kuhusu kufanana kwa msamiati wa lugha ya Kiswahili na lugha zingine za Kibantu. Kwa mfano, Maganga (1997) alifanya utafiti kwa kukusanya na kuchunguza jumla ya maneno 9179 ya Kiswahili. Katika utafiti wake, aligundua kwamba asilimia 60 ya maneno yote yanayoweza kuandikwa na kutamkika katika

FOR ONLINE READING ONLY

lugha ya Kiswahili yana asili ya lugha za Kibantu; asilimia 30 ni lugha ya Kiarabu na asilimia 10 ni lugha zingine za kigeni kama vile Kiingereza, Kijerumani, Kireno, Kihindi, Kiajemi, na Kifaransa. Kwa hiyo, kutokana na idadi kubwa ya maneno hayo kuwa ni ya Kibantu, ni dhahiri kuwa Kiswahili ni Kibantu.

Mtafiti mwingine ni Malcom Guthrie ambaye alifanya utafiti kuhusu uhusiano uliopo baina ya lugha za Kibantu zilizoko katika eneo ambalo Wabantu wanaishi. Guthrie (1971) alichunguza maneno 22,000 kutoka lugha 200 za Kibantu. Katika uchunguzi wake, alibaini kuwa maneno 2,300 yamo katika lugha mbalimbali za Kibantu na Kiswahili kikiwemo. Pia, mashina ya maneno yapatayo 500 ya lugha ya Kiswahili yamo katika lugha mbalimbali za Kibantu kama ifuatavyo:

51% Kiluba kutoka Katanga Zaire (Kwa sasa ni Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo)

54% Kiwemba (Zambia)

44% Kikongo (Zaire Mashariki)

44 % Kiswahili (Pwani ya Afrika Mashariki)

41% Kisukuma (Tanzania)

35% Kiyao (Tanzania /Msumbiji)

20% Kisotho (Botswana)

43% Kirundi (Burundi)

37% Kinyoro (Uganda)

29% Kizulu (Afrika Kusini)

Uchunguzi wa Guthrie unathibitisha kuwa Kiswahili ni Kibantu kwa kuwa kinafanana kimsamiati na lugha zingine za Kibantu.

Hali kadhalika, kuna ushahidi unaonesha kuwa lugha ya Kiswahili na lugha zingine za Kibantu zinafanana katika mpangilio wa mofu na mashina ya maneno. Batibo (2001) alifanya uchunguzi wa Kiswahili na lugha zingine za Kibantu na kugundua yafuatayo:

(i) Kuna mfanano wa muundo wa mofu kwa kuangalia mzizi, vitenzi na mashina ya vitenzi katika Kiswahili. Mizizi ya vitenzi katika lugha ya Kiswahili na lugha zingine za Kibantu ina muundo wa -KIK- (Konsonanti-Irabu-Konsonanti). Tazama mifano katika Jedwali Na. 3.1(a).

FOR ONLINE READING ONLY

*Jedwali Na. 3.1 (a):* Muundo wa mzizi wa Kiswahili na lugha zingine za Kibantu

| *Lugha* | *Kitenzi* | *Mzizi* | *Muundo wa mzizi wa kitenzi* |
|---|---|---|---|
| Kiswahili | pika | -pik- | -KIK- |
| Kilingala | bila | -bil- | -KIK- |
| Kiluguru | kana (kata) | -kan- | -KIK- |

(ii) Mashina ya maneno ya lugha ya Kiswahili na lugha zingine za Kibantu yana muundo wa KIKI (Konsonanti-Irabu-Konsonanti-Irabu). Tazama mifano katika Jedwali Na. 3.1 (b).

*Jedwali Na 3.1 (b):* Muundo wa mashina ya Kiswahili na lugha zingine za Kibantu

| *Lugha* | *Kitenzi* | *Shina* | *Muundo wa shina la kitenzi* |
|---|---|---|---|
| Kiswahili | kucheka | cheka | KIKI |
| Kihaya | okusheka | sheka | KIKI |
| Kinyaturu | uheka | heka | KIKI |
| Kishona | kuseka | seka | KIKI |

Mifano ya mizizi na mashina ya vitenzi katika Majedwali Na. 3.1(a) na 3.1(b) ni uthibitisho wa kufanana kwa mashina ya maneno ya Kiswahili na lugha zingine za Kibantu. Hivyo, ni ushahidi kuwa Kiswahili ni Kibantu.

Wanazuoni wengine waliochunguza kufanana kwa msamiati kunakojitokeza baina ya lugha ya Kiswahili na lugha zingine za Kibantu ni Massamba, Kihore na Hokororo (1999) na Massamba (2017). Hawa waliangazia zaidi msamiati wa msingi. Jedwali Na. 3.2 linaonesha kufanana kwa baadhi ya maneno ya lugha ya Kiswahili na lugha zingine za Kibantu.

*Jedwali Na. 3.2:* Kufanana kwa baadhi ya maneno ya lugha ya Kiswahili na lugha zingine za Kibantu

| *Kiswahili* | *Kindali* | *Kizigua* | *Kijita* | *Kikurya* | *Kindendeule* |
|---|---|---|---|---|---|
| mtu | umu-ndu | m-ntu | omu-nu | omu-ntu | mu-ndu |
| maji | a-mashi | manzi | o-manji | a-manche | maache |
| mwana | umw-ana | mwa-ana | o-mw-ana | omo-na | mwa-ana |

FOR ONLINE READING ONLY

(b) **Ushahidi kuhusu Vitenzi**

Kuna kufanana kwa kiasi kikubwa kati ya vitenzi vya lugha ya Kiswahili na vya lugha zingine za Kibantu. Kufanana huko hujidhihirisha katika vipengele vinavyofafanuliwa katika sehemu zinazofuata.

*(a) Mwanzo wa vitenzi*

Vitenzi vyote vya Kiswahili na vile vya lugha zingine za Kibantu huanza na viambishi awali vipatanishi vya nafsi. Katika mifano ya Jedwali Na. 3.3, viambishi vilivyoandikwa kwa hatimlalo katika vitenzi ni viambishi awali vya nafsi ya kwanza umoja.

*Jedwali Na. 3.3:* Mwanzo wa vitenzi vya Kiswahili na lugha zingine za Kibantu

| *Lugha* | *Vitenzi* |
|---|---|
| Kiswahili | **ni**-nakwenda |
| Kihaya | **ni**-ngenda |
| Kiyao | **n**-gwenda |
| Kindendeule | **ni**-yenda |

*(b) Miisho ya vitenzi*

Vitenzi vingi vya Kiswahili na lugha zingine za Kibantu huishia na irabu *-a* katika hali ya uyakinishi. Tazama mifano ya vitenzi vya Kiswahili, lugha zingine za Kibantu, na vitenzi vyenye asili ya Kiarabu katika Jedwali Na. 3.4.

*Jedwali Na. 3.4:* Miisho ya vitenzi vya Kiswahili na lugha zingine za Kibantu

| *Kiswahili* | *Kihaya* | *Kijita* | *Kinyaturu* | *Kinyakyusa* |
|---|---|---|---|---|
| kulal**a** | okuniam**a** | okumaam**a** | ura**a** | ukulambalal**a** |
| kuva**a** | okujwal**a** | okufwaal**a** | uri**a** | ukufwal**a** |
| kulet**a** | okulet**a** | okuleet**a** | get**a** | ukutwal**a** |
| kwend**a** | okugend**a** | okugenda | gend**a** | ukubhuk**a** |
| kuzik**a** | okuziik**a** | okusiik**a** | uvīk**a** | ukusyil**a** |

FOR ONLINE READING ONLY

### (c) Mnyambuliko wa vitenzi

Vitenzi vya lugha zingine za Kibantu huweza kunyambuliwa kama ilivyo katika vitenzi vya lugha ya Kiswahili. Tazama mifano katika Jedwali Na. 3.5.

**Jedwali Na. 3.5:** Mnyambuliko wa vitenzi vya Kiswahili na lugha zingine za Kibantu

| Lugha | Kitenzi | Mnyambuliko |
|---|---|---|
| Kiswahili | lima | m-ku-lim-a , ki-lim-o |
| Kihaya | lima | o-mu-lim-i , e-i-lim-a |
| Kiha | rima | u-mu-rim-i u-mu-rim-o |
| Kinyaturu | rịma | mụ-rịm -i i-rịm-a |

Mifano katika Jedwali Na. 3.5 inaonesha jinsi vitenzi vya Kiswahili na vya lugha zingine za Kibantu vinavyokubali utaratibu wa unyambulishaji. Aidha, hali hii hujitokeza pia katika uambishaji wa viambishi mbalimbali kwenye mzizi wa vitenzi.

### (d) Uambatizi wa vitenzi

Vitenzi vya lugha zingine za Kibantu vinaweza kupokea viambishi ambatizi katika mzizi kama ilivyo katika vitenzi vya lugha ya Kiswahili. Tazama mifano katika Jedwali Na. 3.6.

**Jedwali Na. 3.6:** Uambatizi wa vitenzi vya Kibantu

| Lugha | Kitenzi | Uambatizi |
|---|---|---|
| Kiswahili | cheza | a-na-chez-a |
| Kihaya | zaana | n-a-zaan-a |
| Kinyaturu | ina | ụ-gụ-in-a |
| Kichaga (Kivunjo) | tema | na-i-tem-a |

Mifano katika Jedwali Na. 3.6 inaonesha uambatizi unavyojitokeza katika vitenzi vya Kiswahili na lugha zingine za Kibantu. Uchanganuzi wa vitenzi hivyo ni kama ifuatavyo:

FOR ONLINE READING ONLY

Kiswahili: **anacheza**:

a- ni kiambishi cha nafsi ya tatu umoja.

-na- ni kiambishi cha wakati uliopo.

-chez- ni mzizi.

-a ni kiambishi tamati, uyakinishi.

Kihaya: **nazana**:

n- ni kiambishi cha wakati uliopo

-a- ni kiambishi cha nafsi ya tatu

-zan- ni mzizi wa neno.

-a ni kiambishi tamati, uyakinishi.

Kinyaturu: **uguina**:

u- ni kiambishi nafsi ya tatu umoja.

-gu- ni kiambishi wakati uliopo.

-in- ni mzizi wa neno.

-a ni kiambishi tamati, uyakinishi.

Kichaga (Kivunjo): **naitema**

na- ni kiambishi cha nafsi ya tatu umoja.

-i- ni kiambishi cha wakati uliopo.

-tem- ni mzizi wa neno.

- a ni kiambishi tamati, uyakinishi.

(c) **Ushahidi wa ngeli za nomino**

Katika lugha ya Kiswahili na lugha zingine za Kibantu, nomino hupangwa katika makundi yaitwayo **ngeli za nomino** kwa kuzingatia kigezo cha maumbo ya umoja na wingi wa nomino hizo au upatanisho wa kisarufi kama ifuatavyo:

(i) Maumbo ya nomino

Maumbo ya umoja na wingi wa majina hutumika kupanga makundi maalumu ya majina yenye sifa zinazofanana katika lugha ya Kiswahili na lugha zingine za Kibantu. Tazama mifano katika Jedwali Na.3.7(a).

FOR ONLINE READING ONLY

**Jedwali Na. 3. 7 (a):** Ngeli za nomino za Kiswahili na lugha zingine za Kibantu kwa kigezo cha maumbo ya majina.

| Lugha | Umoja | Wingi | Ngeli za nomino |
|---|---|---|---|
| Kiswahili | mti | miti | m(u)-/mi- |
| Kinyamwezi | (u)mti | imiti | mu-/mi- |
| Kihehe | umubiki | imibiki | mu-/mi- |
| Kirangi | uti | miti | mu-/mi |

(i) **Upatanisho wa kisarufi**

Utaratibu wa kubainisha makundi ya majina kwa kutumia upatanisho wa kisarufi unaotumika katika Kiswahili, unatumika pia katika lugha zingine za Kibantu. Tazama mifano katika Jedwali Na. 3.7 (b).

**Jedwali Na 3. 7 (b):** Ngeli za nomino za Kiswahili na lugha zingine za Kibantu kwa kigezo cha upatanisho wa kisarufi

| Lugha | Umoja | Wingi | Ngeli za nomino |
|---|---|---|---|
| Kiswahili | mtoto *a*-nacheza | watoto *wa*-nacheza | A - WA |
| Kingoni | mwana *i*-kina | vana *vi*-kina | I - VI |
| Kichaga | mona *a*-itema | wana *wa*-itema | A - WA |
| Kisambaa | ng'wana *a*-shezigha | wana *wa*-shezigha | A - WA |

(d) *Muundo wa tungo*

Muundo wa tungo za lugha zingine za Kibantu hufanana sana na ule wa lugha ya Kiswahili kwa kuzingatia mfuatano na uhusiano wa maneno katika tungo, hususani katika kirai nomino (KN) na kirai kitenzi (KT). Tazama mifano katika Jedwali Na. 3.8.

FOR ONLINE READING ONLY

**Jedwali Na. 3. 8:** Muundo wa tungo za Kiswahili na lugha zingine za Kibantu

| Lugha | KN | | | KT | |
|---|---|---|---|---|---|
| | N | V | V | T | N |
| **Kiswahili** | Mtoto | wangu | mdogo | anacheza | ngoma |
| **Kisukuma** | Ng'wana | wane | ndo | alebina | ng'oma |
| **Kikonongo** | Mwana | nane | mdo | akusapa | ngoma |

Pia, nomino au kiwakilishi cha Kiswahili na lugha zingine za Kibantu hutawala upatanisho wa kisarufi kati yake na maneno mengine yanayoandamana nayo katika tungo. Upatanisho huo hujidhihirisha katika viambishi vya upatanisho wa kisarufi vya maneno hayo. Mifano katika Jedwali Na. 3.9 inathibitisha hoja hii.

**Jedwali Na. 3. 9:** Upatanisho wa kisarufi wa tungo za Kiswahili na lugha zingine za Kibantu

| Lugha | Umoja | Wingi |
|---|---|---|
| Kiswahili | ***m***toto ***m***zuri ***a***nacheza | ***wa***toto ***wa***zuri ***wa***nacheza |
| Kijita | o-***mw***-ana ***w***ekisi keenya | ***a-bh***-ana ***bh***ekisi ***abhee***nya |
| Kilugulu | i-mw-ana i***m***notzi ***k***ofvina | i-***w***-ana i***w***anotzi ***wo***fvina |
| Kihaya | o-***mw***-ana ***om***uruungi ***na***zana | a-***b***-ana ***b***aruungi ni***ba***zana |
| Kinyaturu | ***mw***-ana ***m***uja ugisa | ***v***-ana ***a***ja vigisa |
| Kipare | ***mw***-ana ***w***edi ***e***shinjiga | ***v***-ana ***ve***di ***ve***shinjiga |

Viambishi vilivyoandikwa kwa hatimlalo katika jedwali vinaonesha upatanisho wa kisarufi kati ya nomino, vivumishi, na vitenzi. Huu ni uthibitisho kwamba Kiswahili na lugha zingine za Kibantu hufanana katika utaratibu wa upatanisho wa kisarufi na, hivyo, ni ushahidi kuwa Kiswahili ni Kibantu.

## Zoezi la 3.2

1. Kwa kutumia mifano ya vitenzi na vivumishi vya lugha mbalimbali za Kibantu kutoka vyanzo mbalimbali vya maktaba na ki-TEHAMA, thibitisha Ubantu wa Kiswahili.
2. Tathmini hoja zinazotolewa na wanaisimu wanaodai kuwa asili ya lugha ya Kiswahili ni Kiarabu.
3. Baada ya kusoma hoja mbalimbali zinazohusu asili ya Kiswahili, una mtazamo gani kuhusu asili ya Kiswahili? Toa angalau hoja tano (5) kutetea mtazamo wako.

FOR ONLINE READING ONLY

## Nadharia kuhusu chimbuko la lugha ya Kiswahili

### Shughuli ya 3.4

Chunguza ramani ifuatayo kwa makini, kisha bainisha maeneo ambako unafikiri Kiswahili kilianzia. Toa sababu zinazoshadidia machaguo yako.




**Kielelezo Na. 3.1:** ***Ramani kuonesha maeneo ya Pwani ya Afrika Mashariki***

FOR ONLINE READING ONLY

### Je, wajua ?

Neno chimbuko lina maana ya mahali ambapo kitu kimeanzia. Chimbuko la lugha ya Kiswahili limezungumziwa na wanazuoni mbalimbali. Mitazamo yao inajidhihirisha

kupitia nadhariatete mbalimbali. Nadhariatete zilizokwishabainishwa hadi sasa ni tano. Nadhariatete hizo ni: **Nadhariatete ya Shungwaya Kuu, Nadhariatete ya Ngozi(ni), Nadhariatete ya Kaskazini Mashariki mwa Kenya, Nadhariatete ya Visiwa vya Lamu**, na **Nadhariatete ya Mwachano na Makutano**. Nadhariatete hizi zimefafanuliwa katika vipengele vinavyofuata.

### *1. Nadhariatete ya Shungwaya Kuu*

Nadhariatete hii inadai kuwa chimbuko la Kiswahili ni eneo ambalo lilikuwa Himaya Kuu ya Shungwaya. Mwasisi wa nadhariatete hii ni James de vere Allen. Nadhariatete hii inadai kuwa kulikuwa na himaya moja ambayo ilijulikana kwa jina la Shungwaya Kuu. Himaya hii ilikuwa kubwa na ilikuwa imeenea katika maeneo mengi kama vile Kilindi, Segeju, Chagga, Pare, na Pokomo. Maeneo mengine ni Gikuyu, Meru, Embu, Taita, Assu, Chuka, Tharaka, na Kamba. Aidha, himaya hii ilihusisha watu wa jamii nyingi ambazo zilishirikiana katika shughuli mbalimbali kama vile biashara. Inasemekana kuwa makao makuu ya Waswahili yalikuwapo katika himaya hii. Kwa mujibu wa maelezo hayo, hapo ndipo Kiswahili kilipoanzia kwa kuwa hakuna jamii nyingine inayotajwa katika himaya hii zaidi ya Waswahili ambao wanaelezwa kuwa walikuwa wakizungumza lugha ya Kiswahili.

Hata hivyo, wanazuoni mbalimbali wamehoji uhalali wa madai hayo kwa kudai kuwa hakuna ushahidi wowote kuwa kuliwahi kuwapo Himaya ya Shungwaya katika eneo la Afrika Mashariki. Jambo kubwa linalohojiwa hapa ni kwamba inawezekanaje eneo kubwa kabisa kama hili lisijulikane kwa wasafiri wa kale kabisa kama Al Mas'ud aliyefika katika Upwa wa Afrika Mashariki karne ya 4? Al Mas'ud anajulikana sana kama msafiri wa kale ambaye ameandika habari nyingi zinazohusu Zanj, lakini katika maandiko yake hakuna mahali alipotaja Himaya ya Shungwaya.

Vilevile, himaya hii haitajwi mahali popote kwenye mwongozo maarufu wa **Periplus of the Erythrean Sea** wala kwenye kumbukumbu za Tuang Ch'eng-shih ambazo zinatoa habari nyingi kuhusu Pwani ya Afrika ya Mashariki. Kutokana na madai haya, wanazuoni kama Munro (1967), Saberwal (1967), na Massamba (2007) wanasema kuwa Nadhariatete ya Shungwaya Kuu ni dhaifu na ya kubuni tu kama kisasili.

### *2. Nadhariatete ya Ngozi (ni)*

Nadhariatete hii inadai kuwa Kiswahili kilianzia mahali palipojulikana kama Ngozi(ni). Waasisi wa nadhariatete hii ni Shihabbudin Chiraghddin. Waasisi na wafuasi wa nadhariatete hii wanaeleza kuwa, katika eneo la Ngozi(ni), kulikuwa na watu waliokuwa wakifanya biashara za kupima mashamba kwa kutumia kamba za ngozi na walikuwa wakizungumza Kingozi ambacho inasemekana kilianzia kaskazini mwa eneo ambalo, baadaye, liliitwa Uswahilini. Kutokana na eneo hilo, wafuasi wa nadhariatete

FOR ONLINE READING ONLY

hii wanaamini kwamba Kingozi ni miongoni mwa lugha za Kibantu. Ngozini ni eneo ambalo linadhaniwa kuwa chimbuko la Kiswahili.

Kama ilivyo kwa Nadhariatete ya Shungwaya Kuu, Nadhariatete ya Ngozini nayo inapingwa kwa sababu hadi leo hakuna mahali panapothibitishwa kuwa ndipo palikuwa Ngozini.

### 3. Nadhariatete ya Kaskazini-Mashariki mwa Kenya

Nadhariatete hii inadai kwamba chimbuko la lugha ya Kiswahili ni Kaskazini-Mashariki mwa Kenya. Nadhariatete hii iliasisiwa na Ibrahim Noor Shariff na Alamin Mazrui. Vilevile, wanaungwa mkono na Hussein Soud Elmaawy. Inadaiwa kuwa Kiswahili kilitokana na mchanganyiko wa lugha za Kiafrika kwa kiasi kidogo na Kiarabu kwa kiasi kikubwa. Haya ni matokeo ya kuoana kati ya Waarabu na baadhi ya makabila ya Kiafrika yaliyokuwa yakiishi katika Upwa wa Afrika Mashariki, hususani Kaskazini-Mashariki mwa Kenya. Kutokana na mtagusano huo, pijini ilikomaa na kuwa krioli ambayo ilianza kufanana na lugha za jirani ambazo ni Kipokomo na Kimijikenda, hasa katika kipengele cha muundo na msamiati. Hivyo, kutokana na makutano ya watu hawa, kukazaliwa pijini ambayo baadaye ilikomaa na kuwa krioli ambayo ni lugha ya Kiswahili. Wazungumzaji walioitumia lugha hii kama lugha mama waliitwa Waswahili.

Nadhariatete hii inapingwa na mwanazuoni Massamba (2007) kwa kudai kuwa waasisi wa nadhariatete hii wameshindwa kubainisha hayo makabila yaliyooana na Waarabu ni yapi. Je, walikuwa Wakushiti (Wagalla na Wasomali) au Wabantu? Massamba anaendelea kupinga nadhariatete hii kwa kudai kuwa Kiswahili hakikuanza kama pijini. Anadai kuwa kama Kiswahili kingeanza kama pijini, kisingekuwa kinashabihiana kwa kiwango kikubwa na lugha za Kibantu, hususani kwenye vipengele vyake vya kisarufi.

### 4. Nadhariatete ya Visiwa vya Lamu

Wanazuoni walioasisi nadhariatete hii ni Derick Nurse na Thomas Spear. Nadhariatete hii inadai kuwa Kiswahili kilianzia katika visiwa vya Lamu vilivyopo Kaskazini mwa Kenya. Inadaiwa kuwa Wabantu wa kwanza, ambao wanasadikika kuwa walikuwa Waswahili, waliishi katika visiwa hivyo. Waasisi wa nadhariatete hii wanadai kuwa Waswahili wa kale walikuwa wafua vyuma na walihamia Pwani karne ya 9 -12 B.K. kutokea bara kwa madhumuni ya kuuza bidhaa za chuma kwa wageni. Baadaye, walisambaa katika sehemu mbalimbali za Visiwa vya Lamu. Katika maeneo walimosambaa, walianzisha misingi imara ya jamii ya Kiswahili na utamaduni wao.

Hata hivyo, Massamba (2007) anadai kuwa hoja kwamba Waswahili wa kale walijongea kwenda pwani kufanya biashara na wageni inatia wasiwasi. Hoja hii inaonesha kuwa, wakati huo, tayari kulikuwa na jamii moja ya Waswahili ambao walihama kutoka

FOR ONLINE READING ONLY

bara kwenda pwani, jambo ambalo si la kweli. Tangu enzi hizo hadi leo, kuna jamii mbalimbali za Waswahili. Vilevile, Massamba anasema kwamba madai kuwa Kiswahili kilianzia Lamu yanahitaji mtetezi wa nadharia hii aeleze kilichosababisha kisambae kwenye Upwa wa Afrika Mashariki kutoka Lamu mpaka Sofala, Msumbiji.

**5. Nadhariatete ya Mwachano na Makutano ya Lugha za Kibantu**

Mwasisi wa nadhariatete hii ni Massamba (2007). Massamba anadai kuwa Wabantu walijongea kutoa bara kuelekea Mashariki hadi kandokando ya Bahari ya Hindi. Wabantu hawa walikuwa na lugha yao. Wengine waliendelea kuelekea Kaskazini huku wengine wakielekea Kusini. Humo njiani, wengine walikuwa wakiweka makazi. Baada ya muda, upwa wote wa Bahari ya Hindi ukawa na wakazi. Hawa waliishi kwa vizazi na vizazi mpaka lugha zao zikaanza kutofautiana.

Kutokana na shughuli za uzalishaji mali kama vile uvuvi, lugha zao zilianza kuingiliana tena. Kwa kuwa lugha hizi zilikuwa na mnasaba mmoja, basi, ilikuwa rahisi lugha hizo kuanza kufanana tena. Kwa mujibu wa Massamba, lugha hizo zilizokuwa zinafanana na zilizotapakaa katika Upwa wa Afrika Mashariki ndizo zinaitwa lahaja za Kiswahili. Hivyo, mwanazuoni huyo anadai kuwa lugha ya Kiswahili ilianzia sehemu mbalimbali kwa wakati sawia. Mawazo kama haya ya Massamba yaliwahi pia kutolewa na Freeman-Greenville (1958) pamoja na Oliver na Mathew (1963).

Hata hivyo, nadhariatete hii haielezi ilikuwaje hadi leo bado kuna lugha zilizotapakaa kwenye upwa wa Afrika Mashariki ambazo si lahaja za Kiswahili. Kwa mfano, nadhariatete hii haielezi lugha kama vile Kizaramo, Kikwere, na Kimatumbi ziliibukaje katika Pwani ya Afrika Mashariki, mahali ambapo lahaja nyingine za Kiswahili zinadaiwa kuinukia. Mambo haya yanafanya nadhariatete hii isailike pia.

**Tamrini ya 3**

1. Fikiria kwamba umeona tangazo la mashindano ya kuandika insha inayohusu mjadala wa wanazuoni kuhusu chimbuko la Kiswahili. Andika insha hiyo kwa hoja tano na uoneshe msimamo wako kuhusu mjadala huo.
2. "Lugha ya Kiarabu ina mchango mkubwa katika msamiati na sarufi ya Kiswahili." Kubali au kataa kauli hii kwa mifano maridhawa.
3. Lugha ya Kiswahili ina baadhi ya maneno yaliyotoka katika lugha mbalimbali za kigeni. Tumia mifano maridhawa kuthibitisha kauli hii kutoka lugha tano za kigeni.
4. Kwa kutumia vyanzo mbalimbali vya kimaktaba na kimtandao, tathmini ushahidi wa kihistoria unaothibitisha kuwa Kiswahili ni Kibantu.

FOR ONLINE READING ONLY

# Sura ya Nne
# Kukua na kuenea kwa Kiswahili

## Utangulizi

*Lugha yoyote hukua kimatumizi na kuenea sehemu mbalimbali. Kiswahili, kama moja ya lugha, kinakua na kuenea kutoka sehemu moja hadi nyingine. Katika sura hii, utajifunza kukua na kuenea kwa Kiswahili katika nchi za Afrika Mashariki kabla na baada ya uhuru. Aidha, utajifunza kukua na kuenea kwa Kiswahili kutokana na maendeleo ya sayansi na teknolojia. Umahiri utakaoujenga utakusaidia kutathmini hadhi ya Kiswahili kimatumizi na kimsambao Afrika Mashariki. Pia, umahiri huo utakusaidia kuelewa jinsi sayansi na teknolojia zinavyosaidia kukua na kuenea kwa Kiswahili.*

**Fikiri**

Lugha inavyoongeza msamiati, wazungumzaji na kusambaa

## Kukua na kuenea kwa Kiswahili katika nchi za Afrika Mashariki kabla ya uhuru

**Shughuli ya 4.1**

Tumia vyanzo mbalimbali vya maktabani na mtandaoni kueleza mambo yafuatayo:

(i) Kukua kwa lugha

(ii) Kuenea kwa lugha

(iii) Viashiria vya kukua kwa lugha

(iv) Viashiria vya kuenea kwa lugha

FOR ONLINE READING ONLY

**Je, wajua ?**

Kabla ya kuanza kuelezea kukua na kuenea kwa Kiswahili Afrika Mashariki, inafaa kwanza kuelewa dhana za "kukua" na "kuenea" kwa lugha. Kukua kwa lugha ni kuongezeka kwa msamiati na nyuga za matumizi ya lugha inayohusika. Kuenea kwa lugha ni kuongezeka kwa maeneo ya kijiografia ambayo hapo awali hayakuwa yakitumia lugha hiyo. Katika sehemu hii, tutajadili kukua na kuenea kwa Kiswahili Tanganyika na Zanzibar, Kenya pamoja na Uganda.

**Kukua na kuenea kwa Kiswahili Tanganyika na Zanzibar kabla ya uhuru**

Kabla ya uhuru, lugha ya Kiswahili ilikua na kuenea kwa namna mbalimbali katika maeneo ya Tanganyika, Zanzibar, Kenya na Uganda. Katika sehemu hii, tutaangazia kukua na kuenea kwa lugha hiyo Tanganyika na Zanzibar. Sababu mbalimbali zilichangia kukua na kuenea kwake katika maeneo hayo kabla ya uhuru. Miongoni mwa sababu hizo ni utawala, harakati za kueneza dini, elimu, biashara, harakati za kisiasa, na vyombo vya habari. Sababu hizo zimebainishwa katika vipindi vitatu vya utawala kama zinavyofafanuliwa katika sehemu zinazofuata.

**1. Kipindi cha Utawala wa Waarabu**

Wakati wa utawala wa Waarabu, Sultani wa Zanzibar alitawala visiwa vya Pemba na Unguja. Katika kipindi cha utawala wake, Kiswahili kilikua na kuenea kutokana na shughuli za utawala, harakati za kueneza dini na biashara.

**(a) Utawala**

Katika kipindi cha utawala wa Waarabu, matumizi ya Kiswahili yalihimizwa katika himaya yote ya Sultani wa Zanzibar. Kwa mfano, katika utawala wake, Sultani wa Zanzibar aliandaa mfumo wa utawala uliotumia maakida, majumbe na maliwali ambao walitumwa katika baadhi ya maeneo ya Tanganyika. Watu hao walikuwa wanatoka pwani na walikuwa wanakijua vyema Kiswahili. Viongozi hao walipelekwa hasa sehemu za Kilwa, Bagamoyo, Tanga, Pangani, Kigoma Ujiji, na Mpwapwa. Katika maeneo hayo, walitumia lugha ya Kiswahili, jambo ambalo lilichangia katika kuikuza na kuieneza lugha hii.

**(b) Harakati za kueneza dini**

Harakati za kueneza dini katika maeneo ya Tanganyika na Zanzibar kabla ya uhuru ziliendeshwa na maimamu wa Kiislamu na wamisionari wa Kikristo.

FOR ONLINE READING ONLY

**(i) *Dini ya Kiislamu***

Dini ya Kiislamu ilienezwa na Waarabu ambao walifika Pwani ya Afrika Mashariki yapata karne ya nane B.K. na kuwakuta wenyeji wakizungumza lugha zao za Kibantu, kikiwamo Kiswahili. Waarabu walilazimika kujifunza lugha ya Kiswahili ili waweze kuhubiri na kutafsiri Kurani kwa lugha iliyoeleweka kwa watu wengi. Waarabu walisafiri kutoka pwani hadi bara kueneza dini kwa kutumia lugha ya Kiswahili. Kwa njia hiyo, walisaidia kueneza lugha ya Kiswahili. Aidha, viongozi wa dini ya Kiislamu walianza kuandika Kiswahili kwa kutumia hati ya Kiarabu. Pia, waliwafundisha waumini kasida kwa lugha ya Kiswahili.

**(ii) *Dini ya Kikristo***

Wakati wa utawala wa Waarabu, dini ya Kikristo ilienea Afrika Mashariki kupitia wamisionari kabla ya ujio wa Wajerumeni. Wamisionari hao walikuja chini ya mashirika mbalimbali ya dini kwa lengo la kueneza dini ya Kikristo. Miongoni mwa mashirika hayo ni Holy Ghost Fathers na White Fathers kutoka Ufaransa; na The Universities' Mission to Central Africa (UMCA) na Church Missionary Society (CMS) kutoka Uingereza. Shirika la UMCA liliundwa na Wakatoliki kutoka Amerika, Walutheri kutoka Ujerumani na Wapresibiteri kutoka Uskochi. Katika harakati za kueneza dini ya Kikristo, mashirika hayo yalisaidia kueneza lugha ya Kiswahili kwa kutoa mahubiri na kutafsiri maandiko yaliyohusu dini ya Kikristo kama vile Biblia na vitabu vya nyimbo. Mbali na hayo, mashirika haya pia yaliandika machapisho mengine kuhusu lugha ya Kiswahili kwa Kiswahili. Mwaka 1905, Misheni ya Magila - Tanga ilitoa kitabu cha *Habari za Wakilindi* kinachoelezea historia ya Wasambaa. Shirika la UMCA lilijishughulisha na uandishi wa machapisho mbalimbali kwa kutumia lahaja ya Kiunguja. Mwaka 1870, shirika la The Society for Promoting Christian Knowledge (SPCK) lilichapisha toleo la kwanza la sarufi ya Kiswahili cha Kiunguja lililoitwa *A Handbook of the Swahili Language as Spoken in Zanzibar* ambalo liliandikwa na Askofu Edward Steere. Shirika hili liliendelea kuchapisha machapisho mbalimbali kama vile *A Standard English - Swahili Dictionary* na *Swahili - English Dictionary*. Kamusi hizo zilianza kuandikwa na Askofu E. Steere na kukamilishwa na A. Madan na baadaye kurudiwa na F. Johnson.

Aidha, shirika la UMCA lilichapisha magazeti mbalimbali ya Kiswahili. Miongoni mwa magazeti hayo ni *Habari za Mwezi* (1888) na *Pwani na Bara* (1910). Magazeti haya yalichapishwa na Walutheri. Magazeti yaliyochapishwa na Wakatoliki yalikuwa *Barazani* na *Rafiki Yangu* (1910). Aidha, wamisionari hawa walikuwa na vituo katika maeneo mbalimbali kama vile Bagamoyo (1868), Magila (1864), Mpwapwa (1876), Ujiji (1877), Masasi (1876), Zanzibar (1860), na Ziwa Nyasa (1881). Katika mchakato wa kutimiza malengo yao, walijikuta wakieneza na kukuza lugha ya Kiswahili katika

FOR ONLINE READING ONLY

maeneo yenye vituo hivyo. Kwa ujumla, wamisionari walijikuta wakieneza lugha ya Kiswahili kwa sababu waliihitaji sana katika shughuli zao za kidini.

**(c) Biashara**

Waarabu walifanya biashara ya watumwa Pwani ya Afrika Mashariki. Misafara yao ya biashara ya watumwa ilikuwa ikitoka pwani kwenda bara na bara kwenda pwani. Kulikuwa na misafara iliyotoka maeneo ya Pangani na Saadani kupita njia ya Kaskazini kuelekea maeneo ya Mwanza (taz. Kielelezo Na. 4.1). Kadhalika, kulikua na misafara ya kati ambayo ilitokea maeneo ya Dar es Salaam na Kisiwa cha Unguja ikipita njia ya kati kuelekea maeneo ya Tabora na Ujiji. Kutoka eneo la Tabora misafara iligawanyika; wengine wakaelekea Kanda ya Ziwa Victoria na wengine wakaenda Kusini-Magharibi hadi nchi ya Zambia (taz. Kielelezo Na. 4.1). Mwisho, kulikua na misafara iliyotoka Mafia na kupita njia ya kusini kuelekea maeneo ya Uyao hadi ziwa Nyasa na nchi ya Malawi (taz. Kielelezo Na. 4.1). Mji wa Unguja ulikuwa soko kuu la watumwa. Mbali na biashara ya watumwa, Waarabu pia walichukua bidhaa zingine kutoka bara zikiwamo pembe za ndovu na vifaru, meno ya viboko, gundi ya sandarusi, ngozi za chui, malele ya kutengenezea rangi nyekundu, na magamba ya kobe kwa ajili ya kutengenezea machanuo. Baadhi ya bidhaa zilizokuwa zikipelekwa bara ni nguo, shanga, nyaya za chuma na za shaba kwa ajili ya kutengenezea vito vya thamani na silaha. Miji iliyokuwa maarufu katika kufanya biashara hizo ni Bagamoyo, Kilwa, Tabora, na Kigoma, hasa sehemu za Ujiji. Katika harakati hizo za biashara, Kiswahili kilitumika. Hali hii ilichochea kukua na kuenea kwa lugha hii katika maeneo ya pwani na bara.

## 2. Kipindi cha Utawala wa Wajerumani

Tanganyika lilikuwa koloni la Wajerumani kuanzia mwaka 1885. Wajerumani walifanya mambo mbalimbali yaliyosaidia kukuza na kueneza Kiswahili kama vile kukitumia katika shughuli za utawala, elimu na kilimo.

**(a) Utawala**

Wajerumani walipoingia Tanganyika, walikuta tayari kuna misingi ya lugha ya Kiswahili iliyojengwa na watawala wa Kiarabu na wamisionari. Lengo la Wajerumani lilikuwa kutumia lugha ya Kijerumani katika mawasiliano yote ili kujenga dola imara la Kijerumani katika misingi yote ya kisiasa, kiuchumi, na kiutamaduni. Hata hivyo, lengo lao halikutimia kwa sababu walihofia kwamba wenyeji wasingeweza kujifunza Kijerumani na kukitumia vizuri katika mawasiliano. Hivyo, walilazimika kusisitiza matumizi ya Kiswahili. Kwa msingi huo, waliufanya ujuzi wa Kiswahili kuwa sifa muhimu ya mtu kuajiriwa kama jumbe, liwali na akida, tarishi, karani, au afisa yeyote

FOR ONLINE READING ONLY

wa ngazi za chini. Sharti hili liliwalazimu watu kujifunza Kiswahili. Kwa njia hiyo, Kiswahili kilikua na kuenea kwa haraka.

**(b) Elimu**

Wajerumani walianzisha shule ya kwanza nchini Tanganyika mnamo miaka ya 1890 ambayo ilijengwa Tanga na kupewa jina la Tanga School. Shule zingine zilianzishwa Tabora, Ujiji, Kilimatinde, Kasanga, Mwanza, Tukuyu, na Moshi. Vilevile, walijenga vyuo vya ualimu Tabora na Bukoba. Pia, walianzisha shule kwa ajili ya wafanyakazi wa ngazi za chini. Hadi kufikia miaka ya 1910, Wajerumani walikuwa na shule zipatazo 83 za serikali. Lugha ya Kiswahili ndiyo ilikuwa lugha ya mawasiliano na ya kufundishia katika shule hizo. Walisisitiza lugha ya Kiswahili itumike shuleni kutokana na umuhimu wake. Kijerumani kilifundishwa kama somo. Hivyo, elimu ilisaidia kuenea kwa lugha ya Kiswahili.

**(c) Shughuli za kilimo**

Shughuli za kilimo, hususani kilimo cha mkonge, zilihusisha kuchukua vibarua waliojulikana kama *manamba* kutoka katika baadhi ya maeneo ya Tanganyika. Maeneo hayo ni kama vile Kigoma, Tabora, Ruvuma, Iringa na Singida. Manamba walisafirishwa kwenda maeneo mbalimbali kama vile Tanga, Morogoro na Kilimanjaro. Mawasiliano baina ya manamba, na kati ya wanyapara na manamba yalifanyika kwa Kiswahili. Aidha, manamba waliporudi kwao, waliwafundisha ndugu zao Kiswahili. Kwa njia hiyo, Kiswahili kilikua na kuenea.

**3. Kipindi cha Utawala wa Waingereza**

Utawala wa Waingereza ulianza mwaka 1919 baada tu ya Vita vya Kwanza vya Dunia. Wakati wa utawala huo, masuala ya kiutawala, kielimu na shughuli za kijeshi yalisaidia katika kukua na kuenea kwa Kiswahili.

**(a) Utawala**

Serikali ya Waingereza ilisisitiza matumizi ya Kiswahili, hususani kwa wafanyakazi wa ngazi za chini kama vile makarani, matarishi, machifu na wahudumu wengine wa ofisi. Wafanyakazi hao walilazimishwa kujifunza Kiswahili ili waweze kukitumia katika shughuli za utawala.

**(b) Elimu**

Sera za Waingereza hazikuruhusu Kiswahili kuwa lugha ya kufundishia katika shule za ngazi za juu tofauti na shule za msingi, hususani darasa la I-IV. Kiswahili kilichukuliwa kama lugha duni kikilinganishwa na Kiingereza. Hata hivyo, Waingereza walifanya kazi kubwa katika ukuzaji wa Kiswahili kupitia elimu. Katika utawala wao, waliona

FOR ONLINE READING ONLY

ni vyema kuwa na lugha moja ya kufundishia katika shule za msingi katika makoloni yao ya Afrika Mashariki. Lugha iliyoteuliwa ilikuwa Kiswahili. Ili iweze kutumika kwa namna moja, lugha hiyo ilisanifishwa kutokana na lahaja ya Kiunguja. Matumizi ya lugha ya Kiswahili katika shule za msingi nchini Tanganyika yalisaidia kukuza na kueneza lugha hiyo.

**(c) Mchango wa jeshi la King's African Rifles (KAR)**

Jeshi hili liliundwa na Waingereza mnamo mwaka 1902. Baada ya Vita vya Kwanza vya Dunia (1918), Waingereza walikabidhiwa nchi ya Tanganyika na Shirikisho la Mataifa (League of Nations) kwa ajili ya uangalizi. Waingereza walipanua mfumo wa KAR na kujumuisha Tanganyika na kuwa na vikosi sita ambapo vikosi viwili vilikuwa Kenya, vitatu vilikuwa Tanganyika na kimoja kilikuwa Uganda. Jeshi hili lilikuwa na vikosi vya askari wa miguu; wataalamu wa medani, mawasiliano, mizinga; na vikosi vya huduma. Watu waliojiunga na jeshi hili walitoka makabila mbalimbali na lugha iliyokuwa ikitumika jeshini kuwaunganisha ilikuwa Kiswahili. Askari hawa walisaidia kueneza Kiswahili kwa sababu kila walipokwenda walikuwa wakizungumza Kiswahili. Kwa kufanya hivyo, Kiswahili kilikua na kuenea zaidi.

**(d) Harakati za kisiasa**

Baada ya Vita vya Pili vya Dunia mwaka 1939 -1945, mataifa mengi ya Afrika yalianzisha harakati za kudai uhuru. Katika harakati za kudai uhuru nchini Tanganyika, vyama vya siasa, kama vile TAA (baadaye TANU) pamoja na Umoja wa Vijana wa TANU (TANU Youth League - TYL), viliundwa. Lugha ya Kiswahili ilikuwa nguzo na chombo muhimu sana. Kiswahili kilitumika kuwaunganisha Watanganyika ambao walikuwa na lugha tofautitofauti kushiriki katika harakati za kudai uhuru kutoka kwa wakoloni. Viongozi wa TANU, wakiongozwa na Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, walitumia Kiswahili katika mikutano yao ya kuhamasisha watu kujiunga na TANU. Lugha ya Kiswahili iliweza kuunganisha mawazo, fikira, na mambo mbalimbali yaliyokuwa yakifanywa na chama cha TANU. Lugha ya Kiswahili ndiyo ilikuwa alama ya umoja, uzalendo, Utanganyika, na uhuru; hata wito wa chama ukawa UHURU NA UMOJA. Kwa kutumia Kiswahili katika harakati za kudai uhuru na shughuli za chama, lugha hiyo ilikua na kuenea.

**(e) Shirika la uchapishaji na usambazaji wa vitabu**

Shirika hili lilijulikana kama "East African Literature Bureau (EALB)". Lilikuwa na jukumu la kuvichapa vitabu vyote vilivyokuwa vimeidhinishwa na Kamati ya Lugha ya Afrika Mashariki (Inter-Territorial Language (Swahili) Committee).

FOR ONLINE READING ONLY

Pamoja na ukweli kwamba Kiswahili kilikua na kuenea nchini Tanganyika, Kulikua na changamoto zilizoathiri matumizi ya Kiswahili nchini. Baadhi ya changamoto hizo ni baadhi ya wamisionari kutumia lugha za kikabila katika kueneza dini, hususani katika maeneo ya bara, na kuanzisha vyombo vya habari vilivyotumia lugha za kikabila. Aidha, baadhi ya wananchi hawakupenda kutumia Kiswahili kwa kuwa walikihusisha na vibaraka wa wakoloni (maakida, majumbe na maliwali) na wengine waliamini kuwa Kiswahili ni lugha ya Waislamu.

### Zoezi la 4.1

1. Kwa nini lugha za kijamii hazikuathiri kukua na kuenea kwa Kiswahili nchini Tanganyika?
2. Kiswahili kingeathirikaje nchini Tanganyika iwapo shughuli za uzalishaji mali zisingetilia mkazo matumizi ya lugha hiyo?
3. Unafikiri ni kwa nini lugha ya Kiswahili ilihusishwa na vibaraka wa wakoloni nchini Tanganyika?

**Kukua na kuenea kwa Kiswahili nchini Kenya kabla ya uhuru**

Kukua na kuenea kwa Kiswahili nchini Kenya kunaweza kutazamwa kwa kuzingatia sababu tatu ambazo ni biashara, dini, na elimu.

**(a) Biashara**

Kiswahili kilienea katika eneo la bara ya Kenya kabla ya ujio wa wakoloni. Kuenea kwa Kiswahili wakati huo kulichochewa na wafanyabiashara mbalimbali waliokuwa wanatoa bidhaa bara na kwenda kuziuza Mombasa, mji uliokuwa wa Waswahili. Bidhaa maarufu zilikuwa pembe za ndovu na watumwa. Miji mingine iliyohusika katika biashara hii ni Takaungu, Malindi na Lamu, ambayo yote ipo katika Pwani ya Kenya. Biashara zingine zilizofanyika Mombasa ni mboga na matunda ambayo yalikuwa yakizalishwa katika maeneo ya Kisauni, Changamwe, Mtongwe, na Likoni. Wafanyabiashara hawa walitumia Kiswahili kama lugha yao ya mawasiliano. Walipotoka pwani, walikieneza bara hadi maeneo ya Mumiasi (taz. Kielelezo Na. 4.1). Kufanya hivyo kulisaidia kuenea kwa lugha ya Kiswahili.

**(b) Dini**

Ujio wa wamisionari ulizidi kuchochea kukua na kuenea kwa Kiswahili. Kwa mfano, Johann Ludwig Krapf na Johannes Rebman walianzisha makazi katika eneo la Raban mwaka 1846. Walijifunza lugha, fasihi, na utamaduni wa Waswahili. Shughuli za uenezaji na ukuzaji wa Kiswahili zilishika kasi baada ya ujio wa shirika la Church Missionary

FOR ONLINE READING ONLY

Society (CMS) lililoongozwa na Johann Ludwig Krapf. Shirika hili lilikuwa na makao yake makuu Mombasa. Mwaka 1876, shirika hili liliandika kitabu cha kwanza cha sarufi ya Kiswahili kwa lahaja ya Kimvita. Kitabu hiki kiliitwa **Outline of the Elements of the Kisuaheli Language with Special Reference to the Kinika Dialect**. Shughuli zote hizi zilisaidia kukuza na kueneza Kiswahili nchini Kenya.

### *(c) Elimu*

Nchini Kenya, Kiswahili kilitumika katika ngazi za chini za elimu ya msingi kama lugha ya kufundishia katika shule zilizo kwenye maeneo ya Waswahili kama vile Mombasa. Ingawa tume mbalimbali za elimu, ikiwemo Tume ya Phelps-Stokes, zilipendekeza matumizi ya lugha za jamii katika kutoa elimu, ilikuwa vigumu kupata walimu na machapisho katika lugha hizo. Hivyo, Kiswahili kiliendelea kutumika kama lugha ya kufundishia na ya mawasiliano. Hali hii ilisaidia kukua na kuenea kwa Kiswahili nchini humo kwa wakati huo.

### *(d) Mchango wa jeshi la KAR*

Mbali na biashara, dini na elimu, Kiswahili nchini Kenya kilienezwa pia na Jeshi la KAR. Wanajeshi na wafanyakazi wengine waliokuwa chini ya KAR walilazimishwa kufanya mitihani ya Kiswahili. Ili waweze kufaulu mitihani hiyo, walilazimika kujua vizuri sarufi ya Kiswahili. Jitihada za kutaka kufaulu mitihani zilichochea uimarishaji wa stadi ya kuzungumza Kiswahili kwa ufasaha.

Kwa ujumla, Waingereza ndio waliofanya kazi kubwa ya kukuza lugha ya Kiswahili wakilinganishwa na Wajerumani. Katika kipindi hicho, matumizi ya Kiswahili yalipanuka sana. Hata hivyo, kukua na kuenea kwa Kiswahili nchini Kenya kulikumbwa na changamoto anuwai. Miongoni mwa changamoto hizo ni upinzani wa lugha za kikabila na Kiingereza katika elimu, kuzuiwa kwa misafara ya biashara iliyokuwa inatoka pwani kwenda bara, na baadhi ya Wakenya kutokipenda Kiswahili kwani walikihusisha na Uislamu.

### *Zoezi la 4.2*

1. Lugha za kijamii ziliathiri vipi kukua na kuenea kwa Kiswahili nchini Kenya?
2. Kwa kutumia vyanzo vya maktabani na mtandaoni, eleza mchango wa dini katika kukuza Kiswahili nchini Kenya kabla ya uhuru.
3. Ukiondoa dini, eleza mambo mengine yaliyochochea kukua na kuenea kwa lugha ya Kiswahili nchini Kenya kabla ya uhuru.

FOR ONLINE READING ONLY

**Kukua na kuenea kwa Kiswahili nchini Uganda kabla ya uhuru**

Nchini Uganda, Kiswahili kilianza kukua na kuenea katika karne ya 19. Waarabu ndio walioeneza lugha hiyo kwa kuanzisha shughuli za biashara na kueneza dini ya Kiislamu. Pia, Waarabu walikuwa wakitembelea ikulu ya Kabaka wa Buganda mara kwa mara. Baada ya ujio wa Waarabu, Kiswahili kilianza kutumika katika mabaraza ya kifalme katika himaya za Buganda na Bunyoro. Aidha, Wamisionari wa Church Missionary Society na White Fathers walitumia Kiswahili kuwasiliana na serikali pamoja na kueneza dini ya Kikristo. Walitumia Kiswahili kwa vile walikuta tayari kinatumika katika shughuli mbalimbali. Aidha, lugha ya Kiswahili ilienea sana Kaskazini mwa Uganda ikilinganishwa na sehemu zingine, kwa sababu ilikuwa inatumiwa na wanajeshi wengi katika mawasiliano yao.

Mnamo mwaka 1925 -1926, serikali ya kikoloni, kupitia idara ya elimu, ilipitisha uamuzi kuhusu lugha ya kufundishia katika madarasa ya mwanzo ya shule za msingi. Iliamuliwa kuwa Kiganda kitumike Buganda na sehemu ya kaskazini ya jimbo la Mashariki, eneo lililokuwa likitumia lugha za Kibantu. Kwa upande mwingine, Kiacholi kiliamuliwa kitumike katika Jimbo la Kaskazini, ambako lugha kuu ni za Kinailoti halafu Kiateso kitumike katika Jimbo la Kati.

Matumizi ya lugha hizi yalikabiliwa na changamoto ya upatikanaji wa vitabu vya kufundishia, hali ambayo ilisababisha Kiswahili kipendekezwe kutumika kwa sababu vitabu vya lugha hiyo vilikuwa vinapatikana nchi jirani za Kenya na Tanganyika. Hivyo, ilipendekezwa kuwa Kiswahili kitumike kama lugha ya kufundishia na kama somo katika shule za msingi. Aidha, ilipendekezwa kuwa vitabu vya masomo kama afya, jiografia na kilimo viandikwe kwa Kiswahili. Hata hivyo, kwa miaka miwili ya mwanzo, wanafunzi walifundishwa kwa lugha zao za kwanza, na baada ya miaka hiyo ndipo Kiswahili kilitumika. Vituo vya elimu ya baada ya shule za msingi viliunga mkono sera mpya kuhusu Kiswahili. Kwa mfano, Shule ya Ufundi Kampala iliamua kutumia Kiswahili kama lugha ya kufundishia badala ya Kiingereza.

Mnamo mwaka 1927, juhudi za kukuza Kiswahili ziliendelezwa zaidi. Gavana William Gowers alishauri kwamba Kiswahili kikuzwe katika Jimbo la Mashariki isipokuwa Busoga, Bunyoro, Toro, Ankole na Buganda ambako lugha ya Kiganda ilitumika katika madarasa yote ya shule za msingi.

Mwaka 1928, Serikali ilianzisha chuo cha ualimu wa shule za msingi. Katika chuo hiki, Kiswahili kilitumiwa kama lugha ya kufundishia. Vilevile, Kiswahili kilifundishwa kwa mafanikio katika chuo cha ualimu cha Misheni ya CMS kilichoitwa ***Mukono,*** na chuo cha ualimu cha shirika la ***White Fathers*** kilichoitwa ***Bikira***.

Mnamo mwaka 1930, mradi mahususi wa kufundisha walimu wa vijijini kwa miaka

FOR ONLINE READING ONLY

miwili ulianzishwa. Katika kipindi hicho, vituo ishirini na tisa (29) vilianzishwa katika majimbo ya Mashariki, Kaskazini, na Magharibi. Vituo hivi vilifundisha masomo ya dini, kilimo, mbinu za ufundishaji, afya, na Kiswahili. Lengo kuu la kufundisha Kiswahili lilikuwa kuhakikisha kwamba walimu wa ngazi ya cheti watakaofaulu wawe wameandaliwa vya kutosha kufundisha Kiswahili katika shule zao.

Juhudi za kukuza Kiswahili ziliendelea mwaka hadi mwaka. Mathalani, mwaka 1934 Kamati Kuu ya CMS ya Dayosisi ya Elgon iliamua kwamba masomo yote katika chuo cha kidini na cha ualimu cha Bawanasi yafundishwe kwa Kiswahili. Uamuzi huo wa Kamati Kuu ulizihusu pia shule za msingi za misheni zilizokuwa katika maeneo yenye mchanganyiko wa lugha. Kwa hiyo, masomo yote katika shule hizo yalifundishwa kwa Kiswahili.

Mnamo mwaka 1936, Mkutano wa Wakurugenzi wa Elimu wa Kenya, Uganda, Tanganyika, na Zanzibar ulifanyika Makerere. Jambo muhimu lililojitokeza katika mkutano huo ni kuongeza nguvu katika matumizi ya Kiswahili nchini Uganda. Shule za kati zilizokuwa zinapokea ruzuku ya serikali zilianza kufundisha masomo yote kwa kutumia Kiswahili, isipokuwa Buganda na Busoga. Walimu Waganda wapatao hamsini walikuwa wakifundisha wanafunzi zaidi ya mia saba kwa kutumia Kiswahili.

Mwaka 1937 yalifanyika Mashindano ya uandishi wa Kiswahili. Mashindano hayo yalihusisha washiriki kumi na wanne, na saba kati yao walipata zawadi. Wanne kati ya waliopewa zawadi walikuwa Baganda. Hii inaonesha kuwa, pamoja na Buganda kutotumia Kiswahili kama lugha ya kufundishia katika shule zake, bado Baganda walikuwa wanatumia Kiswahili kwa kiwango cha kuwawezesha kushiriki mashindano ya uandishi wa Kiswahili na kushinda.

Kufikia mwaka 1944, sera ya lugha ilikuwa ikihimiza matumizi ya Kiswahili na lugha za kwanza. Lugha zilizokubaliwa kuwa lugha za kufundishia katika shule za msingi ni Kiganda, Kiswahili, Kinyoro, Kitooro, Kijaluo, Kiateso, na Kilugbara. Kiswahili kilikuwa kimeenea sana Kaskazini mwa Uganda kwa sababu kilikuwa kikitumiwa na wanajeshi wengi katika mawasiliano. Shule za serikali mbili (za pekee) ambako walikuwa wanasoma watoto wa askari polisi na magereza, zilitumia Kiswahili kama lugha ya kufundisha masomo yote.

Pamoja na mafanikio ya kukua na kuenea kwa Kiswahili nchini Uganda, juhudi za kukuza Kiswahili zilikwama kabisa mwaka 1952, pale ambapo serikali ilitangaza kutotumia Kiswahili katika shule zote za Uganda, isipokuwa shule za polisi na magereza na shule za watoto wao.

Changamoto zilizoathiri mchakato huo ni pamoja na Kiswahili kuhusishwa na dini ya

FOR ONLINE READING ONLY

Kiislamu; kufikiriwa kuwa ni lugha ya wanajeshi, ambao hawakuwa wastarabu; na kutoungwa mkono na Baganda, kwa lengo la kulinda lugha yao ya Kiganda. Vilevile, Baganda walipinga Kiswahili kwa sababu walikihusisha na dini ya Kiislamu. Aidha, matumizi ya Kiswahili yalipigwa marufuku kwa lengo la kuhimiza matumizi ya Kingereza. Kwa ujumla, kama ilivyokuwa kwa nchi ya Kenya, Waingereza ndio walifanya kazi kubwa ya kukuza Kiswahili nchini Uganda. Kadhalika, misafara ya biashara ilikuwa na mchango mkubwa nchini Uganda kama ilivyokuwa kwa Kenya na Tanganyika kwani ilikitoa schemu za pwani na kukipeleka schemu za bara kama inavyoonekana katika Kielelezo Na. 4.1.




*Kielelezo Na. 4.1:* **Ramani ya Afrika Mashariki ikionesha misafara ya biashara**

FOR ONLINE READING ONLY

## *Zoezi la 4.3*

1. Tathmini mchango wa dini katika kukua na kuenea kwa Kiswahili nchini Uganda kabla ya uhuru.
2. Linganisha kasi ya kukua na kuenea kwa Kiswahili nchini Tanganyika na nchini Uganda wakati wa ukoloni.
3. Eleza jinsi mabadiliko ya sera nchini Uganda yalivyochangia kukua na kuenea kwa Kiswahili nchini humo kabla ya huru?

## *Shughuli ya 4.2*

Kwa kutumia vyanzo mbalimbali, vikiwamo vya ki-TEHAMA, fafanua changamoto zilizoathiri kukua na kuenea kwa Kiswahili kabla ya uhuru katika kila nchi ya Afrika Mashariki.

### *Mchango wa vyombo vya habari katika kukuza na kueneza Kiswahili Afrika Mashariki kabla ya uhuru*

Katika nchi za Afrika Mashariki, vyombo vya habari vilivyokuza na kueneza Kiswahili vilikuwa vimeanza kujitokeza kabla ya uhuru, lakini havikuwa vingi kama ilivyo leo. Vyombo hivyo vya habari ni redio na magazeti.

#### *Redio*

Redio ilikuwa moja ya vyombo muhimu vya kueneza lugha ya Kiswahili. Vituo vya redio kama vile Tanganyika Broadcasting Corporation (TBC) na Redio Uganda vilikuwa vikitoa matangazo kwa Kiswahili. Matangazo haya yalisaidia sana katika kukuza matumizi ya Kiswahili miongoni mwa jamii za Afrika Mashariki.

#### *Magazeti*

Magazeti yalikuwa miongoni mwa vyombo vya habari vilivyokuwa vikieneza Kiswahili katika nchi za Afrika Mashariki. Magazeti kama vile "Tanganyika Standard" na "Mzalendo" yalitoa sehemu ndogo ya habari zao kwa Kiswahili. Ingawa sehemu kubwa ya habari za magazeti haya ilikuwa kwa Kiingereza, magazeti haya yalikuwa muhimu katika kukuza na kueneza ujuzi wa lugha ya Kiswahili.

## *Zoezi la 4.4*

1. Kwa kutumia mifano, eleza umuhimu wa redio katika kukuza na kueneza Kiswahili Afrika Mashariki kabla ya uhuru.
2. Kwa kutumia mifano maridhawa, pinga au unga mkono kauli hii: "Magazeti

FOR ONLINE READING ONLY

hayakuwa na mchango muhimu katika kukuza na kueneza Kiswahili kabla ya uhuru".

3. Pendekeza suluhisho la changamoto zilizojitokeza kutokana na matumizi ya magazeti katika kukuza na kueneza Kiswahili Afrika Mashariki kabla ya uhuru.

## *Kukua na kuenea kwa Kiswahili katika nchi za Afrika Mashariki baada ya uhuru*

### *Shughuli ya 4.3*

Kwa kutumia vyanzo mbalimbali, vikiwamo vya kiTEHAMA, tathmini namna taasisi na asasi mbalimbali zilizopo kwa sasa zinavyochangia kukua na kuenea kwa Kiswahili katika nchi za Afrika Mashariki.

*Kukua na kuenea kwa Kiswahili nchini Tanzania*

Baada ya kupata uhuru mwaka 1961, Tanganyika ilihitaji kujenga utaifa kwa kuimarisha mawasiliano baina ya serikali na wananchi wake. Lugha ya Kiswahili ilihitajika zaidi ili kukidhi haja hii kwa sababu lugha za jamii zisingekidhi haja ya kujenga utaifa na maendeleo ya nchi nzima. Pia, lugha za kigeni kama vile Kiingereza na Kijerumani hazikuweza kutumika kutokana na wananchi wengi kutozimudu. Kwa hiyo, Serikali ya Tanganyika ilichukua hatua mbalimbali zilizoongeza kasi ya kukua na kuenea kwa Kiswahili. Miongoni mwa hatua hizo ni kukifanya Kiswahili kuwa lugha ya taifa na lugha rasmi; kukitumia katika utawala, elimu, vyombo vya habari, vikundi vya sanaa, na shughuli za biashara; na kuunda vyombo vya kukuza na kueneza Kiswahili.

*1. Kiswahili kuwa lugha ya taifa na lugha rasmi*

Baada ya Tanganyika kupata uhuru, Rais Julius K. Nyerere alihutubia bunge kwa mara ya kwanza kwa lugha ya Kiswahili tarehe 10/12/1962. Tukio hili liliamsha ari ya kutumia lugha ya Kiswahili na kusababisha viongozi wa serikali kutoa matamko mbalimbali kuhusu matumizi ya lugha ya Kiswahili. Mnamo Februari 1963, Serikali ya Tanganyika, kupitia Gazeti la Serikali, ilitangaza kuwa Kiswahili kitakuwa lugha ya taifa na lugha rasmi itakayotumika katika shughuli zote za kiserikali. Jukumu la kusimamia maendeleo ya Kiswahili liliwekwa chini ya Wizara ya Utamaduni wa Taifa na Vijana.

Visiwani Zanzibar, Serikali ilichukua hatua madhubuti za kukuza na kueneza Kiswahili siku tisa tu baada ya Mapinduzi ya mwaka 1964, ambapo ilikitangaza Kiswahili kuwa lugha ya taifa na rasmi. Uamuzi huo mkubwa ulitangazwa kupitia gazeti la Serikali

FOR ONLINE READING ONLY

lililoitwa *Kweupe*. Serikali iliunda Halmashauri ya Kiswahili iliyopewa jukumu la kuanzisha matumizi ya Kiswahili katika wizara, idara na mashirika ya umma. Vilevile, Serikali ya Mapinduzi ilitoa agizo la kupiga marufuku matumizi ya Kiingereza katika shughuli za kiserikali na, hivyo, kukipa Kiswahili nafasi.

**2. Kiswahili katika utawala**

Baada ya Kiswahili kutangazwa kuwa lugha ya taifa na lugha rasmi, hatua mbalimbali zilichukuliwa kuhakikisha kuwa lugha hii inatumiwa katika shughuli za kiutawala. Kuanzia miaka ya 1960, Serikali ilitoa uamuzi kuwa watumishi wa Serikali wanaoajiriwa sharti wawe na ujuzi au uwezo wa kutumia lugha ya Kiswahili ili waweze kuwasiliana na wananchi katika kutoa huduma stahiki wawapo kazini. Kwa upande wa Zanzibar, Serikali ilifuta sheria ya serikali ya kikoloni iliyokifanya Kiingereza kuwa lugha ya serikali. Aidha, ilipiga marufuku kuandika nyaraka kwa Kiingereza katika ofisi za serikali.

Hatua za kuendeleza Kiswahili ziliungwa mkono na viongozi mbalimbali wa serikali, hasa kwa kutoa matamko yaliyokuwa yanalenga kukuza Kiswahili. Mnamo Februari 1967, aliyekuwa Waziri Mkuu na Makamu wa Pili wa Rais wa Serikali ya Awamu ya Kwanza, Rashid Mfaume Kawawa, alitoa tamko lililoelekeza viongozi na watumishi kutumia Kiswahili na kuepuka kuchanganya lugha wakati wa mawasiliano rasmi.

Mwaka 1974, aliyekuwa Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais (Utumishi), Bw. J.D. Mganga, alitoa Waraka wa Utumishi Na. 1 wa 1974 ulioeleza kuhusu matumizi ya Kiswahili katika ofisi za Serikali kwa kutilia mkazo mambo yafuatayo:

(i) Mawasiliano ya barua kati ya wizara na idara yafanywe kwa lugha ya Kiswahili isipokuwa kama barua itaandikwa kwa (na) mtu ambaye si Mtanzania.

(ii) Vibao vyote vya majina ya ofisi au wizara, na matangazo kama ya mahafali na sikukuu za kitaifa viandikwe kwa Kiswahili.

(iii) Madokezo yote baina ya maafisa na fomu zote zijazwe kwa Kiswahili.

Hatua za kukuza Kiswahili hazikuishia katika awamu ya kwanza. Ziliendelea hata katika awamu ya tatu. Mathalani, mnamo Mei 2005, Serikali, kupitia Wizara ya Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Uratibu na Bunge), iliagiza kuwa taarifa za mikutano, semina, na warsha zitolewe kwa lugha ya Kiswahili kwa manufaa ya wananchi. Vilevile, iliagiza kuwa taarifa za miradi inayohusu wananchi, vipeperushi, na nyaraka zitolewe kwa Kiswahili.

Aidha, katika awamu ya nne, jitihada za kukuza Kiswahili ziliendelea kushika hatamu. Mnamo Februari 2010, aliyekuwa Makamu wa Rais, Dkt. Ali Mohamed Shein, katika

FOR ONLINE READING ONLY

kikao cha Baraza la Mawaziri, alisisitiza matumizi ya lugha ya Kiswahili katika shughuli za serikali na kukumbusha watendaji wa serikali kuzingatia waraka wa mwaka 1967 uliotolewa na Waziri Mkuu na Makamu wa Pili wa Rais. Vilevile, Mnamo Aprili 2010, serikali, kupitia Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo, iliagiza Kiswahili kitumike katika dhifa mbalimbali za kitaifa, hotuba, warsha, semina, mikutano ya kitaifa, majina ya barabara, mitaa, na mabango yanayohusu matangazo ya serikali. Katika agizo hilo, maafisa wa serikali na mashirika ya umma walitakiwa pia kutumia Kiswahili katika shughuli za kiutawala.

Pia, agizo hilo lilitaka Kiswahili kitumike katika matangazo na nyaraka zilizobandikwa kwa ajili ya umma. Aidha, sheria zilitakiwa ziandikwe kwa Kiswahili na zile zilizoandikwa kwa lugha za kigeni zitafsiriwe. Zaidi ya hayo, jitihada za makusudi zilitakiwa zifanyike ili shughuli za mahakama ziendeshwe kwa Kiswahili katika ngazi zote. Mijadala inayohusu shughuli za umma, ukiwamo usaili, ilielekezwa iendeshwe kwa Kiswahili na kumbukumbu za mijadala hiyo ziandikwe kwa Kiswahili.

Msukumo mpya wa kutumia Kiswahili katika shughuli zote za kiutawala ulijitokeza baada ya kuanza kwa utawala wa serikali ya awamu ya tano ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Rais wa awamu hii, Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli alijenga desturi ya kuendesha mikutano yote ya kitaifa na kimataifa kwa lugha ya Kiswahili. Kwa mfano, mnamo tarehe 29.01.2017, Hayati Magufuli alihutubia mkutano wa Umoja wa Afrika kwa lugha ya Kiswahili. Mkutano huo uliambatana na hafla ya uzinduzi wa jengo la Kituo cha Mwl. Nyerere, Addis - Ababa (Ethiopia). Uamuzi huu uliitikiwa vizuri na viongozi wengine waandamizi wa serikali na mashirika ya umma. Matumizi ya Kiswahili katika shughuli za utawala yameendelea kukuza na kueneza Kiswahili.

*3. Kiswahili katika elimu*

Baada ya uhuru, mfumo wa elimu uliendelea kama ulivyokuwa wakati wa Mwingereza. Katika mfumo huo, Kiswahili kilitumika kufundishia masomo yote katika elimu ya msingi (darasa la I - IV). Mfumo huo ulibadilika mwaka 1967 baada ya kutangazwa kwa Azimio la Arusha lililotangazwa sambamba na Sera ya Ujamaa na Kujitegemea. Katika kipindi hicho, mabadiliko makubwa yaliyotokea katika elimu ni kutangazwa rasmi kwa matumizi ya Kiswahili kama lugha ya kufundishia masomo yote ya elimu ya msingi, isipokuwa Kiingereza. Kwa upande wa elimu ya sekondari, Kiswahili kilitangazwa kuwa somo la lazima kwa kidato cha I - IV na kufundishia somo la siasa.

Vilevile, Kiswahili kilitumika kufundishia katika vyuo vya ualimu, utumishi wa umma, na maendeleo ya jamii. Aidha, Serikali ilianzisha Elimu ya Watu Wazima (EWW) ili kupambana na ujinga. Madhumuni ya EWW yalikuwa kuwapa fursa watu wazima

FOR ONLINE READING ONLY

ambao hawakupata nafasi ya kwenda shuleni kujifunza kusoma na kuandika. Lugha iliyotumika kufundishia EWW ilikuwa Kiswahili. Aidha, vitabu vyote vilivyotumiwa kufundishia EWW viliandikwa kwa Kiswahili. Hatua hii ilisaidia sana kukuza na kueneza lugha ya Kiswahili.

Baadaye, Kiswahili kilianza kufundishwa kama moja ya masomo ya kidato cha V na VI. Serikali iliruhusu somo la Kiswahili lifundishwe ngazi ya chuo kikuu kuanzia mwaka 1970 ambapo lilianza kufundishwa katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Kiswahili kimeendelea kufundishwa kama somo katika vyuo vikuu mbalimbali vilivyoanzishwa baada ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kama vile Chuo Kikuu cha Mt. Yohana cha Tanzania, Chuo Kikuu cha Waislamu Morogoro, Chuo Kikuu cha Arusha, na Chuo Kikuu cha Mtakatifu Agustino. Pia, programu za shahada za Kiswahili, kuanzia shahada za awali hadi uzamivu, zimeanzishwa katika Chuo Kikuu cha Dodoma, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, na Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar. Matumizi ya Kiswahili katika elimu yamesaidia kukuza na kueneza Kiswahili kwa watu wengi zaidi.

**4. Vyombo vya habari**

Baada ya uhuru, vyombo mbalimbali vya habari vilivyokuwapo kabla ya uhuru vimeendelea kukuza Kiswahili. Vyombo vya habari vilivyokuwapo wakati wa kupata uhuru ni Redio Tanzania (Sauti ya Tanganyika) na magazeti mbalimbali. Aidha, vyombo vipya vya habari vimeendelea kuanzishwa, hasa baada ya kuanzishwa kwa sera ya soko huria. Redio ya Taifa pamoja na magazeti ya Uhuru na Mzalendo ya chama cha TANU (baadaye CCM) vimekuwa vikifanya kazi kubwa ya kutoa habari, kuelimisha, na kuburudisha jamii ya Watanzania kwa kutumia Kiswahili. Kwa mfano, Redio ya Taifa, ambayo imekuwa ikitoa matangazo yake kwa Kiswahili, imekuwa ikisikika nchi nzima. Serikali imekuwa ikiitumia kutoa matangazo na taarifa mbalimbali za utendaji wake kwa wananchi. Licha ya kurusha matangazo yake kwa Kiswahili imekuwa na vipindi maalumu kwa ajili ya lugha ya Kiswahili. Mfano wa vipindi hivyo ni Kiswahili Lugha Yetu na Lugha ya Taifa. Kupitia vipindi hivi, mijadala mbalimbali inayohusu lugha ya Kiswahili hufanyika. Kuwepo kwa vipindi vya michezo, kampeni za kitaifa kama vile Mtu ni Afya, Chakula ni Uhai, na Kupanga ni Kuchagua zilisaidia kukuza na kueneza Kiswahili. Kwa upande wa Tanzania Visiwani, Sauti ya Tanzania Zanzibar imekuwa ikitoa matangazo yake kwa lugha ya Kiswahili. Kituo hiki cha redio husikika katika Visiwa vya Pemba, Unguja, na baadhi ya maeneo ya Tanzania Bara. Idhaa ya Taifa hujiunga na kituo hiki kila siku saa 1:00 jioni kurusha taarifa ya habari.

Baada ya kuanzishwa kwa sera ya soko huria, vituo kadhaa vya redio vilianzishwa. Vituo hivyo ni kama vile Radio One Stereo, Radio Free Africa (RFA), Radio Tumaini, Radio Clouds, Radio Times, Radio EFM, Praise Power Radio, Wapo FM, Radio Imani,

FOR ONLINE READING ONLY

Radio Abood, Radio Maria, Radio Kwizera, Radio Mlimani na kadhalika. Vituo hivi hutoa matangazo yake kwa Kiswahili na husaidia kukuza Kiswahili. Baadhi ya vituo hivi vina vipindi maalumu vya lugha ya Kiswahili. Mfano wa vituo hivi ni Radio One Stereo, ambayo hurusha kipindi maalumu cha Kiswahili kinachoitwa Kumepambazuka Kiswahili. Aidha, Radio Clouds ina utaratibu wa kuteua msamiati wa siku kila siku na kuufafanua (kila baada ya saa kwa siku nzima). Pia, Serikali, kupitia Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI), imekuwa na mkakati wa kuanzisha vituo vya redio ambavyo hutangaza kwa lugha ya Kiswahili katika kila halmashauri za wilaya, miji, na majiji. Mifano ya vituo hivyo ni vile vinavyomilikiwa na Halmashauri ya Jiji la Mbeya na Halmashauri ya Jiji la Tanga.

Vyombo vingine vilivyosaidia kukuza na kueneza Kiswahili ni magazeti. Kama ilivyodokezwa mwanzoni mwa sehemu hii, magazeti ya mwanzo yalimilikiwa na chama cha TANU. Magazeti haya yalisomwa kwa hamasa kubwa sana. Wakati huo, kipimo cha usomi na maendeleo kilikuwa kusoma magazeti. Kwa hiyo, kila mtu alijitahidi kujifunza kusoma ili aweze kusoma magazeti kwa lengo la kuonekana msomi. Kwa njia hiyo, watu wengi walijifunza Kiswahili na, hivyo, kukifanya kikue na kuenea. Pia, magazeti mengine mengi yalianzishwa kutokana na sera ya soko huria. Baadhi ya magazeti hayo ni **Habari Leo** na **Habari Leo Jumapili** (serikali), **Mwananchi**, **Nipashe**, **Tanzania Daima**, **Majira, Jamhuri**, *Zanzibar Leo*, **Rai**, **Raia Mwema**, **Mwanahalisi**, **Kulikoni**, **Spoti Starehe**, **Dimba**, **Mwanaspoti**, **Sayari**, **Tanzania Yetu**, **Simba**, na **Yanga**. Magazeti haya huchapishwa kwa Kiswahili na kusambazwa nchi nzima. Baadhi ya magazeti haya yana makala maalumu kuhusu Kiswahili na maendeleo yake. Magazeti hayo ni pamoja na toleo la Jumatano la gazeti la Mwananchi, ambalo hutoa ukurasa maalumu wa lugha ya Kiswahili. Aidha, toleo la Ijumaa la gazeti la Habari Leo hutoa makala zinazohusu lugha ya Kiswahili na toleo la Jumanne hutoa mada inayofundisha Kiswahili kwa wageni.

Vyombo vingine vya habari ambavyo vimesaidia kukuza na kueneza Kiswahili ni televisheni. Tofauti na redio na magazeti, televisheni zilichelewa kidogo kuanza. Televisheni zimeanza kutumika mwishoni mwa miaka ya 1980 lakini mapinduzi makubwa ya vyombo hivi yametokea miaka ya 1990. Kituo cha mwanzo kilikuwa Televisheni Zanzibar (TVZ) na baadaye kikawa Zanzibar Broadcasting Corporation (ZBC) ambacho kinamilikiwa na Shirika la Utangazaji Zanzibar. Kituo hiki kimekuwa kikitangaza kwa lugha ya Kiswahili. Baadaye, kilipanua huduma kwa kuanzisha idhaa nyingine ya TVZ-2, ambayo baadaye ikaja kujulikana kama ZBC-2. Idhaa hii pia inatangaza kwa Kiswahili.

Vilevile, Serikali ilianzisha kituo cha Televisheni ya Taifa (TVT) Tanzania Bara ambacho baadaye kilibadilishwa jina na kuwa TBC1 baada ya kuwa chini ya Shirika

FOR ONLINE READING ONLY

la Utangazaji Tanzania. Kituo hiki hutangaza kwa Kiswahili. Licha ya kutangaza kwa Kiswahili, kimekuwa na vipindi maalumu vya lugha ya Kiswahili. Vipindi hivyo ni Lulu za Kiswahili na Ulimwengu wa Kiswahili. Vituo vingine vya televisheni vinavyotoa matangazo kwa Kiswahili vinamilikiwa na watu binafsi. Vituo hivyo ni pamoja na Independent Television (ITV), Star TV, Tumaini TV, Mlimani TV, Channel Ten, East Africa Television (EATV), TV1, Sibuka TV, na Azam TV.

Kutokana na maendeleo ya sayansi na teknolojia, kumekuwa na mapinduzi ya hali ya juu katika vyombo vya habari. Suala la mawasiliano na kupashana habari limechukua sura mpya, hasa baada ya kuibuka kwa mitandao ya mawasiliano ya kijamii kama baruapepe, tovuti, blogu, Facebook, WhatsApp, na Tweeter. Kwa sasa, mitandao hii hutumika kwa kiwango kikubwa kuliko redio, magazeti na televisheni, hususani katika mazingira ya mijini. Matumizi ya mitandao hii, kwa kiwango kikubwa, ni kupitia simumaizi. Mawasiliano katika mitandao hii hufanyika kwa lugha ya Kiswahili, hususani kwa watumiaji wa lugha ya Kiswahili. Mbali na mawasiliano, katika mitandao hii, kuna makala na machapisho yanayohusu lugha ya Kiswahili. Makala na machapisho hayo husaidia watu kupata maarifa yanayohusu lugha ya Kiswahili. Aidha, wajifunzaji wa Kiswahili kama lugha ya kigeni huweza kunufaika kwa kujifunza Kiswahili kwa njia ya mtandao.

**5. Biashara**

Biashara ni sekta inayogusa karibu watu wote katika jamii. Sekta ya biashara imeendelea kukua siku hadi siku sambamba na maendeleo ya sayansi na teknolojia. Nchini Tanzania, biashara ilianza kushamiri miaka ya 1980 mara baada ya kuanza kwa sera ya soko huria. Shughuli za biashara zimekuwa zikitumia Kiswahili kama lugha kuu ya mawasiliano. Licha ya kuwa lugha ya mawasiliano ya biashara, Kiswahili kinatumika katika vifungashio vya bidhaa pamoja na maelekezo ya matumizi ya bidhaa. Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba Tanzania (TMDA) inasisitiza kutoa maelezo yanayohusu bidhaa za dawa na chakula kwa Kiswahili. Aidha, matangazo mbalimbali ya biashara katika mabango, vipeperushi, na kwenye vyombo vya habari hutolewa kwa Kiswahili. Kwa njia ya biashara, Kiswahili kimepata maneno mbalimbali mapya.

Vilevile, Serikali ilifungua milango kwa wawekezaji wa nje kwenye sekta mbalimbali za biashara kama vile kampuni za simu, madini, utalii, na kilimo. Katika sekta hizi, watu hutangamana na kuwasiliana kwa kutumia Kiswahili. Kwa njia hii, watu wengi hujifunza Kiswahili ili waweze kuwasiliana. Pia, serikali huratibu maonesho ya biashara ya kimataifa kupitia Bodi ya Biashara za Nje. Maonesho hayo hujumuisha maonesho ya SABASABA, maonesho ya bidhaa za viwandani, maonesho ya viwanda vidogovidogo, maonesho ya mazao na bidhaa za kilimo (NANENANE), na maonesho

FOR ONLINE READING ONLY

ya nchi za nje kama vile Maonesho ya Syria na Maonesho ya Uturuki. Katika maonesho hayo, Kiswahili hutumika na, hivyo, hukua na kuenea.

**6. Kiswahili katika vikundi vya sanaa**

Baada ya uhuru, Kiswahili kimekua na kuenea kwa njia ya vikundi vya sanaa. Kazi za vikundi vya sanaa zilikuwa zikiratibiwa na chama na serikali, mashirika ya umma, na ofisi za utamaduni. Chama na serikali viliendeleza bendi ya muziki ya NUTA Jazz (JUWATA, OTTU na sasa Msondo Ngoma), na vikundi vingine kama vile vikundi vya Mzee Mwinamila na Tengulabei. Pia, Jumuiya ya Umoja wa Vijana ya chama cha TANU, na sasa CCM, ilianzisha bendi ya Vijana Jazz ambayo ilitumia Kiswahili.

Mashirika ya umma na majeshi pia yalikuwa na bendi za muziki na sanaa ambazo zilitumia lugha ya Kiswahili. Baadhi ya bendi hizo ni Tancut Almasi Orchestra, Bima Lee Orchestra, Washirika Muungano Star, UDA Jazz Band, Tanzania One Theatre (TOT), na DDC Mlimani Park Orchestra. Bendi nyingine ni Polisi Jazz (Vangavanga), National Service Jazz Band (Kimbunga Stereo), Mwenge Jazz (Wanapaselepa), na Magereza Jazz Band (Super Mnyanyuo).

Baadhi ya nyimbo pamoja na sanaa za maigizo vilitumika kuelezea sera za nchi kama vile *Ujamaa na Kujitegemea* na kuhamasisha utekelezaji wa kampeni mbalimbali za kiserikali kama vile *Usalama Barabarani na Uraia*, *Kilimo cha Kufa na Kupona* na *Mtu ni Afya*.

Vilevile, nyimbo hizo zilitumika na zinaendelea kutumika kuwapongeza viongozi wa kitaifa. Aidha, Serikali, kupitia Wizara ya Elimu, ilitoa fursa za kufundishwa sanaa mbalimbali kama maigizo, nyimbo, ngonjera, na mashairi shuleni. Maonesho ya kazi hizi yalifanyika katika maadhimisho ya kitaifa na katika mashindano yaliyokuwa yakiratibiwa kupitia wataalamu wa sanaa na fasihi pamoja na maafisa utamaduni wa wilaya na mikoa. Miongoni mwa mashindano hayo ni Umoja wa Michezo na Taaluma kwa Shule za Msingi Tanzania (UMITASHUMTA), Umoja wa Michezo Sekondari Tanzania (UMISETA), na Umoja wa Michezo na Sanaa Vyuo vya Elimu Tanzania (UMISAVETA) ambayo yamekuwa yakifanyika hadi ngazi ya taifa. Kwa ujumla, vikundi vya sanaa vimekuwa vikitumia lugha ya Kiswahili katika kuwasilisha kazi zake, hali ambayo inachangia kukua na kuenea kwa Kiswahili nchini.

FOR ONLINE READING ONLY

### Zoezi la 4.5

1. Eleza hatua zilizochukuliwa na Serikali ya Tanzania katika kukuza na kueneza Kiswahili baada ya uhuru.
2. Fafanua hatua zilizochukuliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kukuza

na kueneza Kiswahili Visiwani baada ya uhuru.

3. Pendekeza mikakati utakayoiweka ili kuzidi kukuza na kueneza lugha ya Kiswahili endapo utapewa nafasi ya kufanya maamuzi katika sekta ya elimu nchini Tanzania.

### *7. Vyombo vya kukuza na kueneza Kiswahili Tanzania baada ya uhuru*

Baada ya uhuru, hatua za kuunda vyombo mbalimbali kwa madhumuni ya kukuza na kueneza Kiswahili zilichukuliwa na serikali, mashirika ya umma pamoja na wapenzi wa Kiswahili. Vyombo vilivyoundwa kwa madhumuni hayo ni Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili (TUKI) na Idara ya Kiswahili ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Baadaye, asasi hizi ziliungana na kuunda Taasisi ya Taaluma za Kiswahili (TATAKI). Vyombo vingine vilivyoundwa ni pamoja na Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA), Taasisi ya Kiswahili na Lugha za Kigeni Zanzibar (TAKILUKI), Baraza la Kiswahili Zanzibar (BAKIZA), na Umoja wa Waandishi wa Vitabu Tanzania (UWAVITA). Katika sehemu hii, tutaangazia madhumuni, mafanikio, na changamoto za vyombo hivyo.

#### *(a) Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili (TUKI)*

Taasisi hii iliundwa mwaka 1964 kutokana na iliyokuwa Kamati ya Lugha ya Afrika Mashariki ya mwaka 1930, ikiwa sehemu ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Hii ilikuwa taasisi pekee iliyojishughulisha na uchunguzi wa Kiswahili.

*Madhumuni ya TUKI*

TUKI ilikuwa na madhumuni yafuatayo:

(i) Kufanya utafiti kuhusu lugha ya Kiswahili;

(ii) Kuwatia moyo watu wanaojishughulisha na uandishi wa vitabu kwa lugha ya Kiswahili;

(iii) Kushughulika na ukuzaji wa istilahi za Kiswahili na uandishi wa kamusi za taaluma mbalimbali;

(iv) Kuhariri vitabu na machapisho mengine;

(v) Kuhifadhi ufasaha wa lugha ya Kiswahili;

(vi) Kutafsiri maandishi yanayohitajika katika matumizi ya lugha ya Kiswahili;

(vii) Kushirikiana na serikali na vikundi vingine vilivyo na lengo la kustawisha lugha ya Kiswahili; na

(viii) Kutoa majarida na machapisho mbalimbali yanayohusiana na Kiswahili.

FOR ONLINE READING ONLY

**Mafanikio ya TUKI**

TUKI ilipata mafanikio yafuatayo:

(i) Kutoa kamusi mbalimbali kama vile *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*, *Kamusi ya Kiingereza – Kiswahili* na *Kamusi ya Kiswahili – Kiingereza*;

(ii) Kutoa jarida la Kiswahili ambalo huchapisha makala za taaluma ya isimu na fasihi ya Kiswahili ambalo lilikua likitolewa mara moja kwa mwaka;

(iii) Kuanzisha na kuchapisha jarida la Mulika kwa ajili ya matumizi ya walimu na wanafunzi wa shule za sekondari za Tanzania;

(iv) Kutoa kamusi za taaluma maalumu kama vile *Kamusi ya Fizikia, Baiolojia na Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugha*;

(v) Kukusanya na kuchapisha mashairi, hadithi, vitendawili, na methali;

(vi) Kuanzisha makavazi ya nyaraka mbalimbali zinazohusiana na lugha;

(vii) Kushirikiana na serikali pamoja na idara nyingine kama vile Idara ya Kiswahili (Chuo Kikuu cha Dar es Salaam), Taasisi ya Elimu na Wizara ya Utamaduni katika kazi mbalimbali kama vile kutafsiri sera na machapisho mbalimbali; na

(viii) Kuhifadhi baadhi ya mashairi ya zamani yaliyoandikwa kwa lugha ya Kiarabu.

**Changamoto za TUKI**

TUKI ilikabiliwa na changamoto zifuatazo:

(i) Uhaba wa fedha za kutekeleza majukumu yake. Hali hii ilisababisha baadhi ya kazi za taasisi kutofanyika kama ilivyopangwa. Mathalani, TUKI ilirithi miswada ya vitabu zaidi ya 800 kutoka Kamati ya Lugha ya Afrika Mashariki lakini ni miswada michache tu iliyofanyiwa kazi.

(ii) Mwamko mdogo wa watu wanaojishughulisha na uandishi wa vitabu kwa lugha ya Kiswahili.

(iii) Ukosefu wa maabara ya lugha na vifaa vya kuchanganulia lugha.

**(b) Idara ya Kiswahili ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam**

Idara hii ilianzishwa mwaka 1970. Baadaye Idara iliungana na TUKI kuunda TATAKI mwaka 2009. Hii ndiyo idara ya kwanza Afrika kutoa mafunzo ya elimu ya juu kwa lugha ya Kiswahili. Idara hii ilifanya kazi sambamba na TUKI. Madhumuni yake yalikuwa yafuatayo:

(i) Kutayarisha walimu kwa ajili ya kufundisha somo la Kiswahili katika ngazi ya elimu ya sekondari na vyuo ndani na nje ya nchi;

(ii) Kufanya tafiti mbalimbali kuhusu lugha ya Kiswahili na lahaja zake;

(iii) Kutoa msaada wa kitaalamu kuhusu lugha ya Kiswahili ulipohitajika ndani na nje ya nchi;

FOR ONLINE READING ONLY

(iv) Kuandaa wataalamu wa lugha ya Kiswahili kama watafiti, wafasiri, wakalimani na wanaleksikografia; na

(v) Kuanzisha na kuchapisha jarida la Kioo cha Lugha kwa ajili ya kuchapisha makala ya kitaaluma.

*Mafanikio ya Idara ya Kiswahili*

Idara ilipata mafanikio mbalimbali kama ifuatavyo:

(i) Kusimamia na kufundisha lugha ya Kiswahili kwa wageni;

(ii) Kuandaa walimu wa somo la Kiswahili wa kufundisha katika ngazi mbalimbali za elimu;

(iii) Kuandaa wataalamu wa lugha ya Kiswahili kwa ajili ya taasisi mbalimbali kama BAKITA na BAKIZA;

(iv) Kushirikiana na TUKI kuandaa machapisho mbalimbali ya lugha ya Kiswahili; na

(v) Kupeleka wahadhiri kufundisha Kiswahili katika vyuo vikuu vya nje ya nchi kwa mfano, Rwanda, Naijeria, na Ghana.

*Changamoto za Idara*

Katika kutimiza majukumu yake, Idara ilikabiliwa na changamoto mbalimbali kama ifuatavyo:

(i) Baadhi ya wataalamu wake kuacha kujishughulisha na lugha ya Kiswahili na kufanya kazi nyingine kama vile za utawala au siasa. Hivyo, kupunguza nguvukazi ya kufundisha na kuendeleza lugha ya Kiswahili.

(ii) Mtazamo hasi kuhusu kusoma Kiswahili. Baadhi ya watu walikuwa na mtazamo hasi na kuona kuwa Kiswahili ni somo lisilokuwa na masilahi. Kwa hiyo, watu wengi walikimbilia taaluma nyingine, hali ambayo ilipunguza wataalamu wa kukiendeleza Kiswahili.

*(c) Taasisi ya Taaluma za Kiswahili (TATAKI)*

Taasisi hii iliundwa mwaka 2009 kwa kuunganisha TUKI na Idara ya Kiswahili ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Lengo la kuunganisha taasisi hizi mbili lilikuwa kupanua wigo wa kukuza, kuendeleza na kustawisha lugha ya Kiswahili. Kwa hiyo, kuundwa kwa TATAKI kulipanua wigo wa kushughulikia mambo yote yanayohusiana na lugha ya Kiswahili. TATAKI ina idara kuu mbili za kitaaluma ambazo ni Idara ya Lugha ya Kiswahili na Isimu (ILUKI), na Idara ya Fasihi, Mawasiliano na Uchapishaji (IFAMU).

FOR ONLINE READING ONLY

**Madhumuni ya TATAKI**

Ili kutimiza majukumu yake, TATAKI inaongozwa na madhumuni yafuatayo:

(i) Kufanya tafiti mbalimbali kuhusu lugha ya Kiswahili katika taaluma za isimu, fasihi na utamaduni wa Kiswahili;

(ii) Kufanya tafiti katika taaluma ya leksikografia, kuandaa na kuandika kamusi mbalimbali za lugha ya Kiswahili;

(iii) Kuratibu msamiati na kuunda istilahi anuwai za kitaaluma na kuziingiza katika kamusi;

(iv) Kuratibu na kutafsiri matini mbalimbali kutoka taasisi za serikali na zile zisizo za serikali;

(v) Kushirikiana na taasisi pamoja na asasi nyingine za kukuza na kueneza lugha ya Kiswahili;

(vi) Kutoa ushauri wa kitaalamu katika vipengele vya lugha, isimu na fasihi;

(vii) Kuandaa na kuchapisha vitabu na majarida ya Kiswahili kwa matumizi ya watu binafsi na taasisi mbalimbali ndani na nje ya nchi; na

(viii) Kuhakikisha kuwa Kiswahili kinakuwa na msingi imara kama lugha ya kufundishia kuanzia ngazi ya elimu ya awali hadi chuo kikuu.

**Mafanikio ya TATAKI**

Taasisi imefanikiwa katika nyanja mbalimbali kama ifuatavyo:

(i) Taasisi imedahili na kufundisha wanafunzi wa shahada za awali, umahiri, na uzamivu. Kila mwaka, kumekuwa na ongezeko la wanafunzi na hii husaidia kuongeza wataalamu wa lugha ya Kiswahili.

(ii) Taasisi imefanikiwa kuratibu na kusimamia ufundishaji wa lugha ya Kiswahili kwa wageni.

(iii) Taasisi imefanya tafiti mbalimbali kuhusu lugha ya Kiswahili na kuchapisha matokeo ya tafiti hizo katika vitabu na majarida ya taasisi na kwingineko.

(iv) Taasisi imefanikiwa kuendelea kuboresha kamusi mbalimbali zilizotolewa hapo awali. Kwa mfano, Taasisi imefanya maboresho ya *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* na *Kamusi ya Kiswahili - Kiingereza* mara kadhaa.

(v) Taasisi imetafsiri na inaendelea kutafsiri nyaraka mbalimbali za serikali na taasisi zake na za watu binafsi.

FOR ONLINE READING ONLY

(vi) Taasisi imeandaa semina, warsha na makongamano ya ndani ya taasisi na ya kimataifa.

(vii) Taasisi imepeleka wahadhiri kufundisha Kiswahili katika vyuo vikuu vya nje.

**Changamoto za TATAKI**

Pamoja na mafanikio yaliyotajwa hapo juu, TATAKI inakabiliwa na changamoto zifuatazo:

(i) Uhaba wa vifaa vya kisasa vya lugha vinavyoendana na kasi ya mabadiliko ya sayansi na teknolojia kama vile vifaa maalumu vya ukalimani na maabara ya lugha.

(ii) Kutosambaza machapisho yake kwa kiwango kinachostahili katika maeneo mbalimbali Afrika Mashariki.

**(d) Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA)**

Baraza la Kiswahili la Taifa liliundwa kwa sheria namba 27 ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1967. Hiki ndicho chombo cha juu kabisa kilichopewa dhamana ya kuratibu, kukuza na kueneza Kiswahili ndani na nje ya nchi. Mwanzoni, BAKITA lilikuwa limegawanyika katika idara tano (5) zilizohusu ukuzaji na uenezi wa Kiswahili. Idara hizo zilikuwa Idara ya Uhariri na Uchapishaji, Idara ya Lugha na Fasihi, Idara ya Tafsiri na Ukalimani, Idara ya Istilahi na Kamusi, na Idara ya Mawasiliano na Umma. Hata hivyo, mwaka 2019, yalifanyika mabadiliko yaliyounda Kurugenzi ya Maendeleo na Matumizi ya Kiswahili. Kurugenzi hiyo ina sehemu tatu ambazo ni Sehemu ya Tafsiri na Ukalimani; Sehemu ya Lugha, Fasihi na Uhariri; na Sehemu ya Istilahi na Leksikografia. Pamoja na jukumu la kuratibu shughuli zote za kukuza na kueneza Kiswahili, BAKITA lina madhumuni yafuatayo:

(i) Kusimamia na kuhimiza matumizi ya Kiswahili fasaha na sanifu;

(ii) Kufanya tafiti mbalimbali za lugha ya Kiswahili, kuchapisha matokeo ya tafiti hizo na kutunza kumbukumbu zinazohusiana na Kiswahili;

(iii) Kusanifisha istilahi za Kiswahili zinazohusiana na fani mbalimbali kama vile sheria, sayansi, tiba, utangazaji na ujenzi;

(iv) Kuweka mazingira mazuri kwa ajili ya maendeleo na matumizi ya Kiswahili nchini;

(v) Kushirikiana na asasi na vyombo vingine vinavyojihusisha na maendeleo ya Kiswahili ili kuinua hadhi ya lugha ya Kiswahili na matumizi yake kwa ujumla;

(vi) Kuchapisha majarida na vitabu vyenye miongozo ya matumizi ya Kiswahili sanifu;

FOR ONLINE READING ONLY

(vii) Kutoa huduma za tafsiri na ukalimani kwa taasisi mbalimbali ndani na nje ya nchi;

(viii) Kushauri, kuratibu na kufuatilia shughuli zote zinazohusu ukuzaji wa Kiswahili zinazofanywa na asasi, vyombo, na watu binafsi;

(ix) Kuainisha asasi na vyombo anuwai vinavyoratibu tafiti za Kiswahili nchini Tanzania;

(x) Kutoa majibu ya maswali mbalimbali yanayoulizwa kuhusu lugha na fasihi ya Kiswahili; na

(xi) Kupitia kazi za waandishi na wafasiri na kutoa ithibati ya lugha.

**Mafanikio ya BAKITA**

Baraza limekuwa na mafanikio katika vipengele vifuatavyo:

(i) Kuelimisha jamii kuhusu mambo mbalimbali yanayohusu matumizi ya lugha ya Kiswahili. Baraza limekuwa na vipindi mbalimbali kama vile Lugha ya Taifa (TBC-Taifa), Kumepambazuka Kiswahili (Radio One Stereo) na Ulimwengu wa Kiswahili (TBC1).

(ii) Kutoa ushauri kwa wanafunzi wa Kiswahili wanaoandika miradi na tasnifu mbalimbali kuhusu lugha ya Kiswahili kwa ngazi mbalimbali.

(iii) Kutafsiri kazi mbalimbali za lugha ya Kiswahili na lugha zingine za kigeni.

(iv) Kubainisha makosa ya lugha kutoka magazetini na vyombo vingine vya habari na vyanzo vingine na kutoa usahihi wake kwa jamii kupitia vyombo vya habari.

(v) Kutoa huduma za tafsiri na ukalimani serikalini, kwenye taasisi mbalimbali za umma na zisizo za umma na kwa watu binafsi.

(vi) Kupitia machapisho yanayoandikwa kwa Kiswahili kabla ya kuyatoa na kutoa ithibati ya lugha, mamlaka ambayo yanatokana na sheria iliyopitishwa na Bunge ya mwaka 1983.

(vii) Kutoa vitabu na kamusi za lugha ya Kiswahili. Kwa mfano, **Mwongozo kwa Waandishi wa Kiswahili Sanifu**, **Kiswahili** na **Utandawazi**, **Istilahi za Kiswahili**, **Kamusi ya Diplomasia** na **Kamusi Kuu ya Kiswahili** (KKK).

(viii) Kutoa mafunzo maalumu ya awali kuhusu lugha ya Kiswahili kwa wageni. Mpango huu ulianza Oktoba 2016.

(ix) Kuendesha semina, warsha na makongamano kuhusu taaluma mbalimbali za lugha ya Kiswahili. Ili kufanikisha suala hili, wawezeshaji hualikwa kutoka

FOR ONLINE READING ONLY

ndani au nje ya BAKITA kuendesha mafunzo hayo.

**Changamoto za BAKITA**

BAKITA limekuwa likikabiliwa na changamoto zifuatazo katika kutekeleza majukumu yake:

(i) Ari ndogo ya watu kupokea na kukubali mabadiliko mbalimbali pamoja na marekebisho yanayotolewa na Baraza kuhusu matumizi sahihi ya Kiswahili;

(ii) Baadhi ya waandishi kutopeleka machapisho yao BAKITA kwa ajili ya kupata ithibati ya lugha.

**(e) Taasisi ya Kiswahili na Lugha za Kigeni Zanzibar (TAKILUKI)**

Taasisi hii ilianzishwa mwaka 1979, makao yake makuu yakiwa mjini Unguja, Zanzibar. Taasisi hii ilikuwa chini ya Ofisi ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali. Kuanzia mwaka 2012, TAKILUKI ilibadilisha jina na majukumu na kuwa Skuli ya Kiswahili na Lugha za Kigeni (SKILUKI). Lengo kuu likiwa kutoa walimu bora wa taaluma za Kiswahili na lugha za kigeni kama vile Kiingereza, Kifaransa, Kiarabu, Kireno, na Kichina. Taasisi hii ina Idara kuu tatu ambazo ni Idara ya Kiswahili, Idara ya Kiswahili kwa Wageni na Idara ya Lugha za Kigeni.

**Madhumuni ya TAKILUKI**

TAKILUKI ilianzishwa kwa madhumuni yafuatayo:

(i) Kutoa mafunzo na kusimamia matumizi ya Kiswahili fasaha na sanifu kwa watumishi wa serikali na wananchi;

(ii) Kufanya tafiti za lahaja zote za Zanzibar na vipengele vya sarufi na fasihi;

(iii) Kufundisha Kiswahili kwa wageni na lugha za kigeni kwa wenyeji;

(iv) Kutayarisha na kuchapisha vitabu na majarida mbalimbali;

(v) Kutoa miongozo ya namna bora ya kutumia Kiswahili sanifu; na

(vi) Kufanya tafiti za tungo mbalimbali za kifasihi zenye asili ya Kiswahili na kuhifadhi taarifa zake.

**Mafanikio ya TAKILUKI**

Yafuatayo ni mafanikio ya TAKILUKI:

(i) Kukusanya taarifa anuwai kuhusu lugha ya Kiswahili na lahaja zake na kuzihifadhi;

FOR ONLINE READING ONLY

(ii) Kutoa mafunzo ya lugha ya Kiswahili kwa wageni na lugha za kigeni kwa wenyeji;

(iii) Kufanya tafiti kuhusu sarufi ya Kiswahili na tamaduni za jamii zinazoendana na lugha ya Kiswahili;

(iv) Kuchapisha vitabu vya lugha ya Kiswahili, mathalani, **Diwani ya Malenga Wapya**; na

(v) Kutoa mafunzo mbalimbali kwa watumishi wa serikali na watangazaji wa Shirika la Utangazaji la Zanzibar kuhusu matumizi ya Kiswahili sanifu.

**Changamoto za TAKILUKI**

TAKILUKI inakabiliwa na changamoto zifuatazo:

(i) Ugumu katika ukusanyaji wa data na taarifa za zamani za fasihi kutokana na jamii kutokuwa na utaratibu wa kuhifadhi taarifa za matukio ya zamani;

(ii) Uhaba wa vifaa vya kufanyia kazi kama vile vyombo vya usafiri ili kurahisisha safari za kitafiti; na

(iii) Uhaba wa fedha za uendeshaji wa shughuli za taasisi na kushindwa kutekeleza baadhi ya majukumu yake.

**(f) Baraza la Kiswahili Zanzibar (BAKIZA)**

Baraza hili lilianzishwa mwaka 1983 likiwa na jukumu la kuratibu shughuli zote za kukuza na kueneza Kiswahili Zanzibar. Hatua hii ilikuja baada ya kuona umuhimu wa kuhimiza matumizi ya lugha ya Kiswahili kwa wananchi wote. Baraza hili linashirikiana na serikali kuwaunganisha watu kwa ajili ya kushiriki katika shughuli za maendeleo ya Kiswahili.

**Madhumuni ya BAKIZA**

BAKIZA liliundwa kwa madhumuni yafuatayo:

(i) Kukuza na kueneza lugha ya Kiswahili visiwani Zanzibar;

(ii) Kusimamia matumizi ya Kiswahili sanifu ndani ya Baraza la Wawakilishi na vyombo vya habari kwa ujumla;

(iii) Kuandaa na kuchapisha kamusi na majarida mbalimbali;

(iv) Kupitia na kusanifu maandiko ya Kiswahili; na

(v) Kutoa huduma za tafsiri na ukalimani.

FOR ONLINE READING ONLY

*Mafanikio ya BAKIZA*
Baraza limefanikiwa katika vipengele vifuatavyo:

(i) Kusimamia matumizi ya Kiswahili sanifu katika vikao vya Baraza la Wawakilishi la Zanzibar

(ii) Kutoa ushauri na kusimamia matumizi ya Kiswahili sanifu katika vyombo vya habari vya Zanzibar

(iii) Kuendesha semina ya kuwakumbuka na kuwaenzi waandishi wakongwe wa Kiswahili Zanzibar kila mwaka. Kwa mfano, semina ya Machi 2017 ilikuwa ya kumkumbuka na kumwenzi mwandishi maarufu wa riwaya pendwa Mohamed Said Abdullah (Bwana Msa).

(iv) Kuandaa na kuchapisha kamusi mbalimbali za lugha ya Kiswahili kama vile Kamusi la Kiswahili Fasaha, Kamusi la Lahaja ya Kipemba na Kamusi la Lahaja ya Kimakunduchi

(v) Kutafsiri machapisho mbalimbali ya serikali na taasisi mbalimbali. Kwa mfano, Baraza limetafsiri miswada mbalimbali ya Baraza la Wawakilishi Zanzibar.

(vi) Kuandaa makongamano ya wasanii wa lugha ya Kiswahili

*Changamoto za BAKIZA*
BAKIZA limekuwa likikabiliwa na changamoto mbalimbali kama ifuatavyo:

(i) Upungufu wa raslimali fedha ikilinganishwa na majukumu na kazi za BAKIZA; na

(ii) Jamii na wataalamu kukosa hamu ya kununua na kusoma vitabu vya Kiswahili.

*(g) Umoja wa Waandishi wa Vitabu Tanzania (UWAVITA)*
Umoja huu ulianzishwa na waandishi wa vitabu vya Kiswahili mwaka 1978. Umoja huu ulianzishwa kwa lengo la kuwaunganisha waandishi ili wafanye kazi zao kwa ufanisi zaidi.

*Madhumuni ya UWAVITA*
Umoja huu ulianzishwa kwa madhumuni yafuatayo:

(i) Kutetea na kusimamia haki na masilahi ya waandishi wa vitabu vya Kiswahili;

(ii) Kuandaa warsha za kuwaelimisha waandishi kuhusu uandishi bora wa vitabu;

(iii) Kuandaa na kuwajulisha waandishi kuhusu mada mbalimbali zinazotakiwa kuandikiwa kulingana na mwelekeo na mahitaji ya jamii;

FOR ONLINE READING ONLY

(iv) Kukitangaza Kiswahili kwa njia ya mijadala na semina kupitia vyombo vya habari; na

(v) Kuamsha ari ya kusoma vitabu vya lugha ya Kiswahili.

*Mafanikio ya UWAVITA*

Yafuatayo ni mafanikio ambayo UWAVITA umeyapata tangu kuanzishwa kwake:

(i) Kuendesha semina mbalimbali kwa waandishi wa vitabu vya Kiswahili;

(ii) Kuongeza vitabu vya fani mbalimbali za Kiswahili kama vile vitabu vya hadithi za watoto, riwaya, tamthiliya, ushairi, na tahakiki; na

(iii) Kuandaa na kushiriki katika maonesho ya vitabu na kuhamasisha usomaji wa vitabu.

*Changamoto za UWAVITA*

Changamoto zinazoikabili UWAVITA ni:

(i) Mwamko mdogo wa kusoma vitabu katika jamii ya Watanzania. Hali hii huwakatisha tamaa waandishi kuendelea kuandika vitabu.

(ii) Kutokuwapo kwa umoja na mshikamano miongoni mwa waandishi na wachapishaji. Baadhi ya waandishi hawajiungi na UWAVITA, hali ambayo inadhoofisha nguvu ya umoja huo.

*Zoezi la 4.6*

1. Tathmini mchango wa vyombo vya habari vya sasa katika maendeleo ya lugha ya Kiswahili nchini Tanzania.
2. "Kuongezeka kwa machapisho ya Kiswahili kunasaidia kukua na kuenea kwa lugha hiyo nchini Tanzania". Jadili kauli hii kwa hoja zisizopungua sita.
3. Pendekeza mambo matano ambayo unaweza kuyafanya ili kutatua changamoto zinazozikabili BAKITA na BAKIZA.

*Maendeleo ya Kiswahili nchini Kenya baada ya uhuru*

Kenya ilipata uhuru mwaka 1963 kutoka kwa Waingereza. Mara baada ya uhuru, Kiswahili kilitangazwa kuwa lugha ya taifa nchini humo ingawa hakukuwa na sera wala sheria iliyohalalisha Kiswahili kuwa lugha ya taifa. Wakenya walikubali Kiswahili kuwa lugha yao ya mawasiliano, biashara, na utawala.

FOR ONLINE READING ONLY

Rais wa Kwanza wa Kenya alikuwa na nia ya kukuza na kueneza Kiswahili. Hili lilidhihirika alipohutubia kwa lugha ya Kiswahili wakati wa ufunguzi wa Bunge la Jamhuri ya Kenya tarehe 14.12.1964. Ingawa hapakuwa na sera wala sheria ambazo zilihalalisha Kiswahili kuwa lugha ya taifa, Rais Jomo Kenyatta alitoa tangazo la kusisitiza kuwa Kiswahili ni lugha ya taifa mwaka 1974. Tamko hilo lilihimiza matumizi ya Kiswahili katika shughuli za kiserikali na bungeni. Mnamo Julai mwaka 1974, Bunge lilipitisha uamuzi wa kutumia lugha ya Kiswahili katika vikao vyake. Rais Jomo Kenyatta alitumia lugha ya Kiswahili kila alipofanya mikutano na wananchi mijini na vijijini. Kupitia hotuba zake kwa Wakenya, Rais alitia hamasa kwa watu wa Kenya kuendelea kujifunza lugha ya Kiswahili. Juhudi za kurasmisha Kiswahili kuwa lugha ya taifa zimeendelea kuzaa matunda ambapo mwaka 2010, katika mabadiliko ya katiba, Kiswahili kilitambuliwa kuwa lugha ya taifa katika ibara ya saba ya katiba hiyo.

Hatua nyingine ya mafanikio ilikuwa matumizi ya lugha ya Kiswahili katika elimu. Mwaka 1963, Serikali iliunda tume ya kutafiti lugha inayofaa kutumika katika elimu. Lengo kuu lilikuwa kukusanya maoni kutoka kwa wananchi kuhusu matumizi ya lugha ya Kiswahili au lugha nyingine katika elimu. Tume hiyo ilipeleka mapendekezo kuwa Kiswahili kifundishwe kama somo bila kutahiniwa. Mapendekezo mengine yalikuwa kuanzishwa kwa Idara ya Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Nairobi, kuendesha mafunzo maalumu ya lugha ya Kiswahili kwa walimu wa shule za msingi, na kufundisha kozi maalumu za Kiswahili kwa wakufunzi wa vyuo vya ualimu.

Tume zingine zilizoundwa ni ya Wamalwa mwaka 1970, ya Gachathi mwaka 1976, na ya Mackay mwaka 1981 - 1982. Tume ya Wamalwa ilipendekeza kuwa kozi za Kiswahili zianzishwe katika taasisi ya usimamizi wa watumishi, na taasisi ya kutoa mafunzo kwa watumishi wa umma. Tume ya Gachathi ilipendekeza kuwa Kiswahili kiwe somo la lazima na la kutahiniwa katika shule za msingi, upili na vyuo vikuu. Pia, ilipendekeza utoaji wa mafunzo ya Kiswahili kwa walimu wa Kiswahili. Tume ya Mackay ilipendekeza Kiswahili kiwe somo la lazima katika shule za msingi na upili kote nchini, ambapo pendekezo hilo lilitekelezwa na, matokeo yake, Kiswahili kilikua na kuenea miongoni mwa Wakenya wengi. Hali kadhalika, tume hii ilipendekeza kuanzishwa kwa chuo cha upili na Kiswahili kufundishwa chuoni kama somo la lazima. Baadhi ya mapendekezo ya tume hizo yametekelezwa kwa ufanisi kuanzia mwaka 1985. Kiswahili kilifanywa kuwa somo la lazima la kutahiniwa katika shule za msingi na za upili. Kwa hiyo, mwanafunzi hutakiwa kupata alama za juu katika somo hilo ili aweze kujiunga na shule ya upili, vyuo vya mafunzo au vyuo vikuu.

Mafanikio mengine ya kukua na kuenea kwa Kiswahili nchini Kenya yalionekana kupitia vyombo vya habari. Baada ya uhuru, matangazo ya redio na televisheni yalianza kutolewa kwa Kiswahili. Kwa upande wa redio, Shirika la Utangazaji la

FOR ONLINE READING ONLY

Kenya (KBC) linalomiliki Redio ya KBC – Nairobi, ambayo hutangaza kwa Kiswahili, lilianzishwa. Redio ya KBC – Nairobi imekuwa na kipindi maalumu cha lugha ya Kiswahili kinachoitwa Lugha Yetu. Kipindi hiki hutoa elimu kuhusu matumizi sahihi ya lugha ya Kiswahili. Kituo kingine cha redio ambacho hutangaza kwa Kiswahili ni Radio Citizen.

Kwa upande wa televisheni, Shirika la Utangazaji la Kenya lina vituo vya televisheni ya KBC1 na televisheni ya KBC2 ambavyo hurusha matangazo yake kwa lugha ya Kiswahili. Televisheni nyingine ambayo hurusha matangazo kwa Kiswahili ni televisheni ya Citizen na televisheni ya K24. Televisheni nchini Kenya zina vipindi mbalimbali vya mijadala ya Kiswahili, ambavyo vina watazamaji na wasikilizaji wengi. Kupitia televisheni, Kiswahili kimekua na kuenea kwa kiwango kikubwa.

Magazeti pia yamesaidia kukuza na kueneza Kiswahili nchini Kenya. Mwaka 1975, serikali iliasisi mradi mkubwa wa kuandaa gazeti linaloitwa *Kisomo* ambalo lilikuwa linaandikwa kwa lugha ya Kiswahili. Gazeti hili lilichapishwa katika mji wa Mrunga na lilikuwa maalumu kwa ajili ya watu wa mashambani. Nakala elfu tano za gazeti hili zilitolewa kila mwezi. Mradi huu ulikua na kuendelea kiasi kwamba kufikia mwaka 1980 kukawa na magazeti zaidi ya 11 yaliyosomwa katika sehemu kubwa ya Kenya. Miongoni mwa magazeti hayo ni *Nyota ya Magharibi*, *Sauti ya Pwani*, *Sauti ya Gasi*, *Nyota ya Mashariki*, *Maarifa*, *Habari*, *Sauti ya Kericho*, *Mwongozo*, *Jicho*, na *Nuru*. Magazeti mengine ambayo hutumia lugha ya Kiswahili ni *Taifa Leo*, *Kenya Leo*, *Taifa la Pili*, na *Baraza*. Sambamba na hilo, kumekuwa na matumizi makubwa ya lugha ya Kiswahili katika mitandao ya kijamii. Kupitia magazeti na mitandao ya kijamii, watu wengi wamejifunza na kuendeleza hadhi ya lugha ya Kiswahili nchini Kenya.

**Vyombo vya kukuza na kueneza Kiswahili nchini Kenya**

Baada ya uhuru, Serikali ya Kenya ilichukua hatua mbalimbali za kukuza na kueneza Kiswahili kwa kuunda vyombo mbalimbali. Vyombo hivyo vilianzishwa na serikali, watu binafsi, na taasisi mbalimbali. Vyombo hivyo ni kama vile Chama cha Kiswahili cha Taifa (CHAKITA) na Idara mbalimbali za vyuo vikuu nchini Kenya. Miongoni mwa idara hizo ni: Idara ya Kiswahili Chuo Kikuu cha Kenyatta, Idara ya Kiswahili Chuo Kikuu cha Nairobi, Chama cha Walimu wa Kiswahili Mkoa wa Nairobi, na Chama cha Kiswahili Chuo Kikuu cha Mount Kenya.

**Chama cha Walimu wa Kiswahili Mkoa wa Nairobi**

Chama hiki kilianzishwa mwaka 1975 mjini Nairobi kikijumuisha walimu wa somo la Kiswahili wa mkoa huo. Mpango wa kuanzisha chama hicho ulifanywa kwa lengo la kuhamasisha wanafunzi wengi kusoma somo la Kiswahili. Walimu hawa walijipa

FOR ONLINE READING ONLY

jukumu la kukikuza na kukitukuza Kiswahili. Malengo mengine ya chama hiki yalikuwa:

(i) Kuwakutanisha walimu wa Kiswahili ili kujadili na kutafuta njia za kutatua changamoto mbalimbali zinazowakabili;

(ii) Kutunga majaribio na mitihani ya somo la Kiswahili kwa shule za sekondari;

(iii) Kuwashirikisha wanafunzi katika shughuli za kukuza na kueneza lugha ya Kiswahili; na

(iv) Kutoa mafunzo mbalimbali kwa walimu na wakufunzi ili kuwapatia ujuzi wa kufundisha lugha ya Kiswahili.

**Mafanikio ya Chama**

Chama hiki kimepata mafanikio yafuatayo:

(i) Chama kimefanikiwa kuwafundisha walimu lugha ya Kiswahili na kuwapa ujuzi wa juu katika kufundisha na kuzungumza. Kupitia mafunzo haya, walimu wanapata moyo na maarifa zaidi katika lugha ya Kiswahili.

(ii) Chama kimeongeza ufaulu wa somo la Kiswahili kwa wanafunzi wa Mkoa wa Nairobi ikilinganishwa na masomo mengine. Hatua hii inawahamasisha wanafunzi wengine kusoma Kiswahili.

(iii) Chama kilianzisha mashindano ya sanaa ya lugha ambayo hufanyika mwezi Juni kila mwaka. Mashindano haya huhusisha usomaji na mazungumzo ya papo kwa papo. Katika mashindano haya, tuzo maalumu hutolewa kwa wanafunzi wanaofanya vizuri.

**Changamoto za Chama**

Pamoja na mafanikio, Chama kinakabiliwa na changamoto zifuatazo:

(i) Kuhamishwa mara kwa mara kwa walimu wa Kiswahili kwenda nje ya Mkoa wa Nairobi; na

(ii) Upungufu mkubwa wa walimu wa lugha ya Kiswahili kulinganisha na idadi ya shule na wanafunzi wanaosoma lugha ya Kiswahili.

**Idara ya Kiswahili na Lugha za Kigeni Chuo Kikuu cha Kenyatta**

Idara hii ilianzishwa mwaka 1987 ambapo lengo lake mojawapo lilikuwa kufundisha lugha ya Kiswahili. Idara hii hutoa shahada za Kiswahili na kufanya tafiti mbalimbali kuhusu lugha ya Kiswahili na lahaja zake.

FOR ONLINE READING ONLY

**Madhumuni ya Idara**

Madhumuni ya idara hii ni:

(i) Kuandaa wataalamu mbalimbali kwa ajili ya kufundisha somo la Kiswahili katika shule na vyuo nchini Kenya;

(ii) Kufanya tafiti mbalimbali kuhusu lugha ya Kiswahili na lahaja zake;

(iii) Kushirikiana na idara za serikali na za binafsi katika kukuza na kueneza lugha ya Kiswahili; na

(iv) Kuchapisha vitabu vya lugha ya Kiswahili kwa ajili ya matumizi ya shule na wageni wanaojifunza Kiswahili.

**Mafanikio ya Idara**

Mafanikio ya idara hii ni yafuatayo:

(i) Kuanzisha maktaba maalumu ya vitabu na machapisho ya lugha ya Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Kenyatta;

(ii) Kufungua maabara ya lugha katika Chuo Kikuu cha Kenyatta kwa ajili ya mafunzo na tafiti kuhusu lugha ya Kiswahili;

(iii) Kuongeza idadi ya wataalamu wa lugha ya Kiswahili wenye shahada mbalimbali; na

(iv) Kuendesha semina mbalimbali kuhusu matumizi ya lugha ya Kiswahili kwa wabunge wa Bunge la Kenya na maafisa wa serikali.

**Changamoto za Idara**

Idara inakabiliwa na changamoto mbalimbali, zikiwamo:

(i) Mwamko mdogo wa wanafunzi wanaosoma lugha ya Kiswahili ambapo wengi hukimbilia taaluma nyingine na kuona lugha ya Kiswahili ni lugha ya kienyeji; na

(ii) Baadhi ya wataalamu wa lugha ya Kiswahili kuacha kufanya kazi za Kiswahili na kufanya kazi au shughuli nyingine, kama siasa na biashara

**Chama cha Kiswahili cha Taifa Kenya (CHAKITA)**

Chama hiki kilianzishwa mwaka 1998 kama jukwaa la wapenzi wa Kiswahili wakiwamo wahadhiri na walimu kwa ajili ya kubadilishana maarifa kuhusu lugha ya Kiswahili kwa maendeleo ya taifa.

FOR ONLINE READING ONLY

**Madhumuni ya Chama**

Madhumuni ya CHAKITA ni:

(i) Kuhakikisha kuwa Kiswahili kinakua na kuenea ndani na nje ya Kenya;

(ii) Kutoa vitabu na machapisho mbalimbali ya lugha ya Kiswahili;

(iii) Kushirikiana na serikali katika masuala ya kukuza na kueneza Kiswahili pamoja na kutoa msaada wa kitaaluma; na

(iv) Kuendesha semina, warsha na makongamano kuhusu lugha ya Kiswahili.

**Mafanikio ya Chama**

Mafanikio ya CHAKITA ni haya yafuatayo:

(i) Kutafsiri na kutoa misaada mingine ya kitaaluma kwa serikali na taasisi nyingine za umma na binafsi; na

(ii) Kuendesha warsha na makongamano ya Kiswahili.

**Changamoto za CHAKITA**

CHAKITA kinakabiliwa na changamoto zifuatazo:

(i) Kiswahili kutopewa hadhi kama ilivyo kwa lugha za jamii na Kiingereza.

(ii) Uhaba wa fedha za kuendesha shughuli mbalimbali za Chama.

Pamoja na juhudi zilizofanyika katika kukuza na kueneza Kiswahili nchini Kenya, kumekuwa na changamoto mbalimbali zinazoathiri maendeleo ya Kiswahili nchini humo. Changamoto hizo ni kama vile Kiingereza kuendelea kutumika zaidi kuliko Kiswahili katika shule na taasisi mbalimbali za elimu, vyombo vya habari, shughuli za kiserikali, na katika mawasiliano ya kila siku. Pia, bado kuna upinzani kutoka lugha za jamii pamoja na kutokuwepo kwa chombo maalumu cha kusimamia maendeleo ya Kiswahili.

FOR ONLINE READING ONLY

**Zoezi la 4.7**

1. Fafanua hatua zilizochukuliwa na Serikali ya Kenya baada ya uhuru ili kukuza na kueneza Kiswahili nchini humo.
2. Eleza jinsi unavyoweza kutatua changamoto zinazokikabili Chama cha Kiswahili cha Taifa Kenya.
3. Ukipewa nafasi ya kuishauri Serikali ya Kenya kuhusu kukuza na kueneza Kiswahili nchini humo, utaishauri mambo gani? Pendekeza ushauri wako kwa hoja zisizopungua sita.

**Kukua na kuenea kwa lugha ya Kiswahili nchini Uganda baada ya uhuru**

Uganda ilipata uhuru tarehe mwaka 1962 kutoka kwa utawala wa Waingereza. Tofauti na nchi zingine za Afrika Mashariki, matumizi ya Kiswahili nchini Uganda yalikuwa madogo. Hadhi ya lugha haikuwa dhahiri ingawa Kiswahili kilikuwa kikizungumzwa na baadhi ya watu kama Lugha ya pili (L2). Pia, Kiswahili kilikuwa hakifundishwi sana.

Mara baada ya uhuru, Uganda ilikabiliwa na tatizo la kuchagua lugha ya taifa, ambapo haikuwa rahisi kwani kulikuwa na mvutano baina ya makundi ya wananchi kuhusu lugha inayofaa. Rais Milton Obote wa Chama cha Uganda Peoples' Congress (UPC) alikusudia kukifanya Kiswahili kuwa lugha ya taifa kama ilivyokuwa kwa Tanzania na Kenya. Hata hivyo, lengo la Rais Obote halikufanikiwa kutokana na upinzani kutoka kwa chama cha Kabaka Yekka kilichopendelea lugha ya Kiganda itumike. Lugha ya Kiganda ilikuwa ikifundishwa na kutumika zaidi katika vyombo vya habari, na mawasiliano ya kawaida kuliko Kiswahili na lugha zingine za makabila ya Uganda. Katika kipindi hicho, Kiswahili kilibaki kuwa lugha ya askari polisi na wanajeshi.

Kutokana na kukosekana kwa mwafaka kati ya vyama vya UPC na Kabaka Yekka, utawala wa Milton Obote haukutambua lugha ya Kiswahili kama lugha rasmi. Kila kabila lilitumia lugha yake katika shughuli za kiutawala. Suala hili lilichangiwa zaidi na utawala wa machifu waliokuwa na nguvu za kukumbatia na kusimamia misingi ya tamaduni zao za jadi. Hata hivyo, Kiganda ndiyo lugha iliyokuwa na nafasi kubwa ya kutumika kuliko lugha zingine za makabila. Aidha, Kiingereza kilitumika sambamba na Kiganda.

Hadhi ya Kiswahili ilianza kubadilika baada ya Idi Amini Dada kushika madaraka ya nchi mwaka 1971, ambapo alitangaza Kiswahili kitumike kama lugha ya taifa kwa sababu aliona kuwa kingefaa kuwaunganisha Waganda wote. Pamoja na Kiswahili kutangazwa kuwa lugha ya taifa, serikali haikutunga sera kuhusu matumizi ya lugha hii. Hata hivyo, Kiswahili kiliendelea kutumiwa na askari pamoja na wanajeshi na kufundishwa katika shule chache kama somo. Hatua nyingine ilikuwa kuanzishwa kwa idhaa ya Kiswahili katika Redio Uganda mwaka 1971. Idhaa hii ilikuwa chini ya Idara ya Matangazo ya Nje. Matangazo ya Kiswahili katika Idara ya Matangazo ya Ndani yaligawanywa kati ya Idhaa ya Taifa na Idhaa ya Mamboleo. Idhaa hizi zilitangaza vipindi kama vile Hodi Hodi Mitaani, Darubini, Kwa Akina Mama, Burudikeni Shoo, Porojo za Mjomba, Dunia Wiki Hii, Jifunze na Uburudike, Usiku Mwema, na Michezo.

Baada ya Rais Yoweri Museveni kuingia madarakani mwaka 1986, Kiswahili kilipata mwamko mpya na kasi ya kuenea, hasa mijini. Rais Museveni amekuwa akitumia Kiswahili katika mikutano yake ya hadhara. Hadhi ya Kiswahili ilipanda zaidi kuanzia

FOR ONLINE READING ONLY

mwaka 2005 baada ya bunge kupiga kura na kuamua Kiswahili kuwa lugha rasmi sambamba na Kiingereza. Kiswahili kimekuwa kikitumika katika kampeni za uchaguzi na mawasiliano ya kiofisi na kibiashara. Kiswahili kimeingizwa katika mfumo wa elimu ambapo kinafundishwa katika shule zote za msingi, vyuo vya ualimu na vyuo vikuu. Vyuo vikuu vinavyofundisha Kiswahili nchini Uganda ni Chuo Kikuu cha Makerere, Chuo Kikuu cha Kiislamu, Chuo Kikuu cha Kyambogo na Chuo Kikuu cha Kampala. Aidha, Baraza la Mitihani la Taifa la Uganda limekuwa likitahini somo la Kiswahili kwa wanafunzi wa shule za msingi na za sekondari.

Kwa ujumla, Kiswahili kinazidi kuwavutia wananchi wengi wa Uganda, hasa baada ya kuwa lugha ya pili rasmi. Vilevile, Kiswahili kinazidi kustawi na kuimarika nchini Uganda kwa kuwa ni lugha ya kikazi ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ambapo Uganda ni nchi mwanachama. Kwa hiyo, inatarajiwa kwamba Kiswahili kitazidi kukua na kustawi zaidi nchini Uganda.

Pamoja na hayo, kukua na kuenea kwa Kiswahili nchini humo kunakabiliwa na changamoto kama vile upinzani kati ya Kiganda na Kiswahili, na kukosekana kwa sera madhubuti kuhusu lugha ya Kiswahili. Changamoto nyingine ni kutokuwepo kwa asasi au taasisi na vyombo maalumu vya kukuza na kueneza Kiswahili. Hali kadhalika, kuna changamoto ya kutokuwepo kwa vyombo vingi vya habari vinavyotumia lugha ya Kiswahili.

**Zoezi la 4.8**

1. Pendekeza mikakati ambayo Serikali ya Uganda inapaswa kutekeleza ili kuzidi kukuza na kueneza Kiswahili nchini humo.
2. "Hadhi ya Kiswahili imepokea mabadiliko chanya nchini Uganda baada ya uhuru." Thibitisha kauli hii kwa kutoa hoja zisizopungua sita.
3. Kwa nini lugha ya Kiswahili ilienea kwa kasi nchini Tanzania kuliko Uganda baada ya uhuru?

**Kukua na kuenea kwa lugha ya Kiswahili nchini Kongo baada ya uhuru**

Kiswahili ni moja ya lugha muhimu na zinazozungumzwa katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo. Kimahususi, lugha hii inazungumzwa katika eneo la Mashariki mwa Kongo. Nchini Kongo Kiswahili kimeendelea kukua na kuenea kutokana na sababu mbalimbali kama vile kutumika katika elimu, vyombo vya habari, na machapisho.

FOR ONLINE READING ONLY

*(a) Elimu*

Nchini Kongo, Kiswahili hufundishwa katika ngazi ya elimu ya msingi kuanzia darasa la kwanza hadi la tatu. Kadhalika, Kiswahili kinafundishwa kama somo katika ngazi ya chuo kikuu. Kwa mfano, kinfundishwa kama somo katika Chuo Kikuu cha Lubumbashi, Idara ya Simu na Lugha.

*(b) Vyombo vya habari*

Kiswahili kinatumika nchini Kongo katika televisheni na redio za kikanda, hususani katika Kanda ya Mashariki. Kwa mfano, Televisheni ya Taifa hutangaza kwa lugha nne na Kiswahili kikiwamo.

*(c) Machapisho*

Nchini Kongo, Kiswahili kinatumika katika uandishi wa vitabu vya kujifunzia na kufundishia stadi za kusoma na kuandika. Kadhalika, wataalamu kadhaa wameandika habari za Kiswahili katika makala mbalimbali. Kwa mfano, Kifungo Jean Paul anazungumzia ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili nchini Kongo katika makala yake yenye jina "Teaching-Learning Kiswahili in a Diaglosic Context: A usability Analysis or Language Habits in Lubumbashi"(Jean Paul, 202)

Pamoja na juhudi za kukuza na kueneza Kiswahili nchini Kongo, kumekua na changamoto mbalimbali. Changamoto hizo ni pamoja na ukosefu wa waalimu wenye uweledi, mwitiko mdogo wa watu kusoma Kiswahili vyuoni.

### *Shughuli ya 4.4*

Kwa kutumia vyanzo mbalimbali, vikiwamo vya ki-TEHAMA tathmini matumizi ya Kiswahili katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo.

*Kukua na kuenea kwa lugha ya Kiswahili nchini Burundi baada ya uhuru*

Burundi ilipata uhuru mwaka 1962. Baada ya kupata uhuru, Kiswahili kimekuwa kikienea na kukua nchini humo kama lugha ya pili au ya tatu kwa matumizi ya kawaida. Japokuwa lugha rasmi ya Burundi ni Kifaransa, Kiswahili kimepata umaarufu kutokana na nchi hiyo kuwa sehemu ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, kutumika katika mawasiliano ya kibiashara, elimu, na vyombo vya habari. Baada ya uhuru wake, Burundi ilichukua hatua kadhaa za kuhakikisha inakuza na kueneza matumizi ya lugha ya Kiswahili. Hatua hizi zililenga kukuza lugha ya Kiswahili kama lugha ya kitaifa na kuiwezesha kusaidia katika mawasiliano ya kitaifa na kimataifa. Baadhi ya hatua hizo ni kukifanya Kiswahili kuwa lugha rasmi, kuwekeza katika elimu ya Kiswahili, kuendeleza rasilimali za Kiswahili, na kukuza matumizi ya Kiswahili katika sekta ya

FOR ONLINE READING ONLY

biashara na utalii. Lengo la kuifanya lugha ya Kiswahili kuwa rasmi ni kuipa umuhimu wa kutumika katika taasisi za serikali, elimu, na mawasiliano rasmi.

Kwa upande wa elimu, Serikali ya Burundi iliwekeza katika mfumo wa elimu kwa kuhakikisha kuwa Kiswahili kinafundishwa katika shule za msingi na sekondari baada ya uhuru. Kwa kufanya hivi, Serikali ililenga kuhakikisha kuwa vizazi vijavyo vinakuwa na ujuzi wa lugha ya Kiswahili na vinaweza kuwasiliana kwa ufanisi kwa kutumia lugha ya Kiswahili. Aidha, mashirika ya kiraia yalichukua hatua za kuendeleza rasilimali za Kiswahili kama vile kamusi, vitabu, na vifaa vya kufundishia. Lengo la kuendeleza rasilimali hizi lilikuwa kuhakikisha kuwa kuna vifaa vya kutosha vya kusaidia katika ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili.

Zaidi ya hayo, Serikali ya Burundi, baada ya uhuru, ilichukua hatua za kukuza matumizi ya Kiswahili katika sekta ya biashara na utalii kwa kuhamasisha wafanyabiashara na watoa huduma za utalii kutumia lugha ya Kiswahili katika mawasiliano yao ya kibiashara.

Pamoja na jitihada za kukuza na kueneza Kiswahili nchini Burundi, jitihada hizo zilikabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuwepo kwa miundombinu duni ya kielimu, upinzani kutoka lugha za makabila mbalimbali, kukosekana kwa maarifa kuhusu umuhimu wa lugha ya Kiswahili katika kukuza maendeleo ya kiuchumi, kijamii na kitamaduni na upungufu wa walimu wenye ujuzi wa kufundisha Kiswahili.

**Zoezi la 4.9**

1. Eleza hatua zilizochukuliwa na Serikali ya Burundi katika kukuza na kueneza Kiswahili nchini humo.
2. Fafanua mambo unayoweza kuishauri Serikali ya Burundi iyafanye ili kueneza zaidi Kiswahili nchini humo.
3. Eleza ni kwa namna gani biashara na shughuli za kijamii vinachangia katika kukua na kuenea kwa Kiswahili Burundi.

**Kukua na kuenea kwa Kiswahili nchini Rwanda**

Mnamo mwaka 1962, baada ya uhuru wa Rwanda, lugha ya Kiswahili ilianza kukua na kuenea japokuwa mtazamo wa Wanyarwanda wengi ulikuwa mbaya kuhusu lugha hii. Hata hivyo, Wanyarwanda wengi walibadilisha mtazamo hasi waliokuwa nao kuhusu lugha hiyo baada ya mauaji ya kimbari dhidi ya Watusi mwaka 1994. Kiswahili kilianza kuenea na kufundishwa katika shule za sekondari na Chuo Kikuu cha Rwanda. Kwa sasa, Kiswahili kimekuwa kikifundishwa katika shule nyingi za msingi na sekondari.

FOR ONLINE READING ONLY

Lengo lilikuwa kujenga umoja wa kitaifa na kuleta maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Ingawa kuna jitihada za kueneza Kiswahili, lugha ya Kinyarwanda ndiyo inayotumiwa zaidi na watu wengi nchini humo, na Kiingereza pia kimekuwa lugha rasmi ya biashara na mawasiliano ya kimataifa. Kiswahili kimekua na kuenea nchini Rwanda kutokana na mwingiliano wa utamaduni, biashara, na elimu. Hata hivyo, kuna hatua mbalimbali zilizochukuliwa nchini humo katika kuhakikisha kuwa Kiswahili kinakuwa na kuenea. Miongoni mwa hatua hizo ni kuingiza Kiswahili katika mtaala wa elimu, kuendeleza mafunzo ya Kiswahili, kukuza utamaduni wa Kiswahili, kuwezesha mawasiliano, na kushirikiana na nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Nchini Rwanda, Kiswahili kinakabiliwa na changamoto kadhaa katika kukua na kuenea kwake. Baadhi ya changamoto hizo ni uhaba wa walimu wa Kiswahili, ukosefu wa vifaa vya kufundishia na mgongano wa lugha ya Kinyarwanda na Kiswahili.

**Zoezi la 4.10**

1. Fafanua mikakati ambayo imechochea Kiswahili kupata umaarufu nchini Rwanda?
2. Kwa nini unafikiri ni muhimu Serikali ya Rwanda kuendelea kusisitiza matumizi ya Kiswahili nchini humo?
3. Fafanua namna ambavyo unaweza kuishauri Serikali ya Rwanda iendelee kueneza Kiswahili nchini humo.

**Kukua na kuenea kwa Kiswahili nchini Sudani Kusini baada ya uhuru**

Sudani Kusini ilipata uhuru mnamo mwaka 2011. Lugha ya Kiswahili imekuwa ikipata umaarufu na kuenea kama lugha ya mawasiliano katika sehemu mbalimbali za nchi hiyo. Mambo yaliyosababisha kukua na kuenea kwa Kiswahili nchini Sudani Kusini yanafafanuliwa katika vipengele vinavyofuata.

**(a) Watu wa Sudani Kusini kuhamia nchi jirani kutokana na vita vya wenyewe kwa wenyewe**

Kutokana na vita, wakazi wengi wa Sudani Kusini walikimbilia nchi za jirani kama vile Kenya, Tanzania, Rwanda, Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Ethiopia, na Uganda ili kutafuta hifadhi. Mataifa haya ya Eneo la Maziwa Makuu, kwa kawaida, huzungumza lugha ya Kiswahili kama lugha ya mawasiliano. Wakimbizi hawa waliporudi nyumbani baada ya vita vya wenyewe kwa wenyewe, walirudi wakiwa wajuzi wa lugha ya Kiswahili ambayo waliitumia katika miktadha tofautitofauti.

**(b) Watoto wa Sudani Kusini kusoma katika nchi jirani za Afrika Mashariki**

Baadhi ya wanafunzi kutoka majimbo ya Sudani Kusini ya Imatong na Numer Nyang

FOR ONLINE READING ONLY

wanapata elimu ya msingi na sekondari katika nchi jirani kama Kenya kwa kutumia mtaala wa nchi hizo. Kwa kufanya hivyo, wamejinasibisha na taasisi za nchi hizo kielimu na hata kiutamaduni. Kutokana na kutumia mitaala ya nchi hizo, wanafunzi wa Sudani Kusini husoma somo la Kiswahili ambalo ni somo la lazima katika mitaala ya elimu ya baadhi ya nchi hizo kama vile Kenya. Wanafunzi hawa wanaporudi katika nchi yao, wanakuza na kueneza Kiswahili kutokana na kukitumia katika miktadha anuwai nchini humo.

(c) **Baadhi ya watu wa Sudani Kusini kupata elimu ya juu katika nchi za Afrika Mashariki**

Baadhi ya Wasudani Kusini hujiunga na vyuo vikuu vya Kenya, Uganda, Burundi, Rwanda na Tanzania. Wafikapo, hujifunza Kiswahili kama lugha ya kutagusana na wenyeji ili waweze kutagusana na watu mbalimbali katika vyuo wanakosomea masomo yao. Wanafunzi hawa wanaporudi nyumbani baada ya kuhitimu masomo, huzungumza Kiswahili na hivyo kukiwezesha kukua na kuenea.

(d) **Biashara za mipakani**

Lugha ambayo hutumika sana katika biashara baina ya watu wa Sudani Kusini na nchi za Afrika Mashariki kama vile Kenya, Uganda na Tanzania ni Kiswahili. Wenyeji wa Sudani Kusini, ambao taifa lao limetatizwa kisiasa, kiuchumi na kiutamaduni kutokana na vita vya wenyewe kwa wenyewe, hujinasibisha na nchi za Afrika Mashariki. Katika hali hii, huishia kutumia lugha ya Kiswahili zaidi katika masuala ya biahara mipakani. Pia, baada ya taifa la Sudani kusitisha vita na Sudani Kusini kupata uhuru wake, wakazi wa mataifa mengi ya Afrika ya Mashariki na Kati walihamia Sudani Kusini kwa shughuli za kibiashara na kuendeleza matumizi ya Kiswahili.

Licha ya Kiswahili kukua na kuenea nchini Sudani Kusini, bado kuna changamoto kadhaa zinazojitokeza. Baadhi ya changamoto hizo ni ukosefu wa vyombo mahususi vya kisera vya kuendeleza Kiswahili; upinzani kutoka lugha za kienyeji kama vile Kidinka, Kinueli, Kiriba na Kizembe; na lugha ya Kingereza kupewa hadhi kubwa ikilinganishwa na Kiswahili.

### *Zoezi la 4.11*

1. Eleza kwa nini Kiswahili kinaweza kuchangia katika kuimarisha umoja na mshikamano miongoni mwa jamii za Sudani Kusini?
2. Fafanua jinsi vita vya wenyewe kwa wenyewe nchini Sudani Kusini vilivyochangia kuenea kwa Kiswahili nchini humo.
3. Fanua mchango wa Kiswahili katika kukuza uchumi wa Sudani Kusini.

FOR ONLINE READING ONLY

**Shughuli ya 4.5**

Kwa kutumia vyanzo vya maktabani na mtandaoni, bainisha changamoto zinazokabili maendeleo ya Kiswahili baada ya uhuru katika nchi za Afrika Mashariki

## Kukua na kuenea kwa Kiswahili kutokana na maendeleo ya sayansi na teknolojia

**Shughuli ya 4.6**

Kwa kutumia vyanzo mbalimbali vya maktabani na mtandaoni, thibitisha dai kuwa maendeleo ya sayansi na teknolojia yanaathiri kuathiri kukua na kuenea kwa Kiswahili.

**Je, wajua ?**

Maendeleo ya sayansi na teknolojia yamechangia katika kukua na kuenea kwa Kiswahili. Moja ya michango mikubwa ni kupitia teknolojia ya habari na mawasiliano ambayo imewezesha Kiswahili kuenea. Pia, zana za kidijiti zimeboresha na kurahisisha upatikanaji wa mafunzo ya Kiswahili. Majukwaa ya mtandaoni yamechochea ubunifu na maendeleo ya maudhui ya Kiswahili na, hivyo, kusaidia kueneza lugha hiyo. Katika sehemu hii, tutajadili jinsi maendeleo ya sayansi na teknolojia yanavyochangia katika kukua na kuenea kwa Kiswahili katika nchi za Afrika Mashariki.

### Mchango wa vyombo vya habari katika kukuza na kueneza Kiswahili Afrika Mashariki

Vyombo vya habari vina jukumu muhimu katika kukuza na kueneza matumizi ya lugha ya Kiswahili katika nchi za Afrika Mashariki. Vyombo vya habari pia vinachangia katika kukua na kuenea kwa Kiswahili kwani vinaibua na kuendeleza msamiati mpya kulingana na mahitaji ya jamii. Kupitia vyombo vya habari kama redio, televisheni, magazeti, na mitandao ya kijamii, lugha ya Kiswahili inaweza kutumiwa kwa njia mbalimbali kama vile kuhabarisha, kuelimisha, na kuburudisha umma. Mchango wa kila chombo unafafanuliwa katika vipengele vinavyofuata.

**Redio**

Nchini Tanzania, kuna redio mbalimbali ambazo zinatumia lugha ya Kiswahili katika matangazo yake. Redio hizi zote zinachangia kukua na kuenea kwa Kiswahili. Baadhi ya redio maarufu ni Clouds FM, Radio One stereo, na Radio Uhuru. Kwa upande wa Kenya, vipo vituo vya redio kama vile Radio Citizen, Radio Maisha, na Radio Jambo ambavyo hutumika kutangaza vipindi vya habari, muziki, michezo, na vipindi vya mazungumzo kwa lugha ya Kiswahili. Nchini Uganda, Redio Simba na Capital FM hurusha vipindi vya matangazo ya michezo, habari, elimu na burudani kwa lugha ya

FOR ONLINE READING ONLY

Kiswahili. Kwa upande wa Kongo, baadhi ya vituo vya redio vinavyorusha matangazo yake kwa Kiswahili ni Redio Sauti ya Injili na Redio Okapi ambayo hurusha vipindi vinavyoelewesha matumizi ya Kiswahili kwa raia wa Kongo. Nchini Burundi, baadhi ya redio zinazotoa maudhui ya lugha ya Kiswahili ni Redio Isanganiro na Redio Bonesha. Redio hizi huelimisha wanajamii kuhusu lugha ya Kiswahili, huunganisha jamii, na hukuza utamaduni. Nchini Rwanda, vituo vya redio vinavyorusha vipindi kwa Kiswahili ni Redio Rwanda na Redio 10. Wakati mwingine, vituo hivi vimekuwa vikisaidia katika kutoa elimu kwa kutumia lugha ya Kiswahili kama lugha ya kufundishia katika vipindi vya elimu. Katika nchi ya Sudani Kusini, kituo cha Redio cha South Sudan kimekuwa kikitoa vipindi vya Kiswahili ambavyo vinawafikia wasikilizaji wengi nchini humo.

**Televisheni**

Televisheni ina umuhimu mkubwa sana katika ukuzaji na ueneaji wa lugha ya Kiswahili nchini Tanzania. Vituo vya televisheni kama vile TBC, ITV, na Clouds TV vinarusha vipindi mbalimbali kwa kutumia lugha ya Kiswahili ikiwa ni pamoja na habari, vipindi vya burudani, na elimu. Kwa kufanya hivyo, vinachangia kwa kiasi kikubwa katika kukua na kuenea kwa lugha ya Kiswahili. Nchini Kenya, kuna vituo vya televisheni kama vile Citizen TV, KTN, na NTV ambavyo hurusha vipindi vingi kwa lugha ya Kiswahili. Vituo hivi vinajumuisha habari za kila siku, vipindi vya mazungumzo, na burudani. Nchini Uganda, vituo vya televisheni vinavyorusha matangazo yake kwa lugha ya Kiswahili ni Azam TV, NBS Television, na Bukedde TV. Ameen TV na Tropicana TV ni miongoni mwa vituo vya televisheni vinavyolenga kukuza na kueneza matumizi ya lugha ya Kiswahili katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo. Vituo hivi vimekuwa vikitangaza vipindi mbalimbali kwa lugha ya Kiswahili.

Televisheni Salama na Heritage TV ni miongoni mwa televisheni ambazo zimekuwa na athari kubwa katika kukua na kuenea kwa lugha ya Kiswahili nchini Burundi kwa kuwa zimekuwa jukwaa muhimu la kutoa maudhui ya elimu kwa lugha ya Kiswahili. Nchini Rwanda, miongoni mwa vituo vya televisheni vinavyorusha vipindi vyake kwa lugha ya Kiswahili ni TV1, RTV, au Radio Télévision des Mille Collines ambavyo hutoa huduma zake kwa lugha ya Kiswahili. Miongoni mwa vituo vya televisheni huko Sudani Kusini ni televisheni ya SSBC ambayo imekuwa ikikuza na kueneza matumizi ya lugha ya Kiswahili nchini humo kwa kutoa baadhi ya matangazo kwa lugha ya Kiswahili.

**Magazeti**

Magazeti ya Kiswahili pia ni vyombo muhimu katika kukuza na kueneza lugha ya Kiswahili nchini Tanzania. Kuna magazeti kama vile *Mwananchi*, *Mtanzania*, *Uhuru*, na *Majira* yanayochapisha makala, habari, na maelezo mengine kwa lugha ya Kiswahili ili kufikisha ujumbe kwa jamii iliyokusudiwa na hivyo kusababisha kukua na kuenea kwa lugha ya Kiswahili. Nchini Kenya, *Daily Nation*, *Taifa Leo*, na *The*

FOR ONLINE READING ONLY

**Standard** ni magazeti ambayo yana baadhi ya sehemu za machapisho yanayotolewa kwa Kiswahili. Baadhi ya magazeti yanayoandikwa kwa lugha ya Kiswahili nchini Uganda ni Bukedde, Etop, Munno na Ruzinga. Nchini Kongo, gazeti la "La Tempête des Tropiques" lililoanzishwa na Antoine-Roger Bolamba mwaka 1943 ni moja ya magazeti yanayosaidia katika kukua na kuenea kwa lugha ya Kiswahili nchini humo kwa kukuza ujuzi wa lugha, kuhamasisha matumizi ya lugha na hata kutetea utamaduni wa Kiafrika. Miongoni mwa magazeti yaliyosaidia kukuza na kueneza Kiswahili nchini Burundi ni gazeti la "Lwacu". Gazeti hili limeiwezesha jamii ya Burundi kufahamu na kutumia lugha ya Kiswahili kwa ufasaha zaidi. Pia, gazeti la "Burundi Tribune" limekuwa likieneza habari na maarifa kwa lugha ya Kiswahili na kuchangia katika kukua kwa matumizi na uelewa wa Kiswahili miongoni mwa jamii ya Burundi. Nchini Rwanda, miongoni mwa magazeti yanayochangia katika kukua na kuenea kwa lugha ya Kiswahili ni **The New Times** ambalo limekuwa likichapisha habari zake kwa lugha ya Kiswahili na, hivyo, kuwapa fursa wasomaji wengi zaidi ambao wanazungumza na kuelewa Kiswahili kupata habari na taarifa muhimu. Huko Sudani Kusini, gazeti la Juba Monitor limekuwa likihamasisha ujuzi wa Kiswahili na, hivyo, kuchangia katika kuhamasisha watu kujifunza na kuboresha ujuzi wao wa lugha ya Kiswahili.

*Kiswahili katika intaneti*

Katika zama hizi za utandawazi, kumekuwa na mapinduzi makubwa ya mawasiliano duniani. Mawasiliano haya yanafanyika katika mifumo maalumu ya kompyuta na simu ambayo huwezeshwa na intaneti. Katika mifumo hiyo, watu huweza kupata na kusambaza habari kwenda kokote duniani. Mapinduzi hayo yamesababisha kuibuka kwa mitandao mbalimbali duniani. Mitandao hiyo ni kama vile Facebook, Twitter, Instagram, WhatsApp, Imo, Viber, Skype, na Telegramu. Mitandao hii huunganisha watu duniani kote. Watu hawa wanapotumia Kiswahili husaidia kukieneza kwani maoni au posti zao huweza kusemwa kokote duniani. Kupitia mitandao hii, watu pia wanaweza kusoma magazeti, kusikiliza redio na kutazama televisheni zinazorusha matangazo yake kwa lugha ya Kiswahili popote pale duniani kwa njia ya intaneti. Aidha, kuna programu za kompyuta zinazotumia lugha ya Kiswahili. Programu hizo ni kama vile Linux Operating System, na Jambo Open Office. Hali kadhalika, mnamo mwaka 2004 – 2005, kampuni ya Microsoft iliunda istilahi za Kiswahili za kompyuta na kutafsiri Windows XP, Power Point, Excel, Word na Outlook. Mnamo mwaka 2008, ilitafsiri Windows 10 na Office 2007. Matumizi ya lugha ya Kiswahili katika uga wa kompyuta yanaonesha kukua kwa lugha hiyo kwani haikuwahi kutumika kabla. Zaidi ya hayo, kuna programu za kutafsiri Kiswahili kama vile Google translator na ChatGPT ambazo huwezesha kutafsiri kutoka lugha ya Kiswahili kwenda lugha zingine na kutoka lugha nyingine kwenda Kiswahili. Kupitia programu mbalimbali zilizoelezwa, msamiati na istilahi mpya za Kiswahili zimepatikana; hivyo, Kiswahili kimezidi kukua na kuenea.

FOR ONLINE READING ONLY

## Shughuli ya 4.7

Kwa kutumia vyanzo mbalimbali, vikiwamo vya ki-TEHAMA:

(a) Eleza unafikiri ni chombo kipi cha habari kinatoa mchango zaidi katika kukuza na kueneza Kiswahili katika nchi za afrika Mashariki. Kwa nini?

(b) Jadili athari za mitandao ya kijamii katika kukuza na kueneza Kiswahili katika nchi za Afrika Mashariki baada ya uhuru.

## Tamrini ya 4

1. Kwa nini Kiswahili kilienea haraka zaidi nchini Tanganyika kuliko Kenya na Uganda kabla ya uhuru?
2. Shughuli za uzalishaji mali ni miongoni mwa sababu zilizochangia kukua na kuenea kwa Kiswahili katika eneo la Afrika Mashariki. Kubali au pinga kauli hii kwa hoja zisizopungua sita.
3. Fafanua mchango wa wasanii katika kukuza na kueneza Kiswahili Afrika Mashariki.
4. Kiswahili kinafaa kutumika kama lugha ya kufundishia kuliko lugha zingine katika eneo la Afrika Mashariki. Jadili kauli hii kwa hoja maridhawa.
5. Tathmini athari ya vyombo vya habari vya sasa nchini Tanzania katika maendeleo ya Kiswahili katika miaka ya hivi karibuni.

FOR ONLINE READING ONLY

# Sura ya Tano

## Matumizi ya lugha

### Utangulizi

*Kwa kuzingatia matumizi, lugha inaweza kuwa rasmi, ya kwanza, ya pili, ya taifa au ya kimataifa. Katika sura hii, utajifunza kuhusu dhana na matumizi ya lugha ya kwanza, lugha ya pili, lugha rasmi, lugha ya taifa, na lugha ya kimataifa. Pia, utajifunza sifa za lugha ya Kiswahili kama lugha ya kimataifa. Umahiri utakaoujenga utakusaidia kuthamini hadhi ya lugha ya Kiswahili kitaifa na kimataifa.*

**Fikiri**

Mambo yanayosababisha lugha kuwa rasmi

## Hadhi ya Kiswahili kimatumizi

### Shughuli ya 5.1

**Ghani shairi lifuatalo, kisha jibu maswali yanayofuata.**

Lugha ni mfumo wa sauti, wanazuoni wanasema,
Lugha kutumika ni shurti, mawasiliano yasikwame,
Lugha ni utambulisho madhubuti, hususani lugha mama,
Kiswahili ni lugha mama, kusema najivunia.

Kiswahili ni lugha mama, kwa wazawa wa lugha hii,
Huiamili tangu zama, toka kwa wazazi na walezi,
Kwa Mswahili ndiyo mama, imemlea na kumkuza,
Kiswahili ni lugha mama, kusema najivunia.

FOR ONLINE READING ONLY

Lugha mama ni lugha ya kwanza, wanazuoni hurejelea,
Kiswahili ni lugha mama, hivyo ni ya kwanza pia,
Tumeipata mwanzoni, kabla ya lugha zinginezo,
Kiswahili ni lugha mama, kusema najivunia.

Lugha ya kwanza huamiliwa, kwa kusikiliza na kuongea,
Huchotwa na msemaji, toka jamii alimokulia,
Hufungamana na tamaduni, za jamii ya mzawa,
Kiswahili ni lugha mama, kusema najivunia.

Lugha hii ni lugha ya kwanza, kwa wengine ni lugha ya pili,
Nao wenye lugha ya kwanza, Kiswahili ni lugha ya pili,
Huipata masomoni, vyuoni na matembezini,
Kiswahili ni lugha mama, kusema najivunia.

Kiswahili lugha ya taifa, Tanzania, Kenya na Uganda,
Tanzania imekita mizizi, tangu enzi na enzi,
Huwezesha mawasiliano, makabila yote nchini,
Kiswahili ni lugha mama, kusema najivunia.

Lugha ya taifa ni moja, kwingine wanazo nyingi,
Tanzania ni Kiswahili, Kongo wanazo nne,
Hutumika masomoni, sokoni na maofisini,
Kiswahili ni lugha mama, kusema najivunia.

Kimataifa imepanda, hutumika kila mahali,
Marekani na Uingereza, Kiswahili kinatamba,
Umoja wa Mataifa, nako huko kinavuma,
Kiswahili ni lugha mama, kusema najivunia.

FOR ONLINE READING ONLY

Ninatamatisha chapisho, hadhi ya Kiswahili kusema,
Lugha ya kwanza na ya pili, ya taifa na kimataifa,
Pengine ni ya kigeni, kwa wageni wajifunzao,
Kiswahili ni lugha mama, kusema najivunia.

## Maswali

1. Pendekeza kichwa cha shairi ulilolighani.
2. Eleza dhima za lugha zilizotajwa katika shairi ulilolighani.
3. Tathmini hadhi ya lugha ya Kiswahili nchini Tanzania kama ilivyoelezwa na mshairi.
4. Mshairi ana maana gani anaposema, "Pengine ni ya kigeni, kwa wageni wajifunzao"?
5. Kutokana na shairi ulilolighani na vyanzo vingine vya taarifa, andika insha kuhusu hadhi ya lugha ya Kiswahili kwa sasa.

## Kiswahili kama lugha ya kwanza na lugha ya pili

**Soma kifungu cha habari kifuatacho, kisha jibu maswali yanayofuata.**

Tupe ni kijana wa kidato cha tano aliyezaliwa katika Kijiji cha Bwete. Baba yake aliitwa Bubeho Baje na mama yake aliitwa Kateho Baki. Tupe alibahatika kusoma elimu ya msingi katika kijiji alimozaliwa, kisha alichaguliwa kujiunga na masomo ya elimu ya sekondari katika Shule ya Sekondari Bibe katika Kijiji cha Bwete. Alifanikiwa kuendelea na masomo ya elimu ya sekondari hatua ya juu. Alipokuwa kidato cha tano, alipata rafiki kutoka eneo tofauti na Kijiji cha Bwete. Rafiki huyo aliitwa Maye Ngibi. Maye alikuwa mcheshi na alipenda chombezachombeza. Tupe alivutiwa sana na namna Maye alivyokuwa akiongea lugha ya Kiswahili kwa madaha na kwa kujiamini. Alitamani kujua Maye alijifunzia wapi lugha ya Kiswahili hadi kuwa mahiri namna ile.

Siku moja, wakati wa mapumziko, Tupe pamoja na Maye walikaa chini ya kivuli cha mwembe mbele ya darasa lao. Tupe alianzisha mazungumzo akiwa na shauku ya kutaka kujua chanzo cha Maye kuzungumza Kiswahili kizuri namna ile. Mazungumzo yao yalikuwa hivi:

FOR ONLINE READING ONLY

*Tupe*: Rafiki yangu Maye, unazungumza Kiswahili kizuri kweli. Nipe siri ya mafanikio jamani.

*Maye*: Ha! Mbona ninazungumza kawaida tu. Hata wewe unazungumza vizuri na unaeleweka.

*Tupe*: Hapana, Maye! Mimi ninaongea, ila Kiswahili changu si kizuri kama chako. Wakati mwingine, ninatamka maneno tofauti na baadhi ya watu hunikosoa. Wewe Kiswahili chako kinanivutia kweli.

*Maye:* Wewe lugha yako ya kwanza ni ipi?

*Tupe*: Lugha ya kwanza? Ni lugha gani hiyo?

*Maye:* Lugha uliyojifunza kwa mara ya kwanza kutoka kwa wazazi au walezi wako.

*Tupe*: Ahaa! Ni Kisukuma.

*Maye:* Sawa! Hiyo ndiyo lugha yako ya kwanza. Baada ya hapo, ulijifunza lugha gani?

*Tupe*: Lugha ya Kiswahili; nilijifunza baada ya kuanza elimu ya msingi. Hivyo, nyumbani sikuwahi kutumia lugha hiyo.

*Maye:* Kumbe! Basi kwako wewe lugha ya Kiswahili ni lugha ya pili. Mimi lugha yangu ya kwanza ni Kiswahili. Wazazi wangu lugha yao ya kwanza ni Kimasai lakini walifanya kazi mjini kwa muda mrefu. Hivyo, mimi nimezaliwa na kujifunza lugha ya Kiswahili ikiwa lugha yangu ya kwanza. Hivyo basi, lugha yangu ya kwanza ni Kiswahili. Kwangu, lugha hii ni lugha mama.

*Tupe*: Sasa ninakuelewa. Ndiyo maana unaimudu vyema lugha hii. Hivi mimi ninaweza kujifunza nikazungumza kama wewe?

*Maye:* Ndiyo! Unaweza. Ukijifunza na kuitumia lugha hiyo, unaweza kuwa mahiri kuliko mimi.

*Tupe:* Asante sana, rafiki yangu! Muda wa mapumziko ulikwisha. Kengele iligongwa, wote wakakimbilia darasani.

FOR ONLINE READING ONLY

*Maswali*

1. Fafanua dhana zifuatazo kwa kuzingatia kifungu cha habari ulichokisoma:
   (b) lugha ya kwanza
   (c) lugha ya pili
2. Kwa nini lugha ya kwanza ya Maye ni Kiswahili ilhali lugha ya kwanza ya wazazi wake ni Kimasai?
3. Unafikiri kwa nini Tupe alikosea baadhi ya matamshi ya maneno ya lugha ya Kiswahili?
4. Bainisha lugha yako ya kwanza na ya pili, kisha eleza matumizi ya lugha hizo.

*Shughuli ya 5.2*

Tembelea jamiilugha yoyote iliyoko karibu na shuleni kwako, kisha fanya yafuatayo:

(a) Chunguza na kubainisha lugha yao ya kwanza na ya pili.

(b) Eleza matumizi ya lugha ulizozibainisha katika kipengele (a) kwa jamii husika.

(c) Bainisha na kufafanua changamoto ambazo jamii uliyoichunguza inakumbana nazo inapotumia lugha ya Kiswahili.

*Lugha ya kwanza*

Hii ni lugha ambayo mtu huiamili kwa mara ya kwanza kutoka kwa wazazi au walezi au jamii inayomzunguka baada ya kuzaliwa. Mtu huamili lugha ya kwanza kwa urahisi na kuwa mahiri kutokana na kukulia katika jamii inayotumia lugha hiyo. Lugha ya kwanza hujulikana pia kama lugha mama kwa sababu ni lugha ambayo hutumika katika kumlea na kumkuza mtu hadi pale anapopata ufahamu wa kuamili au kujifunza lugha zingine. Lugha ya kwanza ina sifa zifuatazo:

(i) Maneno yake huendana na mazingira alimokulia mtu, yaani hueleza vitu vinavyomzunguka;

(ii) Huamiliwa kwa kusikiliza, kuongea, na kuona vitendo vinavyohusiana na maneno yanayotamkwa;

(iii) Hufungamana na utamaduni wa jamii ambayo inatumia lugha hiyo;

(iv) Huwa na uwezo mkubwa wa kufafanua dhana mbalimbali zinazotumika katika jamii au taifa linalotumia lugha hiyo kuliko lugha zingine; na

FOR ONLINE READING ONLY

(v) Huathiri uzungumzaji wa mtu kwa kiwango kikubwa kwa kuwa huwa ndiyo lugha ya kwanza kujifunza na mtu huitumia kwa muda mrefu kabla ya kujifunza lugha nyingine.

Lugha ya kwanza hufanikisha mawasiliano kati ya mtoto, wazazi, na jamii inayomzunguka. Kwa mfano, katika mazingira ya Tanzania, wale waliozaliwa vijijini hujikuta wakiamili lugha za jamii zao kama lugha za kwanza. Kwa upande wa wale waliozaliwa mijini, huwa na nafasi kubwa ya kuamili Kiswahili kama lugha yao ya kwanza.

*Lugha ya pili*

Hii ni lugha ambayo mtu hujifunza baada ya kuamili lugha ya kwanza. Kwa mfano, Kiswahili katika jamii ya Watanzania ni lugha ya pili kwa baadhi ya watu, hususani waliokulia vijijini. Aidha, watu wengi waliozaliwa mijini hujifunza lugha ya Kiingereza kama lugha ya pili. Mtu hujifunza lugha ya pili akiwa na malengo ya kufanya jambo fulani kama vile kufanya mawasiliano na watu wa jamii nyingine katika shughuli za kijamii, kibiashara, kielimu, na kadhalika. Lugha ya pili ina sifa zifuatazo:

(i) Hufundishwa katika mazingira maalumu kama vile darasani ingawa mtu anaweza pia kujifunza katika mazingira asilia; na

(ii) Ni lugha ambayo mtu huiamili au kujifunza akiwa tayari amekwishaamili lugha ya kwanza.

Lugha ya pili huwaunganisha watu wenye lugha tofauti. Vilevile, lugha hii hutumika kama nyenzo ya kufundishia na kujifunzia. Kwa mfano, nchini Tanzania, lugha ya Kiswahili, ambayo ni lugha ya pili kwa baadhi ya Watanzania, hutumika kama lugha ya kufundishia katika elimu ya msingi, hususani katika shule za serikali.

### *Zoezi la 5.1*

1. Fafanua dhana zifuatazo:
   (a) lugha mama
   (b) lugha ya pili
3. Eleza namna mtu anavyoweza kuamili lugha ya kwanza.
4. Unafikiri kuna uwezekano wa mtoto kuamili lugha mbili tofauti kwa wakati mmoja kama lugha za kwanza? Toa sababu kushadidia hoja zako.
5. Kiswahili ni lugha ya pili kwa baadhi ya watu nchini Tanzania. Eleza athari za lugha ya kwanza zinazojitokeza kwa wazungumzaji hao.

FOR ONLINE READING ONLY

6. Unafikiri kwa nini Watanzania wengi wana umahiri wa kuzungumza lugha ya Kiswahili?

## *Kiswahili kama lugha rasmi na lugha ya taifa*

### *Shughuli ya 5.3*

Kwa kutumia vyanzo mbalimbali, vikiwamo vya ki-TEHAMA, bainisha lugha rasmi na lugha ya taifa kwa kila nchi ya Afrika Mashariki, kisha fanya yafuatayo:

(a) Eleza matumizi ya lugha rasmi ulizozibainisha kwa kila nchi.

(b) Kwa kuzingatia matumizi ya lugha nchini Tanzania, tofautisha lugha rasmi na lugha ya taifa.

*Lugha rasmi*

Lugha rasmi ni lugha ambayo huteuliwa na serikali ili itumike katika shughuli za kiserikali. Kiswahili ni lugha rasmi nchini Tanzania. Lugha rasmi inaweza kuwa moja au zaidi kama ilivyo nchini Tanzania ambapo lugha rasmi ni Kiswahili na Kiingereza. Lugha hizi ziliteuliwa kuwa lugha rasmi mnamo mwaka 1963. Kimsingi, lugha rasmi hutumika katika mawasiliano, hususani katika shughuli rasmi za kijamii, ofisini, shuleni na katika mihimili ya serikali kama vile bunge, mahakama na katika baraza la mawaziri. Lugha rasmi ina sifa zifuatazo:

(i) Hutumika katika shughuli za kiserikali zinazofanyika katika maeneo kama vile bungeni, mahakamani, katika dhifa mbalimbali za kitaifa na kadhalika;

(ii) Lazima iwe na tamko la kisheria, yaani itamkwe kisheria; na

(iii) Hutumika katika nyaraka rasmi kama vile katiba, sheria za nchi na kadhalika.

Tofauti na ilivyo, katika nchi ya Tanzania ambapo Kiswahili kina hadhi ya kuwa lugha ya taifa na lugha rasmi, lugha rasmi na lugha ya taifa zinaweza kuwa lugha mbili tofauti katika nchi moja.

*Lugha ya taifa*

Hii ni lugha ambayo huteuliwa na taifa fulani kuwa utambulisho wa taifa hilo na kutumika katika mawasiliano baina ya watu wake. Kwa upande wa Tanzania, Kiswahili ndiyo lugha ya taifa tangu mwaka 1963. Aidha, Kiswahili ni lugha ya taifa katika nchi za Kenya na Uganda. Hivyo, Kiswahili ni utambulisho wa utamaduni wa jamiilugha ya Waswahili kwa jamii nyingine duniani. Lugha ya taifa ina sifa zifuatazo:

FOR ONLINE READING ONLY

(i) Hutosheleza mahitaji ya kimawasiliano baina ya jamii za taifa linalohusika;

(ii) Hutumika kwa namna moja katika jamii mbalimbali za taifa moja;

(iii) Hutumika katika shughuli za biashara ndani ya taifa linalohusika;

(iv) Hutumika katika shughuli za kiserikali katika taifa linalohusika;

(v) Hutumika katika shughuli mbalimbali za kitaifa;

(vi) Hutumika katika vyombo mbalimbali vya habari ndani ya taifa linalohusika; na

(vii) Huwa lugha sanifu.

Taifa moja linaweza kuwa na lugha moja ya taifa au zaidi. Kwa mfano, katika nchi ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, kuna lugha nne za taifa: Kituba, Kiluba, Kilingala, na Kiswahili.

*Zoezi la 5.2*

1. Tumia mifano kueleza namna lugha ya Kiswahili inavyotumika katika shughuli mbalimbali za kiserikali nchini Tanzania.
2. Tathmini mafanikio ya Kiswahili kama lugha ya taifa nchini Tanzania.
3. Bainisha sifa za lugha ya Kiswahili kama lugha rasmi nchini Tanzania.

## *Dhana na sifa za lugha ya kimataifa*

*Shughuli ya 5.4*

Tembelea maktaba au maktabamtandao na chunguza matini zinazohusu lugha ya kimataifa, kisha fanya yafuatayo:

(a) Orodhesha lugha tano za kimataifa ulizozibaini.

(b) Fafanua sifa za lugha ya kimataifa kwa kurejelea lugha tano ulizoziorodhesha katika kipengele (a).

(c) Linganisha sifa ulizozifafanua katika kipengele (b) na sifa za Kiswahili kama lugha ya kimataifa.

*Je, wajua ?*

Lugha ya kimataifa ni lugha inayotumiwa na idadi kubwa ya watu katika mataifa mbalimbali. Hii ni lugha ambayo matumizi yake yamevuka mipaka ya taifa moja;



FOR ONLINE READING ONLY

yaani, hutumika katika mataifa mbalimbali. Husaidia katika kukidhi mahitaji ya kimawasiliano ya watu wenye lugha tofautitofauti kutoka mataifa mbalimbali. Mifano ya lugha za kimataifa ni Kiswahili, Kiingereza, na Kifaransa. Lugha ya kimataifa huwa na sifa zifuatazo:

(i) Hutumiwa na idadi kubwa ya watu katika nchi mbalimbali;
(ii) Hutumiwa kama lugha rasmi na lugha ya taifa katika mataifa mbalimbali;
(iii) Huweza kutumika kama lugha ya kutolea elimu katika nchi mbalimbali;
(iv) Hutumika katika biashara za kimataifa;
(v) Huwa na machapisho mengi;
(vi) Hutumika katika vyombo vya habari vya kimataifa;
(vii) Huweza kutumika katika shughuli za kimataifa kama imeamuliwa hivyo; na
(viii) Hutumika kwenye shughuli za kidiplomasia.

## *Sifa za lugha ya Kiswahili kama lugha ya kimataifa*

### *Shughuli ya 5.5*

Kwa kutumia vyanzo mbalimbali, vikiwamo vya ki-TEHAMA, kusanya hotuba mbalimbali zilizowasilishwa kwa lugha ya Kiswahili katika mikutano ya kitaifa na kimataifa. Chunguza hotuba hizo, kisha fanya yafuatayo:

(a) Bainisha nchi au taifa ambamo hotuba hiyo iliwasilishwa.
(b) Eleza kwa nini lugha ya Kiswahili ilikuwa mwafaka kutumika katika kuwasilisha hotuba ulizozikusanya.
(c) Tathmini changamoto zinazoweza kujitokeza kwa mtoa hotuba au hadhira kutokana na matumizi ya lugha ya Kiswahili katika maeneo ilimotumika.
(d) Eleza namna ya kutatua changamoto ulizozibainisha katika kipengele (c).

### *Je, wajua* ?

Kiswahili kama lugha ya kimataifa, kina sifa mbalimbali. Sifa hizo zimefafanuliwa katika vipengele vinavyofuata.

(a) *Lugha ya Kiswahili inatumika kutolea elimu katika mataifa mbalimbali*
Lugha ya Kiswahili inatumika kutolea elimu nchini Tanzania, hususani katika elimu ya msingi. Pia, Kiswahili kinatumika kufundishia somo la Kiswahili ndani na nje ya Bara la Afrika. Nchi mbalimbali zimeanzisha programu za somo la Kiswahili katika vyuo vikuu na kwenye taasisi zake za lugha za kigeni na hufundishwa kwa lugha ya Kiswahili.

FOR ONLINE READING ONLY

Nchi hizo ni pamoja na Ghana, Burundi, Rwanda, Komoro, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Zimbabwe, na Libya. Nchi nyingine zinazofundisha Kiswahili ni Uingereza, Ujerumani, na China kwa kutaja kwa uchache.

(b) *Lugha ya Kiswahili ina machapisho mengi*

Lugha ya Kiswahili ni miongoni mwa lugha za Kiafrika zenye machapisho mengi, yakiwa ni pamoja na majarida ya kitaaluma ya kitaifa na kimataifa ambayo huchapisha makala za ndani na nje ya nchi zinazohusu Kiswahili na taaluma zake. Miongoni mwa majarida hayo ni *Swahili Forum* (Ujerumani), Nordic *Journal of African Studies* (Uswidi), *Mwanga wa Lugha* (Chuo Kikuu cha Moi, Eldoret), *Mulika*, *Kioo cha Lugha* na *Kiswahili* (TATAKI - Chuo Kikuu cha Dar es Salaam) na *Nuru ya Kiswahili* (Chuo Kikuu cha Dodoma). Pia, kuna kamusi mbalimbali na vitabu vilivyoandikwa kuhusu Kiswahili na kwa Kiswahili ambazo hutumika sehemu mbalimbali duniani.

(c) *Lugha ya Kiswahili inatumika katika vyombo vya habari vya kimataifa*

Lugha ya Kiswahili, kama lugha ya kimataifa, inatumika katika vyombo mbalimbali vya habari vya mataifa mbalimbali. Vyombo hivyo vina vipindi vya redio na televisheni ambavyo husikika sehemu mbalimbali. Baadhi ya vyombo hivyo ni *Idhaa ya Kiswahili ya Redio Tehran (Iran), Idhaa ya Kiswahili ya Redio Japan, Redio Rwanda, Redio Burundi, Redio Komoro, Idhaa ya Kiswahili ya Shirika la Utangazaji la Uingereza (BBC), Idhaa ya Kiswahili ya Sauti ya Amerika (VOA), na Idhaa ya Kiswahili ya Shirika la Utangazaji la Ujerumani (Deutsche Welle-DW).*

(d) *Lugha ya Kiswahili inatumika katika biashara za kimataifa na utalii*

Lugha ya Kiswahili hutumika kuwezesha mawasiliano na ushirikiano baina ya nchi mbalimbali katika shughuli za kibiashara. Nchi nyingi zimesaini mikataba ya biashara za kimataifa ambapo watu wa mataifa mbalimbali hutumia lugha hiyo kuwasiliana. Baadhi ya vituo vya kibiashara hupatikana katika miji ya Beijing (China), Dubai (Falme za Kiarabu), Moscow (Urusi), New York (Marekani), na London (Uingereza). Pia, watalii na wafanyabiashara kutoka mataifa mbalimbali wanapotembelea nchi za Afrika Mashariki kama Tanzania, Kenya, na Uganda hujifunza na kutumia lugha ya Kiswahili.

(e) *Lugha ya Kiswahili inatumika katika shughuli za kidiplomasia*

Lugha ya Kiswahili inatumika katika vikao na shughuli za kidiplomasia barani Afrika na duniani kote. Lugha hii inajenga uhusiano na ushirikiano wa kimataifa. Kwa mfano, hutumika katika Jumuiya ya Afrika Mashariki; yaani, katika nchi za Tanzania, Kenya, Uganda, Rwanda, Burundi na Sudani Kusini. Pia, hutumika katika mikutano ya jumuiya

FOR ONLINE READING ONLY

hiyo, ikiwamo ya Bunge la Afrika Mashariki. Zaidi ya hayo, hutumika katika Kamisheni ya Kiswahili ya Afrika Mashariki katika kuleta maendeleo na ushirikiano wa kikanda na kimataifa katika nyanja mbalimbali. Aidha, lugha hii hutumika katika vikao vya Umoja wa Afrika na katika baadhi ya shughuli za mashirika ya Umoja wa Mataifa kama vile UNESCO, UNICEF na UNHCR.

(f) *Lugha ya Kiswahili inatumiwa na idadi kubwa ya watu katika mawasiliano ndani na nje ya Tanzania*

Lugha ya Kiswahili inatumiwa na watu wengi wa mataifa mbalimbali katika kuwasiliana ana kwa ana au kwa njia ya mtandao. Hutumika katika mawasiliano kwa njia ya mifumo maalumu ya kompyuta na simu ambayo huwezeshwa na intaneti. Kwa kutumia lugha hii, watu huwasiliana kupitia mitandao ya kijamii kama vile *Telegram, Facebook, Twitter, Instagram, WhatsApp, Imo, Viber, Skype, Zoom,* tovuti na blogu.

(g) *Lugha ya Kiswahili inatumiwa na wanamuziki wa kimataifa*

Lugha ya Kiswahili inatumiwa na baadhi ya wanamuziki wa kimataifa kwa kutumia maneno ya Kiswahili katika baadhi ya nyimbo zao. Baadhi ya wanamuziki hao ni Harry Belafonte (wa Karibe), na Miriam Makeba (wa Afrika Kusini) ambao waliimba wimbo wa Malaika.

(h) *Lugha ya Kiswahili hutumiwa kama lugha rasmi na lugha ya taifa katika mataifa mbalimbali*

Sifa nyingine ya lugha ya kimataifa ni kuwa lugha ya taifa na lugha rasmi. Lugha ya Kiswahili ni lugha ya taifa katika nchi mbalimbali, ikiwa ni pamoja na Tanzania, Kenya, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na Uganda. Pia, lugha hii ni rasmi katika baadhi ya nchi za Afrika.

### *Zoezi la 5.3*

1. Bainisha nchi za Afrika ambamo Kiswahili hutumika kama lugha rasmi.
2. Eleza matukio au shughuli walau tatu za kimataifa ambapo lugha ya Kiswahili inaweza kutumika kama lugha rasmi.
3. Fafanua faida za lugha ya Kiswahili kuwa lugha ya kimataifa kwa Watanzania.
4. Tathmini nafasi ya Kiswahili kama lugha ya kimataifa katika tasnia ya sanaa.

FOR ONLINE READING ONLY

## Umahiri wa lugha

**Shughuli ya 5.6**

Fanya utafiti mdogo kuhusu matumizi ya lugha ya Kiswahili katika jamii inayokuzunguka, kisha fanya yafuatayo:

(a) Eleza mapungufu yanayojitokeza katika jamii hiyo inapotumia lugha ya Kiswahili.

(b) Unafikiri mapungufu uliyoyabaini katika kipengele (a) yanasababishwa na nini?

(c) Pendekeza namna ya kupunguza au kuondoa mapungufu uliyoubaini.

**Je, wajua ?**

Umahiri wa lugha ni uwezo wa mtu kumudu stadi nne za lugha, ambazo ni kusikiliza, kuzungumza, kuandika, na kusoma, katika mawasiliano yake ya kila siku pamoja na kuuelewa utamaduni wa lugha inayohusika. Umahiri huo unatokana na kumudu vizuri vipengele vya lugha kama vile msamiati, miundo, matamshi, maana, na mbinu za utumiaji wa lugha katika miktadha mbalimbali. Watumiaji wa lugha ambao bado hawajamudu stadi hizo za lugha huwa si mahiri wa lugha.

**Mambo yanayomwezesha mtu kuwa mahiri wa lugha**

Mambo ya msingi yanayoweza kumsaidia mtumiaji wa lugha kupata umahiri wa lugha hiyo yanafafanuliwa katika vipengele vinavyofuata.

(a) *Matumizi ya lugha katika shughuli mbalimbali*

Shughuli mbalimbali anazofanya mzungumzaji wa lugha humwezesha kumudu stadi za lugha hiyo. Kwa mfano, shughuli zinazohusiana na elimu, kusoma vitabu na magazeti, kusikiliza redio na televisheni; kuhudhuria mikutano mbalimbali; na kuhudhuria na kushiriki katika shughuli mbalimbali katika maeneo kama vile mahakamani, kanisani, misikitini, na kadhalika. Kadiri mtu anavyozidi kushiriki katika shughuli kama hizi, ndivyo anavyozidi kukuza umahiri wake wa lugha.

(b) *Kusomea lugha kwa kiwango cha juu*

Umahiri pia hupatikana kwa kujifunza lugha inayohusika kwa kiwango cha juu. Jambo hili humpa mtu uwezo wa kubainisha na kutumia mitindo mbalimbali ya lugha katika mazingira mbalimbali. Kwa mfano, kuna wataalamu mbalimbali wa lugha ya Kiswahili ambao wamesomea lugha hiyo katika ngazi mbalimbali za elimu kama vile stashahada, shahada ya awali, shahada ya umahiri, na shahada ya uzamivu.

FOR ONLINE READING ONLY

Umahiri wa lugha wa watu hawa ni mkubwa. Wengine wamekuwa mahiri kwa kuwa wamekuwa wakiitumia lugha hiyo katika miktadha na taaluma mbalimbali.

(c) **Kuchangamana na watumiaji mahiri wa lugha**

Kuchangamana na wazungumzaji wa lugha inayohusika husaidia kuongeza kiwango cha umahiri. Kwa mfano, mtu akichangamana na wazungumzaji wa lugha ya Kiswahili, huweza kumudu zaidi lugha hiyo kwa kusikiliza na kujirekebisha, au kurekebishwa na watumiaji hao mahiri.

*Athari za kukosa umahiri wa lugha*

Kukosa umahiri kunaweza kusababisha athari mbalimbali. Athari hizo zinafafanuliwa katika vipengele vinavyofuata.

(a) **Athari katika matamshi**

Katika jamii ambamo mna lugha zaidi ya moja, mtumiaji wa lugha zaidi ya moja, asipokuwa makini, anaweza kuathiri utamkaji wa maneno katika lugha ya pili. Kwa mfano, Mkurya akizungumza neno la Kiswahili, anaweza kutamka **chakura** badala ya **chakula**. Hii inatokana na athari ya lugha yake ya kwanza ambayo ni Kikurya.

(b) **Athari katika msamiati**

Baadhi ya wazungumzaji wa lugha katika jamii yenye lugha zaidi ya moja wanaweza kuchanganya maneno ya lugha mbili wakati wa mazungumzo. Kwa mfano, mzungumzaji anaweza kuchanganya lugha ya Kiswahili na Kiha kwa kusema "Ninaenda mtoni kuvoma maji" badala ya kusema "Ninaenda mtoni kuchota maji".

(c) **Athari za kimuundo**

Muundo wa tungo huweza kutofautiana kati ya lugha moja na nyingine. Tofauti hizo huweza kujitokeza katika mpangilio wa maneno au upatanisho wa kisarufi. Mathalani, mzungumzaji wa lugha ya Kihehe hutumia wingi anapozungumza na mtu ambaye anamheshimu. Kwa mfano, anapozungumza Kiswahili kama lugha ya pili, anaweza kuuliza, "Baba, mtakula nini?" akimaanisha, "Baba utakula nini?" Hii hutokana na athari ya lugha ya Kihehe katika kipengele cha upatanisho wa kisarufi.

(d) **Athari katika maana**

Athari hii hujitokeza wakati kunapokuwa na maneno ya lugha mbili yanayoeleza dhana moja. Neno la lugha moja linaweza kuwa na maana pana zaidi kuliko lugha zingine. Kwa mfano, maneno katika tungo, "Wash your hands" yanaweza kutafsiriwa kwa Kiswahili kama "Osha mikono yako" wakati kiuhalisi katika Kiswahili tunasema, "Nawa mikono yako."

FOR ONLINE READING ONLY

**Mambo yanayopoteza umahiri wa lugha**

Kuendelea kuwa na umahiri wa lugha hutegemea ni kwa kiasi gani mtu anaendelea kutumia lugha husika. Umahiri wa lugha unaweza kuathiriwa na mambo yanayoelezwa katika vipengele vinavyofuata.

(a) *Matumizi madogo ya lugha inayohusika*

Umahiri wa lugha kwa mzungumzaji hudumaa ikiwa mzungumzaji haitumii lugha hiyo mara kwa mara. Kwa hiyo, kadiri mtumiaji anavyoendelea kuitumia lugha, ndivyo anavyokuza umahiri wake katika lugha hiyo. Asipoitumia lugha hiyo, hudumaza umahiri wake.

(b) *Kupunguza kusoma machapisho na kusikiliza vyombo vya habari*

Mtumiaji wa lugha anapopunguza kusoma machapisho kama vile vitabu, majarida, magazeti, vipeperushi, na kusikiliza vipindi mbalimbali vya redio na televisheni, huweza kufifisha umahiri wake katika lugha inayohusika. Kusoma na kusikiliza vyombo vya habari kunasaidia kuongeza msamiati na ujuzi wa miundo na mitindo mbalimbali ya lugha na matumizi yake katika miktadha stahiki.

(c) *Kuishi katika jamii isiyotumia lugha inayohusika*

Umahiri wa lugha hukuzwa iwapo mtumiaji wa lugha ataishi katika jamii inayotumia lugha hiyo. Iwapo ataishi katika jamii ambayo haitumii kabisa lugha hiyo, basi umahiri wake unaweza kupungua.

(d) *Kuchanganya lugha katika matumizi*

Kuchanganya lugha mbili au zaidi katika matumizi hufifisha umahiri wa lugha. Kila lugha ina muundo na mtindo wake kimatumizi. Kuchanganya lugha mbili au zaidi katika matumizi kunaharibu sarufi na utaratibu wote wa matumizi ya lugha inayohusika. Kwa mfano, baadhi ya watu waliosoma, hasa nchini Tanzania, huchanganya lugha ya Kiswahili na Kiingereza. Tabia hii hufifisha umahiri katika lugha zote mbili.

(e) *Kukosa ari ya kutumia lugha inayohusika*

Baadhi ya watu hukosa ari ya kutumia lugha yao kwa sababu mbalimbali kama vile kuinasibisha na jamii fulani, uduni, kundi fulani la kisiasa, au kundi la dini fulani. Hali hii hupunguza umahiri wao katika lugha hiyo.

(f) *Kubadili mfumo wa maisha*

Wakati mwingine, mtumiaji wa lugha anapobadili mfumo wa maisha, hupunguza au hupoteza umahiri wa lugha. Kwa mfano, mtu anapoingia na kuishi katika jamii ambamo kiwango na ujuzi wa lugha alionao hauhitajiki sana, hujikuta akitumia kiwango cha

FOR ONLINE READING ONLY

chini cha lugha. Jambo hili hupunguza umahiri wake katika lugha.

### Tamrini ya 5

1. Fafanua dhana zifuatazo:
   (a) lugha ya kimataifa
   (b) lugha rasmi
3. Watanzania wengi wana lugha zao za makabila lakini lugha ya kwanza kwa walio wengi, hususani vijana na watoto, ni Kiswahili. Kwa kutumia mifano, eleza sababu za kujitokeza kwa hali hiyo.
4. Kwa kutumia mfano wa lugha ya Kiswahili, eleza tofauti kati ya lugha ya taifa na lugha ya kimataifa.
5. Kwa kutumia mifano, eleza ni kwa nini lugha ya Kiswahili inafaa kuwa lugha rasmi nchini Tanzania.
6. Unafikiri ni kwa nini baadhi ya Watanzania wanakosa umahiri wa kutumia Kiswahili katika mawasiliano?
7. Rugendo alizaliwa mkoani Kagera na kuamili Kihaya kama lugha yake ya kwanza. Akiwa na umri wa miaka 6, alihamia jijini Arusha na kujifunza Kiswahili. Alikisahau Kihaya na kubaki na lugha moja tu ya Kiswahili mpaka alipofika Kidato cha Kwanza na kujifunza Kiingereza. Kutokana na kisa hiki, lugha mama ya Rugendo ni ipi? Kwa nini?

FOR ONLINE READING ONLY

# Sura ya Sita

# Uhariri

## Utangulizi

*Andiko lolote linaweza kueleweka kwa msomaji kutokana na ubora wake wa kiuandishi. Ili andiko liwe na ubora wa kiuandishi, ni lazima lifanyiwe uhariri. Katika sura hii, utajifunza kanuni za uhariri na vipengele vya lugha na maudhui vinavyozingatiwa katika uhariri. Vilevile, utajifunza namna ya kutumia alama mbalimbali za uhariri wakati wa kuhariri. Aidha, utafanya uhariri wa matini za kawaida. Sanjari na hayo, utajifunza kutathmini matini zilizohaririwa na wahariri wengine. Umahiri utakaoujenga utakuwezesha kuhariri matini za kawaida na kutathmini uhariri uliofanywa na wahariri wengine.*

**Fikiri**

Uandishi bila uhariri

## Kanuni za uhariri

**Shughuli ya 6.1**

**Chunguza matini ifuatayo, kisha ihariri ili iwasilishe ujumbe uliokusudiwa. Bainisha mambo uliyoyazingatia katika kuihariri matini hiyo.**

Tanzania ni nchi mzuri na yenye kupendeza sana. Nchi hii ina vyanzo vyingi vya maji ambavyo ni bahari, maziwa, mito na mabwawa. Hata hivyo, inapata mvua nyingi sambamba na vyanzo hivyo. Vilevile, ina misitu mizito yenye miti mirefu, vichaka na majani mengi. Lakini ina ardhi kubwa yenye rutuba na inayolima mazao mbalimbali. Watanzania hunufaishwa sana na rasilimali hizi, yaani wanapata faida kubwa sana.

FOR ONLINE READING ONLY

## Je, wajua ?

Ili uhariri ufanyike kwa ufasaha na kwa ufanisi, mhariri hana budi kuzingatia kanuni mbalimbali za uhariri. Kanuni hizo ni pamoja na usahihi, uwazi, uwekevu, uasili, na urari/ulinganifu. Hizi ni kanuni muhimu sana katika uhariri; huliwezesha andiko kuwasilisha ujumbe wa mwandishi kwa namna ilivyokusudiwa.

*Usahihi*

Hii ni hali ya andiko kutokuwa na makosa. Hivyo, mhariri anapaswa kuahakikisha andiko halina makosa ya kimantiki, kimaudhui, kisarufi na kiuandishi. Kanuni hii inapaswa kuzingatiwa kila wakati uhariri unapofanyika na katika kila neno, tungo, aya na matini. Taarifa inayotolewa inapaswa iwe na usahihi na isipotoshwe; uteuzi wa maneno unapaswa uwe sahihi; mpangilio wa mawazo unapaswa kuwa mzuri; na lugha inayotumika inapaswa kuwa fasaha.

*Uwazi*

Kanuni hii inahusu kueleweka kwa ujumbe na maana iliyokusudiwa na mwandishi. Hivyo, mhariri anapaswa kuhakikisha kwamba ujumbe si fiche. Vilevile, uwazi unamaanisha kuwapo kwa taarifa zote zinazohitajika, lugha inayoeleweka kulinagana na muktadha, usahihi wa matumizi ya alama mbalimbali za uandishi, na utumiaji wa maneno na sentensi zinazoeleweka kirahisi kwa msomaji.

*Uwekevu*

Hii ni kanuni inayohusu kuepuka mrundikano wa taarifa zisizohitajika, kuepuka lugha ya mzunguko na matumizi ya maneno mengi ilhali kuna neno moja lenye kueleza dhana husika kwa ukamilifu, na kuwa na sentensi fupifupi zinazoeleweka. Hivyo, uchache wa maneno unahitajika.

*Uasili*

Kanuni hii inahusu kutunza/kudumisha uasili wa andiko wakati wa uhariri. Hii inamaanisha kutunza/kudumisha mtindo wa mwandishi na mtindo wa uandishi wa uwanja husika.

*Urari*

Kanuni hii inamtaka mhariri ahakikishe kuwa mwandishi hachanganyi istihali katika matini moja wala hahamihami kimawazo. Kwa hiyo, mhariri anapofanya kazi yake, anapaswa kuhakikisha kwamba istilahi na dhana zinazotumiwa zinatumika na kurejelewa kwa namna inayofanana. Hii itasaidia kulifanya andiko lisimyumbishe msomaji.

FOR ONLINE READING ONLY

Ili kutekeleza kwa usahihi kanuni hizi, mhariri anapaswa kuwa anajiuliza na kupata majibu ya maswali yafuatayo:

**Nini?** Swali hili linahusu kitu au ujumbe ulioandikwa. Linamsaidia mhariri kuelewa uteuzi mwafaka wa msamiati, lugha ya kutumia na namna ya kueleza suala husika.

**Nani?** Swali hili linahusu hadhira iliyoandikiwa. Humsaidia mhariri kujua uteuzi stahiki wa msamiati kulingana na hadhira husika na, lugha inayotumika (rahisi au ngumu, yenye istilahi nyingi au chache).

**Kivipi?** Swali hili linaangazia namna matini ilivyoandikiwa; je, imeandikwa kwa mtindo gani na ujumbe umetolewa kwa lugha gani? Hapa, matini inaweza kuwa na mtindo wa kishairi, barua, kumbukumbu, na kadhalika.

**Lini?** Swali hili linamwongoza mhariri kujua matini imeandikwa wakati gani na hadhira iko katika wakati gani. Humsaidia kufanya uteuzi wa maneno kulingana na wakati husika.

**Wapi?** Swali hili huhusu mazingira inakokwenda matini au iliko hadhira. Mazingira haya yana umuhimu mkubwa katika uteuzi wa maneno, mtindo wa uandishi na uchangamani wa sentensi. Hivyo, ni muhimu kuelewa tofauti za kimazingira kwani matumizi ya lugha hutawaliwa na mazingira.

## *Vipengele vya lugha na maudhui vinavyozingatiwa katika uhariri*

### *Shughuli ya 6.2*

Chunguza habari ifuatayo kisha fanya yafuatayo:

(a) Bainisha makosa ya kiuandishi yanayojitokeza na aina zake.

(b) Ihariri matini hiyo ili kuyaondoa makosa hayo.

(c) Bainisha mambo yaliyokuongoza katika kuhakiki usahihi wa uhariri ulioufanya?

Ndugu Mhariri,

Naomba kuchukua fursa hii kuwakilisha maoni yangu kwa njia ya kupitia ukurasa wa gazeti lako. Maoni yangu yanaelekezwa katika mfumo wa elimu hususani mchango wa teknolojia katika kuboresha utoaji na upataji wa elimu kwa lengo na madhumuni ya kuboresha mfumo wa utoaji na upataji wa elimu kuna mambo mengi ambayo

FOR ONLINE READING ONLY

teknolojia inaweza kutumika kuyafanya. Mosi, teknolojia inaweza kutumika kama chanzo cha maarifa mbalimbali. Mathalani wanafunzi na walimu wanaweza kupakua vitabu, majarida na machapisho mbalimbali ambayo yatatumika kuimarisha maarifa yanayopatikana katika somo linalofundishwa.

Pili, teknolojia inaweza kutumika katika uwasilishaji wa somo darasa. Katika hili, mwalimu anaweza kutumia kompyuta na projekta ambavyo vitamwezesha kufundisha mambo mengi kwa muda mrefu na kwa ufanisi. Aidha, mwalimu anaweza kuonesha mambo mbalimbali kwa kuyatengeneza kwa programu za kompyuta au kuyapakua kwenye mtandao na kuyaonesha darasa kwa kutumia projekta kama mifano.

Tatu, teknolojia inaweza kutumika kufundishia darasani kubwa kwa wakati mmoja. Hata hivyo, inaweza kutumika katika kuweka usawa kwa darasa yote, mwalimu mmoja wa somo fulani anaweza kufundisha pia nchi nzima na walimu wengine wakawa wanatumika katika kuwawezesha wanafunzi kuelewa somo linalo fundishwa na kusimamia ufanyaji wa mazoezi kama ilivyo nchi China.

Aidha, ninapenda kutoa maoni haya kupitia ukurasa huu ili jamii ione umuhimu wa kutumia teknolojia katika kuboresha elimu nchini mwetu.

Ni mimi,

Mkereketwa wa Teknolojia,

S.L.P. 2013,

Mpanda, Katavi. Simu: 0141-010209.

**Je, wajua ?**

Uhariri wa matini umegawanyika katika aina mbili, uhariri wa lugha na uhariri wa maudhui. Aina hizo zinafafanuliwa katika vipengele vinavyofuata.

**1. Uhariri wa lugha**

Katika uhariri wa lugha, kuna vipengele au masuala kadhaa ambayo mhariri anapaswa kuyazingatia. Masuala hayo ni: uakifishaji, ushikamani, tahajia, upatanisho wa kisarufi, uteuzi wa msamiati, na muwala.

**(a) Uakifishaji**

Huu ni utumiaji wa alama za uandishi zinazoliwezesha andiko kusomeka vizuri na kutoa maana angavu. Alama kuu za uandishi kama vile kiulizo, nukta na alama ya mshangao hujumuisha pia matumizi ya herufi kubwa. Hivi ni kusema, alama hizo zinapotumika, tungo zinazozifuata huanza kwa herufi kubwa.

FOR ONLINE READING ONLY

**(b) Ushikamani**

Hii ni dhana inayorejelea utumizi wa lugha au vipengele vya kisarufi ili kuweka muunganiko wa sentensi na sentensi, aya na aya, na wazo na wazo katika matini. Husadia kutiririsha vizuri wazo linaloelezewa. Viungo vinavyotumika ni kama vile viungo vya kuongeza wazo: *aidha, pamoja na hayo, vilevile, sanjari na hayo, jambo jingine,* n.k.; viungo vya kulinganua: *lakini, wakati, ilhali, hata hivyo*; viungo vinavyohitimisha: *hivyo, kwa hiyo, kwa ujumla, kwa kuhitimisha,* n.k.; viungo vya kutolea mifano: *mathalani, kwa mfano, kama vile,* n.k. na vingine vingi. Vyote hivi huunganisha sentensi na sentensi au wazo na wazo na kulifanya andiko liwe kitu kimoja. Ala nyingine za ushikamani ni urejezi, ubadala, udondoshaji, uwakilishaji, na uunganishaji. Ufuatao ni mfano wa matini iliyoshikamanishwa vizuri.

*Wanafunzi waliosimamishwa masomo kutokana na utukutu wao wamefukuzwa shule. Aidha, taarifa za utukutu wao zimeingizwa katika kanzidata ya taarifa zao za uraia. Taarifa hizo zitatazamwa hata wakati wa kuajiriwa. Wao walidhani wanawakomoa walimu; kumbe walikuwa wanajikomoa wenyewe.*

Katika kifungu hiki, maneno *wao* na *wenyewe* ni vibadala vya neno *wanafunzi'*; na kifungu cha maneno *taarifa hizo* kinarejelea *utukutu* na *kufukuzwa shule*.

**(c) Tahajia**

Hii huhusu usahihi wa umbo la neno, yaani uandishi wa neno kwa usahihi kulingana na taratibu za uandishi za lugha inayohusika.

**(d) Upatanisho wa kisarufi**

Hii ni dhana inayohusu ulinganifu wa kiambishi cha ngeli (au umoja na wingi katika nomino kiima au kivumishi) na viambishi vingine katika kitenzi au kivumishi ndani ya tungo.

**(e) Uteuzi wa msamiati**

Hurejelea utumiaji wa msamiati sahihi kulingana na dhana inayoelezwa, uga wa kitaaluma unaohusika na muktadha kwa ujumla wake.

**(f) Muwala**

Huu ni muumano wa wazo na wazo ambao hujenga mtiririko wa mawazo katika matini. Kwa sehemu kubwa, huwezeshwa na ushikamani na mpangilio mzuri wa mawazo. Muwala huleta mtiririko wa mawazo wenye mantiki. Husaidia kuunganisha wazo la kwanza na linalofuatia, wazo kuu na ushahidi wake, na kadhalika. Hulenga kulifanya andiko zima liwe na uhusiano na liwe na maana. Aidha, muwala huhusu kuzingatia kanuni zote za kisarufi za lugha husika kama vile kuhakikisha kwamba tungo zina pande mbili, kiima na kiarifu; sentensi zimekamilika, zinasomeka na zenye urefu unaokubalika.

FOR ONLINE READING ONLY

## 2. Uhariri wa maudhui

Katika uhariri wa maudhui, mhariri humakinikia ujumbe au maana iliyokusudiwa na mwandishi ambayo anakusudia iifikie hadhira yake. Katika kuhariri maudhui, mhariri anapaswa kuzingatia usahihi, ulinganifu na utoshelevu wa taarifa; mantiki; na kuendana kwa maudhui na viwango vya walengwa.

### (a) Usahihi, ulinganifu na utoshelevu wa taarifa

Mhariri anatakiwa kuhakikisha ukweli wa taarifa na kuepuka upotoshaji wa kile kilichokusudiwa na mwandishi. Kadhalika, anatakiwa kuhakikisha kuwa taarifa hizo zina muumano wa pamoja. Aidha, mhariri anapaswa kuhakikisha kuwa maana au taarifa inayotolewa ni toshelevu. Kusiwe na udondoshaji wa taarifa muhimu wala uongezaji wa taarifa isiyohitajika. Hili hufanyika kwa kuwa na uangalifu katika kudondsha au kuongeza taarifa wakati wa uhariri.

### (b) Mantiki

Hii ni dhana inayohusisha ukubalifu na ukweli wa hoja inayotolewa kuelezea au kushadidia jambo fulani. Mhariri anapaswa kuunyoosha vizuri ujumbe au hoja na kuepuka uongo au udanganyifu, utata na ukinzani wa hoja au maelezo, na ukinzani wa kimantiki. Kwa mfano, kuandika '*Wasichana wa kike wana busara sana*' au '*Darasa lina wasichana kumi na vijana wanane*'ni kuleta ukinzani wa kimantiki. Hii ni kwa sababu hakuna wasichana wa kiume, na vijana hujumuisha pia wasichana.

### (c) Kuendana kwa maudhui na viwango vya walengwa

Miongoni mwa maswali ambayo mhariri anapaswa kujiuliza ni "nani" ambapo mhariri anapaswa kufahamu mwandishi amelenga hadhira ya aina gani. Kila andiko huwa na walengwa wa kiwango fulani ambacho kinaweza kuamuliwa na elimu yao, umri wao, mahali wanapoishi, vipato vyao na kadhalika. Kwa hiyo, maudhui ya andiko yanapaswa kuendana na kiwango cha walengwa. Maudhui yasiyoendana na kiwango cha walengwa ni kinyume cha matakwa ya kanuni ya uwazi. Mhariri anapohakiki kama maudhui yanaendana na kiwango cha walengwa, anapaswa kujiuliza maswali mengine yanayohusiana na swali kuu la 'nani?'. Maswali hayo ni: "Je, msomaji ni wa umri gani? Ni wa jinsia gani? Anafanya kazi gani? Ana kiwango gani cha elimu? Anapendelea nini? Ana uzoefu au tajiriba gani? Maswali haya yatamsaidia kupima iwapo maudhui ya andiko yanaendana na kiwango cha walengwa.

**Zoezi la 6.1**

1. Kwa kutumia vyanzo mbalimbali vya maktabani na mtandaoni, eleza tofauti baina ya muwala na ushikamani.
2. Chunguza habari ifuatayo, kisha:

FOR ONLINE READING ONLY

(a) Bainisha viungo na ala zote za ushikamani na muwala zilizomo katika habari hiyo.

(b) Hariri na kuiandika habari hiyo kwa kuzingatia vipengele vyote ulivyojifunza.

**Nasaha za mzazi**

*Mtoto wetu mpendwa, kwanza kabisa ninapenda kukupongeza kwa jitihada na juhudi zako katika masomo. Sisi, wazazi wako, tunafurahi sana mioyoni mwetu kila tunapokuona ukizidi kuyapenda masomo, kusoma kwa bidii, kupenda shule na kujiepusha na makundi ya wenye tabia mbaya, ikiwamo kuacha masomo au kujiingiza katika vitendo viovu kama uasherati, utumiaji wa dawa za kulevya na kadhalika. Mwanetu, hatuwezi kusema kila wakati ila tunasikia kujivunia wewe kila tunapoona unafaulu kutoka kiwango kimoja cha elimu kuingia kingine. Kazi yetu ni kukuombea tu kwa Mungu na kuhakikisha unapata mahitaji yanayotakiwa ili uendelee na masomo. Kwa hakika, unatuheshimisha sana hata mtaani kwetu.*

*Pamoja na hayo yote mwanagu, tunapenda usisahau kuwa sisi wazazi wako tuna hali ngumu ya kimaisha. Tunapambana kufa na kupona ili usikwame katika masomo yako. Tunajua kuwa kuna nyakati hupati mahitaji yako yote kama ilivyopaswa, ila tunakuomba usiutupe uvumilivu wako na kujiingiza katika kujitafutia hayo mahitaji kwa njia za kuuza utu, afya, ndoto na mustakabali wako. Tunajua huko shuleni kuna wanafunzi wengine ambao wanatoka katika familia zenye uchumi wa juu na wengine uchumi wa kati. Kwa namna moja au nyingine unaweza kushawishiwa na hali ya utoshelevu wa mahitaji yao, lakini tunakusihi usitafute njia mbadala ya kufikia uhitaji wako. Wala usijiingize katika mahusiano ya kimapenzi ya jinsi moja wala jinsi mbili ili upate mahitaji. Mwanetu tunakusihi sana uyazingatie hayo ili uzidi kutufurahisha, kujenga mustakabali wako na watoto wako hapo baadaye.*

*Sanjari na hayo, tunakunasihi kwamba usijiingize katika ahadi za kuoana ukiwa bado katika masomo, hasa shule hizi za sekondari. Suala la kuoana lipo na sisi tunakuombea kwa Mungu upate mwenza mwema katika maisha yako ambaye mtaishi kwa furaha, amani, mafanikio na utulivu. Hata hivyo, si vyema kuyaanzisha mahusiano hayo kabla ya wakati muafaka kufika. Wanafunzi wengi huwa wanadanganyana katika ngazi hii ya masomo ila wakishafika vyuo vikuu hutelekezana, huumizana mioyo na huwa hawaoani. Huko huwaona wengine. Pia, wengi katika umri huu huwa wanaongozwa na tamaa tu za mwili na hujikuta wanasababishiana ujauzito usiotarajiwa, kuambukizana magonjwa au kuharibu utulivu katika masomo hata kutofanya vizuri.*

*Mwisho kabisa, mwanetu, kumbuka kuwa sisi wazazi wako hatuna kipato kikubwa.*

FOR ONLINE READING ONLY

**Tunalima mahindi na kuuza ili ninyi msome. Pia, tunapika maandazi na kuamka alfajiri kwenda kuuza, tunatembeza uji na kuungua na jua siku nzima kutembeza karanga. Haya yote ni kwa ajili yenu msome, mle na mfanikiwe katika maisha yenu. Tunakutakia masomo mema, afya njema na safari njema. Kesho alfajiri, saa kumi na nusu tutaamkia sokoni kulangua karoti na ndizi za gengeni; hivyo, hatutaonana. Kwa heri.**

3. Tafuta matini yoyote iliyoandikwa, kisha eleza jinsi ilivyozingatia au kukiuka vipengele vya kiuhariri vya maudhui na lugha.

## *Alama za uhariri*

### *Shughuli ya 6.3*

Chunguza kifungu cha habari kifuatacho, kisha fanya yafuatayo:

(a) Bainisha alama za uhariri zilizotumika.

(b) Eleza maana za alama zilizotumika katika kifungu ulichokichunguza.

(c) Eleza nini kinachotakiwa kufanyika kwa mujibu wa maelekezo ya alama za uhariri zilizotumika.

Uhariri ni hatua muhimu sana katika uandishwa andiko lolote lile. ikiwa huhariri autafanyika ipasavyo jinsi andiko litakosa ushikamani, muwala na ujumbe hautafika kama ulivyo kusudiwa. Hivyo, ni lazima uhariri ufanyika kabla andiko halijapelekwa hadhara lengwa.

### *Je, wajua*

Mhariri, anapofanya uhariri, anapaswa kutumia alama za uhariri katika andiko husika ili kumrahisishia mwandishi kuelewa kilichorekebishwa. Alama hizo ziko nyingi na kila moja inatoa taarifa yake ya kiuhariri. Hata hivyo, inashauriwa kwamba mhariri atumie alama ambazo zinaeleweka kwa mteja wake au aweke ufunguo. Aidha, marekebisho ya makosa ya uhariri yanapaswa kufanywa ndani ya andiko kwa kutumia alama hizo. Mhariri anaweza kuhamisha sentensi au neno kwa kutumia alama hizo. Ikiwa kuna sentensi imeongezeka, basi alama zitatumika kuonesha inapaswa kuingia wapi. Hivyo, alama hizo ni muhimu sana katika uhariri. Tazama kielelezo kinachofuata kwa ufafanuzi zaidi.

FOR ONLINE READING ONLY

| Na. | Alama | Maelezo | Mfano |
|---|---|---|---|
| 1 | ≡ | Tumia herufi kubwa | Anaishi mkoa wa tabora |
| 2 | / | Tumia herufi ndogo | Amenunua daftari na Kalamu |
| 3 | tah. | Kosa la tahajia | Ukisoma kwa bidii utafaulu mtihani |
| 4 | ⊙ | Weka nukta | Wanafunzi wenzetu wameripoti leo |
| 5 | ∂ | Futa/dondosha | Waliokuja wamefanikiwa kupata mgawo |
| 6 | ^ | Chopeka neno | Tunapenda jinsi wanavyocheza mpira wa pete |
| 7 | ^ | Weka mkato | Mazao yanayolimwa Tanzania ni pamoja na mahindi, viazi, mtama mpunga, adizi na maharage |
| 8 | ∼ | Badilishanisha nafasi za maneno/herufi | Tunataka namna kuona alavyo chakulache |
| 9 | V | Weka ritifaa | Walinunua ngombe wawili |
| 10 | VV | Weka mnukuo | Rais alisema, Tushikamane na kuwa na umoja |
| 11 | # | Acha nafasi | Uvivu husababishamtu umaskini |
| 12 | ◌ | Punguza/ondoa nafasi | Watanzania ni wakarimu sana |
| 13 | ¶ | Anza aya mpya | Nchi ya Tanzania imejaa utajiri. Hii ni kutokana na wingi wa maliasili zilizomo nchini humu. ... ¶Aidha, nchi hii inapata vipindi vya mvua na vya jua ambavyo vinafaa kwa kilimo cha mazao karibu yote. Hakika hii ni nchi nzuri sana |
| 14 | Stet | Acha ilivyo | Waafrika wanapenda kuishi kwa umoja. |
| 15 | ⊂ | Unganisha mistari/aya | Kula matunda kunafanya mwili upate vitamini zinazotakiwa mwilini.<br>Vilevile, husaidia kuufanya mwili utengeneze kingamwili za kutosha. |
| 16 | Z | Anza mstari mpya | Kula matunda kunafanya mwili upate vitamini zinazotakiwa mwilini. vilevile husaidia kuufanya mwili utengeneze kingamwili za kutosha. |
| 17 | ‖ | Linganisha mistari | Uandishi wenye makosa unachosha kusoma. Hivyo, ni muhimu kufanya uhariri wa lugha na maudhui kwa kila andiko hata kama lina mistari michache. |
| 18 | ⊓⊔ | Hamisha kifungu cha maneno | Leo, katika kipindi cha Kiswahili, tutajifunza kuhariri matini sahili. |

FOR ONLINE READING ONLY

| Na. | Alama | Maelezo | Mfano |
|---|---|---|---|
| 19 | | Sogeza kulia | Kutumia alama katika uandishi husaidia kutotumia nafasi kubwa katika kutoa maoni. |
| 20 | | Sogeza kushoto | Usipojua matumizi ya alama za uhariri utapata ugumu katika kuhariri matini. |

**Kielelezo Na. 6. 1:** *Baadhi ya alama za uhariri*

### Je, wajua

Pamoja na alama za uhariri zilizooneshwa katika Kielelezo Na. 6.1, baadhi ya maelekezo ya uhariri yanaweza kutolewa kwa maneno au vifupisho ambavyo mhariri ataviwekea ufunguo ili mteja wake avielewe kwa urahisi. Mathalani, *laza* huweza kutumika kumaanisha *tumia hatimlazo* na *koza* kwa maana ya *tumia hati iliyokoza.*

## Kuhariri na kutathimini matini za kawaida

### Shughuli ya 6.4

1. Hariri matini ifuatayo kwa kuzingatia kanuni za uhariri, vipengele vinavyopaswa kuzingatiwa katika uhariri, na matumizi sahihi ya alama za uhariri.

*Chalimo alikuwa ni kijana mdadisi na anaye penda kufanya vitu vinavyo husiana na teknolojia tangu utotoni Baada ya kumaliza masomo yake ya Kidato cha Sita alijuinga na Chuo Kikuu ambapo alipata shahada ya sayansi ya kompyuta. Alipokuwa chuo, aliona wanafunzi wenzake wakipata changamoto za kuaribikiwa na kompyuta ambapo gharama za ufundi zilikuwa kubwa sana. Chalimo alipata wazo la kipekee la kuainzisha kazi ya ufundi wa komppyuta pindi atakapohitimu ili kuwawezesha watu kupata huduma kwa urahisi na nafuu kwa gharama. Chalimo alipohitimu masomo yake ya shahada aliamua kuanzisha kazi hiyo yeye mwenyewe badala ya kutafuta kazi za kuajiriwa.*

*Chalimo alianzakwakutumiaakibayakeyafedhakuanzishaajilayakendogo.Kadiri sikuzilivyosogeaaliendeleakufanyakazikwabidiihukuakiendeleakujifunzakupitia programuzakwenyemitandaombalimbali.Alitumiamtandaowakijamiikujitangaza na kuwasiliana na wataalamu wengine kwa ajili kupata mwongoz na maoni yao. Miezi kadhaa baada ya kupita ya kazi nzito, chalimo alianza kuitangaza katika*

FOR ONLINE READING ONLY

**mikutano ya tekenolojia na kwenye majukwaa ya kwenye intaneti. Kazi yake ilipata umaarufu haraka na watu wengi walivutiwa na huduma zake zilizokuwa ni rahisi kupatikana.**

**Kutokana kuongezeka kwa idadi ya wateja Chilamo alianza kupata kipato kikubwa alikuza timu yake kwa kuajiri watalamu wengine wa teknolojia na kukarabati huduma zake. Baada ya muda kupita alikuwa na mtaji mkubwa kiasi cha kuanza kuagiza vifaa vya komputa nje ya Nchi. Leo hii, Chalimo ni mjasiria mali mwenye mafanikio katika ufundi wa kompyuta. Ufundi na biashara yake mpya inamwingizia kipato kikubwa kweli. Hivi sasa aliweza kutoa ajira kwa vijana wa kike na wavulana wa kiume wengine na kuwa na kuwa ni miongoni mwa waajiriwa wengine nchini tanzania. Usubutu wake umemwezesha kupata umaharufu, kupata mafanikio katika maisha na kuwa mwajiri wa vijana wenzake.**

2. Chunguza habari ifuatayo, kisha bainisha ubora na upungufu wa kiuhariri unaojitokeza halafu ihariri upya kwa kuzingatia kanuni na vipengele muhimu vya kiuhariri.

**Magongo ni kijana aliyeishi kijiji cha Lufu. Kijana huyu alipendwa sana na wana kijiji kwasababu ya tabia yake ya kujituma na kufanya kazi kwa bidii. Siku moja kulikuwa na uchaguzi wa uongozi wa kijiji. Baadhi ya wanakijiji walipendekeza Magongo awe miongoni mwa wangombea. Aidha, baadhi ya wanakijiji hawakupenda awe miongoni mwa wagombea kutokana na kuwa na umri mdogo. Kwani alikadiriwa kuwa na miaka ya umri kati ya 18 - 20.**

**Mwenyekiti aliyekuwa anamaliza muda wake wa uongozi aliwaeleza wanakijiji kwamba, katika kuchagua kiongozi hatuangalii sura wala kimo bali tunapaswa kuangalia mtu mwenye uwezo wa kuleta maendeleo katika kijiji chetu.**

**Baada ya kupita uchaguzi, Magongo alikuwa miongoni mwa wateuliwa kijijini hapo. Alifanya kazi yake kwa bidii katika kuhakikisha anaitendea haki nafasi aliyopewa. Magongo aliendelea na kasi hiyo lakini baadaye aligundua kua baadhi ya wanakijiji walimchukia kwa alivyokuwa mchapakazi na sifa zake zilivyo kuwa zikienea.**

**Pamoja na hali hiyo, Magongo hakukata tamaa bali aliendelea kufanya kazi na kuhakikisha kijiji chao kinapata mandeleo. Kwa kufanya hivyo, kijiji cha Lufu kililkuwa na maendeleo makubwa sana.**

FOR ONLINE READING ONLY

### Je, wajua

Kutathimini uhariri uliofanywa ni zoezi la kupitia matini iliyohaririwa na mhariri mwingine kwa lengo la kubaini ubora au udhaifu wa kiuhariri ambao unadhihirishwa na makosa ya kiuandishi yaliyoachwa na mhariri huyo. Katika kujifunza uhariri, hili ni zoezi muhimu sana kwani husaidia kujua jinsi wengine wanavyofanya uhariri na hata kubaini dosari wanazofanya. Tathmini inaweza kufanywa kwa kuisoma matini iliyohaririwa yenyewe tu, ambayo bado ina alama za uhariri kabla ya kuboreshwa au kwa kufanya ulinganishi na matini ya awali kabla ya kufanyiwa uhariri.

### Tamrini ya 6

1. Unaelewa nini kuhusu uhariri? Fafanua mambo ya msingi yanayojitokeza katika fasili uliyoitoa kuhusiana na dhana ya uhariri.
2. Tafuta matini kuhusu habari yoyote katika gazeti lolote na uihariri upya.
3. Kwa kutumia vyanzo vya maktabani au mtandaoni, tafuta insha kuhusu mada yoyote, kisha ifanyie uhariri.
4. Eleza ni kwa namna gani kutozingatiwa kwa viungo vya ushikamani kunaweza kusababisha andiko lisiwe na muwala?
5. Kwa kutumia vyanzo mbalimbali, tafuta alama nyingine za uhariri, tofauti na zile ulizojifunza, kisha zitumie katika kuhariri matini yoyote kutoka katika gazeti au chanzo kingine chochote.

FOR ONLINE READING ONLY

# Sura ya Saba

# Tafsiri

## Utangulizi

*Tafsiri ni njia muhimu ya kufanikisha mawasiliano baina ya watu wanaotumia lugha tofauti. Katika sura hii, utajifunza mbinu mbalimbali za tafsiri. Aidha, utatafsiri matini za kawaida kwa kutumia mbinu ya tafsiri sisisi, tafsiri ya kisemantiki na tafsiri ya kimawasiliano. Umahiri utakaoujenga utakuwezesha kutafsiri matini mbalimbali za kawaida kwa kutumia mbinu mwafaka kwa kuzingatia miktadha mbalimbali.*

### Fikiri

Changamoto za kutafsiri matini ambayo hujaelewa muktadha wake

## Mbinu za tafsiri na jinsi ya kuzitumia katika kutafsiri matini za kawaida

### Shughuli ya 7.1

**Tafsiri matini zifuatazo, kisha eleza mbinu ulizotumia kutafsiri matini hizo.**

A. Maisha ni safari. Hakika, ni safari ndefu sana. Pamoja na urefu wake, ina mwisho wake, kama ilivyo na mwanzo wake. Mwanzo wa safari ni kuzaliwa na mwisho wake ni kufa. Hapa katikati kuna wakati wa utoto, wakati wa masomo, na wakati wa kuwa katika familia ili kuyaendesha maisha. Wakati wa masomo ni wakati mzuri wa kujipatia maarifa mbalimbali ya kutumia wakati wa kuendesha familia. Wakati huu ndio umri wa ujana. Umri wa ujana unafaa sana katika kuyaandaa maisha ya uzeeni. Wakati huu wa ujana, hadi takribani miaka 45, binadamu huwa na nguvu na uwezo wa kufanya mambo mengi ambayo yatamsaidia wakati ujao pale nguvu zitakapopungua. Hivyo, ni vizuri sana kuutumia vizuri wakati huu. Kila dakika inapaswa itumiwe kwa madhumuni ya kuuandaa wakati ujao.

FOR ONLINE READING ONLY

B. Success in life depends on access to information. Information is power. Through information, one knows what has been done, what is being done, what more needs to be done, and whether things can be done differently. Successful people and good speakers search for information, which gives them evidence to act on, make informed decisions, and justify what they are doing. Listening to the news on the radio or watching it on TV and other channels can help one get relevant information. However, just switching on such news broadcast devices does not make one an effective listener. One has to possess listening skills, which are learnt.

**Chanzo:** TIE (2022:10)

**Je, wajua**

Mbinu za tafsiri ni njia ambazo mfasiri huzitumia katika kutekeleza jukumu lake la kuhawilisha ujumbe kutoka lugha moja kwenda nyingine. Mbinu hizo zinafafanuliwa katika sehemu zinazofuata.

**Mbinu ya tafsiri sisisi**

Mbinu hii hujulikana pia kama tafsiri ya neno kwa neno. Hii ni mbinu ya kutafsiri ambapo tungo za lugha chanzi hutafsiriwa zikiwa pwekepweke kwa kuzingatia maana zake za msingi bila kujali muktadha zilimotumika. Huzingatia zaidi mpangilio wa vijenzi vya lugha chanzi. Misemo na maneno ya kitamaduni au ya uwanja maalumu hutafsiriwa kwa kuzingatia maana zake za msingi. Aghalabu, tafsiri huandikwa chini ya sentensi ya lugha chanzi kwa kufuata sarufi ya lugha chanzi. Sarufi ya lugha lengwa hufuatwa katika hatua ya pili ambapo maana iliyolengwa huandikwa lakini bila kuzingatia muktadha.

**Mifano:**

Kiswahili: Wa- li- cheza mi-chezo mingi
Kiingereza: they/past/ play//plural/game/many.
"They played many games".

Kiingereza: She will cook delicious food
Kiswahili: a/-ta-/pika/kitamu/chakula
"Atapika chakula kitamu"

Kiingereza: Pull up your socks.
Kiswahili: Vuta/juu/-yako/soksi
"Vuta juu soksi zako"

FOR ONLINE READING ONLY

Kiingereza: She bought me a book.
Kiswahili: Yeye /alininunua/mimi/kitabu
"Alininunua mimi kitabu"

Kiswahili: Mtoto wa nyoka ni nyoka.
Kiingereza: Child/ of/snake/ is/snake
"The child of a snake is a snake"

Kiingereza: Central Bank of Kenya
Kiswahili: kati/benki/ya/Kenya
" Benki ya Kati ya Kenya"

Kiingereza: Pass away
Kiswahili: Pita/mbali
" Pita mbali"

### *Je, wajua* ?

Mbinu hii ina udhaifu katika kueleza kwa uangavu maana iliyokusudiwa katika matini chanzi. Pia, haiwezi kutumika kutafsiria misemo kwa usahihi kwani maana za misemo aghalabu hazitokani na maana za maneno yanayoijenga. Hata hivyo, mbinu hii husaidia kuelewa maumbo ya maneno ya lugha chanzi na jinsi vipashio vyake vinavyofungamana. Kadhalika, mbinu hii inashindwa kufikisha ujumbe wa lugha chanzi katika lugha lengwa kwa ufanisi kwa sababu kuna wakati kunakuwa na upotoshaji wa maana ya lugha chanzi katika matini lengwa. Mbinu hii hutumika zaidi katika tafsiri za data za kiisimu ambapo wanaisimu huchambua sarufi ya lugha.

### *Shughuli ya 7.2*

1. Tafsiri matini zifuatazo kwa mbinu ya tafsiri ya neno kwa neno.
   (b) My name is Elephant. I am in form five right now. I study hard in order to achieve my goals. My friends and I are waiting eagerly to sit for the form six examinations next year. We are sure that we will make it.
   (c) Vitabu vya Kiswahili walivyoviazima wanafunzi vinatakiwa kurudishwa keshokutwa. Hili ni agizo la mwalimu wa taaluma. Zoezi hili linapaswa kukamilika kabla shule haijafungwa.
2. Tunga sentensi tano kwa lugha yako ya kwanza. Kisha, zitafsiri kwa kutumia mbinu ya tafsiri sisisi.

FOR ONLINE READING ONLY

## *Shughuli ya 7.3*

Tafsiri matini zifuatazo kwa mbinu ya tafsiri sisisi.

A.

Tunza Mazingira,
S.L.P. 2121,
Newala.

Kumb. Na. AY/P3/20/015. 02/09/2016.

Mwana Bwerere,
Meneja wa Soko la Mitimirefu,
S. L.P. 51,
Mtwara.

Ndugu,

*YAH: MWALIKO WA KUWA MGENI RASMI KATIKA MAADHIMISHO YA MIAKA KUMI YA KIKUNDI CHA TUNZA MAZINGIRA*

Tafadhali husika na kichwa cha barua hapo juu.

Kikundi cha Tunza Mazingira (TM) kinaadhimisha miaka kumi tangu kianzishwe. Sherehe ya maadhimisho hayo itafanyika tarehe 20/10/2016 saa 10:00 jioni, katika Ukumbi wa Changamkeni.

Katika sherehe hiyo, tunakuomba uwe mgeni rasmi. Vilevile, tutakuomba uwatunuku vyeti wanachama walioshiriki kikamilifu katika kuyatunza mazingira tangu kikundi kilipoanzishwa.

Tunatumaini maombi yetu yatakubaliwa.

Wako katika kutunza mazingira,

Yovina Bichuro

*Mwenyekiti*

FOR ONLINE READING ONLY

A. Mashavu is a little boy in Mtapenda Village. One day, when Mashavu was passing through the village grassland, he saw an elephant. Slowly, the elephant approached him. He was so afraid. He started running and screaming for help, "Help me! Help

me! I am dying!" Suddenly, Jakalanda heard him. He ran very fast towards him and picked him. After picking him, he ran very fast with him to the village. When running, they heard the elephant saying, "Why are you running? Stop running from me. I am a friend and not an enemy. Mashavu and Jakalanda did not believe the elephant. Jakalanda even increased the speed. He ran very fast until they reached home. They hid themselves in the house. All of a sudden, the elephant reached their house and said, "Why are you hiding, friends? Believe me, I am a good friend". Seeing that the elephant did not intend to harm them, they decided to believe it. They let the elephant in and ate together. It was very fun to eat and talk with the elephant. Suddenly, Mashavu was awoken by his mother. "Oh, it was a dream!" Mashavu said to himself.

**Mbinu ya tafsiri ya kisemantiki**

Hii ni mbinu ya tafsiri ambayo huegemea zaidi kwa mwandishi wa matini chanzi ambapo maana na vipengele vidogovidogo vya lugha chanzi hutiliwa maanani. Mbinu hii ya tafsiri huifanya kazi ya tafsiri iwe na taarifa nyingi kwani aghalabu hujali kila alichokiweka mwandishi. Mara nyingi, tafsiri ya kisemantiki hujali zaidi maana na muundo wa matini chanzi.

**Mifano:**

(i) Tanzania Electric Supply Company Ltd.

*Shirika la Ugavi wa Umeme Tanzania*

(ii) Where there is a purpose, there is no failure.

*Palipo na nia, hapana kushindwa.*

(iii) Tunauza barafu hapa.

*We sell icecream here.*

Katika mifano hii, kila neno limetafsiriwa isipokuwa "Ltd" katika mfano wa (i). Kutokana na hali hii, matini lengwa zimekuwa na taarifa nyingi na baadhi si sahihi.

Mbinu hii ina uwezo mkubwa wa kuendeleza lugha lengwa kwa kuiingizia miundo na misemo kutoka katika lugha chanzi. Kwa mfano, kupitia mbinu hii, lugha ya Kiswahili imepata miundo mbalimbali kutoka lugha ya Kiingereza kama inavyoonekana katika mifano ifuatayo:

FOR ONLINE READING ONLY

(i) Ladies and gentlemen -*mabibi na mabwana*

(ii) At the end of the day -*mwisho wa siku*

(iii) Weekend -*mwisho wa wiki (wikiendi)*

(iv) Under the chairmanship of …-*chini ya uenyekiti* wa …

Udhaifu wa mbinu hii unajitokeza katika kutafsiri misemo na dhana nyingine za kitamaduni. Kwa kuwa tafsiri ya kisemantiki hujielekeza katika maana ya msingi, hushindwa kutafsiri misemo kwa kuwa maana zake hutegemea muktadha.

Tafsiri ya kisemantiki hutumika zaidi katika matini elezi kama vile wasifu binafsi, maelekezo ya kisayansi, nyaraka za kisheria, na kisiasa na fasihi iliyobuniwa kwa umakini. Aghalabu, maandiko haya hayahitaji udondoshaji wa maneno yake kwani maana zake huhitajika. Kufuatia maendeleo ya TEHAMA, tafsiri ya kisemantiki inaweza kufanywa kwa msaada wa programu za akili unde (AU)

### Shughuli ya 7.4

**Tafsiri matini ifuatayo kwa kutumia mbinu ya tafsiri ya kisemantiki.**

(a) *I have only two priorities here at school: improving academic performance and tightening discipline. During my one term here, I've noticed that the school's performance is good, but it is affected by poor discipline among a few students. For example, during prep, some students sleep in their dormitories. This habit reduces their chances of doing well in the exams. In academics, I hope to see all students pass with Division One, ranging from three to seven points. To realise this objective, I'll encourage my fellow students to attend classes, prep sessions and library studies. In doing so, they will improve their performance. In addition, I'll passionately co-operate with other leaders to advise the school administration accordingly on providing adequate textbooks and supplementary books to increase the accessibility of reading materials among students. Lastly, I'll encourage the students to communicate in English since it is the medium of instruction for all subjects, except Kiswahili. Research indicates that one can perform better if taught in the language they know best. It should, therefore, be our mission to learn English comprehensively. I believe that practice makes perfect. The more the practice, the better the performance.*

**Chanzo**: Imeboreshwa kutoka (TIE, 2022)

(b) *Mlima Kilimanjaro ni mlima mrefu kuliko yote barani Afrika. Ni chanzo cha maji*

FOR ONLINE READING ONLY

*katika Mji wa Moshi. Licha ya kuwa chanzo cha maji, pia ni kivutio cha watalii nchini Tanzania. Watalii wanapotembelea Mlima Kilimanjaro, hutuletea fedha za kigeni na kuinua uchumi wa nchi yetu. Tunapaswa kutunza rasilimali hii muhimu kwa maendeleo endelevu.*

**Mbinu ya tafsiri ya kimawasiliano**

Hii ni mbinu ya tafsiri ambayo huzingatia kueleweka kwa ujumbe kwa hadhira lengwa. Huzingatia pia historia, muktadha, utamaduni, na itikadi ya mzungumzaji wa lugha lengwa. Kwa hiyo, ni tafsiri inayoilenga hadhira kwa vile humjali zaidi msomaji wa matini lengwa. Ni tafsiri iliyo wazi, huru na inayoeleweka kwa urahisi. Wakati mwingine, hujulikana pia kama tafsiri huru. Hii ndiyo mbinu ambayo inaonekana kuwa na mashiko zaidi kwa sababu aghalabu haileti utata wowote kwa hadhira ya lugha lengwa. Mfasiri hapaswi kufungwa na miundo ya lugha chanzi kwani kinacholengwa ni kueleweka kwa ujumbe kwa hadhira. Mfasiri hufuata sarufi ya lugha lengwa na yuko huru kutafuta maneno au mafungu ya maneno yanayolingana na nahau, misemo, methali, tamaduni, na mazingira ya lugha lengwa katika kuelezea ujumbe unaotolewa na matini chanzi. Chunguza mifano ifuatayo:

(i) Tanzania Electric Supply Company Limited
*Shirika la Umeme Tanzania*

(ii) Where there is a purpose, there is no failure.
*Penye nia, pana njia.*

(iii) At the end of the day
*Hatimaye*

(iv) Kawia ufike
*Better late than never*

Katika mifano hapo juu, tafsiri zimefanyika kwa kuzingatia miundo na maana za lugha lengwa. Hii ndiyo sababu ya kutofanyika kwa tafsiri ya kila neno likiwa pwekepweke. Aidha, msemo katika mfano wa (iii) umetafutiwa msemo unaofanana nao katika lugha lengwa badala ya kutafsiriwa kisisisi. Tafsiri ya kimawasiliano hutumika zaidi katika kufasiri matini arifu kama vile za sayansi na teknolojia, za kibiashara, ripoti za mikutano, na kazi za kifasihi. Mbinu ya tafsiri ya kimawasiliano ndiyo inayotumika kuliko mbinu nyingine za tafsiri.

FOR ONLINE READING ONLY

## *Shughuli ya 7.5*

Tafsiri matini ifuatayo kwa kutumia mbinu ya tafsiri ya kimawasiliano.

A. **Good morning, everyone! I hope you're all doing well today. We have an important announcement to make regarding the upcoming project deadline. Due to unforeseen circumstances, we have had to extend the deadline by one week. This decision was made to ensure that we deliver a high-quality product without compromising on quality. Please, adjust your schedules accordingly and let's work together to meet the new deadline. Thank you for your understanding and cooperation.**

B. ***HOTUBA YA MGENI RASMI KATIKA MAHAFALI YA KUHITIMU KIDATO CHA SITA KATIKA SHULE YA SEKONDARI MSITUNI TAREHE 10 MEI 2023***

**Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa,**

**Mwenyekiti wa Bodi ya Shule,**

**Mkuu wa Shule,**

**Wajumbe wa Bodi ya Shule,**

**Walimu wote,**

**Wazazi na walezi wa wanafunzi,**

**Wahitimu wa kidato cha sita,**

**Wanafunzi wote,**

**Mabibi na mabwana,**

**Habari za mchana!**

**Ndugu Mkuu wa Shule, kwanza ninapenda kutoa shukurani zangu za dhati kwa uongozi wa shule kwa kunialika kujumuika nanyi katika mahafali haya kama mgeni rasmi. Aidha, ninatumia nafasi hii kukupongeza wewe na walimu wote wa Shule ya Sekondari Msituni kwa kuwaandaa wanafunzi hawa wanaohitimu leo. Mmefanya kazi kubwa na, hivyo, mnastahili pongezi nyingi.**

**Ndugu Mkuu wa Shule, ninawapongeza pia Wajumbe wa Bodi ya Shule ambao wameshirikiana na wazazi, na walezi katika kusimamia shule hii na kufanikiwa kujenga maabara kubwa na ya kisasa. Ninapenda kukuhakikishia kuwa serikali inawaunga mkono na ninawataarifu kuwa tayari tumetenga fedha za kutosha kununua vifaa vya maabara hii. Ndugu Mkuu wa Shule, ninaomba sasa nitoe nasaha kwa wahitimu wetu. Vijana mnaohitimu leo, ninapenda mfahamu kwamba mnategemewa sana na serikali kuwa chachu ya maendeleo ya taifa letu katika**

FOR ONLINE READING ONLY

nyanja mbalimbali. Kwa hiyo, kila mmoja wenu ajiandae kutumia maarifa aliyoyapata kwa manufaa ya taifa letu. Tumieni nguvu na uwezo wenu wote wa kitaaluma mlioupata kwa miaka hii kulijenga taifa lenu hili, lenye amani na utulivu. Muvae uzalendo kamili wa taifa letu, ambalo lina rasilimali za kutosha ambazo, mkizilinda na kuzisimamia vizuri, zina uwezo wa kuwaletea mafanikio makubwa, ninyi binafsi na taifa letu kwa ujumla.

Aidha, ninapenda kuwakumbusha kujiepusha na vitendo ambavyo vinaweza kuzima ndoto zenu za maisha ya baadaye. Ninafahamu kuwa walimu wamewafundisha mambo mengi kama vile kujiepusha na vikundi vya watu wanaotumia dawa za kulevya, ujambazi, na kadhalika. Vilevile, ninapenda kuwakumbusha kujiepusha na vitendo vinavyochochea maambukizi ya virusi vya UKIMWI. Ni jukumu la kila mmoja kujilinda na kujiepusha na vitendo vinavyoweza kumtumbukiza katika hatari ya kuambukizwa VVU na kujikuta anafupisha maisha yake. Kwa hiyo, ninawasihi mzingatie hayo yote ili ninyi wenyewe, familia zenu, na taifa kwa ujumla linufaike na elimu mliyoipata.

Ndugu Mkuu wa Shule, nimalizie kwa kuwaomba wanafunzi wanaobaki hapa shuleni kuendelea kuwa na nidhamu, na kutia bidii katika masomo. Vilevile, ninazidi kuwaomba walimu, wazazi, na walezi muendelee kushirikiana katika kuwalea na kuwasaidia vijana hawa ili wapate elimu bora kwa mustakabali wa maisha yao na taifa letu.

Ninawatakieni mafanikio mema katika kujenga nchi yetu nzuri ya Tanzania. Asanteni kwa kunisikiliza!

FOR ONLINE READING ONLY

## Tamrini ya 7

1. Eleza umuhimu wa kuzingatia mbinu za tafsiri katika kufanya tafsiri.
2. Kutokana na shughuli za kutafsiri ulizokwishafanya, unadhani mbinu ipi ya tafsiri inafaa kati ya mbinu ya tafsiri ya kisemantiki na tafsiri ya kimawasiliano? Tetea jibu lako.
3. (a) Tunga sentensi changamani tano za Kiswahili, kisha zitafsiri kwa lugha ya kigeni kama vile Kichina, Kiingereza, Kiarabu au Kifaransa kwa kutumia mbinu ya tafsiri ya kisemantiki na tafsiri ya kimawasiliano.

   (b) Linganisha ubora wa tafsiri hizo kwa kutoa mifano kutoka katika tafsiri hizo.
4. (a) Tafsiri matini ifuatayo kwa Kiswahili kwa kutumia mbinu za tafsiri sisisi, tafsiri ya kisemantiki na tafsiri ya mawasiliano.

(b) Chagua tafsiri bora kati ya tafsiri ulizofanya na ueleze sababu za chaguo lako.

**Fighting corruption in Africa**

**Corruption has no doubt posed a serious challenge to many countries, but the consequences have been especially severe in Africa. The questions that we must now ask ourselves are as follows: For how long shall we keep lamenting about Africa's problems? For how long shall we blame our leaders? When shall we start** *doing something to remedy the ills that afflict the continent?*

**My argument is that Africa needs to unite and speak with one voice against the vices that bedevil its people. We must rekindle the Pan-Africanist ideals borne and initiated by the "founding fathers" of the continent in the 1960s, notably the late President Kwame Nkrumah of Ghana, Julius Nyerere of Tanzania,** *Kenneth Kaunda of Zambia, and Abdel Nasser of Egypt. The dream enshrined* **in the movement entailed dealing with African challenges with a united front. It was founded on the belief that Africa could only move forward on a platform of unity and harmonisation of initiatives to free Africa from the stranglehold of backwardness.**

**Chanzo**: TIE (2022:24)

FOR ONLINE READING ONLY

# Sura ya Nane

# Ukalimani

## Utangulizi

Ukalimani ni miongoni mwa njia za kufanikisha mawasiliano ya papo kwa papo miongoni mwa wazungumzaji wa lugha tofauti. Ukalimani hufanyika kwa namna mbalimbali na una stadi zake muhimu zinazouwezesha kufanyika kwa ufanisi. Katika sura hii, utajifunza stadi ya kusikiliza huku ukinukuu hoja muhimu wakati wa kukalimani. Pia, utajifunza aina mbalimbali za ukalimani. Aidha, utajifunza kukalimani mazungumzo kwa ukalimani fuatizi, nong'onezi na kiungo. Umahiri utakaoujenga utakuwezesha kukalimani mazungumzo mbalimbali kwa kutumia mbinu za ukalimani fuatizi, nong'onezi na kiungo katika miktadha mbalimbali.

**Fikiri**

Mawasiliano katika jamii bila ukalimani

## Stadi ya kusikiliza na kunukuu kumbukumbu muhimu wakati wa ukalimani

**Shughuli ya 8.1**

**Sikiliza habari hii ikisomwa, kisha nukuu mambo muhimu.**

Siku moja, Bwana Makumbusho alipokuwa katika matembezi yake ya kawaida katika Soko la Kariakoo, alikutana na watalii ambao walikuwa wametokea nchini Uingereza. Walimsimamisha na kumwomba afuatane nao katika maeneo ambayo wangepita ili awasaidie kuwasiliana na wenyeji, hususani wafanyabiashara wa Soko la Kariakoo ili waweze kununua bidhaa mbalimbali. Watalii hao hawakujua Kiswahili. Hivyo, walihitaji mtu anayeelewa Kiswahili na Kiingereza ili awasaidie kufanya ukalimani

FOR ONLINE READING ONLY

kwa lengo la kuwasiliana na wenyeji. Wakati huo Bwana Makumbusho alikuwa ameshahitimu kidato cha sita katika Shule ya Sekondari Kilimahewa. Yeye alikuwa amesoma tahasusi ya Kiswahili, Kiingereza na Kifaransa (KLF) na alijifunza vizuri sana ukalimani na kufanya mazoezi ya kutosha alipokuwa shuleni. Alikuwa na ujasiri, ujuzi na ufahamu wa kutosha kuhusu ukalimani na tamaduni za watu wa lugha zote mbili. Hivyo, Makumbusho alikubali na kufuatana nao kila mahali walipokwenda ili kununua bidhaa za Kitanzania sokoni Kariakoo.

Kila walipofika, watalii hao waliulizia bei za bidhaa na kuchagua bidhaa. Bwana Makumbusho alisikiliza kwa makini ili aelewe wanachokitaka. Makumbusho alikalimani kwa Kiswahili kwa wauzaji nao wakamtajia bei ya kila bidhaa. Makumbusho alitumia stadi yake ya kusikiliza kwa makini. Mtalii mmoja alivutiwa na biashara ya viungo na kutamani kuanzisha biashara kama hiyo akirejea kwao. Kwa hiyo, alimwomba mfanyabiashara wa viungo amwelekeze mahitaji ya biashara hiyo. Katika ufafanuzi wake, kulikuwa na maelekezo mengi ambayo Makumbusho asingeweza kuyakumbuka yote. Hivyo, alianza kunukuu kumbukumbu. Lengo la kunukuu ni kutopoteza kumbukumbu ya mambo muhimu, hasa bidhaa na bei zake. Kunukuu kumbukumbu muhimu kulimsaidia kuhakikisha usahihi na ufanisi wa mawasiliano kati ya watumiaji wa lugha mbili tofauti. Wakati wa kunukuu kumbukumbu muhimu, Makumbusho alizingatia umakini wa kusikiliza na kuelewa mambo muhimu ya kunukuu. Baadaye, alizikalimani taarifa hizo kwa usahihi. Kutokana na kuzingatia mambo hayo, Makumbusho alikalimani kwa ustadi mkubwa.

Watalii hao walimshukuru Makumbusho kwa kukalimani vizuri mazungumzo kati yao na wafanyabiashara na kuwawezesha kuelewana. Walimlipa kiasi cha Dola za Kimarekani 250. Makumbusho naye aliwashukuru watalii hao, kisha waliagana na kuelekea Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Kambarage Nyerere ili kurudi kwao Uingereza. Walichukua mawasiliano ya Makumbusho na yeye akachukua yao kisha wakaagana.

Baada ya mwezi mmoja kupita, wageni hao walimtafuta Makumbusho ili awasaidie kukalimani katika kesi ya mwenzao. Siku iliyofuata, baada ya mawasiliano yao, Makumbusho aliitwa katika Mahakama ya Kisutu jijini Dar es Salaam kwa ajili ya kukalimani mwenendo wa shauri la jinai la watuhumiwa kutoka nje ya nchi ambao walikuwa wameingia nchini kinyume cha sheria. Watuhumiwa hao walikuwa hawajui Kiswahili. Hivyo, ilibidi watafutiwe mkalimani ambaye angekalimani mashtaka yaliyosomwa dhidi yao. Muda wa shauri ulipofika, watuhumiwa walisomewa mashtaka na waliruhusiwa kuzungumza kwa kukiri au kukana mashtaka dhidi yao. Wakati mashitaka yanasomwa, Makumbusho alikuwa anasikiliza kwa makini na

FOR ONLINE READING ONLY

kunukuu kumbukumbu muhimu ili zimsaidie kukumbuka wakati wa kukalimani. Kabla washtakiwa hawajazungumza chochote, Makumbusho alisogea karibu na kukaa pembeni yao ili akalimani kwa kuwanong'oneza kila walichokuwa wanakisema msoma mashtaka na hakimu. Hakimu alikuwa anampa muda mkalimani ili awakalimanie wageni hao. Alifanya hivyo kwa sauti ndogo ili asimwathiri mtu mwingine yeyote ambaye hahusiki. Baada ya kuelewa vizuri, watuhumiwa walijibu kwa kukana mashtaka na hakimu aliahirisha kesi na watuhumiwa walirudishwa rumande hadi upepelezi ukamilike.

Baada ya hakimu kuahirisha kesi, Makumbusho aliagana na wateja wake na kurudi nyumbani kwao Tandale. Akiwa njiani, alipigiwa simu na mtu aliyejitambulisha kwa cheo cha Mratibu wa Mkutano wa Uchumi wa Nchi za Kiafrika ambao ungefanyika kesho yake jijini Arusha katika Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Arusha (AICC). Alimwomba Bwana Makumbusho afike siku hiyo Arusha kwa ajili ya maandalizi ya kukalimani katika mkutano huo wa kimataifa. Hivyo, Bwana Makumbusho alikata tiketi ya ndege kutoka Dar es Salaam kwenda Arusha. Aliikata kwa njia ya mtandao. Alipomaliza kukata tiketi, alichukua mizigo yake na kuelekea Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere na alipanda ndege mnamo saa sita na robo mchana na kuwasili Arusha mnamo saa saba na robo mchana. Alipofika Arusha, alienda moja kwa moja hadi Kituo cha Kimataifa cha Mikutano Arusha ambapo alikutana na mwenyeji wake na kufanya mazungumzo mafupi kuhusiana na mada za mkutano, ukubwa wa kazi na sifa za wazungumzaji. Alioneshwa mahali pa kukaa wakati wa zoezi la ukalimani. Makumbusho alipewa mkataba akausaini kisha, alifanya maandalizi ya kutosha na alipomaliza aliondoka kwenda hotelini kupumzika akisubiri zoezi la ukalimani kwa siku iliyofuata. Siku ilipofika, alikalimani vizuri na alipongezwa sana.

## Je, wajua ?

Unapokalimani mazungumzo, kuna matukio matatu ambayo aghalabu hutokea. Matukio hayo ni kusikiliza, kunukuu na kukalimani. Stadi ya kusikiliza katika ukalimani ni muhimu kwa mkalimani ili aweze kufanya ukalimani wake kwa ufanisi. Hata hivyo, kusikiliza pekee hakutoshi kumwezesha mkalimani afanye kazi yake vizuri. Inatakiwa anaposikiliza awe anatunza kumbukumbu. Mkalimani anaweza kutunza kumbukumbu kichwani au kwa kuandika mahali fulani mambo muhimu yanayozungumzwa. Kwa mfano, anaweza kuandika kwenye shajara au daftari, tabuleti, kompyuta pakatwa au vifaa vingine vya ki-TEHAMA kwa msaada au bila msaada wa akili unde (AU). Pamoja na kwamba mkalimani anapaswa kuwa na uwezo mkubwa wa kukumbuka, bado anaweza kuandika mambo ya msingi ili asiyasahau, hasa takwimu na masuala ya

FOR ONLINE READING ONLY

data, majina ya watu au mahali, na kadhalika.

Kuna mambo ya msingi ambayo mkalimani anapaswa kuyazingatia wakati wa kusikiliza na kunukuu kumbukumbu muhimu ili zimsaidie wakati wa kukalimani. Mambo hayo yanafafanuliwa katika vipengele vinavyofuata.

(a) **Kumwangalia usoni mzungumzaji**

Kumwangalia usoni mzungumzaji kunaweza kumsaidia mkalimani kupata ishara za kimwili kama vile mjongeo wa macho na ishara nyingine ambazo husaidia kung'amua ujumbe, hata ulio fiche. Aidha, kutamsaidia kuelewa mawasilano mengine yanayofanyika bila kutumia lugha ya maneno. Watu hutumia lugha ya mwili au ishara za uso kuwasilisha mambo ambayo hawasemi kwa maneno.

(b) **Kutowaza mambo mengine nje ya mazungumzo**

Jambo hili humsaidia mkalimani kuongeza umakini katika kusikiliza ili kuyapata mawazo ya msingi kutoka katika mazungumzo na kuyahifadhi kichwani au katika daftari na kupunguza vikwazo vya usikivu na uelewa. Mawazo yanayomtoa mtu katika muktadha wa mazungumzo hukwamisha usikivu na kumfanya mkalimani ashindwe kunukuu mambo muhimu. Kutowaza mambo mengine humruhusu mkalimani kuzingatia kikamilifu kile kinachosemwa na kuelewa vyema ujumbe uliokusudiwa.

(c) **Kuwa na utulivu**

Kuwa na utulivu humsaidia mkalimani kudumisha umakini wakati wote wa mazungumzo na kuepuka kunukuu mambo ambayo hayajazungumzwa na mzungumzaji.

(d) **Kunukuu hoja za msingi**

Mkalimani anaposikiliza mazungumzo, anapaswa kuwa na mahali pa kuandikia hoja za msingi zinazobeba ujumbe na maana nzima ya mazungumzo. Stadi hii ya kunukuu kumbukumbu hujumuisha kudondoa hoja muhimu kutoka katika mazungumzo na kuzihifadhi kichwani au kuziandika katika shajara au daftari au kifaa kingine chochote cha kuandikia.

Ili mkalimani aweze kunukuu hoja za msingi kutoka katika mazungumzo wakati wa kukalimani, anapaswa kufanya au kuzingatia yafuatayo:

(a) Kusikiliza kwa makini
(b) Kubaini hoja zinazobeba ujumbe wa mazungumzo
(c) Kuwa na mikakati ya kunukuu hoja za msingi kama vile kutumia vifupisho au alama ambazo atazikumbuka kwa urahisi

FOR ONLINE READING ONLY

(d) Kuwa na mahali pa kuandikia hoja zinazobeba ujumbe
(e) Kunukuu hoja za msingi

Hata hivyo, pamoja na kunukuu hoja za msingi katika daftari au kifaa kingine chochote, mkalimani anapaswa kujua kuwa ukalimani unategemea zaidi kumbukumbu za kichwani. Kunukuu hoja katika daftari au kifaa kingine kunasaidia kuiongezea uwezo kumbukumbu ya kichwani. Unukuzi wa kumbukumbu hutumika zaidi katika ukalimnai fuatizi.

**Umuhimu wa kunukuu kumbukumbu**
Kuna manufaa anuwai ya kuandika kumbukumbu katika ukalimani fuatizi. Kwanza, husaidia kufanya mazungumzo chanzi yatiririke kawaida kwa kupunguza haja ya mkalimani kumdukiza au kumkatiza mzungumzaji mara kwa mara. Pili, huruhusu pande mbili zinazowasiliana kuwasilisha mafungu marefumarefu zaidi ya ujumbe, kama ambavyo mazungumzo ya kawaida yangefanyika. Kuchambua mafungu marefu ya ujumbe humpatia mkalimani fursa ya kuelewa vyema maana, muktadha na dhana kuu za kile kinachowasilishwa.

Tatu, kunukuu kumbukumbu humsaidia mkalimani kuuhifadhi na kuuwasilisha ujumbe kwa usahihi na ukamilifu wake. Nne, kuandika kumbukumbu kunamwezesha mkalimani kunasa taarifa muhumu zinazosahaulika kwa urahisi, hasa zinazohusiana na majina, anwani, namba (kwa mfano, tarehe, muda/nyakati, kiasi cha fedha, dozi za dawa, na namba za simu).

**Njia za kunukuu kumbukumbu**
Kumbukumbu zinaweza kuandikwa kwa mkono au kwa kutumia vifaa vya kidiijiti. Ingawa wakalimani wanaweza kutumia vifaa vya kidijiti, matumizi ya vifaa hivyo yana hasara kuliko manufaa. Kuandika kwa mkono humwezesha mkalimani kuzikumbuka kumbukumbu zake kwa urahisi kuliko anapoandika kwa kutumia vifaa vya kidijiti. Aidha, watu wanapoandika kumbukumbu kwa njia ya kidijiti, aghalabu hunakili moja kwa moja maneno ya kile kinachosemwa na mzungumzaji badala ya kuandika kumbukumbu, tofauti na inavyokuwa waandikapo kwa mkono. Hali hii huzifanya kumbukumbu zilizoandikwa kidijiti kuchukua muda mrefu zaidi kuzing'amua. Kwa kuwa kuandika kumbukumbu kunakusudiwa kumsaidia mkalimani kufupisha mchakato wa kukalimani na si kuurefusha, inafaa zaidi kuandika kumbukumbu kwa mkono. Mwisho, kuandika kumbukumbu kwa mkono humruhusu mkalimani kutumia alama na michoro anayoipendelea ambayo huenda isipatikane kwenye vifaa vya kidijiti.

FOR ONLINE READING ONLY

**Mbinu za kunukuu kumbukumbu**

Kunukuu kumbukumbu kunaweza kufanyika kwa kutumia mbinu tatu: mbinu zinazohusiana na lugha; mbinu zinazohusiana na michoro; na mbinu zinazohusiana na alama.

***Mbinu zinazohusiana na lugha*** ni pamoja na: kudondosha irabu wakati wa kuandika maneno yenye herufi tatu au zaidi (kwa mfano, 'mf' badala ya 'mfano', 'shdn' badala ya 'shindano', na 'ktn' badala ya 'kutokana na'); kufupisha maneno na kubakiza herufi nne au tano (kwa mfano, kufupisha 'dawati' kuwa 'dwti'); kuandika herufi ya kwanza ya kila neno (kwa mfano, kuandika 'shinikizo la damu' kama 'SD', 'kwa niaba ya' kama 'kny'); na kufupisha maneno kwa kutumia ritifaa (kwa mfano, kufupisha 'nikuvute' kama n'kvte).

***Mbinu zinazohusiana na michoro*** huhusisha matumizi ya mishale, mistari na maumbo ili kuwasilisha maana. Mbinu zinazohusiana na michoro ni pamoja na: kupiga mstari chini ya neno ili kusisitiza maana; kulizungushia neno kiduara au kisanduku ili kusisitiza maana; kuchora mstari kuanzia mwanzoni hadi mwishoni mwa neno kwa kulikata katikati ili kuonesha maana hasi; kutumia mishale kuashiria yaliyopita (←), yajayo au matokeo/athari (→) na kuonesha mpando/ongezeko (↑) au mshuko/anguko (↓).

***Mbinu zinazohusiana na alama*** humhusu mkalimani binafsi zaidi kwa kuwa hutoa nafasi kwa kila mkalimani kujibunia alama zake. Kwa kuwa alama ni anuwai, mkalimani anashauriwa asijiundie alama nyingi na tata kiasi cha kumkanganya. Anashauriwa atumie alama sahili ili aweze kuzikumbuka haraka na kuzielewa kwa urahisi. Baadhi ya alama zinazotumika ni alama ya kopa (♥) kuashiria upendo au matamanio; alama mbili za kubwa-kuliko (>>) kuonesha pendekezo/kupendekeza; umbo la pembetatu sawa iliyotazama juu (▲) kuonesha ongezeko au iliyotazama kulia (►) kuonesha badiliko; umbo la duara (O) kuashiria dunia; umbo la nyumba (⌂) kuashiria nyumba, na alama za fedha kama vile dola ($) na paundi (£) kuashiria pesa; alama za nyuso kuashiria hisia mbalimbali kama vile furaha (☺); alama zinazoonesha jinsi kama vile ya kike (♀) na ya kiume (♂) na kadhalika.

## Shughuli ya 8.2

Kalimani taarifa kutoka idhaa ya Kiswahili, kupitia redioni, runingani au mtandaoni huku ukinukuu mambo muhimu

FOR ONLINE READING ONLY

### Zoezi la 8.1

1. Kwa kutumia vyanzo vya maktabani na/au mtandaoni, eleza kwa hoja zisizopungua sita umuhimu wa kunukuu kumbukumbu wakati wa ukalimani fuatizi.
2. Ukiwa mjuzi wa lugha ya Kiswahili, umepata mwaliko wa kwenda kukalimani katika warsha ya mafunzo ya kuwajengea uwezo wanasiasa chipukizi katika viwanja vya wazi. Je, unadhani utatakiwa kunukuu kumbukumbu au la? Kwa nini?
3. Kuandika takribani kila kinachosemwa na mzungumzaji wakati wa ukalimani humwezesha mkalimani kukumbuka kwa urahisi mambo ya kukalimani kuliko anapoandika vidokezo. Kubali au kataa kauli hii kwa hoja maridhawa zisizopungua sita.

## Kukalimani mazungumzo ya kawaida

### Shughuli ya 8.3

Fanikisha mawasiliano kati ya muuzaji na mnunuzi ambao wanatumia lugha mbili tofauti kwa kukalimani, kisha eleza jinsi ukalimani huo ulivyofanyika.

**Aina za ukalimani**

Kuna aina nne za ukalimani kwa kuzingatia kigezo cha mbinu za kukalimani. Katika kiwango hiki, utajifunza aina tatu ambazo ni ukalimani fuatizi, nong'onezi na kiungo.

**Ukalimani fuatizi**

Huu ni ukalimani unaofanyika kwa kupokezana, ambapo mzungumzaji huanza kuzungumza kisha humwachia nafasi mkalimani ili akalimani na kuendelea kupokezana hivyo mpaka mwisho wa mazungumzo. Mkalimani na mzungumzaji wanaweza kukubaliana juu ya urefu wa mazungumzo. Mathalani, wanaweza kukubaliana kwamba akalimani kila sentensi au fungu la sentensi kadhaa. Aidha, mzungumzaji na mkalimani wanaweza kuwa pamoja katika jukwaa au mkalimani akawa amekaa sehemu nyingine. Aghalabu, mzungumzaji na mkalimani huwa pamoja jukwaani.

Ukalimani fuatizi ni wa mwanzo kabisa ambao pia unafaa zaidi katika mikutano mikubwa, katika majadiliano au hafla ambapo mzungumzaji anahitaji kutoa maelezo marefu. Katika ukalimani huu, mkalimani anaweza kuchukua kumbukumbu, hasa pale mzungumzaji anapompa mkalimani nafasi baada ya kutoa fungu la sentensi kadhaa au mazungumzo marefu.

Ukalimani huu hutumika na hupendwa zaidi kwani hauna gharama kubwa. Hii ni kwa sababu hauhitaji vifaa zaidi ya maikrofoni na spika. Wakati mwingine, sauti ya

FOR ONLINE READING ONLY

mzungumzaji na mkalimani bila kifaa inatosha. Changamoto ya ukalimani huu ni kuyafanya mazungumzo kutumia muda mrefu zaidi kutokana na kupokezana kwa mzungumzaji na mkalimani. Kwa upande wa mkalimani, ukalimani huu unaweza kumpatia fursa ya kumwomba mzungumzaji arudie alichosema ikiwa hajasikia vizuri. Pia, anapata muda wa kunukuu hoja za msingi wakati mzungumzaji akizungumza.

Mambo ya kuzingatia mkalimani anapofanya ukalimani fuatizi jukwaani ni kuvaa mavazi nadhifu ambayo yatamfanya awe huru na ambayo hayataibua mgogoro wowote kwa hadhira yake. Pia, mkalimani anapaswa kuwa na ujuzi wa kuiga matendo ya mzungumzaji na kuwa na kasi katika kukalimani kulingana na kasi ya mzungumzaji. Mkalimani pia anapaswa kuwa jasiri na kuwa na mwonekano wa kujiamini mbele ya hadhira yake ili hadhira pia ijenge imani naye. Aidha, ni vyema kuwatazama hadhira badala ya kuwaonea aibu na kuonesha hofu. Kwa kuwa mkalimani anakuwa na mzungumzaji jukwaani, ni vizuri kuomba mzungumzaji arudie ikiwa hajasikia badala ya kudanganya au kuwa na hofu. Hata hivyo, uulizaji ukizidi, utamchosha mzungumzaji na wasikilizaji. Ikiwa hakuna vyombo kama maikrofoni na spika, basi mkalimani anapaswa kukalimani kwa sauti inayosikika vyema.

### Zoezi la 8.2

1. Eleza namna ukalimani fuatizi unavyofanyika.
2. Eleza mazingira ambamo ukalimani fuatizi unaweza kufanyika.
3. Fafanua faida na changamoto za ukalimani fuatizi.
4. Eleza namna hofu, aina ya mavazi, sauti ndogo, na kutoiga vitendo vya mzungumzaji vinaweza kudunisha ukalimani fuatizi.

### Shughuli ya 8.4

A. Umeteuliwa kuwa mkalimani wa kikundi cha utunzaji wa mazingira. Fanya ukalimani fuatizi wa mazungumzo ya Kiswahili kwenda lugha yoyote ya kigeni huku ukizingatia taratibu zote za ukalimani fuatizi jukwaani.

B. Fanya ukalimani fuatizi wa mazungumzo yaliyo katika Kiingereza au lugha nyingine ya kigeni kama vile Kifaransa, Kichina, au Kiarabu kwenda Kiswahili huku ukizingatia taratibu zote za ukalimani fuatizi ukiwa jukwaani.

**Ukalimani nong'onezi**

Huu ni ukalimani unaofanyika kwa mkalimani kumnong'oneza msikilizaji wake kwa lugha lengwa huku akiendelea kusikiliza mazungumzo. Katika ukalimani huu,

FOR ONLINE READING ONLY

mkalimani hukaa pembeni ya msikilizaji wake anayefanyiwa ukalimani huo. Ukalimani huu hufanyika katika mikutano ambapo wasioelewa lugha chanzi ni wachache; mmoja, wawili au watatu, ambapo hahitajiki mkalimani jukwaani. Hivyo, mkalimani hukalimani kwa sauti ya chini sana ili asiwasumbue wasikilizaji wengine ambao hawahitaji ukalimani. Hii ndiyo sababu iliyofanya ukalimani huu uitwe ukalimani nong'onezi, kwani hufanyika kwa kunong'oneza. Mazingira ambamo ukalimani huu hufanyika ni pamoja na mikutano mikubwa ya kitaifa, mikutano ya kibiashara, na kanisani. Katika ukalimani huu, mkalimani huzungumza sambamba na mzungumzaji kwani mzungumzaji hana muda wa kumsubiri mkalimani kwani huwa mbali naye na anaweza hata asiwe anamwona. Pia, katika ukalimani huu, mkalimani anapaswa kusikiliza, kukumbuka na kukalimani.

Ukalimani huu unaweza kuwa na hasara kwa msikilzaji ikiwa mkalimni hatakuwa na maadili ya ukalimani kwani anaweza kumdanganya msikilizaji wake na asiwepo wa kujua. Hivyo, mkalimani anapaswa kuwa mwaminifu na mwadilifu.

**Zoezi la 8.3**

1. Eleza namna ukalimani nong'onezi unavyoweza kumwathiri msikilizaji.
2. Fafanua sababu za baadhi ya mazingira kuhitaji ukalimani nong'onezi?
3. Bainisha mazingira ambamo ukalimani nong'onezi unaweza kufanyika.

**Shughuli ya 8.5**

A. Chukulia kuwa wewe ni mtaalamu wa ukalimani. Umeteuliwa kukalimani mazungumzo ya kiongozi wa mtaa na wageni kutoka nje ya nchi. Kalimani mazungumzo yaliyo katika Kiswahili kwenda lugha nyingine yoyote ya kigeni kwa kutumia mbinu ya ukalimani nong'onezi huku ukizingatia maadili ya mkalimani.

B. Kalimani mazungumzo yaliyo katika Kiingereza au lugha nyingine ya kigeni kama vile Kifaransa, Kichina, au Kiarabu kwenda Kiswahili kwa ukalimani nong'onezi.

**Ukalimani kiungo**

Ukalimani kiungo ni ukalimani usio rasmi ambao hutumika kuwezesha maelewano baina ya pande mbili zinazozungumza lugha tofauti, ambazo zinaweza kuwa watu wawili, mtu mmoja na kikundi kidogo, au vikundi viwili vidogo. Kwa mfano, hutumiwa katika mazungumzo ya kawaida kwenye mikutano ya kibiashara; chakula cha mchana au cha jioni; wakati wa kujadili mikataba; wakati wa ziara za wajumbe wa kigeni watembeleapo viwanda, makampuni, makumbusho, matukio ya michezo;

FOR ONLINE READING ONLY

na maonesho ya kibiashara. Kadhalika, hutumiwa wakati wa usindikizaji wa wageni katika utalii, sokoni, uwandani ambapo wageni hao wanafanya utafiti, na shughuli za kijeshi. Kwa sababu hiyo, ukalimani huu hujulikana pia kama ukalimani sindikizi au ukalimani changamani. Katika ukalimani huu, mkalimani huziunganisha hizo pande mbili za wazungumzaji na kuwa kama kiungo au daraja ambapo huhawilisha ujumbe kutoka upande wa kwanza na kuupeleka upande wa pili na kuuchukua ule wa upande wa pili na kuupeleka upande wa kwanza. Kwa hivyo, unamhitaji mfasiri awe na umahiri wa lugha zote mbili anazofanyia kazi.

Ingawa ukalimani huu ni kama aina ya ukalimani fuatizi, wenyewe una sifa zake bainifu. Kwanza, hauhitaji kunukuu kumbukumbu. Pili, hufanyika kwa uelekeo wa kuwili, yaani, mkalimani anakalimani kutoka lugha chanzi kwenda lugha lengwa na kutoka lugha lengwa kwenda lugha chanzi. Hii ni kusema kwamba lugha lengwa huwa lugha chanzi na lugha chanzi huwa lugha lengwa. Kwa hivyo, unamhitaji mfasiri awe na umahiri wa lugha zote mbili anazofanyia kazi. Tatu, wakalimani kiungo hukaa pamoja na wazungumzaji. Ukalimani kiungo hautumii vifaa maalumu. Nne, wakalimani wanapaswa kuonesha sifa zote zisizo za lugha, kama vile ishara za mwili. Mwisho, mkalimani kiungo anapaswa kuzingatia suala la maadili katika kazi yake.

Stadi zinazohitajika katika ukalimani huu, ukiondoa ile ya kuwa na umahiri wa lugha za kufanyia kazi, ni pamoja na mkalimani kuwa na maarifa ya mawasiliano, hususani kupeana zamu wakati wa kuzungumza; kuzungumza kwa sauti inayosikika vizuri; na kuhakikisha kwamba ujumbe wowote wa upande wowote hauachwi bila kukalimaniwa.

## Zoezi la 8.4

1. Chukulia kuwa wewe ni mkalimani mzoefu wa ukalimani kiungo. Fafanua mazingira na namna ukalimani huo unavyofanyika.
2. Chukulia kuwa wewe ni mdogo wake Kamagaza. Siku moja, Kamagaza alidondoka kwenye pikipiki akaumia. Wasamaria wema walimpeleka hospitalini. Walipofika hospitalini, walimkuta daktari mgeni asiyejua Kiswahili. Alikuwa akiongea Kiingereza lakini hakukuwa na mtu hata mmoja aliyejua Kiingereza. Kwa kuwa wewe unasoma sekondari, ilibidi uitwe usaidie kuokoa jahazi. Sasa, kalimani maswali na maelekezo ya daktari kwa Kamagaza na majibu ya Kamagaza kwa daktari.

Daktari: Hello, Kamagaza! I am told you've had a bit of a fall. What were you doing? Going too fast?

Wewe:

FOR ONLINE READING ONLY

Kamagaza: Ndiyo, daktari! Ni kweli nimeanguka lakini mimi nilikuwa abiria tu.

Wewe:

Daktari: You'd better get off your outfits then, and we'll take a look at you.

Wewe:

Kamagaza: Sawasawa!

Wewe:

Daktari: Um! That's a nasty cut. I'll have to put a couple of stitches in it.

Wewe:

Kamagaza: Aisee! Mimi ninaogopa sana sindano.

Wewe:

Daktari: There is no other option, young man. Oh, I see! There won't be any need for stiches as the cut just looks worse than it is. It's only a graze. The nurse will clean it up for you. It'll sting, but that's all. Now, does it hurt anywhere else?

Wewe:

Kamagaza: Ashukuriwe Mola! Ninakushukuru nawe daktari pia. Ninasikia maumivu sehemu ya bega. Ni kama kuna mfupa umevunjika.

Wewe:

Daktari: Well! There is nothing broken, but you've bruised your shoulder. It'll be sore for a few days. Now, did you bang your head at all?

Wewe:

Kamagaza: Ndiyo! Nilijigonga chini upande wa kulia.

Wewe:

FOR ONLINE READING ONLY

| | |
|---|---|
| Daktari: | Did you feel dizzy? |
| Wewe: | |
| Kamagaza: | Ndiyo! Lakini ilikuwa kwa muda mfupi tu. |
| Wewe: | |
| Daktari: | Yes! There is an injury here. I think this one will need the stiches. Okay, look up there! I'm just going to shine this light into your eyes. No, that's fine. I'll just do the stitches, and the nurse will put a dressing on it. Then, you can go home in peace. |
| Wewe: | |
| Kamagaza: | Dah! Nilijua nimepona kuchomwa sindano, kumbe wapi! |
| Wewe: | |

### Shughuli ya 8.6

Fanya ukalimani kiungo kati ya wazungumzaji wa lugha mbili tofauti, mathalani, Kiswahili na Kiingereza, Kiswahili na Kichina, Kiswahili na Kiarabu au Kiswahili na Kifaransa wakiwa katika mazigira ya sokoni, utalii, nyumbani, mtaani, katika michezo, au hospitalini.

### Tamrini ya 8

1. Fafanua mifano ya hoja ambazo zinaweza kuhitaji kunukuliwa wakati wa kufanya ukalimani.
2. Eleza mambo ambayo mkalimani anapaswa kufanya ili aweze kusikiliza na kubaini hoja kuu wakati wa kukalimani mazungumzo.
3. Fanya ukalimani nong'onezi wa Kiingereza kwenda Kiswahili kwa mwanafunzi mwenzako wakati wa mazungumzo na wenzake.
4. Fanya ukalimani fuatizi wa hotuba, risala au hadithi inayotolewa na mwenzako huku ukizingatia misingi ya ukalimani bora.
5. Fanya ukalimani kiungo wa hospitalini, mahakamani, nyumbani na mtaani kwa Kiswahili na lugha nyingine ya kigeni kama vile Kifaransa, Kichina, Kiingereza au Kiarabu.

FOR ONLINE READING ONLY

# Sura ya Tisa

# Kuthamini kazi za fasihi

## Utangulizi

**Fasihi ni sanaa yenye chimbuko lake. Sanaa hii imekuwa ikipitia maendeleo anuwai katika vipindi mbalimbali. Katika sura hii, utajifunza mitazamo mbalimbali kuhusu dhana ya fasihi, nadharia za chimbuko la fasihi, maendeleo ya fasihi kabla na baada ya ujio wa wageni, na maendeleo ya fasihi baada ya uhuru. Umahiri utakaoujenga utakuwezesha kupambanua mitazamo kuhusu dhana ya fasihi na chimbuko lake. Pia, utaweza kuthamini mfungamano uliopo kati ya fasihi na jamii.**

### Fikiri

Mabadiliko ya fasihi katika jamii

## Mitazamo kuhusu dhana ya fasihi

### Shughuli ya 9.1

Kwa kutumia vyanzo mbalimbali, eleza mitazamo tofautitofauti ya dhana ya fasihi, kisha bainisha mtazamo wenye mashiko zaidi huku ukitoa sababu za kuuteua mtazamo huo.

### Je, wajua ?

Dhana ya fasihi imeelezwa kwa namna mbalimbali kwa kujiegemeza katika mitazamo tofautitofauti. Mitazamo iliyopo hadi sasa huona fasihi kama maandishi, hisi, sanaa ya lugha yenye ubunifu, maandiko bora ya kisanaa, na tokeo la matumizi ya lugha kwa

FOR ONLINE READING ONLY

njia isiyo ya kawaida. Mitazamo hii inafafanuliwa katika vipengele vinavyofuata:

(a) **Fasihi ni maandishi**

Kwa mujibu wa Wellek na Warren (1986), fasihi ni jumla ya maandishi na machapisho yote katika lugha fulani. Hii inamaanisha kuwa maandishi yoyote, yakiwamo matangazo ya biashara, mafunzo ya historia, jiografia, sayansi na kadhalika yanaweza kujumuishwa kama fasihi. Upungufu wa mtazamo huu unaweza kujitokeza pale tunapojiuliza swali kuhusu fasihi simulizi ambayo kimsingi haipo katika maandishi. Je, fasihi simulizi si fasihi kwa sababu haipo katika maandishi? Vilevile, mtazamo huu unaupanua mno uwanja wa fasihi kutokana na kujumuishwa kwa maandiko mengine ambayo si kazi za kifasihi kama vile jiografia, hesabu, na kadhalika.

(b) **Fasihi ni hisi zinazojibainisha kupitia lugha**

Wafuasi wa mtazamo huu ni Ramadhani (1973), Balisidya, (1973) Sengo na Kiango (1973). Hawa wanadai kuwa, ili mtunzi aweze kueleza au kuandika jambo kifasihi, hapana budi kuwapo na mguso utakaochochea kutimizwa kwa azma yake. Wataalamu hawa wanasema kuwa hisi inaweza kuwa ya njaa, baridi, joto, uchovu au kuumwa. Kwa hiyo, ili kuwe na kazi ya fasihi lazima hisi ziwe zimeguswa. Wataalamu wengine, mathalani Mulokozi (2017), wanapinga mtazamo huu kwa kueleza kuwa mtazamo huu unachanganya mambo matatu ambayo ni fasihi yenyewe, mambo yaelezwayo na fasihi, na mtindo wa kifasihi. Kwa hiyo, fasihi si hisi pekee bali huweza kutumia vipengele mbalimbali vya fani na maudhui kudhihirisha hisia mahususi. Mathalani, fasihi inaweza tu kipengele cha taswira au tamathali za semi kuelezea mapenzi lakini fasihi yenyewe si mapenzi.

(c) **Fasihi ni sanaa ya lugha yenye ubunifu**

Mtazamo huu unaona kwamba kazi yoyote ya fasihi, ama iwe imeandikwa au haikuandikwa, inapaswa kutungwa kwa lugha yenye ubunifu. Andiko lolote lisilokuwa na ubunifu haliwezi kuwa fasihi. Kwa mujibu wa mtazamo huu, hata nyimbo na masimulizi ya kisanaa ni fasihi, ijapokuwa hayakuandikwa. Akiwakilisha mtazamo huu, Kirumbi (1975) anasema kuwa fasihi ni taaluma ya sanaa inayowasilishwa kwa njia ya lugha katika muundo wa maandishi au matamshi. Mtazamo huu ndio uliozoeleka katika taaluma ya fasihi ya Kiswahili. Inadaiwa kuwa neno fasihi limetokana na neno la Kiarabu "**fasuh**" lenye maana ya ufasaha au uzuri wa lugha. Hivyo, istilahi ya "fasihi" katika taaluma ya Kiswahili inatofautiana na istilahi ya "**literature**" inayotumika katika Kiingereza, ambayo maana yake mojawapo ni 'andiko'. Dhana hii katika Kiswahili inazingatia aina zote za fasihi, yaani fasihi simulizi na andishi. Kwa ujumla, mtazamo huu umehusisha fasihi na sanaa itumiayo lugha ya maandishi au mazungumzo.

FOR ONLINE READING ONLY

(d) **Fasihi ni maandiko bora ya kisanaa**

Huu ni mtazamo unaoiangalia fasihi kama kazi iliyoandikwa kwa kutumia mbinu zinazoibua mvuto wa kisanaa na kuzifanya kuwa na manufaa ya kudumu. Akijifungamanisha na mtazamo huu, Summers (1989) anasema kuwa fasihi ni sanaa inayojumuisha zaidi maneno yaliyoandikwa. Pamoja na kwamba mtazamo huu unaupa uzito ufundi wa kubuni, unafinya mawanda ya fasihi kwa kuhusisha mawazo yaliyo bora tu. Ni vigumu kuupima ubora huo unaotofautiana kati ya jamii na jamii, na hata kwa mtu mmojammoja.

(e) **Fasihi ni matokeo ya matumizi ya lugha kwa njia isiyo ya kawaida yenye athari kwa hadhira**

Mtazamo huu unaiona fasihi kuwa ni kazi ambayo hutumia lugha kiufundi ili kuleta athari maalumu kwa jamii. Kwa mujibu wa Mulokozi (2017), waasisi wa mtazamo huu ni Roman Jakobson, Boris Tomashevsky na Viktor Shklovsky. Kwa maelezo ya wataalamu hawa, fasihi hukiuka taratibu za kawaida za matumizi ya lugha katika sarufi, maana na sauti ili kumvutia na kumuathiri msikilizaji au msomaji. Hivyo, ili kufikisha athari zake kwa jamii, hujiegemeza kwenye matumizi ya lugha ya kiufundi zaidi hata kuifanya ionekane kuwa si ile lugha ya kawaida. Udhaifu wa mtazamo huu ni msisitizo katika kuitafakari lugha yenyewe badala ya kuutafakari ujumbe unaowasilishwa na lugha hiyo. Vilevile, mtazamo huu unaonekana kuelemea zaidi upande wa fani na kupuuza maudhui, maana na muktadha wa kazi za fasihi.

Kwa ujumla, mjadala huu unaonesha kuwa kila mtazamo una ubora na udhaifu wake. Kwa hiyo, tunaweza kusema kuwa badala ya kuielezea dhana ya fasihi kwa mtazamo mmoja, mitazamo yote inapaswa kujumuishwa. Hivyo, kwa kufuata mkabala huo fasihi inaweza kufasiliwa kuwa ni sanaa inayotumia lugha kiufundi kuwasilisha masuala mbalimbali yanayomhusu mwanadamu na maisha yake kwa njia ya maandishi au mdomo. Lugha inayozungumziwa katika fasili hii haina maana ya uzungumzaji wa kutumia sauti tu, kwani mara nyingi hujumuisha pia mjongeo wa viungo vya mwili, ishara na vitendo.

**Zoezi la 9.1**

1. Dhana ya fasihi imefasiliwa na wanazuoni kwa mitazamo anuwai. Fafanua umuhimu wa mitazamo hiyo.
2. Bainisha na fafanua masuala matatu ya msingi yanayojitokeza katika kila mtazamo kuhusu dhana ya fasihi.
3. Tathmini ubora na udhaifu wa mitazamo inayohusu dhana ya fasihi, kisha toa mawazo yako kuhusu dhana hiyo.

FOR ONLINE READING ONLY

## Nadharia za chimbuko la fasihi

**Shughuli ya 9.2**

Kwa kutumia vyanzo anuwai, tathmini mitazamo mbalimbali kuhusu chimbuko la fasihi, kisha bainisha mtazamo wenye mashiko zaidi huku ukitoa ushahidi kutetea hoja zako.

**Je, wajua**

Nadharia za chimbuko la fasihi ni maelezo ya mitazamo kuhusu namna fasihi ilivyoanza. Suala la chimbuko la fasihi limewashughulisha wataalamu mbalimbali wa fasihi kwa karne kadhaa. Hata hivyo, jumla ya mawazo yao yanaangukia katika mitazamo mikuu miwili ambayo ni: mtazamo wa kidhanifu na mtazamo wa kiyakinifu.

(a) **Mtazamo wa kidhanifu**

Mtazamo huu umejikita katika 'kudhani'. Mawazo yake hayawezi kuthibitika katika mazingira ya kawaida. Waasisi wa mtazamo huu ni Plato na Socrates, wanafalsafa wa Kiyunani. Waasisi wa mtazamo huu wanaamini kuwa fasihi na sanaa vimetoka kwa Mungu. Hivyo, mwanafasihi huipokea sanaa ikiwa tayari imeivishwa na Mungu. Hii ina maana kuwa fasihi haikugunduliwa wala kutokea katika kipindi fulani tu katika harakati za binadamu kukabiliana na mazingira yake, bali ni zawadi ya Mungu kwa mwanadamu. Wataalamu wengine wenye mtazamo wa kidhanifu ni Felician Nkwera na John Ramadhani.

Ramadhani (1975), anadai kwamba ingawa fasihi ni hisi, kitendo cha mtu kuibuni kazi ya sanaa ni uigaji wa Mungu ambaye ndiye mfalme wa sanaa zote. Akiunga mkono mtazamo huu, Nkwera (1976) anasema, "Fasihi ni sanaa ambayo huanzia kwa Muumba, na humfikia mtu katika vipengele mbalimbali". Anaendelea kueleza kuwa, fasihi ni hekima ambayo mtu ameshirikishwa apate kumtambua Muumba wake". Kwa mtazamo wa Nkwera, maelezo hayo yanathibitisha kwamba chimbuko la fasihi ni Mungu. Mawazo ya wanafalsafa wa mtazamo huu hayana uthibitisho wowote zaidi ya kumtenga msanii na jamii yake kwa kumkweza na kuonekana yuko karibu na Mungu kuliko wanajamii wengine. Aidha, wafuasi wa mtazamo huu wanaamini kuwa mwanafasihi hawezi kubuni kitu chochote zaidi ya kuiga sanaa ambayo tayari Mungu ameitengeneza.

(b) **Mtazamo wa kiyakinifu**

Wataalamu wa fasihi ambao wanaamini katika mtazamo huu, wakiwemo Senkoro (1988) na Mulokozi (2017), wanasema kuwa chimbuko la sanaa na fasihi ni mazingira

FOR ONLINE READING ONLY

halisi ya jamii. Wanatoa mfano wa jinsi ambavyo sanaa ya mwanzo ilifungamana na uzalishaji mali. Hii inamaanisha kwamba harakati za binadamu kudhibiti mazingira yake ndicho chanzo cha fasihi na sanaa kwa ujumla. Katika harakati za kukabili mazingira yake, ilimlazimu binadamu kufanya kazi. Iliwalazimu kutumia nyenzo kadha wa kadha ili kupambana na mazingira hayo. Huo ndio ulikuwa mwanzo wa kutafuta mbinu za kurekebisha nyenzo zao. Mathalani, waliyachonga mawe butu ili yawe na ncha kali zinazofaa katika uwindaji. Uchongaji huo ndio ulikuwa sanaa yenyewe. Kwa namna hiyo, hisia za kisanaa zilifungamana na maendeleo ya binadamu katika kupambana na mazingira yake na katika kufanya kazi. Aidha, mtazamo wa kiyakinifu unaona kuwa, kwa kiasi kikubwa, fasihi inaathiriwa na mabadiliko yanayotokea katika jamii. Mtazamo huu una mwelekeo zaidi kwani unakubaliana na fikra kuwa wanadamu walianza mawasiliano kupitia kazi zao. Kwa mantiki hiyo, chimbuko la sanaa ni kazi.

Kadiri binadamu alivyoendelea, ndivyo alivyozidi kuwa na mahitaji mengine zaidi ya msingi. Mahitaji hayo yaliamsha hisia za kuchora vielelezo vinavyohusu shughuli zake za kujikimu. Michoro ya mapangoni iliyopo Kondoa (Tanzania) ni mifano mizuri ya vielelezo hivyo. Kuzuka kwa lugha kuliongeza aina nyingine ya sanaa ambayo ni fasihi. Fasihi hii haikutoka kwa Mungu wala haikutokana na hisi tu.

Fasihi, kama zilivyo sanaa zingine, ilitokana na kazi alizofanya binadamu katika kupambana na mazingira yake. Fasihi ilianzia katika nyimbo za kazi. Baadaye, tanzu zingine za fasihi zilitungwa na kusimuliwa kwa malengo ya kufunza, kukosoa, kuadibu, kuchokoza fikra na kuliwaza jamii wakati na baada ya kazi. Kadiri maendeleo ya uzalishaji mali yalivyoongezeka, binadamu alipata muda wa kupumzika na kustarehe kwa njia ya sanaa. Hapo ndipo fasihi ilipoanza kutengana na shughuli za uzalishaji. Kwa njia hii, fasihi ikawa shughuli maalumu ya jamii katika matukio mbalimbali kama vile sherehe na ibada. Fasihi na sanaa zingine zilirithishwa kizazi hadi kizazi kwa njia ya masimulizi mpaka maandishi yalipogundulika.

**Zoezi la 9.2**

1. Thibitisha kwa mifano uthabiti wa mtazamo wa kiyanikifu kuhusu chimbuko la fasihi.
2. Linganisha hoja za mtazamo wa kidhanifu na wa kiyakinifu kuhusu chimbuko la fasihi, kisha bainisha ubora na udhaifu wa kila mtazamo.
3. Fafanua sababu za chimbuko la fasihi kuhusihwa na jamii badala ya Mungu.
4. Kwa mtazamo wako, chimbuko la fasihi ni nini?

FOR ONLINE READING ONLY

## Maendeleo ya fasihi kabla ya ujio wa wageni Afrika

### Shughuli ya 9.3

(a) Chunguza kwa makini nyimbo zifuatazo, kisha fafanua namna zinavyohusiana na fasihi ya kipindi cha kabla ya ujio wa wageni.

**Wimbo wa 1**

Twanga
Twanga
Twanga kituli
Twanga

**Wimbo wa 2**

Tulime
Tulime
Tulime
Tupate mazao
Ya leo na kesho

**Chanzo: Umahiri katika Fasihi ya Kiswahili** (Samwel, 2015:17)

(b) Kwa kutumia vyanzo mbalimbali, wakiwamo wazee, eleza kazi za fasihi zilizokuwapo kabla ya ujio wa wageni, kisha fafanua namna kazi hizo za fasihi zilivyotumika katika miktadha tofauti.

**Je, wajua ?**

Mfumo wa uzalishaji mali uliotawala katika baadhi ya maeneo kabla ya ujio wa wageni ulikuwa ujima. Huu ni mfumo wa awali kabisa wa jamii katika maisha ya mwanadamu. Katika mfumo huu, watu waliishi katika makundi kwa usawa, wakimiliki kila kitu kwa pamoja huku wakishirikiana kupambana na mazingira kama vile ukame na wanyama wakali. Kila walichokipata walikipata kwa umoja na waligawana kwa usawa.

Fasihi ya kipindi hiki iliambatana na shughuli za uzalishaji mali kama vile uwindaji. Kwa hiyo, ilitumiwa kama nyenzo ya kazi. Baadaye, binadamu alitumia nyimbo katika shughuli zake za kilimo kwa lengo la kufanya kazi kwa muda mrefu pasipo kuchoka. Pia, kwa mujibu wa Senkoro (1987), fasihi ya wakati huo ilikuwa na lengo la kuwaunganisha watu ili kufanya kazi kwa pamoja, hususani katika shughuli za kilimo. Aidha, fasihi ya kipindi hicho haikuwa ya kitabaka kwa sababu jamii ilikuwa haijagawanyika katika

FOR ONLINE READING ONLY

matabaka mbalimbali. Kwa hiyo, fasihi iliwanufaisha watu wengi katika jamii.

Vilevile, katika jamii za kitemi, binadamu walitumia fasihi simulizi kama chombo cha kuwasifu na kuwapongeza viongozi wao, watemi, au mashujaa waliokuwa wakijitokeza katika jamii hizo. Mashujaa hao walitungiwa nyimbo za kuwasifu au walijitungia wenyewe nyimbo za kujisifu mbele ya jamii zao.

Kabla ya ujio wa wageni, jamii mbalimbali za Kiafrika zilikuwa na fasihi zao. Takribani jamii zote zilikuwa na tanzu za ushairi, semi na hadithi. Baadhi ya vipera vya tanzu hizo vilifanana na kutumiwa katika maeneo mengi. Mathalani, kila jamii ilikuwa na vitendawili kwenye fasihi ya watoto, ambavyo vilichangamsha akili za watoto hao na kuwafanya wayaelewe mazingira yao. Katika utanzu wa ushairi, kila jamii ilikuwa na sanaa ya nyimbo zilizoimbwa katika matukio mbalimbali. Vilevile, katika utanzu wa hadithi, karibu kila jamii ilikuwa na kipera cha ngano. Kwa upande wa semi, kila jamii ilikuwa na methali pamoja na misemo iliyotumiwa katika nyimbo na mazungumzo ya watu wazima. Tanzu hizi zilitumiwa kama nyenzo mojawapo ya kuchochea shughuli za kijamii, kisiasa na kiuchumi.

Kutokana na maendeleo ya mifumo ya kiutawala, baadhi ya jamii zilikuwa na vipera tofauti na jamii zingine. Kwa kuwa masuala ya utawala yalianza kujenga matabaka katika jamii, baadhi ya watu walipewa sifa kuliko wengine. Kwa mfano, jamii zilizokuwa na utawala wa kichifu au kifalme zilikuwa na vipera vinavyowasifu viongozi au mashujaa wa jamii hiyo. Fasihi za jamii hizi ziliakisi mifumo hiyo ya kiutawala. Mfano mzuri wa vipera vilivyopatikana katika jamii hizo ni tendi na majigambo. Aina hii ya fasihi haikupatikana katika jamii zilizoishi kwenye mfumo wa kijima.

*Zoezi la 9.3*

1. Eleza dhima za fasihi simulizi kwa jamii za Kitanzania kabla ya ujio wa wageni.
2. Fasihi simulizi ni nyenzo muhimu ya kuhamasisha shughuli za maendeleo ya kijamii na kisiasa. Thibitisha kauli hii kwa mifano maridhawa kutoka katika jamii inayokuzunguka.
3. Fafanua miktadha ya matumizi ya fasihi simulizi kabla ya ujio wa wageni Afrika Mashariki.

## *Maendeleo ya fasihi baada ya ujio wa wageni Afrika*

*Shughuli ya 9.4*

Chunguza vitendawili, methali na shairi katika vipengele (a) - (b), kisha eleza namna

FOR ONLINE READING ONLY

tanzu hizi zinavyohusiana na shughuli za jamii za Kitanzania baada ya ujio wa wageni.

(a) Vitendawili

Pruuu mpaka Maka. (Utelezi)
Mzungu anachungulia dirishani. (Kamasi)
Mzungu katupwa jalalani. (Machicha ya nazi)

(b) Methali

Baniani mbaya, kiatu chake dawa.
Ukistaajabu ya Musa, utaona ya Firauni.
Gome la udi, si la mnuka uvundo.

(c) Shairi

ONDOKA NCHINI MWETU

1. Raia tumekutana, mbele ya wakubwa wetu
Raia tumeungana, kuunda taifa letu,
Na sisi tuwe mabwana, kutawala nchi yetu,
Ondoka nchini mwetu, mwishoni mwa mwaka huu.

2. TANU inalia sana, wote wanachama wetu,
Wanakulilia bwana, uondoke hapa kwetu,
Bwana tafadhali sana, ondoka nchini mwetu,
Ondoka nchini mwetu, mwishoni mwa mwaka huu.

3. Nchi tunayoinena, hii Tanganyika yetu,
Nchi yote kuungana, Afrika ni ya kwetu,
Afrika yakazana, tokeni tokeni mwetu,
Ondoka nchini mwetu, mwishoni mwa mwaka huu.

4. Sheria yajulikana, na kwa viumbe wenzetu,
Uingereza hata China, kwamba hii nchi yetu,
Haipendezi hiyana, chako kukifanya chetu,
Ondoka nchini mwetu, mwishoni mwa mwaka huu.

5. Kumkataza kunena, Kenyatta Mzee wetu,

FOR ONLINE READING ONLY

Si tendo la kiungwana, latuchoma mioyo yetu,
Tunawaombeni sana, asema Mzee wetu,
Ondoka nchini mwetu, mwishoni mwa mwaka huu.

6. Maombi yetu bayana, hatujamficha mtu,
Wazee hata vijana, twawatangazia watu,
Tuwe huru kama Ghana, nasi tutawale kwetu,
Ondoka nchini mwetu, mwishoni mwa mwaka huu

7. Ondoka tukilingana, tuje kwenu uje kwetu,
Mikono tukipeana, huru Afrika yetu
Si vyema kupunjana, mle vyenu tule vyetu,
Ondoka nchini mwetu, mwishoni mwa mwaka huu.

*Chanzo:* **Mashairi ya Saadani** (Kandoro, 1988: 141-142)

*Je, wajua* ?

Ujio wa wagenii barani Afrika ulisababisha kuwapo kwa mtagusano wa kijamii ambao uliathiri fasihi iliyokuwapo kiuwasilishaji, kifani na kimaudhui. Mtagusano huo ulisababisha kuibuka kwa fasihi andishi, ambayo haikuwapo kabla. Inafahamika kwamba fasihi andishi ni zao la fasihi simulizi.

Kama tulivyodokeza hapo awali, kabla ya ujio wa wageni, barani Afrika kulikuwa na mifumo mingi ya kiuzalishaji mali kama vile ujima na ukabaila. Baadhi ya jamii ziliishi kijima kwa kushirikiana katika kazi na kugawana mazao yaliyotokana na shughuli zao. Katika mfumo huu wa maisha, fasihi ilikuwa na maudhui ya kusisitiza ushirikiano.

Kadhalika, kupitia mfumo wa utumwa, ambao haukuenea sana barani Afrika kama ilivyokuwa katika maeneo ya Ulaya, Mashariki ya Kati na Asia, matajiri walimiliki ardhi, migodi na watumwa kama nyenzo ya uzalishaji. Kwa hiyo, waliwatumia watumwa hao kuzalisha mali. Kwa minajili hii, iliibuka fasihi ya tabaka tawala ya kutukuza wamiliki wa watumwa na mali zao na kuwatweza watumwa. Fasihi ya watumwa iliyopinga mfumo huo ilienezwa kwa siri. Watunzi wa fasihi hii walipogunduliwa waliadhibiwa vikali. Pamoja na masaibu yote hayo, baadhi ya watumwa hawakuacha kutumia fasihi katika kujitetea au kuelezea ubaya wa mfumo huo kwa lengo la kujikomboa.

Mfumo mwingine wa maisha katika kipindi hiki ni ukabaila. Katika mfumo huu, mtaji mkubwa wa uzalishaji ulikuwa ardhi. Uhusiano wa utwana na ubwana ulifikia hatua

FOR ONLINE READING ONLY

mpya ambapo tabaka tawala lilihodhi njia zote za kiuchumi na kiutamaduni. Mbinu mojawapo ya kutawala uchumi iliyoshamiri wakati huo ni kukodisha mashamba. Kabaila alikodisha mashamba, ambapo mtwana alitoa fungu kubwa kwa kabaila wakati wa mavuno. Fasihi ilitawaliwa na falsafa zilizohalalisha uhusiano wa mabwana (makabaila) na watwana (waishio kwa jasho lao). Mfumo huu ulikuwa na uozo mwingi. Uozo mmojawapo uliojitokeza katika mfumo huu ni kusisitiza starehe na mapambo yaliyopitiliza na yasiyo na maana. Pia, kazi za fasihi ziliathiriwa na uozo huu na zilisisitiza mapambo. Kazi za fasihi kama zile za *Al-Inkishafi* (Sayyid Abdallah bin Ali bin Nasir, 1800) na *Utenzi wa Mwanakupona* (Mwanakupona bint Mshamu, 1858) ni mifano mizuri ya kazi za wakati huo.

Kazi za fasihi katika mfumo huu ziliathiri pia nafasi ya mwanamke katika jamii. Mwanamke alisawiriwa kama pambo la mwanamume kama inavyodhihirika katika beti zifuatazo:

Nawe ipambe libasi,
Ukae kama arusi,
Maguu tia kugesi,
Na mikononi makoa.

Na kidani na kifungo,
Sitoe katika shingo,
Muili siwate mwengo,
Kwa marashi nadalia.

Nyumba yako inadhifu,
Mumeo umsharifu,
Wakutanapo sufufu,
Msifu na kumtaya.

Mume wako mtukuze,
Sifa zake zieneze,
Wala simsharutize,
Asichoweza kutoa.

**Chanzo:** *Tenzi Tatu za Kale* (Mulokozi, 1999: 129-130)

FOR ONLINE READING ONLY

Beti hizo hapo juu zinasisitiza umuhimu wa mapambo kwa wanawake. Mwanakupona anamuusia binti yake akubali kuwa pambo kwa mume wake. Fasihi katika mfumo huu ilitumiwa kumuasa mwanamke aelekeze akili yake katika kumsifu, kumfurahisha na kumhudumia mumewe.

Baada ya mfumo wa kikabaila kuanguka, uliibuka mfumo wa kibepari ambao ulipewa msukumo na maendeleo makubwa ya viwanda barani Ulaya. Msingi mkuu wa mfumo wa kibepari ni mtaji. Hali hii ilitoa msukumo wa kuibuka kwa fasihi pendwa inayouzika zaidi kuliko fasihi dhati. Fasihi katika mfumo huu, iliegemea zaidi kwenye kuburudisha kuliko kuibua fikra za maisha halisi waliyo nayo watu. Watunzi wa kazi za fasihi walitumia, na wameendelea kutumia, vipaji vyao ili kujipatia fedha. Aidha, inaelezwa kuwa katika mfumo wa kibepari, mara nyingi, fasihi husawiri maisha ya mtu mmojammoja badala ya jamii nzima.

Kukua kwa mfumo wa ubepari kulisababisha mataifa ya Kimagharibi kutawala jamii za maeneo mbalimbali duniani, ikiwamo Afrika. Hadi kufikia nusu ya pili ya karne ya kumi na tisa, ukoloni ulikuwa umeshashika mizizi katika Bara la Afrika, yakiwemo maeneo ya Waswahili (Samwel, 2015). Kiu ya wakoloni ya kupata malighafi, nguvu-kazi, na masoko ya bidhaa zao iliwasukuma kuwatawala Waafrika kimabavu. Hali hii ilisababisha kuibuka kwa kazi mbalimbali za fasihi zilizokuwa na mwegamo wa kuupinga utawala wa kikoloni.

**Maendeleo ya Fasihi ya Kiswahili baada ya Ujio wa Wageni**

Katika jamii za Afrika Mashariki, kama ilivyokwisha elezwa, fasihi andishi ilianza pale jamii hizo zilipoanza kuweka amali zao kama vile historia na tamaduni katika maandishi. Hati za maandishi ziliietwa na wageni waliotoka Bara la Asia na Ulaya. Wageni hao ni Waajemi, Wareno, Waarabu, Wajerumani na Waingereza. Wageni ambao walileta elimu ya kigeni iliyojumuisha maarifa ya kusoma na kuandika. Kwa hiyo, miongoni mwa athari za ujio wao ni maandishi ambayo baadaye yalianza kutumiwa kuandikia kazi za fasihi. Hati ya Kiarabu ilianza kutumiwa kuandika Kiswahili tangu karne ya 9 (inakisiwa miaka ya 800 BK). Maandiko ya kale ya Kiswahili, hasa tendi, tenzi, na tarihi yaliandikwa kwa hati hiyo. Baadhi ya kazi hizo za fasihi ni *Utendi wa Tambuka* (Bwana Mwengo, 2019) na *Al-Inkishafi* (Sayyid Abdallah bin Ali bin Nasir, 1800). Kuanzia karne ya 19, baada ya ujio wa wakoloni wa Kizungu, hati ya Kirumi ilianza kutumiwa kuandika fasihi ya Kiswahili. Wakati wa ukoloni wa Kijerumani na Kiingereza, hati hiyo ya Kirumi ilienezwa na kutumika zaidi kupitia mfumo wa elimu. Hati hiyo inaendelea kutumika hadi leo.

FOR ONLINE READING ONLY

Maendeleo ya fasihi andishi kabla ya uhuru yana uhusiano mkubwa na wageni (wamisionari na watawala). Wageni hawa, walipofika Pwani ya Afrika Mashariki kuanzia karne ya 16, waliwakuta wenyeji wakiwa na fasihi yao, hususani kazi za ushairi. Baadhi ya tenzi za zamani ni ule Utenzi wa Fumo Liyongo, ambao baadaye,uliwekwa katika maandishi. Aidha, inasemekana kuwa tenzi hizi zilitokana na nyimbo ambazo zinaelezwa kuwa fasihi ya awali. Vilevile, chimbuko la riwaya za Kiswahili linaweza kuwa ni ngano na hekaya simulizi.

Kulikuwa na wanafasihi wenyeji waliokuwa wakiandika mashairi na fani nyinginezo kama tarihi na masimulizi ya wasafiri. Pia, kulikuwapo na ngano na hekaya mbalimbali zilizotafsiriwa na kuwa msingi wa riwaya za Kiswahili. Miongoni mwa hadithi hizo ni *Swahili Tales as Told by the Natives of Zanzibar* (1870) zilizotafsiriwa na Edward Steere. Ngano nyingine zimechapishwa katika kitabu cha **Prosa und Poesie der Suaheli** (1907) kilichohaririwa na Carl Velten, pamoja na **Mazungumzo ya Alfu Lela Ulela,** Juzuu 1-4 (1928) kilichotafsiriwa na Edwin Brenn na kuhaririwa na Frederick Johnson. Vilevile, kulikuwa na riwaya za kutoka nje zilizotafsiriwa kwa Kiswahili. Baadhi ya riwaya hizo ni **Mashujaa: Hadithi za Wayunani** (Charles Kingsley, 1889), **Hekaya za Abunuwasi** (Samwel Chiponde, 1928), **Kisiwa chenye Hazina** (Frederick Johnson, 1929), **Safari za Gulliver** (Jonathan Swift, 1932), **Mashimo ya Mfalme Sulemani** (Ridder Haggard, 1937) na *Safari ya Msafiri* (John Bunyan, 1925).

Kadiri muda ulivyokwenda, Waafrika walianza kuandika kazi za kinathari. Miongoni mwa kazi hizo ni **Habari za Wakilindi** (Abdalla Hemed el Ajjemi, 1972), **Maisha ya Hemed bin Muhamed el Murjebi au Tippu Tip** (Wilfred Whiteley, 1902) (Mhariri), (1950), **Uhuru wa Watumwa** (James Mbotela, 1934), **Tulivyofanya na Tulivyoona Uingereza** (Martin Kayamba, 1932) na **Mwaka katika Minyororo** (Samwil Sehoza, 1921).

Kuanzia miaka ya 1940 hadi 1960, riwaya nyingi zilifuata mkondo wa hekaya na ngano. Kimaudhui, riwaya nyingi zilielezea mambo ya mila na desturi kama njia ya kutunza maadili. Baadhi ya riwaya hizi zilitokana na fasihi ya Kiarabu. Mifano ni kama vile *Msafiri katika Nyumba ya Sultani* (David Diva, 1949) na **Kisa cha Mwana wa Mfalme Mohamed bin Suleiman** (Akida Waziri, 1944).

Aidha, fasihi zilizoandikwa na Waafrika zilihusu mila na desturi zao. Maandiko hayo pia yalihusu maadili mbalimbali na changamoto zilizohusu jamii ya wakati huo. Vilevile, baadhi ya maandiko hayo yalisisitiza utu wa mtu kama njia mojawapo ya kukomesha manyanyaso yaliyokuwa yakifanywa na wakoloni. Miongoni mwa kazi hizo ni **Adili na Nduguze** (Shaaban Robert, 1952), **Bwana Myombekere na Bibi Bugonoka na Ntulanalwo na Bulihwali** (Aniceti Kitereza, iliyoandikwa 1945 na kuchapishwa 1980),

FOR ONLINE READING ONLY

na **Kurwa na Doto** (Mohamed Saleh Farsy,1960).

Hali kadhalika, kulikuwa na kazi mbalimbali za fasihi zilizokuwa zimeathiriwa na tamaduni za Kizungu ingawa ziliandikwa na wazawa wa nchi za Afrika Mashariki. Kazi hizi zilikuwa na maudhui yanayohusu upelelezi na ujambazi wa kutumia silaha. Miongoni mwa kazi hizo ni **Mzimu wa Watu wa Kale** (Mohammed Said Abdulla, 1957).

Kazi zingine zilizoandikwa miaka ya 1940-1960 zilikuwa na mwelekeo wa kupinga ukoloni. Kazi hizi zilionesha madhara ya kutawaliwa na wakoloni. Miongoni mwa kazi hizo ni *Kufikirika* (1951) na **Kusadikika** (1952) za Shabaan Robert. Pia, walikuwapo waandishi wengine kama vile Saadan Kandoro, Mathias Mnyampala, na Kaluta Amri Abedi walioandika kuupinga ukoloni. Hata hivyo, baadhi ya kazi za waandishi hawa ziliandikwa miaka ya mwanzo baada ya uhuru kwani zina maudhui yanayohusu kudai uhuru.

### *Zoezi la 9.4*

1. Eleza mabadiliko ya kimaudhui yaliyojitokeza katika fasihi baada ya ujio wa wageni.
2. Fafanua athari za ujio wa wakoloni katika maendeleo ya fasihi nchini Tanzania.
3. Tathmini thamani ya fasihi ya Kiswahili katika kipindi cha ukoloni.

## *Maendeleo ya fasihi baada ya uhuru*

### *Shughuli ya 9.5*

Soma kwa makini shairi na ngonjera ifuatayo, kisha fafanua namna kazi hizi zinavyohusiana na kipindi cha baada ya uhuru.

(a) Shairi

TUMSHUKURU MANANI

1. Nalia nafurahiwa, tukumbuke ya zamani,  
Tukumbuke majaliwa, kutawaliwa nchini,  
Viumbe kutawaliwa, tulikuwa utumwani,  
Tumshukuru manani, uhuru tumejaliwa.

2. Tabu nyingi tulitiwa, sharia ziso imani,  
Uguzi ukatiwa, hata vyoo safarini,  
Sisi tulibaguliwa, hata kula hotelini,  
Tumshukuru manani, uhuru tumejaliwa.

FOR ONLINE READING ONLY

3. Tulifanywa ni wakiwa, tungemlilia nani,
Tukisemwa hutishwa, tutatiwa gerezani,
Ndivyo tulivyotumiwa, kama punda mizegani,
Tumshukuru manani, uhuru tumejaliwa.

4. Tulifanywa kama njiwa, waliotiwa tunduni,
Mtama tukitiliwa, kama ndege kifungoni,
Bure tulidhulumiwa, tulikosa kosa gani,
Tumshukuru manani, uhuru tumejaliwa.

5. Pasi na kuchunguliwa, ya kwamba tu masikani,
Kodi inapotakiwa, hufungwa kamba shingoni,
Pamwe na kuadhiriwa, kupitishwa mitaani,
Tumshukuru manani, uhuru tumejaliwa.

6. Shuleni hatukutiwa, ili tuwe ujingani,
Fasi hatukupatiwa, kutiwa utajirini,
Kucha kutwa hukomewa, kama majitu haini,
Tumshukuru manani, uhuru tumejaliwa.

7. Leo nasi twajaliwa, tuwe huru duniani,
Tuondokwe na ukiwa, tuwe viumbe thamani,
Tupate kuthaminiwa, baraza ya duniani,
Tumshukuru manani, uhuru tumejaliwa.

8. Uhuru kuachiliwa, kwamba haiwezekani,
Ndivyo tulivyoambiwa, si sisi wana chuoni,
Vizingiti vilitiwa, tubabaike njiani,
Tumshukuru manani, uhuru tumejaliwa.

9. Mafumbo tulifumbiwa, kama watoto shuleni,
Wengine kuadhiriwa, na kufukizwa mijini,
Kesi zilifunguliwa, na kutozwa mafaini,
Tumshukuru manani, uhuru tumejaliwa.

FOR ONLINE READING ONLY

10. Si kwamba ninachukiwa, kukumbuia shairini,
Haya ndiyo majaliwa, ya giza letu zamani,
Leo tunafunguliwa, na Mola wetu manani,
Tumshukuru manani, uhuru tumejaliwa.

11. Uhuru tumejaliwa, sasa na tufanye nini,
Wananchi twaambiwa, kazi zizidi nchini,
Ardhi kufukuliwa, iwe kazi namba wani,
Tumshukuru manani, uhuru tumejaliwa.

12. Vyama kifunguliwa, vya mapato ya nchini,
Ndipo tutapojaliwa, kuyafaidi madini,
Uvivu tukiingia, wote tutarudi chini,
Tumshukuru manani, uhuru tumejaliwa.

13. Maadui twaambiwa, ni watatu twabaini,
Ujinga twasimuliwa, ni adui namba wani,
Na maradhi yametiwa, pamoja umasikini,
Tumshukuru manani, uhuru tumejaliwa.

14. Tusipate kutatiwa, kushindwa nao katani,
Tukazane watatiwa, kufikiwa aridhini,
Tusije kutawaliwa, na kutiwa hatarini,
Tumshukuru manani, uhuru tumejaliwa.

15. Ijapo tukitolewa, fedha kutoka London,
Ya kwamba tulitetewa, na viongozi nchini,
Na iwapo mtalewa, mtarudi utumwani,
Tumshukuru manani, uhuru tumejaliwa.

**Chanzo:** *Mashairi ya Saadani* (Kandoro, 1988: 146-148)

FOR ONLINE READING ONLY

(b) Ngonjera

AZIMIO LA ARUSHA

**Mwana:** Baba tafadhali sana, nakuomba kwa hisani,
Mimi ningali kijana, mengi sijayabaini,
Sijaelewa maana, ni mgeni duniani,
Azimio la Arusha, nambie nilielewe.

Nambie lielewekе, niondoke ujingani,
Taratibu yatamke, mimi ni mwanao duni,
Lau ni mwana mteke, yataningia moyoni,
Azimio la Arusha, nambie nilielewe.

Nielewe Azimio, unambie kwa makini,
Liniondoke pumbao, mimi na dada nyumbani,
Wajue sisi wanao, tuondoke ujingani,
Azimio la Arusha, nambie nilielewe.

**Baba:** Ahsante ewe mwana, maneno yako matamu,
Utakayo yana maana, una akili timamu,
Lau ungali kijana, takwambia ufahamu,
Azimio la Arusha, laneemesha taifa,
Laneemesha taifa, laondoa madhalimu,
Wale wajipao sifa, kula mali ya kaumu,
Wameangushwa vifafa, kama walikula sumu,
Azimio la Arusha, laneemesha taifa.

Limeleta mambo mengi, Azimio hilo zuri,
Halikubagua rangi, akiwa mtu wa heri,
Ila wale wasarangi, wanyonyaji mabepari,
Azimio la Arusha, laneemesha taifa.

FOR ONLINE READING ONLY

*Mwana:* Ala, hivyo baba kweli, mabepari ni mirija?
Hujikusanyia mali, kwa sababu ya ujanja,
Uongo huzusha kweli, haki zetu kutupunja,
Azimio la Arusha, limeleta haki kweli?

*Baba:* Azimio lenye heri, mkono ninaliunga,
Alijalie Kahari, Rabi Mola Mwenye anga,
Tukayafyeke mapori, shoka mundu na mapanga,
Azimio la Arusha, laneemesha taifa.

Azimio ni jeupe, limeleta sura njema,
Mwanangu tusiwe kupe, tujitegemee vema,
Na uzembe tuutupe, na tuwe raia wema,
Azimio la Arusha, laneemesha taifa.

Azimio limenena, elewa mwanangu hasa,
Ni haramu kunyonyana, papa kummeza kasa,
Baba mama hata mwana, tuondoe hivyo visa,
Azimio la Arusha, laneemesha taifa.

Azimio ni azizi, kwa kila mtanzania,
Tusifanye upuuzi, tuzikaze zetu nia,
Tuwakabe mabazazi, watupotezao njia,
Azimio la Arusha, laneemesha taifa.

*Mwana:* Baba Azimio tamu, mwanao nimesikia,
Sasa nami naazimu, mjini kujihamia,
Nao wale madhalimu, wote wataangamia,
Azimio la Arusha, laneemesha taifa.

FOR ONLINE READING ONLY

Nanyi ndugu ikhiwani, mlio pwani na bara,
Tulinde yetu amani, tusimame kwa imara,
Na wale watu haini, wabaki wahangarara,
Azimio la Arusha, laneemesha taifa.

Wito wako twafurahi, ewe baba wa taifa,
Waovu tumewawahi, waharibifu wa sifa,
Wamekuwa majeruhi, wameona bora kufa,
Azimio la Arusha, ufunguo wa faraja.

**Chanzo:** *Ngonjera za Ukuta* (Mathias Mnyampala, 1970: 45 - 47)

### Je, wajua ?

Mataifa mengi ya Afrika yalipata uhuru kuanzia miaka ya 1960. Tanganyika ilipata uhuru wake mwaka 1961. Baada ya uhuru, fasihi andishi iliendelea kupata sura mpya kulingana na mahitaji. Waafrika walijikita katika kusherekea uhuru. Suala hili liliakisiwa katika kazi mbalimbali za fasihi zilizotungwa wakati huo. Kazi hizi zilijitokeza katika magazeti ambapo mashairi na hadithi nyingi zilionesha shamrashamra za kushangilia uhuru. Mifano ya kazi za fasihi zilizotungwa kuakisi hali hiyo ni pamoja na *Utenzi wa Uhuru wa Tanganyika* (Mwinyi Khatibu Muhammed Amri, 1967) pamoja na mashairi mbalimbali ya Saadan Kandoro kama vile, "Nyerere pokea hicho" na "Tumshukuru Manani" yaliyomo katika diwani ya *Mashairi ya Saadan*.

Hali kadhalika, katika kipindi hiki, kazi zingine za kifasihi zilitungwa ili kuhimiza ujenzi wa jamii mpya kwa kuwaasa wanajamii kuondokana na tabia pamoja na mienendo isiyofaa, na kuhimiza suala la kuzingatia uadilifu katika nyanja mbalimbali za maisha. Mifano ya kazi hizo ni *Utubora Mkulima* (Robert, 1968) na *Kuishi Kwingi Kuona Mengi* (Somba, 1968).

Kwa upande wa Zanzibar, kufuatia mapinduzi ya tarehe 12 Januari 1964, kuliibuka kazi za fasihi ambazo zilihusu ukombozi wa mnyonge. Baadhi ya kazi hizo ni *Kasri ya Mwinyi Fuadi* (Shafi Adam Shafi, 1978), *Nyota ya Rehema* (Mohamed Suleiman Mohamed, 1978), *Kuli* (Shafi Adam Shafi, 1979), *Dunia Mti Mkavu* (1980), '*Sikate Tamaa* (1983) na *Utengano* (1980) za Said Ahmed Mohamed, na *Utenzi wa Ukombozi wa Zanzibar* (Muhammed Seif Khatib, 1978).

Aidha, kipindi hiki kilifuatiwa na kipindi cha Azimio la Arusha ambalo liliasisiwa na

FOR ONLINE READING ONLY

Mwalimu Julius K. Nyerere mnamo mwaka 1967. Azimio hili lililenga kukomesha unyonyaji na unyanyasaji. Unyonyaji na unyanyasaji huo ulifanywa na baadhi ya watu wenye mali na wale waliopewa dhamana ya uongozi ambao walijikita katika kujineemesha wao wenyewe badala ya kuwatumikia wananchi. Falsafa kuu ya Azimio la Arusha ilikuwa Ujamaa na Kujitegemea. Pamoja na mabadiliko mengine, fasihi andishi pia ilipata sura mpya. Fasihi ya kipindi hicho ililenga kutukuza maadili na amali zilizotokana na tamko la Azimio la Arusha. Kazi nyingi za fasihi andishi za wakati huo zilisifu Azimio la Arusha. Miongoni mwa kazi hizo ni *Matunda ya Azimio* (Wah. Lucas Honero, Shaaban Ngole, na Tigiti Sengo, 1980), *Mashairi ya Miaka Kumi ya Azimio la Arusha* (UKUTA, 1977), na *Ngonjera za UKUTA* (Mathias Mnyampala,1970).

Kutokana na Azimio la Arusha kusisitiza vijiji vya ujamaa pamoja na shughuli za kilimo, kazi za fasihi andishi zilisawiri ubora wa maisha ya vijijini yakilinganishwa na yale ya mjini. Kazi zenye maudhui ya aina hiyo ni kama vile *Mtu ni Utu* (George Mhina, 1971), *Ndoto ya Ndaria* (John Ngomoi, 1975), na *Njozi za Usiku* (William Seme, 1975), na *Hatia* (Penina Muhando 1972).

Pamoja na kuwapo kwa kazi zilizosifu Azimio la Arusha, baadhi ya kazi zilihakiki azimio hilo kitunduizi. Baadhi ya kazi zilionesha kushindwa kwa Azimio la Arusha kutokana na sababu mbalimbali, ikiwa ni pamoja na baadhi ya viongozi kushindwa kulielewa vizuri Azimio hilo; hivyo, kushindwa kusimamia utekelezaji wake. Miongoni mwa kazi hizo ni *Njozi Iliyopotea* (Claude Mung'ong'o, 1979), *Lina Ubani* (Penina Muhando, 1984) na *Dunia Uwanja wa Fujo* (1978), *Gamba la Nyoka* (1978), na *Kaptula la Marx* (1999) za Euphrase Kezilahabi.

Katika miaka ya 1970 -1980, liliibuka wimbi la riwaya na hadithi fupi za upelelezi na za mapenzi. Waandishi wengi wa mkondo huu waliandika ili kuchuma fedha. Kazi zao zilisisimua wasomaji kutokana na fani yake ya kuvutia. Kwa upande mwingine, kazi hizi zilitimiza masharti ya mfumo wa kibepari kwa sababu hazikujishughulisha na matatizo halisi ya watu wa kawaida. Hata pale zilipoyashughulikia, zilipotosha ukweli na uhalisi wake. Hili lilitokana na kutoa majibu ya mkato ambayo hayakulenga kuonesha suluhisho la matatizo, zaidi ya kusisitiza utatuzi wa changamoto zilizobainishwa kwa kutumia polisi, mahakama na jela. Baadhi ya kazi hizo ni *Simu ya Kifo* cha Faraji Katalambula; *Njama* (1981), *Hofu* (1988), *Kikosi cha Kisasi* (2018) na *Kivuli* (2019) za Elvis Musiba; na kazi za Muhamed Said Abdulla kama vile vya *Mzimu wa Watu wa Kale*, *Kisima cha Giningi*, *Mke Mmoja Waume Watatu*, na *Kosa la Bwana Msa*.

Pamoja na kuzuka kwa riwaya pendwa, baadhi ya waandishi waliandika kazi zao zilizosawiri hali halisi ya maisha ya Mtanzania. Mifano ya kazi hizo ni *Fungate ya Uhuru* (Khatib 1974), *Raha Karaha* (Mvungi,1982), *Chungu Tamu* (Mvungi,1985) na

FOR ONLINE READING ONLY

*Kunga za Ushairi na Diwani Yetu* (Mulokozi na Kahigi, 1979).

Mwishoni mwa miaka ya 1980, ziliibuka riwaya za kimajaribio zinazokiuka au kutengua baadhi ya kaida za uandishi wa riwaya. Kazi hizi zilikuwa na sifa mbalimbali kama vile kukosa msuko ulio dhahiri, wakati mwingine zilikosa mhusika mkuu, na mara nyingi zilikwenda nje ya wakati (kama vile kuonesha mtu wa karne ya 16 akimtembelea mtu wa karne ya 20). Mara nyingi, riwaya za aina hii huwa na maudhui mazito ya kifalsafa yenye uchangamani mkubwa. Mifano ni riwaya za Kezilahabi za *Nagona* (1990) na *Mzingile* (1991), *Babu Alipofufuka* (Mohamed, 2001) na *Bin-Adamu* (Wamitila, 2002).

### Zoezi la 9.5

1. "Fasihi huakisi jamii kulingana na wakati. Tetea hoja hii ukirejelea fasihi ya Kiswahili katika miaka ya 1960.
2. Mambo gani yaliathiri dhamira za kazi za fasihi mwishoni mwa miaka ya 1960 na mwanzoni mwa miaka ya 1970? Fafanua kwa kutumia mifano maridhawa.
3. Linganisha dhamira za kazi za fasihi za miaka ya 1970 hadi 1980 na kazi za fasihi za miaka ya 2000 hadi 2020.

### Tamrini ya 9

1. Tumia mifano anuwai kueleza jinsi ujio wa wageni ulivyoathiri maudhui ya vitendawili, methali na mashairi ya Kiswahili.
2. "Fasihi ni kioo cha jamii". Fafanua hoja hii kwa kurejelea maendeleo ya fasihi kabla na baada ya ujio wa wageni.
3. Linganisha vipengele vya fani kama vinavyojitokeza katika kazi za fasihi za miaka ya 1960 - 1990 na 2000 - 2020.
4. "Dhima kuu ya fasihi ni kuielimisha na kuiburudisha jamii". Thibitisha kauli hii kwa kurejelea fasihi ya kabla na baada ya ujio wa wageni.
5. Ni kwa namna gani shairi la "Ondoka Nchini Kwetu" katika *Mashairi ya Saadani* linasadifu kipindi cha ukoloni? Fafanua kwa kujiegemeza katika kipengele cha dhamira.

FOR ONLINE READING ONLY

# Sura ya Kumi

# Uhakiki wa kazi za fasihi

### Utangulizi

**Uhakiki wa kazi za fasihi ni kipengele muhimu katika uchambuzi wa kazi hizo. Katika sura hii utajifunza kuhakiki fani na maudhui katika riwaya na tamthiliya. Pia, utajifunza kuhusianisha ujumbe unaopatikana katika riwaya na tamthiliya na maisha ya kila siku ya jamii husika. Umahiri utakaoujenga utakusaidia kukuza maarifa na mbinu za kuchambua kazi za fasihi.**

### Fikiri

Uwasilishaji wa kazi za fasihi katika jamii

## *Kuhakiki fani na maudhui katika riwaya*

### *Shughuli ya 10.1*

Chagua riwaya moja kutoka katika riwaya teule, kisha chambua ujitokezaji wa vipengele vya fani na maudhui katika riwaya hiyo.

### *Je, wajua*

Uhakiki wa kazi za fasihi unahusu uchambuzi wa vipengele vikuu viundavyo kazi ya fasihi. Vipengele vikuu vinavyounda kazi ya fasihi ni fani na maudhui. Fani na maudhui ni vipengele vinavyohusiana katika kukamilisha kazi ya fasihi. Fani ni jumla ya mbinu za kisanaa zinazotumiwa na mtunzi katika kuwasilisha maudhui ya kazi ya fasihi ilhali maudhui ni jumla ya mawazo yanayowasilishwa na mtunzi.

FOR ONLINE READING ONLY

Suala la uhusiano wa fani na maudhui limewashughulisha wataalamu wengi wa fasihi. Wapo wanaoona kuwa vipengele hivi vinaweza kutenganishwa (Nkwera, 1978) na wengine wanaona kwamba haviwezi kutenganishwa (Kahigi na Mulokozi, 1982; Senkoro, 2011). Ufafanuzi utakaotolewa hapa utazingatia mtazamo wa pili unaoeleza kuwa fani na maudhui ni vipengele visivyoweza kutenganishwa kwa sababu fani na maudhui huingiliana na kukamilishana.

*Vipengele vya fani katika uhakiki wa riwaya*

Vipengele vya fani vinavyopaswa kuzingatiwa katika uhakiki wa riwaya ni muundo, mtindo, wahusika, mandhari, na matumizi ya lugha. Ufafanuzi wa vipengele vya uhakiki katika riwaya unatolewa katika maelezo yanayofuata.

(a) **Muundo**

Uhakiki wa muundo katika riwaya unazingatia namna kazi ya kifasihi ilivyojengwa. Muundo hubainisha umbo la nje la kazi ya fasihi (Madumulla, 2022). Mbali na kukamilisha lengo la mtunzi, muundo una mchango katika kudhihirisha sifa za utanzu husika. Suala la msingi linalochunguzwa kwenye muundo wa riwaya ni msuko. Msuko ni mpangilio wa matukio kuanzia mwanzo hadi mwisho wa simulizi. Tukio ni kipengele muhimu katika kuukamilisha msuko. Mtiririko wa matukio unapaswa kuwa katika hali ya kujengana. Aidha, mtiririko wa matukio katika riwaya unaweza kufanywa kwa njia ya moja kwa moja au kwa ujereshi. Hali hii inaibua aina kuu mbili za msuko ambazo ni msuko wa moja kwa moja unaojulikana pia kama msuko mwepesi au msago, na msuko changamani. Hivi ni kusema kuwa msuko wa moja kwa moja hujengwa kwa kuzingatia mfuatano rahisi wa matukio. Mathalani, katika kuelezea maisha ya mtu, simulizi huanza toka mtu huyo anapozaliwa, matukio mbalimbali aliyopitia katika makuzi na utu uzima wake, mpaka kufa kwake. Nao msuko changamani unaweza kuanzia katika tokeo la masimulizi kisha kurudi kati au mwanzo. Mpangilio mzuri wa matukio humsaidia msomaji kuona lengo la mwandishi. Kwa hiyo, uhakiki wa msuko katika riwaya unapaswa kuzingatia mpangilio huo wa matukio na kuhusiana kwake katika kukamilisha kusudio la kisanaa.

(b) **Mtindo**

Mtindo ni namna ya kuisanifu kazi ya kifasihi ili kuibua uzuri wa kisanaa. Njogu na Chimerah (2011) na Senkoro (2011) wanaeleza kuwa mtindo ni mbinu ya utungaji inayompambanua mtunzi mmoja na mwingine. Uchambuzi wa mtindo katika riwaya unapaswa kuhusisha mbinu mbalimbali za kisanaa zilizotumiwa na mtunzi katika kuibua uzuri wa kisanaa. Matumizi ya mbinu hizi hutofautiana kati ya mtunzi mmoja na mwingine, na huweza kuathiriwa na jambo linalozungumzwa.

FOR ONLINE READING ONLY

(c) **Wahusika**

Wahusika ni watu, wanyama, vitu, miungu, na viumbe wengine ambao hutumiwa na mtunzi katika kazi ya fasihi. Kwa kutumia kigezo cha majukumu, kuna aina kuu mbili za wahusika ambazo ni:

(i) Wahusika wakuu

(ii) Wahusika wasaidizi

Wahusika wakuu hubeba wazo kuu la kazi husika na hujitokeza katika sehemu kubwa ya kazi. Wahusika wasaidizi huchangamana na kusaidiana na wahusika wakuu ili kutimiza lengo la mtunzi.

Kigezo kingine kinachotumika kuwaainisha wahusika ni tabia. Kigezo hiki kinaibua aina mbalimbali za wahusika kama vile:

(i) Wahusika bapa- hawa ni wahusika ambao hawabadikili kitabia na hata katika matendo yao katika miktadha mbalimbali.

(ii) Wahusika mviringo - hawa ni wahusika ambao hubadilika kitabia na matendo kulingana na mazingira.

(iii) Wahusika kivuli - hawa ni wahusika ambao hawatendi matendo yoyote katika simulizi, bali hutajwa tu bila kutolewa maelezo ya kutosha.

(iv) Wahusika shinda - hawa ni wahusika ambao hawana maamuzi yao peke yao, bali maamuzi yao hutegemea wahusika wengine.

Wahusika wakuu na wahusika wasaidizi walioainishwa kwa kutumia kigezo cha majukumu wanaweza kubeba sifa mbalimbali kitabia. Kwa mfano, mhusika mkuu anaweza kuwa na sifa za ubapa pia. Hivyo, uchambuzi wa wahusika katika riwaya unapaswa kufanywa kwa kuangalia majukumu yao yakihusishwa na tabia zao. Pia, uchambuzi huo unapaswa ufanywe kwa kuangalia namna walivyochangia kukamilika kwa lengo la mtunzi, hasa kwa kujikita katika maudhui.

(d) **Mandhari**

Mandhari ni mazingira na muktadha katika uwasilishaji wa visa na matukio yaundayo riwaya. Matukio katika riwaya hutokea mahali fulani, wakati fulani, na katika muktadha fulani mahususi. Mahali hubainisha eneo au maeneo yanamotukia matukio mbalimbali katika simulizi kama vile mlimani, baharini, nyumbani au angani. Wakati hubainisha muda na majira yanapotukia matukio husika. Kipengele hiki kinajumuisha saa na majira kama vile siku, usiku au mchana, asubuhi au jioni, masika, kiangazi au kipupwe. Muktadha husaidia kuonesha tukio limetokea kwenye mazingira gani. Kuna miktadha mingi ambayo inaweza kuathiri mwenendo na matendo ya wahusika. Baadhi

FOR ONLINE READING ONLY

ya miktadha hiyo inaweza kuwa sherehe, ugomvi, au matukio yanayohuzunisha na kutia simanzi. Mandhari katika riwaya husaidia katika ujengaji wa maudhui kupitia wahusika ambao hutenda au huonesha mienendo katika mazingira husika. Sifa za kimwonekano na kitabia za wahusika huweza kuathiriwa na kubadilishwa kutokana na uchangamani wao na mandhari. Uhakiki wa mandhari katika riwaya unapaswa kufungamanishwa na wahusika pamoja na matukio kwa sababu matukio yanayowasilishwa na mtunzi huwahusu wahusika na hufanyika katika mazingira mahususi.

(e) **Matumizi ya lugha**

Lugha ni kipengele muhimu kinachotumiwa na mtunzi wa kazi za fasihi ili kuwasilisha mawazo aliyoyakusudia. Kipengele hiki ndicho kinachotofautisha kazi za fasihi na sanaa nyingine. Maudhui ya kazi ya fasihi yanaweza kuathiriwa na matumizi ya lugha. Lugha inayotumika katika fasihi ni ya kisanaa inayoifanya iwe ya kipekee. Kuna vipengele mbalimbali vya lugha na mbinu za kisanaa zinazotumiwa na mhakiki katika kuchambua kazi za fasihi kama vile taswira, ishara tamathali za semi, semi mbalimbali, uteuzi wa maneno ya kuzungumzwa, takriri, usambamba, kejeli, na ucheshi.

*Zoezi la 10.1*

1. Linganisha miundo ya riwaya teule mbili ulizosoma.
2. Chagua riwaya teule moja, kisha hakiki jinsi wahusika walivyotumika kubeba dhamira za riwaya hiyo.
3. Hakiki namna tamathali za semi zilivyotumika kuibua dhamira katika riwaya teule mbili.
4. Kwa kutumia wahusika wawili kwa kila tamthiliya kati ya tamthiliya teule mbili, fafanua namna tabia na matendo yao yanavyosawiriwa na mandhari.

*Vipengele vya maudhui katika uhakiki wa riwaya*

Vipengele vya maudhui vinavyopaswa kuzingatiwa katika uhakiki wa riwaya ni dhamira, ujumbe, mtazamo, msimamo, falsafa, na itikadi. Ufafanuzi wa vipengele hivyo unatolewa katika maelezo yanayofuata.

(a) **Dhamira**

Dhamira ni wazo au mawazo makuu yanayopatikana katika kazi ya fasihi. Kwa kawaida, kazi za fasihi zina dhamira kuu na dhamira ndogondogo. Dhamira kuu hubainishwa katika kiini cha kazi ilhali dhamira ndogondogo husaidia kujenga dhamira kuu. Kazi moja ya fasihi inaweza kuwa na dhamira kuu moja au zaidi. Mifano ya dhamira ni elimu, ndoa, matabaka na mapenzi.

FOR ONLINE READING ONLY

(b) **Ujumbe**

Ujumbe ni mafunzo mbalimbali ambayo msomaji huyapata baada ya kusoma kazi ya fasihi. Wasomaji wa kazi za kifasihi, zikiwamo riwaya, wanaweza kupata ujumbe wa kazi hizo, unaoifaa jamii husika. Ujumbe hudhihirika kupitia dhamira zilizomo kwenye kazi ya fasihi. Ujumbe upatikanao kutokana na kusoma riwaya unaweza kutolewa kwa maelezo ya kawaida au kwa kutumia methali na ufafanuzi wake, pamoja na misemo mbalimbali. Aidha, ujumbe unaweza kupatikana waziwazi au kwa kificho. Mathalani, ujumbe mmojawapo katika riwaya ya **Kusadikika** (Shaaban Robert, 1951) ni 'juhudi ni ngazi ya mafanikio'; yaani, ukitaka mafanikio sharti uyatafute kwa kufanya kazi kwa bidii na kutumia maarifa.

(c) **Migogoro**

Mgogoro ni ukinzani au mvutano baina ya pande mbili au zaidi zinazotofautiana kimawazo. Kwa kawaida, migogoro huhusisha wahusika mbalimbali. Hata hivyo, katika fasihi, ni kawaida kuwa na migogoro binafsi, yaani ukinzani au mivutano inayotokea katika akili ya mhusika. Migogoro husababishwa na ukinzani au mivutano inayojitokeza ama ndani ya nafsi ya mtu, kati ya mtu na mtu, kati ya mtu na kundi la watu au kati ya kundi moja na kundi jingine la watu. Migogoro katika kazi ya fasihi husababishwa na tofauti za kimawazo au kimaisha baina ya wahusika au ndani ya mhusika binafsi. Tofauti hizo husababisha kuibuka kwa mvutano kati ya mtu na mtu, mtu na nafsi yake au baina ya mtu na jamii yake. Migogoro pia inaweza kuegemezwa katika siasa, utamaduni, uchumi na jamii.

Katika kuhakiki kipengele hiki cha migogoro katika riwaya, ni lazima mhakiki azingatie sababu zinazoibua migogoro na usuluhishi wa migogoro hiyo. Usuluhishi wa migogoro unatakiwa kutoa fundisho kwa jamii ili jamii iwe na mwenendo mzuri.

(d) **Falsafa**

Falsafa ni tafakuri au mawazo ya kina kuhusu masuala mbalimbali katika maisha. Tunapohakiki kipengele cha falsafa katika riwaya, pamoja na masuala mengine, tunachunguza mtazamo wa mwandishi kuhusu masuala mbalimbali katika maisha. Falsafa ya mwandishi inaweza kubadilika kulingana na muktadha na jinsi anavyoutazama ulimwengu na maisha kwa wakati huo. Hata hivyo, misingi ya falsafa ya waandishi wengine huwa haibadiliki. Mfano wa waandishi ambao falsafa zao hazionekani kubadilika ni Shaaban Robert na Euphrase Kezilahabi. Falsafa ya Shaaban Robert imekitwa katika msingi wa daima wema hushinda ubaya. Aidha, Shaaban Robert anahimiza watu wawe na mwenendo mwema ili uwafae katika maisha yao ya duniani na ya ahera. Kwa upande mwingine, Euphrase Kezilahabi anaona kuwa maisha hayana maana kwa sababu hata wanaoishi hawajui kwa nini wanaishi.

FOR ONLINE READING ONLY

Falsafa ya kazi ya fasihi au ya mwandishi fulani ni wazo ambalo mwandishi wa kazi hiyo analiamini kuwa ndilo lenye ukweli kuhusu maisha. Falsafa huweza kujitokeza kupitia mtindo uliotumika katika kuisana kazi hiyo. Aidha, uteuzi wa mada au dhamira za kushughulikia, na maadili yanayosisitizwa katika kazi hiyo ni sehemu ya falsafa. Aghalabu, tunaweza kuing'amua falsafa ya mwandishi kupitia kazi zake mbalimbali na si kazi moja tu.

Mara nyingi, falsafa huingiliana na kujengana na mtazamo na msimamo unaojitokeza katika kazi za fasihi. Kwa mfano, akieleza maana ya msimamo, Madumulla (2009, 2022) anasema kuwa, kutokana na mawazo, mafunzo na falsafa, msanii huweza kubainisha msimamo wake kuhusu masuala mbalimbali ya kijamii. Maelezo yanayofuata yanaonesha jinsi vipengele hivi vinavyotofautiana kiasi cha kufanya kila kimoja kiwe na umahsusi fulani.

(e) **Mtazamo**

Mtazamo ni jinsi ya kuyaona mambo yanayotokea katika maisha. Ni maoni ya mtu binafsi. Kila mtu ana namna ya kuyatazama masuala yanayomzunguka katika maisha yake. Namna hiyo hutofautiana na ya mtu mwingine. Kuna aina mbili za mitazamo ambayo huwaongoza wasanii kutunga kazi zao za sanaa na wahakiki kuhakiki kazi za kifasihi. Mitazamo hiyo ni mtazamo wa kidhanifu na mtazamo wa kiyakinifu (kisayansi). Mtazamo wa kidhanifu ni ule ambao unahisi msanii kuutazama ulimwengu kwa kudhania au kufikiri tu bila kuhusisha na uhalisi unaoweza kuthibitishwa. Kwa mfano, mdhanifu anaweza kuutazama ulimwengu kama kitu kinachoweza kubadilika kulingana na matakwa ya Mungu. Hii inamaanisha kuwa mabadiliko yanayoikumba jamii husababishwa na Mungu.

Kwa upande mwingine, mtazamo wa kiyakinifu ni mtazamo ambao unahusu msanii na mhakiki kuyatazama mabadiliko ya mambo katika jamii kisayansi. Hii inamaanisha kwamba mabadiliko katika jamii huendana na hali halisi iliyopo katika jamii. Mabadiliko hayo yanaweza kuthibitishwa kwa hoja, mifano na sababu dhahiri.

(f) **Msimamo**

Katika uhakiki wa kazi za fasihi, msimamo hutazamwa kama hali ya mtu kutetea jambo fulani bila kutetereka. Mara nyingi, msimamo wa msanii kuhusu jambo fulani huwa haubadiliki kwa sababu ndivyo anavyoongozwa na fikra zake kuhusu suala hilo katika muktadha fulani.

(g) **Itikadi**

Mawazo na imani kuhusu miongozo na mahusiano ya watu katika jamii huunda itikadi. Itikadi huongoza, kuhalalisha au kuhoji matendo na mahusiano ya watu kwa

FOR ONLINE READING ONLY

lengo la ama kuyadumisha au kuyabadilisha. Wakati mwingine, mivutano ya kijamii hujidhihirisha katika migongano ya kiitikadi ambapo kila kundi au tabaka huibua itikadi yake ili kutetea na kulinda masilahi yake. Hivyo, itikadi huweza kupotosha ukweli ili kulinda maslahi ya kundi fulani ndani ya jamii. Itikadi zinaweza kuwekwa katika mikondo mitano ambayo ni: Itikadi ya kijadi iliyojikita kwenye imani ya nguvu asilia; itikadi ya Ki-marx inayoitazama jamii kwa kuzingatia makundi ya kitabaka; itikadi ya kijamaa inayosisitiza ushirikiano wa kijamii; itikadi ya kibepari ambayo msingi wake mkuu ni umiliki binafsi wa nyenzo za uzalishaji mali; na itikadi ya kiliberali inayoweka msisitizo katika uhuru wa kujichagulia mambo na kufanya uamuzi.

Vipengele vya fani na maudhui vinavyozingatiwa katika uhakiki wa kazi za fasihi vimeoneshwa kwa muhtasari katika Kielelezo Na. 10.1.




**Kielelezo Na. 10.1.** *Vipengele vya uhakiki wa kazi za fasihi*

**Zoezi la 10.2**

1. Chagua riwaya teule mbili, kisha fafanua jinsi itikadi ya waandishi wa riwaya hizo inavyosawiri hulka ya jamii ya Kitanzania.
2. Kwa kutumia mifano kutoka katika riwaya moja teule, fafanua ujumbe unaojitokeza katika riwaya hiyo.
3. Chagua riwaya teule moja kisha fafanua falsafa ya mwandishi wa riwaya hiyo.

FOR ONLINE READING ONLY

4. "Kazi ya mwandishi ni kuibua uovu uliomo katika jamii." Tumia riwaya teule mbili kuthibitisha ukweli huu kwa kurejelea jamii ya Kitanzania.

## Uhusiano wa ujumbe unaopatikana katika riwaya na maisha ya kila siku

### Shughuli ya 10.2

Soma riwaya teule mojawapo, kisha bainisha ujumbe unaopatikana katika riwaya husika, na uhusianishe na maisha halisi ya kila siku.

FOR ONLINE READING ONLY

**Je, wajua ?**

Ili kuijadili vyema dhana ya ujumbe katika riwaya na namna inavyohusiana na jamii, ni muhimu kuanza kwa kuichunguza dhana ya riwaya yenyewe. Senkoro (1982) anasema kuwa riwaya ni hadithi ndefu ya kubuni, yenye visa vingi, wahusika zaidi ya mmoja na yenye mazungumzo na maelezo yanayozingatia maisha ya jamii kwa undani na upana. Anaendelea kusema kuwa riwaya inatoa picha ya ujumla wa maisha ya mtu kutoka nyumbani hadi katika kiwango cha taifa, na hata dunia nzima. Maelezo ya mtaalamu huyu yanaonesha namna maisha ya mwanadamu na mahusiano yake ya kijamii yanavyoweza kusawiriwa kwa kina kupitia riwaya. Naye Madumulla (2022: 23) anatoa hoja inayoonesha uhusiano wa ujumbe utolewao katika riwaya na jamii pale anapozungumzia umuhimu wa kipengele cha usimulizi katika ujenzi wa utanzu huu. Anasema:

> *"Ijapokuwa hatuihisi riwaya kwa macho yetu, na kwamba macho huona herufi tu, lakini hadithi hupenya katika fahamu zetu na kutufanya tuone, tusikie, tunuse, tuguse, na hata kuonja. Hutufanya tuingiwe na hamu, matamanio, woga na kutuwezesha kuchagua upande tunaopendelea."*

Kwa mujibu wa dondoo hili, riwaya hugusa hisia na milango ya fahamu za watu (wanajamii) kwa namna mbalimbali. Miguso hiyo huweza kutofautiana kulingana na hali halisi aliyonayo au aliyoipitia mwanadamu katika kipindi cha maisha yake. Hivyo, ujumbe unaowasilishwa katika riwaya unaakisi maisha ya wanajamii.

Aidha, vipengele vya fani na maudhui vinavyounda riwaya kama vile wahusika, matendo yao, mazungumzo yao, matukio yanayoibuliwa na mtiririko wake, mandhari na matumizi ya lugha havitoki nje ya maisha ya mwanadamu. Hii inamaanisha kuwa ujumbe unaowasilishwa katika riwaya unaibuliwa na dhamira zinazotokana na mwingiliano wa vipengele hivyo ambavyo si rahisi kuvitenganisha na maisha ya

mwanadamu. Ifuatayo ni mifano ya namna ya kubaini ujumbe katika riwaya na namna unavyohusiana na maisha halisi:

**Mfano wa 1:**

> Kila alipokutana na shida, ndipo bidii yake ilipozidi kukua. Baadhi ya watu hulegea mioyo mbele ya dhiki, lakini wengine hukazana mpaka wameishinda. Bidii ya Buruhani ilifanya mwangaza kama wa taa mbele yake, akazidi kupanua hatua kufululiza katika kazi aliyotumwa kwa uthabiti na furaha kubwa. Mwana mwema huyu, msafiri hodari na mjumbe wa kujivuniwa na Kusadikika nzima aliondoka hapa alipokuwa kijana. Aliporudi kwao alikuwa mzee aliyeyaonja mashaka na mabadiliko mbalimbali. Alijaribiwa na kila taabu, akashawishiwa na anasa zilizo ngumu kuzuilika. Hakusita kwenda mbele kwa uchungu wa shida wala hakughairi kurudi kwao kwa tamu ya anasa.
>
> **Chanzo:** *Kusadikika* (Robert, 1991:13)

Ujumbe wa matini hii unaweza kuwa "bidii, kujituma na kutokata tamaa ni msingi wa mafanikio." Ujumbe huu umetokana na dhamira ya bidii na kujituma inayobainika kupitia mhusika Buruhani. Ujumbe unaopatikana kutokana na kifungu hicho cha matini ya riwaya unahusiana na hali halisi katika jamii. Kwa kawaida, mtu yeyote anayeonesha bidii na kutokata tamaa katika kutimiza malengo yake hujiweka katika nafasi nzuri ya kufanikiwa. Tuchukue mfano wa mwanafunzi yeyote anayesoma. Suala la kusoma humlazimu mwanafunzi asitishe mambo mengine ambayo anapenda kuyafanya kama vile kuamka kwa muda anaoutaka yeye, na kutumia muda mwingi kufanya mambo yasiyo na tija. Kuachana na mambo hayo na kutia bidii katika masomo kunamsaidia mwanafunzi huyo kufaulu vizuri, na hatimaye kuajiriwa au kujiajiri baada ya kuhitimu.

**Mfano wa 2:**

> Jumba hilo kubwa ndilo lililokuwa kasri la mwenyewe Maksuudi ambalo aliponafasika na shughuli zake mjini, alipenda kwenda kupumzika na kutafaraji. Pengine alimchukua mama watoto na mtoto wake wa kike. Na hapo yeye mwenyewe tu ndiye aliyeonekana nje. Watoto wake daima walikuwa ndani. Na siku zile ambazo Mussa alimfuata babaake, ndiye aliyeonekana kwenda viamboni kuzungumza na kuchanganyika na watu. Lakini Mussa sasa yuko chuo kikuu mwaka wa tatu tena.
>
> **Chanzo:** *Utengano*, (Mohamed, 2011:99)

FOR ONLINE READING ONLY

Ujumbe mmojawapo unaoweza kupatikana kutokana na matini hii unahusu malezi na mahusiano yanayojengwa katika misingi ya ubaguzi wa kijinsia. Ubaguzi wa aina hii ni kikwazo katika kujenga usawa wa kijinsia. Katika muktadha wa matini hiyo, ujumbe huu umetokana na dhamira ya malezi na mahusiano ya kifamilia inayotokana na masimulizi yanayomhusu mhusika Maksuudi na namna alivyohusiana na familia yake. Aidha, ujumbe uliopatikana katika matini hiyo unahusiana na hali halisi iliyopo katika jamii. Ijapokuwa juhudi kubwa zimefanyika na zinaendelea kufanyika ili kuondoa suala la unyanyasaji na ubaguzi wa kijinsia, bado kuna jamii ambazo zinaendekeza mila na desturi zinazomnyanyasa na kumkandamiza mwanamke kama vile kumuweka utawa. Ndiyo maana elimu inazidi kutolewa na asasi za kiserikali na zisizo za kiserikali ili kujenga jamii yenye mahusiano bora kwa ustawi wa jamii.

### Zoezi la 10.3

1. Soma riwaya mbili, kisha eleza namna ujumbe wake unavyoakisi maisha ya jamii inayokuzunguka.
2. Kwa kutumia riwaya teule mbili, fafanua kauli inayodai kuwa ujumbe ni sura nyingine ya maudhui.
3. Husianisha ujumbe unaopatikana katika riwaya teule mbili na uhalisia wa maisha katika jamii unamoishi.

## Kuhakiki fani na maudhui katika tamthiliya

### Shughuli ya 10.3

Chagua tamthiliya teule moja, kisha isome na kufafanua jinsi visa na matukio yanavyofuatana.

### Je, wajua ?

Tamthiliya ni utanzu wa fasihi andishi unaoegemea katika umithilishaji. Kumithilisha ni kufananisha. Mhakiki wa tamthiliya anapaswa kuzingatia kuwa binadamu anatagusana na binadamu wengine pamoja na mazingira yanayomzunguka. Kuzungumza na kutenda ni miongoni mwa njia zinazotumika kufanikisha mtagusano huo. Kwa hiyo, mazungumzo ni nyenzo kuu ya uwasilishaji wa tamthiliya. Kinachomithilishwa ni mazungumzo na matendo ya wahusika huku kukiwa na nafasi ndogo ya masimulizi nje ya mazungumzo hayo. Hii ina maana kwamba tunawajua wahusika kutokana na maneno pamoja na matendo yao. Ijapokuwa tamthiliya inaweza kulinganishwa

FOR ONLINE READING ONLY

na riwaya kwa maana ya kazi ya kifasihi inayotumia lugha ya kisanaa kwa ajili ya kuwasilisha mawazo na mtazamo wa mtunzi, tanzu hizi zinatofautiana katika namna ya uundwaji wake.

Pamoja na kuzingatia vipengele vya fani na maudhui katika kuhakiki tamthiliya, sifa zinazoupambanua utanzu huu hazina budi kuwekewa mkazo. Inamaaninisha kuwa, ijapokuwa baadhi ya vipengele vya uhakiki wa tamthiliya hufanana na vya uhakiki wa riwaya, kinakachozingatiwa katika ufafanuzi wake ni namna vinavyojitokeza katika tamthiliya kwa kujiegemeza katika sifa za utanzu huu.

(a) **Mazungumzo**

Mazungumzo ni maongezi ya kujibizana yanayofanywa na wahusika katika kazi za kifasihi. Katika tamthiliya, mazungumzo ya wahusika ndiyo sifa inayoitofautisha tamthiliya na tanzu zingine. Mazungumzo ndiyo njia kuu ya kuwasilisha mawazo ya mwandishi. Umuhimu na namna mazungumzo haya yanavyopaswa kutumika unadokezwa na Wamitila (2003) anaposema, "Mazungumzo huhusisha mambo ambayo ni muhimu tu katika uendelezaji wa msuko wa kazi ya kifasihi na yanapaswa kuwa na sifa ya kutuwezesha kuwatambua wahusika wanaoshiriki katika maongezi hayo kutokana na uteuzi wao wa maneno, lugha zao, na matamshi yao. Kwa kuwa msingi wa tamthiliya ni mazungumzo kama wanavyobainisha Njogu na Chimerah (2011), kila kitendo kinapaswa kusukumwa na mazungumzo ili kufikia upeo au kilele chake.

(b) **Utendaji**

Vitendo vya wahusika huwa na thamani vinapoleta mabadiliko ya aina fulani katika mazingira au tabia za wahusika hao. Kwa jumla, vitendo katika tamthiliya vinapaswa kutegemeana ili tendo moja lisababishe kutokea kwa jingine. Aidha, vitushi viundavyo tamthiliya, zaidi ya kusababishana, vinapaswa pia kuingiliana. Kwa hiyo, uchunguzi wa matendo ya wahusika na namna yanavyowasilishwa ni muhimu katika uhakiki wa tamthiliya.

(c) **Maelekezo ya jukwaa**

Haya ni maelezo yanayoongoza uigizwaji wa tamthiliya husika ambapo hubainisha namna ya kuingia na kutoka kwa wahusika, mtindo wao wa uwasilishaji, miondoko ya wahusika, ishara zao, mandhari na mazingira ya igizo (Wamitila, 2003). Kwa kuwa yanafafanua zaidi simulizi, maelekezo ya jukwaa yanamsaidia msomaji au mtazamaji kuelewa vizuri tamthiliya na mwigizaji kupata misingi ya kuigiza uhusika fulani. Kama yanavyoisaidia hadhira kuielewa simulizi, maelekezo ya jukwaa humsaidia pia mhakiki kwa sababu yanafafanua zaidi muktadha wa tukio.

FOR ONLINE READING ONLY

(d) **Wahusika**

Wahusika wa tamthiliya wanaweza kutazamwa kwa kujikita katika mazungumzo yao, utendaji wao na kupitia maelekezo ya jukwaa. Kupitia vipengele hivyo, sifa, uhusika na mahusiano yao katika kutimiza kusudio la kutungwa kwa tamthiliya husika huweza kudhihirika.

(e) **Migogoro**

Kama ilivyo katika riwaya, migogoro ndani ya tamthiliya inaweza kuwa ya kiuchumi, kiutamaduni, kisiasa, baina ya wazo na wazo, na hata migogoro ya nafsi ndani ya mhusika. Migogoro husaidia kuwaunda wahusika na kuyajenga maudhui ya tamthiliya.

(f) **Muundo**

Mpangilio wa maonesho au matendo katika tamthiliya hutengeneza muundo wa tamthiliya hiyo. Baadhi ya tamthiliya zimegawanyika katika matendo ambapo tendo moja linaweza kuwa na maonesho kadhaa ndani yake. Tamthiliya nyingine zimegawanyika katika maonesho. Vilevile, baadhi ya tamthiliya zina muundo wa moja kwa moja, ambapo simulizi inaanza mwanzo hadi mwisho. Muundo wa moja kwa moja ulipendekezwa na Aristotle. Kama tulivyoona katika maelezo kuhusu riwaya, kwa upande mwingine, kuna tamthiliya ambazo hazina muundo wa moja kwa moja. Hizi ni zile zilizokiuka kanuni za Kiaristotle.

(g) **Mtindo**

Mtindo wa tamthiliya, kama ilivyo katika tanzu zingine za fasihi andishi, unatokana na ubunifu wa mtunzi. Mwandishi mwenye uwezo mkubwa wa kisanaa anaweza kufinyanga barabara fani itakayoongeza ujumi unaomvutia msomaji wakati huohuo ikifikisha maudhui yake kwa jamii. Ufundi huu wa mtunzi unapaswa kufungamana na sifa ya tamthiliya ya kutumia mazungumzo. Kama ilivyo katika tanzu zingine, mtindo wa tamthiliya hudhihirika katika matumizi ya lugha na mbinu nyingine za kisanaa. Vigezo vya uchambuzi wa lugha ni vilevile katika tanzu zote za fasihi. Hata hivyo, kwa kuwa tamthiliya hutumia mazungumzo, basi uhakiki wa lugha unapaswa kuzingatia kigezo na sifa hiyo. Matumizi ya lugha huzingatia utumiaji wa tamathali mbalimbali za semi, uteuzi wa maneno ya kuzungumzwa kufuatana na muktadha. Mbinu zingine zinazotazamwa katika kuudhihirisha mtindo wa tamthiliya ni takriri, usambamba, ucheshi, matumizi ya nyimbo na ngoma, na mitindo mbalimbali ya usimulizi na uzungumzaji. Aidha, mtindo wa tamthiliya unaweza kutazamwa kwa kutumia motifu inayotawala katika tamthiliya husika.

Pamoja na sifa za kifani, zile za maudhui pia zinapaswa kuzingatiwa katika uhakiki wa tamthiliya. Sifa hizo hazitofautiani na zile zinazotumika katika kuhakiki riwaya; zinajumuisha vipengele vya dhamira, ujumbe, msimamo, mgogoro, mtazamo, falsafa, na itikadi.

FOR ONLINE READING ONLY

**Zoezi la 10.4**

1. Kwa kutumia mifano kutoka katika tamthiliya teule moja, fafanua jinsi mtindo uliotumika katika tamthiliya hiyo unavyofungamana na tabia za wahusika wa tamthiliya hiyo.
2. Kwa kutumia mifano kutoka katika tamthiliya teule mojawapo, hakiki jinsi migogoro inavyoathiri maendeleo ya jamii katika tamthiliya hiyo.
3. Kutoka katika tamthiliya teule mbili, teua wahusika wawili kwa kila tamthiliya, kisha fafanua jinsi wahusika hao wanavyosawiri maisha ya baadhi ya watu katika jamii ya Watanzania.

## Kuhusianisha ujumbe unaopatikana katika tamthiliya na maisha ya kila siku

**Shughuli ya 10.4**

Soma tamthiliya teule, kisha fafanua ujumbe unaopatikana katika tamthiliya hiyo na uhusianishe na maisha halisi ya kila siku.

**Je, wajua ?**

Ujumbe unaopatikana katika tamthiliya unaweza kuhusianishwa na maisha ya kila siku kwa sababu maudhui yaliyofumbatwa katika dayalojia huakisi masuala mbalimbali miongoni mwa wanajamii. Aidha, ujumbe huo unaweza kuhusishwa na maisha ya kila siku kwa sababu tamthiliya imejikita kwenye kuiga kinachofanyika katika jamii. Njogu na Chimerah (2011) wanasisitiza kwamba tamthiliya ni mwigo wa maisha ya kawaida, yaani wahusika mbalimbali wanaakisi maisha ya binadamu katika jamii.

Maelezo ya Njogu na Chimerah yanashadidia uhusiano wa masuala yanayowasilishwa katika tamthiliya na maisha halisi ya jamii. Uigizaji unaofanywa na wahusika wa tamthiliya huakisi matukio na matendo yaliyopo kwenye jamii. Uigizaji huo huwa haufanywi kisisisi kwa maana ya kuiga kila kitu kama kinavyotokea katika uhalisi wake. Hufanywa kwa kuongezewa ubunifu. Maelezo zaidi kuhusu suala hili la uhusiano wa ujumbe unaowasilishwa katika tamthiliya na maisha ya jamii yanatolewa na Samwel (2015) anayeeleza kuwa, ingawa waigizaji na wahusika hawaigi sifa halisi, uigizaji huo husawiri sifa zilizoko kwenye jamii. Kwa hiyo, kwa kuwa jamii inaundwa na watu, na watu hao huhusiana kwa namna mbalimbali, ni dhahiri kuwa athari ya mahusiano yao huakisiwa kimatendo na kimazungumzo. Sifa hii ndiyo inayoifanya fasihi kuwa na

FOR ONLINE READING ONLY

dhima mbalimbali kwa jamii, ikiwamo kuboresha maisha ya wanajamii. Ifuatayo ni mifano ya namna ya kubaini ujumbe kwenye tamthiliya na kuhusiana kwake na maisha halisi:

Mfano wa 1:

*MITOMINGI:* Sisi kama utuonavyo tuko shughulini, shughuli hiyo si nyingine bali hiyo niliyosema sasa hivi kuhesabu watu. Na huyu kijana ndiye karani mwenyewe ahusikaye. Ingekuwa bora kama wewe na wanao wote mngetoka nje ili tufanye kazi yetu.

*MAMA:* Sasa baba mbona itakuwa ngumu.

*MITOMINGI:* Kwa vipi?

*MAMA:* Kama utatuhesabu wewe basi u mchawi.

*MITOMINGI:* Mbona sikuelewi?

*MAMA:* Mchawi ndiye anayehesabu watoto wa wanzake ili awaroge. Sasa wewe u mchawi? Hata kama si mchawi siwezi kukubali utuhesabu maana siwezi kujua nia yako ni mbaya au nzuri.

*MITOMINGI:* Mtu akuwaniaye uovu haji kweupe.

*MAMA:* Sawa usemavyo baba.

*Chanzo*: **Ngoswe: Penzi Kitovu cha Uzembe** (Semzaba, 2006:14)

Ujumbe katika dayalojia hapo juu unaweza kuwa "imani za kishirikina ni kikwazo cha maendeleo". Imani za kishirikina zinaweza kuficha au kupotosha taarifa sahihi za idadi ya watu. Matokeo yake, mipango ya serikali haitaweza kutekelezwa kwa usahihi kwa sababu baadhi ya taarifa kama vile idadi ya watu iliyoko si sahihi. Wananchi wanapaswa kutoa taarifa sahihi za sensa kwa manufaa ya taifa.

FOR ONLINE READING ONLY

Mfano wa 2:

*Mama Beti:* Ni haki yake, usimwonee wivu. Kumbuka wivu ni adui wa maendeleo. Unajua ameanza kuuza maji tangu mwanangu Beti akiwa ananyonya? Ni muda mrefu. Kweli kinachojenga nyumba siyo kazi unayofanya au kiasi cha pesa unayopata.

*Mama Vera:* Bali?

*Mama Beti:* Akili ya mtu na mpango wa matumizi mazuri ya fedha inayopatikana. Isitoshe, ushirikiano na maelewano ndani ya nyumba ni muhimu sana ili kuleta maendeleo katika familia.

*Chanzo:* **Halahala** (Mbijima, 2019: 3-4)

Ujumbe unaoweza kupatikana katika matini hii ni pamoja na 'kufanya kazi kwa juhudi na maarifa kuna manufaa,' na 'wivu ni adui wa maendeleo.' Ujumbe wa kwanza unaibuka kutokana na dhamira ya kufanya kazi kwa weledi iliyobainika kupitia mazungumzo ya Mama Beti kuhusu mmojawapo wa wahusika wa tamthiliya. Ujumbe huu unahusiana na maisha halisi kwani wapo watu waliofanikiwa kutokana na kufanya kazi kwa juhudi na maarifa. Kwa upande mwingine, ujumbe wa pili unabainisha kwamba kuna watu ambao huwa hawapendi kuona wengine wakifanikiwa. Hufanya jitihada za kuzuia au kubeza mafanikio ya watu wengine. Jumbe hizi, hususani wa kwanza, zinaweza kuelezwa kwa kutumia methali kama vile "Mchumia juani hulia kivulini", "Haba na haba hujaza kibaba", na "Mgagaa na upwa hali wali mkavu."

### *Zoezi la 10.5*

1. Tumia tamthiliya teule mbili kueleza namna ujumbe unaopatikana unavyohusiana na maisha halisi ya Kitanzania.
2. Msanii ni mwalimu bora wa jamii. Tathmini kauli hii kwa kutumia tamthiliya teule mbili ukizingatia jamii ya Kitanzania.

### *Tamrini ya 10*

1. Chagua riwaya teule mbili, kisha eleza jinsi methali zilivyotumika kuibua maudhui ya riwaya hizo. Toa hoja tano kwa kila riwaya.
2. "Mazungumzo ni nyenzo muhimu katika ujenzi wa tamthiliya." Tumia mifano kutoka katika tamthiliya teule mbili kuthibitisha kauli hiyo.
3. "Fasihi haitoki katika ombwe". Thibitisha kauli hii kwa hoja sita kutoka katika riwaya teule mbili.
4. Tumia tamthiliya teule mbili kufafanua jinsi mtindo wa mwandishi unavyotumika kuipa uhai kazi ya fasihi andishi.
5. "Jina la kitabu hubeba dhamira ya mwandishi." Thibitisha kauli hii kwa mifano bayana kutoka katika riwaya teule mbili.

FOR ONLINE READING ONLY

# Sura ya Kumi na moja
# Utungaji wa kazi za fasihi

### Utangulizi

**Utungaji wa kazi za fasihi huzingatia mbinu mahususi. Katika sura hii, utajifunza utungaji wa riwaya na tamthiliya kwa kuzingatia mbinu mwafaka. Umahiri utakaoujenga utakusaidia kubuni na kutunga riwaya na tamthiliya.**

### Fikiri

Jamii bila kazi za fasihi

## *Mbinu za utungaji wa riwaya*

### *Shughuli ya 11.1*

Chagua riwaya zozote tatu, kisha fafanua mbinu zilizotumika katika utunzi wa kila riwaya.

### *Je, wajua*

Utungaji wa riwaya unazingatia kanuni maalumu za kisanaa. Kama ilivyo katika utungaji wa tanzu zingine, utungaji wa riwaya humtaka mtunzi kuwa mbunifu ili aweze kutunga kazi yenye upekee na ambayo haitakuwa nakala ya kazi zilizotangulia. Ubunifu hutofautiana kati ya mtunzi mmoja na mwingine. Hata hivyo, jambo la msingi linalopaswa kuzingatiwa katika utungaji ni maarifa ya jumla kuhusu utanzu wenyewe na kaida zake. Kaida hizo ndizo zinazosaidia kutofautisha utanzu mmoja na mwingine. Mathalani, tofauti na tamthiliya, riwaya ni utungo wa kinathari kwa sababu unatumia

FOR ONLINE READING ONLY

lugha ya mjazo. Pamoja na mtunzi kufungwa na kanuni za kikaida za muundo wa riwaya, bado mwandishi ana nafasi kubwa ya kuongeza ubunifu wake.

Vipengele hivi viwili, yaani kanuni za utunzi na ubunifu wa mwandishi, ni vyema vikakamilishana ili kuwa na riwaya inayokidhi sifa za kitanzu na wakati huohuo kuwa na upekee. Ufafanuzi wa mbinu mbalimbali zinazotumika katika utungaji wa riwaya umetolewa katika vipengele vinavyofuata.

(a) **Mbinu ya usimulizi**

Usimulizi hujumuisha njia mbalimbali anazozitumia mtunzi wa riwaya kueleza matukio katika hadithi yake. Kuna aina kadhaa za usimulizi katika utungaji wa riwaya. Mathalani, kuna usimulizi unaofanywa na mhusika kwa nafsi ya kwanza. Aghalabu, katika usimulizi huu, mhusika huwa mshiriki katika matendo au matukio ya hadithi, na husaidia kujenga uhusiano wa karibu baina ya msomaji wa hadithi na hadithi yenyewe. Vilevile, kuna usimulizi-rejeshi ambapo hadithi hurejelea mambo yaliyotokea na kumfanya msomaji ayaunganishe na yale yanayotokea sasa katika riwaya husika. Ijapokuwa haya huweza kusimuliwa miongoni mwa wahusika wa riwaya, kwa kawaida, mhusika mkuu hutumia nafsi ya kwanza kuyasimulia. Nafsi ya kwanza ina ukaribu zaidi na msomaji kuliko nafasi ya tatu, kwa sababu katika nafsi ya kwanza, mtunzi anaonekana kama anazungumza na msomaji. Katika usimulizi wa nafsi ya tatu, mwandishi hueleza mambo yaliyofanywa na mtu au watu wengine. Usimulizi huu umezoeleka zaidi kwa sababu ya upana wa mawanda yake unaomruhusu msimuliaji aeleze hata mambo ambayo msimuliaji wa nafsi ya kwanza asingeweza kuyashuhudia. Nafsi ya tatu kwa kawaida inamuweka mwandishi mbali na msomaji kwa sababu mtunzi anasimulia matendo ya wahusika wengine.

Ndani ya usimulizi ndimo ambamo mbinu mbalimbali za kisanaa hutumika ili kumchechemua msomaji. Kwa hiyo, mtunzi yeyote hana budi kujifunza mbinu hizo anuwai ili azitumie anapoandika riwaya. Mbinu hizo hujumuisha ufafanuzi wa matukio hatua kwa hatua kwa namna inayomrahisishia msomaji kuielewa vizuri simulizi. Matumizi ya mbinu hizi humsaidia msomaji asibaki na maswali mengi yanayotokana na udhaifu wa usimulizi kwani yanamfanya ahisi kuwa anaishi katika matukio yanayosimuliwa. Kwa kufanya hivi, mtungaji wa riwaya huibua hisia na hata taharuki ambayo humfanya msomaji avutiwe na simulizi. Kwa ujumla, usimulizi mzuri humsaidia msomaji kuvutiwa kusoma na kuielewa riwaya vizuri.

(b) **Mbinu ya muundo**

Riwaya ni simulizi ndefu. Wakati mwingine, wanaotaka kuandika riwaya hawajui waanzie wapi na waishie wapi. Hapa ndipo suala la muundo linapokuja. Hutokea kuwa

FOR ONLINE READING ONLY

mwandishi anajua simulizi yake yote mwanzo hadi mwisho, lakini anapata changamoto kuhusu namna ya kuiandika ili itiririke vizuri. Ni muhimu basi kujifunza kipengele hiki cha muundo wa riwaya.

Muundo wa riwaya ni mpangilio wa sehemu mbalimbali za riwaya. Mpangilio huo wa visa na matukio hugawanywa katika mafungu kwa kuzingatia ukamilifu wa jambo linalowasilishwa. Si rahisi kusimulia matukio yote mfululizo kwa sababu riwaya hujumuisha mawanda mapana katika kuzungumzia masuala mbalimbali ya kijamii. Ndiyo maana, riwaya nyingi zina uchangamani wa visa na matukio. Usimulizi wa matukio unapogawanywa katika mafungu, humsaidia mtunzi kupangilia vizuri mtiririko na uwasilishaji wa mawazo yake. Vilevile, humrahisishia msomaji kufuatilia vizuri matukio bila kuyachanganya. Kwa mujibu wa Madumulla (2022), sura moja inaweza kujengwa na kisa kimoja kinachojitegemea, na kazi ndefu zinaweza kuwa na sehemu zaidi ya moja zinazoelezea kisa kimoja. Kwa hiyo, mtunzi anapaswa aandae muundo wa simulizi nzima, kisha agawe sehemu zinazojenga simulizi kabla ya kuanza kuandika.

Katika hatua za awali, mtunzi anapaswa amakinikie sura au sehemu mojamoja. Suala la msingi ni kuhakikisha kuwa kila sehemu ina mgogoro mkuu unaosukuma simulizi. Inashauriwa kuwa mtunzi mchanga aanze na migogoro inayohusisha wahusika wawili au zaidi ambapo kuna mvutano wa kutaka kutimiza jambo fulani. Hili litamsaidia kubainisha mivutano bayana baina yao. Migogoro itamsaidia mtunzi kuibua hisia na taharuki katika kila sehemu ya riwaya. Baada ya hapo, mtunzi ahakikishe kuwa sehemu mbalimbali zinaunganishwa barabara ili simulizi ishikamane. Hili litamfanya msomaji avutiwe kusoma riwaya yote kwa sababu kila sehemu inavutia.

Suala jingine la msingi sana ni kuhakikisha kuwa muundo wa riwaya unafuata taratibu za utunzi. Mathalani, katika sehemu ya utangulizi, mhusika mkuu anatambulishwa, na sifa na hulka za mhusika huyu hubainishwa sambamba na kudhihirishwa kwa migogoro aliyo nayo. Baada ya hapo, sehemu ya pili huonesha ukuaji wa migogoro ambapo wahusika wanapambana na kukuza zaidi migogoro baina yao. Mwisho, ni kilele cha simulizi ambapo migogoro inafikia ukomo na kutatuliwa na simulizi kuelekea ukingoni.

(c) **Mbinu ya ujenzi wa wahusika**

Wahusika ni nyenzo muhimu anayoitumia mtunzi kuwasilisha mawazo yake. Mtunzi wa riwaya anapaswa kuzingatia mambo kadhaa katika kuwajenga wahusika atakaowatumia katika kazi yake. Kwanza, mtunzi wa riwaya ateue idadi ya wahusika inayoendana na mawanda ya riwaya anayokusudia kuiandika. Wahusika wasirundikwe bila kuwapo kwa sababu ya msingi, bali kila mhusika abebe uhusika utakaochangia kukamilisha kusudio la mtunzi. Mhusika au wahusika wakuu wabebe wazo kuu la



FOR ONLINE READING ONLY

mtunzi, na wahusika wasaidizi wachangie kukamilika kwa wazo hilo. Pili, mtunzi wa riwaya anapaswa kuwafahamu vizuri wahusika wake. Hii itasaidia kuwapa wahusika hao uwezo wa kuzungumza na kutenda kulingana na uhusika wao. Tatu, wahusika wajengwe kwa namna inayosaidia kusukuma mbele msuko wa hadithi na si kuugandisha. Nne, mtunzi ahakikishe kuwa anampa msomaji maelezo kuhusu mwonekano wa wajihi wa wahusika ikiwa ni pamoja na sura zao na hata mavazi waliyovaa. Inatarajiwa kuwa maelezo kuhusu wahusika wakuu yatakuwa marefu zaidi ya yale ya wahusika wadogo. Mwisho, wahusika katika riwaya wasisimuliwe tu, bali wanapaswa kupewa uwezo wa kuzungumza na kutenda, japokuwa si kama inavyokuwa katika tamthiliya. Wahusika katika riwaya wanapopewa uwezo wa kuzungumza wao kwa wao, kunasaidia kuleta uhalisia, kuibua taharuki na kusisitiza wazo lisemwalo.

(d) **Mbinu ya usawiri wa mandhari**

Namna ya kusawiri mandhari katika riwaya haipaswi kuishia tu katika kutaja mazingira na muktadha wa utokeaji wa matukio, bali kuwapo kwa mazingira na miktadha hiyo kusaidie uibuaji wa hisia mbalimbali kwa msomaji. Mandhari yakiundwa vizuri, humhamisha msomaji kutoka pale alipo na kumwingiza ndani ya riwaya ambapo ataibua hisia zinazoakisi mandhari husika. Kwa mfano, mazingira ya msituni, mapangoni, na makaburini huweza kuibua hisia ya uoga au ujasiri. Mandhari katika utunzi wa riwaya inapaswa kukamilisha simulizi ya jambo linalosimuliwa. Vilevile, mtunzi wa riwaya anapaswa kufahamu vyema mandhari ya utunzi wa riwaya yake ili aweze kutamba katika mawanda mapana. Mtunzi hana budi kufahamu utamaduni wa jamii husika na vipengele vyake kama vile vyakula vyao, shughuli zao, mavazi yao, dini zao, na makabila yao. Hii ni muhimu pia katika kujenga uhalisi wa yale yanayosimuliwa na namna yanavyosimuliwa.

(e) **Mbinu ya mtindo**

Zaidi ya matumizi ya lugha, mtindo katika utunzi wa riwaya hujidhihirisha katika vipengele mbalimbali kutokana na ubunifu wa mtunzi mwenyewe. Mtindo wa riwaya fulani utang'amuliwa na namna mtunzi atakavyovitumia vipengele hivyo ili kuonesha umahususi wake unaomtofautisha na watunzi wengine. Baadhi ya vipengele hivyo ni:

(i) Utomelezi: huhusisha matumizi ya tanzu zingine ndani ya utanzu wa riwaya.

(ii) Matumizi ya nafsi: kama ilivyokwishaelezwa, nafsi ni kipengele muhimu katika kazi za fasihi kwa sababu kinaathiri ukaribu wa mtunzi, wahusika na msomaji. Ingawa kuna nafsi tatu, yaani nafsi ya kwanza, ya pili na ya tatu, kwa kawaida, riwaya nyingi huandikwa kwa nafsi ya tatu, na chache nafsi ya kwanza. Nafsi ya pili hutumiwa kwa nadra sana.

FOR ONLINE READING ONLY

(iii) Mbinu ya kuhoji: Hii ni mbinu inayotumiwa na msanii katika kuelezea mawazo yake kwa hadhira. Kunakuwa na hali ya kuhoji hata kama masuala yanayozungumziwa yanaeleweka. Pamoja na malengo mengine, mbinu hii hutumiwa ili kumfikirisha msomaji au msikilizaji.

(iv) Matumizi ya barua: Msanii anaweza kutumia mtindo wa barua katika kuandika kazi yake kama ilivyo katika **Barua Ndefu Kama Hii** (Mariama Bâ, 2009).

(v) Ujadi: Kupitia mbinu hii, vipengele vya fasihi simulizi, kama vile mianzo na miisho ya kifomula na wahusika, hutumika katika utunzi wa riwaya.

(f) **Mbinu ya matumizi ya lugha**

Utunzi wa riwaya humtaka mwandishi kuwa na uwezo mkubwa wa kuitumia lugha. Umahiri wake katika matumizi ya lugha haupaswi kuishia tu katika kujua kanuni zinazoitawala lugha husika, bali anapaswa kuwa na uwezo mkubwa wa kuitumia lugha hiyo kwa kuzingatia uhusiano wake na wanajamii wengine. Mtunzi wa riwaya anapaswa kuwa mbunifu wa kuitumia lugha katika miktadha mbalimbali kwa sababu matumizi ya lugha huathiriwa na muktadha. Pia, mtunzi anapaswa kufahamu tamathali za semi, ishara, taswira na alama mbalimbali zinazotumiwa katika jamii husika pamoja na maana zake. Hii itamsaidia mtunzi kuwa na uwekevu katika matumizi ya lugha. Kwa ujumla, weledi wa kuitumia lugha ya kisanaa ni jambo muhimu kwa mtunzi wa riwaya.

### Zoezi la 11.1

1. "Wahusika ni kipengele muhimu katika utungaji wa kazi za fasihi." Fafanua jinsi utakavyotumia kipengele hicho kama mbinu ya kutunga riwaya.
2. Fikiria kuwa wewe ni mtunzi mahiri wa riwaya. Eleza mambo ambayo unazingatia katika uteuzi wa mada.
3. Eleza jinsi muundo unavyotumika kusuka visa na matukio katika utunzi wa riwaya.

## Mbinu za utungaji wa tamthiliya

### Shughuli ya 11.2

Chunguza tamthiliya zisizopungua tatu, kisha fafanua mbinu za utungaji zilizotumika katika kila tamthiliya.

FOR ONLINE READING ONLY

**Je, wajua ?**

Mbinu za utungaji wa tamthiliya zinapaswa kuhusiana na sifa za utanzu wenyewe. Msingi wa tamthiliya ni mazungumzo au dayalojia. Katika vipengele vinavyofuata, mbinu zinazotoa mwongozo wa utunzi wa tamthiliya zimefafanuliwa.

*Mbinu ya mazungumzo*

Mtunzi wa tamthiliya anapaswa kufahamu kwamba sifa bainifu ya tamthiliya ni mazungumzo au dayalojia. Wazo linalowasilishwa katika tamthiliya linapaswa kutolewa kwa njia ya mazungumzo ya wahusika. Mwandishi anapaswa kuwasilisha mawazo yake kupitia kwa wahusika hao; asitoe wazo waziwazi kama mwandishi bali wazo hilo liibukie kwenye mazungumzo/mabishano ya wahusika. Mazungumzo hayo yanapaswa kujengwa kisanaa ili kukamilisha vitendo ndani ya tamthiliya.

*Mbinu ya maelekezo ya jukwaa*

Usimulizi katika tamthiliya ni namna mtunzi anavyoipambanua simulizi yake. Kwa kuwa msingi wa tamthiliya ni mazungumzo, mtunzi anapaswa adhihirishe usimulizi kwa kutumia mazungumzo. Ili kufanikisha lengo la usimulizi, mtunzi hana budi kutumia njia mbalimbali za kifasihi ili kuishirikisha hadhira yake. Njia hizo huzingatia uandishi mzuri wa maelekezo ya jukwaa, na maelekezo hayo huandikwa kwa hati mlazo ndani ya mabano. Pamoja na dhima nyingine, maelekezo ya jukwaa humsaidia msomaji kupata picha ya jumla na mielekeo ya namna wahusika wanavyotenda. Kwa hiyo, maelekezo ya jukwaa humsaidia msomaji kuelewa zaidi tamthiliya.

*Mbinu ya muundo*

Muundo wa tamthiliya ni mpangilio wa vitendo au maonesho katika tamthiliya. Baadhi ya tamthiliya zimegawanyika katika matendo yenye maonesho kadhaa ndani yake, na tamthiliya zingine zinatumia maonesho pekee. Mwandishi anaweza kuchagua mfumo anaoupendelea kulingana na uchangamani wa simulizi yake. Tamthiliya nyingi zina muundo wa moja kwa moja kama ilivyopendekezwa na Aristotle, yaani mwanzo, katikati na mwisho. Muundo huu umezoeleka katika simulizi mbalimbali katika jamii. Sehemu ya mwanzo inatoa utangulizi kuhusu wahusika, mandhari na wakati mwingine hudokeza mwanzo wa mgogoro. Sehemu inayofuata inahusu migogoro ambayo imekua zaidi hadi kufikia kileleni. Katika sehemu hii, migogoro aghalabu hupata suluhu. Sehemu hii inafuatiwa na sehemu ya tatu ambayo ni mwisho wa tamthiliya. Katika sehemu hii, migogoro aghalabu huwa inatatuliwa na ndipo tamthiliya inapoishia. Hata hivyo, kuna tamthiliya chache ambazo hazina muundo huu. Hizi huundwa kwa maonesho yanayojitegemea. Kila onesho lina simulizi yake ambapo mgogoro hukua

FOR ONLINE READING ONLY

na kufikia kilele. Hata hivyo, kwa kuwa zina wazo kuu moja na wahusika ni walewale, kimaudhui, inabaki kuwa tamthiliya moja.

Kwa hiyo, mtunzi wa tamthiliya anapaswa aamue aina ya muundo anaoutumia. Muundo unaotumiwa unasababishwa na aina ya uchangamani wa simulizi. Katika aina ya kwanza, anapaswa ahakikishe kwamba simulizi inatiririka kutoka mwanzo hadi mwisho. Akitaka kutumia muundo wa wazi usio wa moja kwa moja, basi ahakikishe kuwa kila onesho linasukumwa na migogoro ambapo kuna simulizi yenye mwanzo, katikati, na mwisho.

**Mbinu ya uumbaji wa wahusika**

Mtunzi wa tamthiliya anapaswa kuwa mweledi katika uteuzi na matumizi ya wahusika. Kutokana na tamthiliya kubeba sifa ya mazungumzo, wahusika wake wanapaswa kujengwa kwa kuzingatia mazungumzo yatakayosawiri migongano iliyopo. Mtunzi anatakiwa ahakikishe kuwa anawaumba wahusika ambao tabia na matendo yao vinachukuana ili msomaji asione ugumu wa kuhusisha wahusika na uhusika wao unaowakilisha wanajamii.

**Mbinu ya mtindo**

Tamthiliya, kama tanzu zingine za fasihi andishi, huandikwa kwa mitindo mbalimbali. Mtindo ni upekee wa vipengele mbalimbali vya tamthiliya fulani. Kuna vigezo mbalimbali vinavyoweza kutumiwa kuchambua dhana ya mtindo katika tamthiliya. Miongoni mwa vigezo hivyo ni namna mwandishi anavyojitofautisha na wenzake katika masuala kama vile uumbaji wa wahusika wake, lugha anayotumia, muundo anaoupendelea, ploti anazozitumia na mengine mengi. Kwa mfano, katika tamthiliya ya **Ngoswe: Penzi Kitovu cha Uzembe**, badala ya mtunzi kutumia matendo au maonesho, ametumia "Kijito", "Vijito", "Mto", "Jito" na "Baharini". Majina ya maonesho hayo yanaakisi mtiririko wa visa na maudhui.

**Mbinu ya matumizi ya lugha**

Mambo muhimu ya kuzingatia kuhusu matumizi ya lugha katika tamthiliya ni pamoja na ufundi wa kuitumia lugha hiyo. Ikumbukwe kuwa tamthiliya ni andiko linalolengwa kuigizwa jukwaani. Ili tamthiliya ivutie, ni lazima iwe na lugha inayoibua hisia kwa hadhira. Kwa hiyo, lugha ya tamthiliya inapaswa kuwa nyepesi ambayo inamuwezesha kila mtumiaji wa lugha kuelewa bila kuhitaji matumizi makubwa ya kamusi. Kwa kuwa fasihi ni kazi ya sanaa, basi mtunzi anapaswa kutumia lugha kisanaa ili kuitofautisha na lugha ya kawaida. Aidha, mtunzi anatakiwa ahakikishe kuwa anatumia lugha inayoakisi miktadha ya matumizi. Kila mhusika lazima azungumze lugha inayoakisi mazingira yake na uhusika wake. Kwa mfano, mazungumzo ya wazazi na watoto nyumbani

FOR ONLINE READING ONLY

hayawezi kufanana na lugha ya hotuba. Kila mhusika azungumze lugha inayodhihirika katika jamii.

**Zoezi la 11.2**

1. Eleza sababu za migogoro kuwa msingi wa utunzi wa tamthiliya.
2. Wewe kama mtunzi wa tamthiliya, eleza jinsi unavyoweza kutumia migogoro iliyomo katika jamii unamoishi kutunga tamthiliya.
3. "Lugha ya kisanaa hubeba masuala mazito yasiyoweza kuelezeka kwa lugha ya kawaida katika utunzi wa tamthiliya." Tathmini kauli hii kwa hoja sita zenye mifano maridhawa.

**Hatua za utungaji wa riwaya na tamthiliya**

Shughuli ya kutunga kazi za kifasihi, hususani riwaya na tamthiliya, haiwezi kufanywa kiholela. Ujuzi wa mbinu zinazotumika kutunga riwaya na tamthiliya ni hatua mojawapo ya kufanikisha shughuli hiyo. Zipo hatua mahususi zinazopaswa kuzingatiwa katika utungaji wa riwaya na tamthiliya. Hatua hizi zimebainishwa na wataalamu mbalimbali, wakiwamo Khamis (2003) na Wamitila (2018). Hatua hizo zimefafanuliwa katika vipengele vinavyofuata.

(a) *Kuwa na wazo la kuandikia*

Hatua hii inahusika na jambo lililomsukuma mtunzi kuandika kazi yake. Jambo hilo huweza kuchimbuka kutokana na matukio yanayotokea katika jamii, historia, migogoro iliyopo, na visa na mikasa. Matukio haya ni vichocheo vinavyomsukuma mtunzi kuandika ili kuunga mkono wazo fulani, kuripoti, kukosoa au kuelimisha. Mtunzi huyaona na huyasikia matukio haya kupitia milango yake ya fahamu. Kwa maneno mengine, milango mitano ya fahamu ni njia muhimu za upatikanaji wa wazo la kutungia riwaya au tamthiliya. Kupitia kuona, kusikia, kunusa, kugusa na kuonja, mtunzi anaweza kupata na kutumia hisi mbalimbali kwenye utunzi wake, kama vile furaha, huzuni, uchungu, woga, na tamaa kwa kuzitaja kwa uchache. Hivyo, ni vigumu kutunga kazi kutoka katika ombwe. Katika hatua hii, mtunzi anapaswa kufikiri kuhusu suala la kulitungia riwaya au tamthiliya. Kwa hiyo, utunzi wa riwaya na tamthiliya si suala linalohitaji papara, bali linahitaji utulivu wa kifikra maana, bila utulivu wa fikra, mtunzi hawezi kupata wazo la kuandika.

(b) *Kuwa na msukumo wa utunzi*

Baada ya kupata wazo, mtunzi anapaswa kufikiri kuhusu lengo la kutaka kutunga kazi yake. Msukumo wa kutunga kazi ya fasihi hutokana na lengo alilonalo mtunzi. Hapa, mtunzi anapaswa kujiuliza: Je, kwa nini kuna haja ya kulitoa kwa njia ya sanaa

FOR ONLINE READING ONLY

wazo nililolifikiria? Je, ninataka lifahamike tu? Je, likishafahamika ninatarajia nini? Je, jambo ninaloliwasilisha lina athari yoyote katika jamii? Kwa ujumla, ni vigumu kutunga riwaya na tamthiliya bila kuwa na msukumo unaotokana na mguso wa kihisia aupatao mtunzi ili kuweza kuyawasilisha yale yanayomsibu au yaliyomo katika jamii.

(c) *Kufikiria hadhira lengwa*
Hadhira ni watu waliolengwa kufikishiwa ujumbe. Mtunzi wa kazi za kifasihi ni vyema afikiri kuhusu hadhira anayoilenga. Katika jamii, kuna makundi mbalimbali ya watu ambayo hayafanani. Miongoni mwa vigezo vya kuwapo kwa makundi hayo ni umri, elimu, kipato na jamii. Kwa mfano, katika kigezo cha umri kuna watoto, vijana, watu wazima, na wazee. Makundi haya yanatofautiana kitajiriba, kiurazini, ushiriki wao katika shughuli za uzalishaji, na umilisi wa lugha. Tukichukua mfano wa kundi la watoto, tajiriba na urazini wao si wa kiwango kikubwa ikilinganishwa na watu wazima. Hii ina maana kwamba kazi za kifasihi, hususani riwaya na tamthiliya, zitakazotungwa kwa ajili ya makundi haya mawili haziwezi kulingana. Kwa hiyo, kufahamu hadhira iliyolengwa na sifa zake ni jambo muhimu linalopaswa kuzingatiwa katika utunzi. Hii itasaidia katika uteuzi wa mada, lugha ya kutumiwa na mbinu nyingine mbalimbali za kiutunzi.

(d) *Kutafuta taarifa (kutafiti)*
Kupata wazo la kutungia tamthiliya au riwaya hakumaanishi kuwa tayari mtunzi ana ufahamu wa kina kuhusu wazo husika kiasi cha kuweza kulitungia kazi ya kibunifu. Hali hii inaibua haja ya kutafuta taarifa na maarifa zaidi ili kuwa na mawanda mapana ya kiuandishi. Utafiti unamsaidia mtunzi kupata taarifa sahihi ambazo huenda atapenda kuzitumia katika kazi yake. Utafutaji wa taarifa unaweza kufanywa kwa njia mbalimbali ikiwamo kufanya utafiti juu ya mambo ya kuyaandikia. Mtunzi anapaswa kufahamu mambo zaidi ya mtu wa kawaida; hivyo, udadisi ni jambo muhimu kwake. Kwa mfano, mtunzi anapoona mafiga matatu asiishie kuyaangalia kama nyenzo zinazowezesha upikaji wa chakula na kwamba likiondolewa figa moja basi ni vigumu kukamilisha shughuli ya upishi kwa kuwa chungu au sufuria itaanguka. Anaweza kuyatazama mafiga hayo kwa kuyahusianisha na dhana ya ushirikiano. Ili watu waweze kupata ustawi katika nyanja mbalimbali, ni vyema kuungana katika utekelezaji wa majukumu yao. Katika hatua hii, mtunzi anahimizwa kuwa na jicho la kuona uhalisi uliopo katika jamii kama vile matatizo yaliyopo katika jamii na namna yanavyoweza kuwaathiri wanajamii.

(e) *Kufikiria utanzu wa kuuandikia na mbinu za kiutunzi*
Jambo linalohimizwa katika hatua hii ni maarifa ya kiutunzi. Uwezo wa kutunga riwaya

FOR ONLINE READING ONLY

na tamthiliya si suala linalotokea lenyewe tu kibahati nasibu, bali huhitaji maandalizi na kuwa na uelewa kuhusu utanzu wenyewe. Hapa, mtunzi anapaswa kuweka mikakati ya kukuza uelewa juu ya mambo ya msingi kuhusu utanzu aliouteua na maisha kwa jumla. Mkakati mmojawapo unaoweza kuwekwa ni kusoma na kuhakiki kazi za waandishi mbalimbali ili kujua sifa za jumla za utanzu husika na kupata mwongozo wa mbinu zinazotumiwa katika utungaji wa utanzu huo, ambapo kwa muktadha wa hapa ni riwaya na tamthiliya.

(f) **Kuandaa mpango na utaratibu (mbinu na uoanishaji wake na maudhui)**

Katika hatua hii, mtunzi wa riwaya au tamthiliya anapaswa kuandaa maelezo mafupi yanayotoa dira ya namna kazi yake itakavyokuwa. Ni muhimu mtunzi atafakari kuhusu mpangilio wa kazi yake akizingatia namna mwanzo, kati, na mwisho wa kazi hiyo utakavyokuwa. Aidha, mtunzi anapaswa kufikiri namna ya kuwasilisha vipengele vya fani kama vile wahusika, mandhari, muundo, na matumizi ya lugha kuhusiana na mawazo yanayotakiwa kuwasilishwa. Mpango huo unaweza kuandaliwa kwa njia ya dondoo au mchoro. Ni muhimu pia mwandishi awe na kijitabu cha kumbukumbu au shajara ambayo ataitumia kuandikia mambo anayokutana nayo katika sehemu mbalimbali, watu anaokutana nao, au hata kuhusu ndoto anazoziota ambazo huenda zikawa na umuhimu katika uandishi wake.

(g) **Kuandika muswada**

Katika hatua hii, mtunzi wa riwaya au tamthiliya huanza kuandika kazi yake. Uandishi unaweza kufanywa kwa njia ya mkono kisha kuchapa, au unaweza kufanywa kwa kuchapa moja kwa moja. Wakati wa uandishi, hasa katika hatua za mwanzo, mtunzi hushauriwa kuandika bila kufikiria sana usahihi wa kazi, hususani kanuni za kiuandishi. Hii itamsaidia kusonga mbele, badala ya kupoteza muda kwa kusahihisha.

(h) **Kuhariri muswada**

Hatua hii hufanywa baada ya muswada kukamilika. Katika hatua hii, mtunzi anapaswa kurudia kuusoma muswada wake na kuufanyia uhariri mara kadhaa. Baada ya hapo, muswada utolewe kwa watu wengine wenye weledi kuhusu uhariri ili wausome na kuuhariri. Kuhariri muswada husaidia kupunguza au kuondoa kabisa makosa ya kiuandishi, pamoja na kurekebisha maudhui.

(i) **Kuchapisha kitabu**

Hii ni hatua ya mwisho katika mchakato wa uandishi wa riwaya na tamthiliya. Katika hatua hii, mtunzi hutakiwa kupeleka muswada kwa wachapishaji kwa ajili ya mchakato wa kuchapisha. Hata hivyo, baadhi ya waandishi huamua kuchapisha wenyewe. Kwa hiyo, baada ya uhariri wa kina, mtunzi anaweza kuchapisha kazi yake mwenyewe. Hata

FOR ONLINE READING ONLY

hivyo, inashauriwa kuwa, kwa waandishi wachanga, ni vyema wakapeleka miswada yao kwa wachapishaji ili ichujwe zaidi.

## Kutunga riwaya

**Shughuli ya 11.3**

Kwa kuzingatia mbinu za utungaji wa riwaya, tunga riwaya yenye kurasa hamsini kuhusu mambo yanayoibua kero katika jamii yako.

## Kutunga tamthiliya

**Shughuli ya 11.4**

Kwa kuzingatia mbinu za utungaji wa tamthiliya, tunga tamthiliya yenye kurasa ishirini kuhusu mambo yanayokwamisha maendeleo katika jamii inayokuzunguka.

**Tamrini ya 11**

1. Fafanua changamoto zinazoweza kuikabili tamthiliya iliyotungwa na mtu asiyeijua hadhira yake kwa undani?
2. Pamoja na kufanana kimbinu, kuna tofauti kadhaa katika utunzi wa riwaya na tamthiliya. Bainisha na kufafanua tofauti hizo kwa mifano maridhawa.
3. "Tamthiliya haitungwi kiholela." Thibitisha kauli hii kwa hoja sita zenye mifano maridhawa.
4. "Uandishi wa riwaya huzingatia hatua za uandishi wa kazi za fasihi." Fafanua changamoto zinazoweza kumkabili mtunzi ambaye hajazingatia hatua hizo.
5. Teua riwaya mbili tofauti na riwaya teule, kisha fafanua mbinu zilizotumika katika utunzi wa kila riwaya.

**Kazimradi**

Chagua eneo lolote unalolipenda, ambalo linahusisha matumizi ya lugha ya Kiswahili, kisha fanya kazimradi kuhusu mada yoyote unayoipenda.

FOR ONLINE READING ONLY

## Faharasa

| | |
|---|---|
| **Adibu** | fundisha mwenendo mwema au tabia njema |
| **Amili** | pata uelewa wa lugha |
| **Blogu** | tovuti au ukurasa wa tovuti wenye taarifa au mawazo mbalimbali kutoka kwa mtu au watu fulani kuhusiana na mada fulani |
| **Chechemua** | tia hamasa |
| **Dhifa** | chakula rasmi aghalabu cha jioni, cha mkusanyiko wa watu wengi kwa ajili ya heshima ya mgeni mahususi au sherehe maalumu ambapo hotuba hutolewa pia |
| **Isimu** | taaluma inayochunguza na kuchambua lugha kisayansi |
| **Kategoria** | jumla ya vitu vya aina fulani vinavyoweza kuwekwa pamoja kwa mujibu wa sifa zinazofanana |
| **Kibaraka** | kiongozi wa serikali ya taifa huru anayetumiwa na serikali za kibeberu kwa faida yao |
| **Lahaja** | tofauti katika matamshi, maumbo na matumizi ya maneno katika maeneo mbalimbali kwa lugha yenye asili moja |
| **Leksikografia** | taaluma inayoshughulikia nadharia, mitazamo na mbinu za utungaji wa kamusi za aina mbalimbali |
| **Lugha chanzi** | lugha inayotumika kuwa ni msingi wa kurejelewa wakati wa kutafsiri matini |
| **Lugha lengwa** | lugha ambayo mada au maelezo kutoka lugha moja huelekezwa, kufasiliwa au hufasiriwa |
| **Majilio** | kuja au kutokea kwa mara ya kwanza kwa jambo au kitu fulani |
| **Manamba** | wafanyakazi wahamiaji kutoka maeneo ya mbali kwa ajili ya kufanya kazi katika mashamba makubwa kama vibarua |
| **Mawanda** | eneo ambalo mtu au akili inaweza kutalii, kwa mfano, mawanda ya kitaaluma |
| **Mnasaba** | uhusiano baina ya lugha moja na nyingine |
| **Motifu** | dhana inayotumika kuelezea elementi fulani ya kimuundo au kimaudhui inayotawala kazi fulani |
| **Mseto** | hali ya kuwa na mchanganyiko wa makabila |

FOR ONLINE READING ONLY

| | |
|---|---|
| *Mtaala* | utaratibu wa masomo wa kiwango fulani |
| *Nathari* | kazi za kifasihi zinazotungwa kwa kutumia lugha ya mjazo ambazo hazihusiani na ushairi |
| *Raghba* | hamu inayomfanya mtu atende jambo fulani, hisia |
| *Rasimisha* | fanya kitu au jambo kuwa rasmi |
| *Saili* | uliza maswali kwa madhumuni ya kutaka kujua jambo |
| *Tajiriba* | uzoefu alio nao mtu katika kutenda jambo fulani |
| *Tamrini* | kazi inayotolewa na mwalimu darasani kwa wanafunzi baada ya kufundisha umahiri fulani |
| *Tarishi* | mhudumu wa ofisi anayetumwa kupeleka barua au habari |
| *Tweza* | dunisha |
| *Uamilifu* | kazi |
| *Ujumi* | kanuni za uzuri au ubaya wa kazi za sanaa |
| *Umahiri* | ujuzi wa kufanya jambo fulani |
| *Urazini* | hali ya kuwa na ufahamu na utambuzi wa jambo au kitu |
| *Usuli* | taarifa ambayo ni muhimu katika kuelewa tatizo au hali |
| *Utendi* | utungo wa kishairi unaosimulia maisha ya shujaa |
| *Utenzi* | utungo mrefu wa kishairi unaoelezea historia au kisa fulani na ambao hauna vina vya kati katika mistari yake, bali kila ubeti una vina vya namna moja katika mistari yake isipokuwa mstari wa mwisho wa ubeti |
| *Uwekevu* | utumiaji wa maneno machache kueleza jambo |
| *Vitushi* | utungo mfupi wa kifasihi ambapo fanani huibua papo kwa papo kwa lengo la kuchekesha hadhira |
| *Wanaakiolojia* | wanataaluma wa mambo ya kale na ugunduzi wa vitu |
| *Weledi* | hali ya kubobea katika jambo fulani |
| *Zongoa:* | toa ufafanuzi wa jambo fulani lililokuwa linawatatiza watu |

FOR ONLINE READING ONLY

# Bibliografia


Abdulla, M. S. (1980). *Dunia mti mkavu*. Longman.

Abdulla, M. S. (1980). *Utengano*. Longohorn Publishers

Abdulla, M. S (1983). '*Sikate tamaa*. Longhorn Publishers.

Abdulla, M. S. 1957). *Mzimu wa watu wa kale*. East African Literature Bureau.

Amri, M. K. M. (1967). *Utenzi wa uhuru wa Tanganyika*. Idara ya Utangazaji na Utalii.

Balisidya, N. (1973). *Shida*. Foundation Books.

bin Ali bin Nasir, S. A. (1800). *Al-Inkishafi*. Longman.

Bodi ya Elimu Rwanda. (2019). *Kiswahili kwa shule za Rwanda: Mchepuo wa lugha kitabu cha mwanafunzi kidato cha nne*. Bodi ya Elimu Rwanda.

Brenn, E. & Johnson, F. (mh) (1928). *Mazungumzo ya Alfu Lela Ulela: Juzuu (1- 4)*. Longmans.

Bunyan, J. (1925) *Safari ya msafiri*. Society for Promoting Christian Knowledge.

Chacha, L. M. & Malangwa, P. S. (2019). *Semantiki*. Longhorn publishers.

Chiponde, S. (1928). *Hekaya za Abunuwasi*. Macmillan.

Diva, D. (1949). *Msafiri katika nyumba ya Sultani*. Sheldon Press.

el Ajjemi, A. H. (1972). *Habari za Wakilindi*. East African Literature Bureau.

Farsy, M. S. (1960). *Kurwa na Doto*. East African Literature Bureau.

Freeman- Grenville, G. S. P. (1958). " Swahili Literature and the History and Archeology of the East African Coast. *Journal of the East African Swahili Committee*, 28: 10-23.

Habwe, J. H. (2021). *Maenezi ya lugha ya Kiswahili nchini Sudani Kusini: Mafanikio na changamoto Swahili forum* 28:58-71.

Haggard, R. (1937). *Mashimo ya Mfalme Sulemani*. Longmans.

Honero L., Ngole, S., na Sengo, T. Wah. (1980) *Matunda ya Azimio*. Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.

Johnson, F. (1929). *Kisiwa chenye Hazina*. Longmans.

K. M. S. (1978). *Utenzi wa Ukombozi wa Zanzibar*. Oxford University Press.

Kahigi K. & Mulokozi, M. (1979). Kunga za ushairi na diwani yetu. Tanzania Publishing House.


FOR ONLINE READING ONLY

Kahigi, K. K. (2019). *Misingi ya semantiki na pragmatiki ya Kiswahili.* KAUTTU.

Kandoro, S. A. (1972). *Mashairi ya Saadani.* KIUTA.

Katalambula, F. *Simu ya Kifo.* East African Literature Bureau.

Kayamba, M. (1932). *Tulivyofanya na tulivyoona Uingereza.* Sheldon Press.

Kezilahabi, E. (1990). *Nagona*. Dar es Salaam University Press.

Kezilahabi, E. (1991). *Mzingile*. Dar es Salaam Univefrsity Press.

Kezilahabi, E. (1978). *Dunia uwanja wa fujo.* Vide Muwa.

Kezilahabi, E. (1978). *Gamba la nyoka*. Vide Muwa.

Kezilahabi, E. (1999). *Kaptula la Marx*. Dar es Salaam University Press.

Khatib, M. S. (1974). *Fungate ya uhuru*. Macmillan Aidan.

Khatib, M. S. (1978) *Utenzi wa ukombozi wa Zanzibar*. Oxford University Press.

*Kingsley, C. (1889). Mashujaa: Hadithi za Kiyunani. Inter-territorial Language (Swahili) Committee to the East African Dependencies.*

Kipango, R. (2014). "*Umuhimu wa elimu maalumu katika jamii*". Mwananchi. 9 *Desemba 2014, uk.19*

Kirumbi, P. (1975). *Misingi ya fasihi simulizi*. Shungwaya Publishers.

Kitereza, A. (1980). *Bwana Myombekere na Bibi Bugonoka na Ntulanalwo na Bulihwali.* Tanzania Publishing House

Madumulla, J. S. (2022). *Riwaya ya Kiswahili: Nadharia, historia na misingi ya uchambuzi. Afroplus Industries Limited.*

Massamba, D. P. B. (2004). *Kamusi ya isimu na falsafa ya lugha.* TUKI.

Massamba, D. P. B. (2007). *Kiswahili origins and the Bantu divergence – convergence theory: Professorial inaugural lecture serial No*. 48. Institute of Kiswahili Research.

Massamba, D. P. B. (2010). *Phonological theory: History and development* (*Toleo la pili*). TUKI.

Massamba, D. P. B. (2017). *Historia ya Kiswahili mtazamo mpya 100KK hadi 2000BK.* Kiswahili Development Limited.

Massamba, D. P. B., Kihore, Y.M., & Hokororo, J.I. (1999). *Sarufi miundo ya Kiswahili sanifu (SAMIKISA): Sekondari na vyuo.* TUKI.

Massamba, D. P. B., Kihore, Y.M., & Msanjila, Y.P. (2004). *Fonolojia ya*

FOR ONLINE READING ONLY

*Kiswahili sanifu (FOKISA): Sekondari na vyuo*. TUKI.

Massamba, D.P.B. (2002). *Historia ya Kiswahili: 50 BK hadi 1500 BK*. Jomo Kenyatta Foundation.

Matei, A. K. (2008). *Darubini ya sarufi: Ufafanuzi kamili wa sarufi ya Kiswahili*. Phoenix publishers.

Matinde, R. S. (2012). *Dafina ya lugha: Isimu na nadharia*. Serengeti Educational Publishers Limited.

Mazrui, A. M. & Shariff I.N. (1994). *The Swahili: idiom and identity of an African people*. Africa World Press.

Mbotela, J. (1934). *Uhuru wa Watumwa*. Nelson.

Mdee, J. S. (1999). "*Faharasa za Shaaban Robert na mchango katika leksikografia ya Kiswahili*". *Mulika*. Na. 24,14 - 31.

Mgullu, R. S. (1999). *Mtalaa wa isimu: fonetiki, fonolojia na mofolojia ya Kiswahili*. Longhorn Publishers.

Mhina, G. (1971). *Mtu ni utu*. Tanzania Publishing House.

Mnyampala, M. (1970). *Ngonjera za UKUTA*. Oxford University Press.

Mnyampala, M. (1977) *Mashairi ya miaka kumi ya Azimio la Arusha*, UKUTA

Mnyampala, M. E. (1970). Ngonjera za UKUTA: Kitabu cha kwanza. Oxford University Press.

Mohamed, M. S. 1978). *Nyota ya Rehema*. Oxford University Press.

Mohamed, S. (1990). *Kivuli kinaishi*. Oxford University Press.

Mohamed, S. A. (2001) *Babu alipofufuka*. Jomo Kenyatta Foundation

Mohamed, S. A. (1980). *Utengano*. Longhorn Publishers.

Mohamed, S. M. (1978). *Nyota ya Rehema*. Oxford University Press.

Mohammed, M. A. (1986). *Modern Swahili grammar*. East African Educational Publishers.

Mohammed, S. A. (1980). *Utengano*. Longman.

Mohammed, S. A. (1980). *Dunia mti mkavu*. Longhorn Publishers.

Mohammed, S. A. (1983). '*Sikate tamaa*. Longman.

Mreta, A. na Ochieng, D. (2022). *Kitangulizi cha semantiki na pragmatiki*. Shighatini Book Centre.

Msiba, E. (1981). *Njama*. Lioness Transcommunication Ltd

Msiba, E. (1988). *Hofu*. Mkuki na Nyota

Msiba, E. (2018). *Kikosi cha kisasi*. Mkuki na Nyota.

FOR ONLINE READING ONLY

Msiba, E. (2019). *Kivuli*. Orion Nairobi Press.

Muhando, P. (1972). *Hatia*. East African Publishing House.

Muhando, P. *(1984). Lina ubani*. Dar es Salaam University Press.

Mulokozi, M. M. (2017). *Utangulizi wa fasihi ya Kiswahili: Kozi za fasihi vyuoni na vyuo vikuu*. KAUTTU.

Mulokozi, M. na Kahigi, K. (1982). *Kunga za ushairi na diwani yetu*. Tanzania Publishing House.

Mulokozi. M. M. (1999). *Tenzi tatu za kale*. TUKI.

Mung'ong'o, C. (1979). *Njozi iliyopotea*. Tanzania Publishing House.

Mvungi, T. (1982). *Raha karaha.*Continental Publishers Limited.

Mvungi, T. (1985). *Chungu tamu*. Tanzania Publishing House.

Mwansoko, H. J. M., Mekacha, R. D. K., Masoko, D. L. W. na Mtesigwa, P. C. K. (2015). *Kitangulizi cha tafsiri: Nadharia na mbinu*. TUKI.

Ngomoi, J. *(1975). Ndoto ya Ndaria.* Tanzania Publishing House.

Njogu, K. & Chimerah, R. (2011). *Ufundishaji wa fasihi: Nadharia na mbinu*. Jomo Kenyatta Foundation.

Nkwera, F. (1976). "Fasihi," katika Mbonde, J.M. (1967). *Uandishi wa Tanzania: Insha*. East African Literature Bureau.

Oliver, R. and Mathew, G. (1963). *History of East Africa. Vol.1* . Oxford University Press.

Open University of Tanzania. (2005). *OSW 101 Utangulizi wa lugha na isimu*. Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Pöchhacker (2004). *Introducing interpreting studies*. Routledge.

Ramadhani, J. (1973). "Fasihi ya Kiswahili" katika *Mulika* 2:6-11

Resani, M. (2014). *Semantiki na pragmatiki ya Kiswahili.* Karljamer Print Technology.

Robert, S. *(1951). Kufikirika*. Oxford University Press.

Robert, S. (1952). *Adili na nduguze*. Nelson.

Robert, S. (1952). *Kusadikika.* Nelson

Robert, S. (1968). *Utubora mkulima*. Nelson.

Robert, S. (2010). *Adili na nduguze*. Mkuki na Nyota.

Samwel, M. (2015). *Umahiri katika fasihi ya Kiswahili: Mwongozo kwa mwanafunzi na mwalimu wa fasihi simulizi na andishi.* Meveli

FOR ONLINE READING ONLY

publishers.

Sehoza, S. (1921). *Mwaka katika minyororo*. U.M.C.A.

Seme, W. (1975). *Njozi za usiku*. Longman.

Sengo, T.S.Y. na Kiango, S. D. (1973). *Hisi Zetu*. Chuo cha Uchunguzi wa Kiswahili.

Senkoro, F. E. M. K. (1987). *Fasihi na jamii*. Press and Publicity Centre.

Senkoro, F. E. M. K. (1988). Ushairi: Nadharia na tahakiki. Dar es Salaam University Press.

Senkoro, F. E. M. K. (2011). *Fasihi*. KAUTTU

Shafi, A. S. (1978). *Kasri ya Mwinyi Fuad*. Acme Press Kenya Ltd.

Shafi, A. S. (1979). *Kuli*. Tanzania Publishing House.

Somba, J. N. (1968). *Kuishi kwingi kuona mengi*. East African Publishing House.

Swift, J. (1932). *Safari za Gulliver*. Sheldon Press.

Taasisi ya Elimu Tanzania. (2019). *Kiswahili shule za sekondari kitabu cha mwanafunzi kidato cha tano na sita: Fasihi*. Taasisi ya Elimu Tanzania.

Taasisi ya Elimu Tanzania. (2022). *Kiswahili shule za sekondari kitabu cha mwanafunzi kidato cha nne*. Taasisi ya Elimu Tanzania.

Taasisi ya Uchungunzi wa Kiswahili. (2003). *Makala za semina ya kimataifa ya waandishi wa Kiswahili: Fasihi*. TUKI.

Tanzania Institute of Education. (2022). *English for advanced secondary schools student's book - form five*. Tanzania Institute of Education.

Velten, C. (1907). *Prosa und poesie der Suaheli*. Im Selbstverlag des Verfassers.

Wamitila, K. (2002). *Bin-Adamu*. Phoenix Publishers.

Wamitila, K. W. (2003). *Kamusi ya fasihi na istilahi na nadharia*. Focus Publications Ltd.

Wamitila, K. W. (2018). *Mwenge wa uandishi: Mbinu za insha na utunzi (Toleo jipya)*. Vide~Muwa Publishers Limited.

Wanjala, F. S. (2002). *Misingi ya ukalimani na tafsiri kwa shule vyuo na ndaki*. Serengeti Educational Publishers (T) Ltd.

FOR ONLINE READING ONLY